NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 15 Mei, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaanza Kikao chetu cha Ishirini na Tisa katika Mkutano wetu wa Kumi na Moja. Katibu.

**NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. LINAH KITOSI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Swali letu la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Saul Henry Amon, Mbunge wa Rungwe na linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 241

**Kumaliza Ujenzi wa Vituo vya Afya – Jimbo la Rungwe**

**MHE. COSATO D. CHUMI (K.n.y. SAUL H. AMON)** aliuliza:-

Jimbo la Rungwe ambalo lina kata 29 lina vituo viwili tu vya afya ambavyo ni Masukulu na Ikati; wananchi wa Kata ya Mpuguso na Isongole kwa nguvu zao wameanzisha ujenzi wa vituo vya afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia kumaliza ujenzi huo ili kuwapunguzia adha ya kusafiri umbali mrefu kufuata matibabu katika Hospitali ya Wilaya ambayo baadhi ya maeneo ni takriban kilometa 50 na usafiri usio wa uhakika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saul Henry Amon, Mbunge wa Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na uboreshaji wa vituo vya afya 208 nchi nzima ili kuboresha

utoaji wa huduma za afya kwa wagonjwa karibu na wanapoishi. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 1, yaani mwezi Septemba, 2017 ilipeleka Sh.500,000,000 kwenye Kituo cha Afya cha Ikuti kwa ajili ya kujenga jengo la wagonjwa wa nje *(OPD),* chumba cha upasuaji, wodi ya watoto, wodi ya akina mama wajawazito, jengo la kuhifadhia maiti, jengo la kufulia la kisasa, mtambo wa *oxygen* na kukarabati miundombinu ili kuhakikisha huduma za upasuaji wa dharura kwa mama wajawazito na huduma nyingine zinapatikana katika Kata ya Ikuti badala ya kufuata huduma hizo kwenye hospitali ya wilaya ambayo iko mbali. Aidha, mwezi Aprili, 2018 Serikali imepeleka Sh.500,000,000 kwenye Kituo cha Afya cha Masukulu ili kujenga na kukarabati miundombinu itakayoboresha huduma kama ilivyo kwa Kituo cha Afya cha Ikuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Kituo cha Afya cha Mpuguso kimetengewa shilingi milioni 100 kutoka kwenye mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kumalizia jengo la wagonjwa wa nje *(OPD).* Sambamba na kuitaka halmashauri itenge fedha za mapato ya ndani ili kuendeleza ujenzi kwenye Kituo cha Afya cha Mpuguso na kuanza ujenzi kwenye Kituo cha Afya cha Isongole, napenda kutoa ahadi kwamba Serikali itavipa vituo hivyo kipaumbele cha juu ili ikiwezekana vikamilike mwakani.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali imeziagiza halmashauri ziwasilishe miradi viporo ambayo ilihubiriwa na wananchi isiyozidi kiasi cha shilingi bilioni 1 na kwamba fedha hizo zitaletwa katika mwaka huu wa fedha ili kuwapa wananchi nguvu waweze kumalizia miradi ile ambayo waliianzisha kwa nguvu zao. Je, ni lini Serikali sasa inaleta fedha zile kwa sababu umebaki takriban mwezi

mmoja mwaka wa fedha kuisha na ni Serikali yenyewe ndiyo ilituambia sisi halmashauri tulete hizo fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, pale Mafinga tunakusudia kukamilisha Kituo cha Afya cha Bumilayinga pamoja na zahanati mbili na kujenga nyumba za watumishi kwa maana ya wauguzi watakaoishi katika hizo nyumba kwenye Kituo cha Afya cha Bumilayinga na zahanati mbili za Ulole na Kisada pamoja na ile zahanati ya Sao-*Hill.* Je, ni lini Serikali inatuletea fedha ili tukamilishe miradi hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu swali moja tu lile la kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Cosato Chumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tulielekeza orodha ya miradi viporo iletwe TAMISEMI lakini hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya kujipanga vizuri kuweza kuwasaidia au kuunga mkono nguvu za wananchi. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Chumi na Waheshimiwa Wabunge wote kwenye halmashauri zao wawe na subira wakati Serikali inaendelea kujipanga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson.

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo hili la Rungwe ni kubwa sana. Hiyo ahadi iliyotolewa hapo na Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu Kituo cha Mpuguso na Isongole, ndiyo, wadau wameendelea kuchangia lakini sijasikia namna

ambavyo Serikali imejipanga. Kwa sababu amesema shilingi milioni 100 zitatoka katika mapato ya ndani, hayo yamekuwepo kila wakati, je, Serikali imejipangaje? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tena kwa ukamilifu tu. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika jibu la msingi nimeeleza kwamba halmashauri ya wilaya imetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa *OPD* katika Kituo cha Afya cha Mpuguso ambacho wameanza wenyewe kujenga kwa kushirikiana na wananchi. Nimetoa ahadi kwamba Serikali katika mwaka 2018/2019 itahakikisha kwamba vituo hivi viwili; cha Mpuguso na Isongole vinakamilishwa kwa utaratibu uleule ambao tumeutekeleza mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, kwa Rungwe, tutakuwa na vituo hivyo viwili kwa kuanzia. Naomba sana Mheshimiwa Mbunge tuwe na mawasiliano ya karibu, inapofika mwezi wa Agosti au Septemba kusudi tuhakikishe kwamba vituo hivi viwili vinapatiwa fedha za ujenzi ili viweze kukamilika 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapo hapo tuendelee kuwa na mawasiliano ya karibu kwa sababu Jimbo la Rungwe ni kubwa sana ili kusudi tuangalie na maeneo mengine.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sannda.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika kuipunguzia mzigo Hospitali ya Halmashauri ya Mji, Kondoa ambayo inahudumia zaidi ya halmashauri tatu, zahanati za Kata mbili za Kolo pamoja na Kingale zimewekwa katika mpango wa kupandishwa hadhi

na kuwa vituo vya afya. Je, ni lini sasa Serikali italeta hizo fedha kwa ajili ya kutekeleza hiyo awamu ya kuweka vituo vya afya?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ni lini mtaleta hizo fedha?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ME. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Edwin Sannda, Mbunge Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Zahanati za Kolo na Kingale zikipandishwa hadhi zinaweza sana kupunguzia mzigo hospitali ya wilaya. Kama nilivyojibu swali la Mheshimiwa Dkt. Tulia, naomba awe karibu sana kimawasiliano, mwezi Agosti na Septemba ili tuone namna ya kuzipatia fedha zahanati hizi hatimaye ziweze kupandishwa hadhi na Wizara ya Afya ziwe vituo vya afya.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na Swali 242 na linaulizwa na Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini.

Na. 242

**Kuwapatia Mafunzo Watendaji wa Vijiji Nchini**

**MHE. EDWARD F. MWALONGO** aliuliza:-

Watendaji wa Vijiji ni kada muhimu sana katika kuwahudumia wananchi walio vijijini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara watumishi hawa ili kuboresha utumishi wao na utoaji huduma kwa wananchi walioko vijijini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watendaji wa Vijiji kama walivyo watumishi wengine wa umma wanapaswa kupewa mafunzo mara kwa mara ili kuboresha utendaji na kuongeza ufanisi. Mafunzo yanayotolewa kwa Watendaji wa Vijiji hujumuisha masuala ya utawala bora, mapambano dhidi ya rushwa, mapambano dhidi ya UKIMWI mahali pa kazi, maadili ya utumishi wa umma pamoja na majukumu yao katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia ruzuku ya maendeleo kwa Serikali za Mitaa ambayo inajumuisha Mpango wa Mafunzo kwa watumishi wa kada mbalimbali, Watendaji wa Vijiji 1,840 walipewa mafunzo katika mwaka wa fedha 2016/17. Kuanzia Julai 2017 hadi Aprili 2018 kwa mwaka huu unaoendelea, Watendaji wa Vijiji 1,543 wamepewa mafunzo. Mpango huu ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuziagiza halmashauri zote nchini kuweka kipaumbele na kutenga bajeti ya mafunzo kwa kada hii muhimu na kuanzia mwakani tutaanza kufuatilia utekelezaji wa agizo hili ili kuhakikisha kuwa limezingatiwa na halmashauri zote wakati wa bajeti.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwalongo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majibu ya Serikali ni dhahiri kwamba mafunzo haya hayafuatiliwi ndiyo maana sasa wanaagiza. Katika mafunzo yanayotolewa hayahusu mafunzo ya ukakamavu, je, Serikali iko tayari kuweka mpango wa kuwapeleka baadhi ya Watendaji wa vijiji kupata mafunzo ya JKT ili kusudi kuwaimarisha kiutumishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika kutekeleza majukumu yao, Watendaji wa Vijiji wamekuwa wakipata madhara ikiwemo kudondoka na pikipiki na wengine kuumizwa na wananchi. Ni nani anayewajibika kuwalipa fidia pale wanapokuwa wamepata madhara hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili ya nyongeza, Mheshimiwa Joseph Kakunda, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwalongo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza, napenda kumpongeza sana kwa sababu anahitaji sana Watendaji wetu wawe wakakamavu. Napenda kumpa taarifa na kulipa taarifa Bunge lako Tukufu kwamba wale Watendaji wote ambao walipitia JKT kwa mujibu wa sheria kabla utaratibu huo haujasimamishwa kwa muda, hao hawahitaji kupatiwa mafunzo tena kwa sababu tayari hao ni *service girls and women.* Kwa hiyo, wale ambao hawakupitia mafunzo hayo, tumepokea wazo lake zuri, tutaandaa utaratibu siyo lazima kuwapeleka JKT bali wanaweza wakahudhuria mafunzo ya mgambo ambayo huendeshwa na Washauri wa Mgambo katika wilaya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili kuhusu fidia, zipo Sheria za Utumishi zinazoelekeza kuhusu fidia. Kwa hiyo, suala hili kwa sababu ni la kisheria, naomba sana watumishi wote ambao wanapata ajali au kuumia kazini sheria zipo zitumike. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunikumbuka maana mara nyingi sikumbukwi kwenye maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu liko sawasawa na la Mheshimiwa Mwalongo, ni kwamba kwenye Jimbo langu la Same Mashariki unakuta kata na vijiji hazina Watendaji, badala yake wanatumiwa Maafisa Ugani na wala wao hawana mafunzo ya kufanya kazi za utendaji. Ni lini Jimbo la Same Mashariki litasaidiwa ili tupate watendaji ambao wanakidhi hadhi ya kazi hiyo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu kwa kifupi, ni lini.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika nchi tuna tatizo kubwa la Watendaji hasa ngazi ya Watendaji wa Kata na Vijiji. Maeneo/halmashauri nyingi zina upungufu mkubwa sana wa Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji. Kwa hiyo, kutokana na upungufu huo wamekuwa wakitumika maafisa, wakati mwingine Maafisa Elimu wa Kata, Maafisa Ugani, Maafisa Kilimo wanakaimu.

**MWENYEKITI:** Ni lini mtawapeleka?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala hili kwa sababu tunaliweka katika utaratibu wa kuomba vibali vya utumishi, napenda kuahidi nchi nzima kwamba suala hili litakuwa limekwisha ifikapo mwaka 2020.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa pamoja na mafunzo ambayo wanapata Watendaji wa Vijiji katika utekelezaji wanakwenda kushirikiana na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vitongoji na Vijiji ambao wamekuwa wakilalamikia sana kuhusu maslahi yao. Napenda kujua, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha maslahi ya Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Vitongoji pamoja na kupewa mafunzo kama watakayopewa Watendaji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema kwamba tunafanya mafunzo mengi kwa ajili ya Watendaji, lakini napenda nimhakikishie kwamba mafunzo ya aina nyingi vilevile, hasa ya uongozi yamekuwa yakitolea kwa Wenyeviti wa Serikali za Vitongoji, Wenyeviti wa Serikali za Vijiji, Madiwani na viongozi wengine wa kuchaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maslahi, suala hilo kwa sababu liko katika maelekezo ya Serikali kwamba walipwe kupitia 20% zile za mapato ya ndani ya halmashauri, napenda kumuahidi kwamba mimi mwenyewe nitaanza ufuatiliaji wa karibu sana kuanzia mwaka ujao wa fedha ili kuhakikisha kwamba Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji wanalipwa.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali Na. 243, linaulizwa na Mheshimiwa Amina Saleh Mollel.

Na. 243

**Agizo la Bunge Kukusanya Kodi Katika Hoteli Zilizo Kwenye Hifadhi za Taifa**

**MHE. AMINA S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, ni kwa kiwango gani Serikali imetekeleza agizo la Bunge la kukusanya kodi katika huduma za mahoteli kwenye Hifadhi za Taifa kwa njia ya *Concession Fee Fixed Rate?*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Hasunga.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji wa Tozo ya *Concession Fees* kwa utaratibu mpya wa *Fixed Rate* ulianza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2017 kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na.234 la mwaka 2017. Kwa mujibu wa Tangazo hilo, kila mgeni anatozwa kati ya Dola za Kimarekani 25 na 50 kulingana na hadhi ya hifadhi husika. Kwa mfano, Hifadhi ya Taifa ya Mikumi ni Dola za Kimarekani 25 na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ni Dola 50 za Kimarekani. Kwa hivi sasa wawekezaji wote wanalipa tozo hiyo kwa viwango vilivyoainishwa katika Tangazo hilo la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha Tozo ya *Concession Fees* kilichokusanywa katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2020 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni shilingi bilioni 18.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.9 iliyokusanywa katika kipindi hicho mwaka 2016/2017. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 11.9 ambazo ni sawa na 174%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* iliyokusanywa kutoka katika makusanyo ya

Tozo ya *Concession Fees* kwa kipindi hicho ni shilingi bilioni 3.4 ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.2 zilikusanywa na kupelekwa *TRA.*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniopa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza na vilevile naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini pia nimpongeze Waziri kwa kushughulikia mgogoro wa Loliondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, tunafahamu awali kulikuwa na tatizo baadhi ya watu na zikiwemo baadhi ya hoteli zilikaidi kukusanya makusanyo haya. Nilitaka tu kujua pamoja na majibu haya mazuri, ni hatua zipi zimechukuliwa kwa wale ambao walikaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni hatua zipi zilichukuliwa kwa hoteli ambazo zilikiuka ukusanyaji huu wa kodi hii yaani *concession fees?*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Amina Mollel kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya, hasa katika kuwatetea watu wenye ulemavu. Amekuwa akifanya kazi hiyo vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wakati tunaanza utekelezaji wa tozo hii baadhi ya hoteli zilikuwa bado hazijapata elimu ya kutosha kwa nini tozo hi imeanzishwa. Kutokana na jitihada ambazo Serikali ilichukua kuwaelimisha

wamiliki wa hoteli zote hizo kwa nini tumeanzisha tozo hiyo na kwa nini ni muhimu kulipa na kwa nini tumeachana na mtindo wa zamani, basi hoteli zote hivi sasa zimeelimika na zote zinatekeleza. kwa sababu, zote zina-*comply* na utaratibu huu mpya basi hakuna hatua ambazo zimechukuliwa. Kwa wale ambao watakaidi ndiyo hapo tutachukua hatua lakini kwa hivi sasa zote zinatekeleza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine Magige.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana Watanzania wamekuwa wakilipa *Concession Fee* sawa na wageni. Je, ni kwa nini Serikali isione umuhimu wa kuwa-*charge Concession Fee* Watanzania tofauti na wageni?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Hasunga.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumjibu Mheshimiwa Catherine Magige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Concession Fees* inalipwa katika hoteli za kitalii na ni kwa wageni wanaotoka sana sana nje ya nchi, kwa wenyeji hawatozwi. Katika hilo, zile hoteli ambazo zinamilikiwa na Shirika la Hifadhi ya Taifa hazitozwi hiyo *Concession Fee.* Kwa hiyo, hii ni *specifically* kwa zile hoteli za kitalii.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii inachangia takribani 17% ya pato la Taifa na wamiliki wa hoteli hizi za

kitalii wamekuwa wakitozwa kodi nyingi au tozo nyingi sana takribani 46 na wamekuwa na malalamiko ya muda mrefu. Je, ni kwa nini Serikali isifikirie utaratibu mwingine wa kuwarahisishia hao wawekezaji kwenye hoteli za kitalii ulipaji wa tozo hizo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Hasunga majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paresso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa na kodi na tozo nyingi ambazo zimekuwepo katika baadhi ya hoteli, lakini jitihada zilizochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha hizi kodi zote zinahuishwa zinabaki chache. Mwaka jana, kama mtakumbuka, kuna baadhi ya kodi ziliondolewa na mwaka huu hivi sasa kuna kazi inaendelea kwa ajili ya kuhuisha kuangalia hizi kodi ziunganishwe kwa pamoja ili kurahisisha walipaji hao kusudi wasiwe na kodi za hapa na pale. Kwa hiyo, jitihada hizo zinafanyika na Mheshimiwa awe na subira, pale tutakaposoma bajeti yetu atasikia ni hatua gani ambazo tunakusudia kuzichukua.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunasonga mbele, swali linalofuata, swali 244 linaulizwa na Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum, linaulizwa kwa Waziri wa Madini.

Na. 244

### Wachimbaji Wadogo wa Madini Kupatiwa Maeneo

**MHE. UPENDO F. PENEZA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawapatia wachimbaji wadogo wadogo maeneo yaliyopimwa na kuwa na uwepo wa madini

kama dhahabu, ikiwemo Moroko katika Mkoa wa Geita na maeneo mengine yenye madini nchini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Naibu Waziri, Wizara ya Madini, Mheshimiwa Doto Biteko.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 1996, Serikali kupitia Wizara ya Madini imekuwa ikitenga maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini. Tangu kipindi hicho hadi sasa, Wizara ya Madini imetenga jumla ya maeneo 46 katika sehemu mbalimbali nchini yenye ukubwa wa hekta 281,533.69. Serikali kupitia Wizara ya Madini itaendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo kadiri yatakavyokuwa yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Geita Wizara imetenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini na kutoa leseni kama ifuatavyo: Eneo la Nyarugusu leseni 41; eneo la Rwamgasa leseni 36; eneo la Isamilo/ Lwenge leseni 22 na eneo la Mgusu leseni 22. Kwa sasa eneo la Moroko alilolitaja Mheshimiwa Mbunge lipo ndani ya leseni ya utafiti yenye Na.8278 ya mwaka 2012 inayomilikiwa na Mgodi wa Dhahabu wa Geita. Maeneo mengine ya mkoa huo yataendelea kutengwa kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 16 cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na Marekebisho yake ya mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara kwa kutumia taasisi zake za *GST* pamoja na *STAMICO* itaendelea kufanya utafiti ili kubaini uwezo wa mashapo ya madini katika maeneo mbalimbali nchini na kuyatenga kwa ajili ya uchimbaji mdogo

wa madini. Hii itawezesha wachimbaji wadogo wa madini kufanya kazi na kuchimba kwa uchimbaji wa tija. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Peneza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mwaka 2016, Serikali ilitoa Kauli kupitia Naibu Waziri wa Madini kipindi hicho Mheshimiwa Dkt. Merdad Kalemani, kuwa Serikali inafanya mazungumzo na *Geita Gold Mine* ili uweze kupunguza baadhi ya maeneo ambayo yako katika leseni yake. Swali la kwanza, napenda kujua kwamba, hayo mazungumzo yamefikia wapi ili wananchi walau waweze kupata maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, wachimbaji wadogo wadogo Geita kati ya malalamiko ambayo wamekuwa nayo ni pamoja na maeneo yanayotengwa dhahabu kuwa mbali sana na kutokana na vifaa vyao duni wanashindwa kuweza kuzifikia. Serikali kupitia *corporate social responsibility* kwa maana ya huduma za jamii ambayo mgodi umekuwa ukitoa kama vitu vya afya na vinginevyo, haioni kwamba ni muhimu sasa ikatoa mwongozo kwa *Geita Gold Mine* na maeneo mengine ili katika upande wa *corporate social responsibility* kuwajibika kuwasaidia wachimbaji wadogo katika maeneo yao hata katika ule msimu wa kupasua miamba ili walau waweze kuzifikia dhahabu katika maeneo hayo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri, Wizara ya Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Upendo Peneza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza lile alilolizungumza la mazungumzo kati ya Serikali na Mgodi wa *GGM* kuwapatia maeneo ya kuchimba wachimbaji wadogo, ni kwamba Serikali inaendelea na mazungumzo hayo kwa maeneo

mbalimbali ambayo migodi inaona kwamba inaweza kuyaachia kuwapatia wachimbaji wadogo. Hii siyo kwa *GGM* peke yake tu, wachimbaji na wenye leseni wengi kuna mahali tunazungumza nao ili waweze kuachia maeneo ya wachimbaji wadogo. Hii itawasaidia wale wanaochimba wenye leseni kuwa na mahusiano mazuri na jamii. Kwa sababu haina maana yoyote kama anachimba halafu kuna uvamizi unaendelea. Kwa hiyo, ili kudhibiti hilo, ni vizuri wakaangalia eneo fulani wawagawie wachimbaji wadogo ili kuwe na amani kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili juu ya matumizi ya *CSR* kwa ajili ya kuasaidia wachimbaji wadogo. Sheria na Kanuni mpya ya Madini *CSR* kwa sasa mpango unaandaliwa na mwenye leseni lakini mpango huo unapelekwa kwenye halmashauri, halmashauri yenyewe wajibu wake ni ku-*approve* kuona kwamba hicho wanachotaka kukifanya wanakihitaji. Kwa hiyo, naomba halmashauri pamoja na wenye migodi wakae chini wazungumze waone kama kipaumbele chao ni kutumia *CSR* kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wanaweza kufanya hivyo. Hata hivyo, Mgodi wa *GGM* umefanya kazi kubwa sana, tunajenga kituo cha mfano kule Rwamgasa cha uchenjuaji, Mgodi wa *GGM* umetoa fedha kwa ajili ya kusaidia kazi hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Niipongeze sana Wizara ya Madini kwa kipindi cha mpito toka Mheshimiwa Rais aliposema leseni ambazo hazifanyiwi kazi na watu wanaomiliki leseni nyingi na zinazoisha waruhusiwe wachimbaji wadogo waweze kuchimba. Mkoa wa Geita una raha kwa kuachiwa maeneo ya Rwamgasa, Nyakafulu, Stamico, *Tembo-Mine* na Bingwa. Je, Wizara ni lini mtawamilikisha wachimbaji wadogo ambao tayari wako kwenye maeneo ambayo yalikuwa leseni zake zimeisha na nyingine hazitumiki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Naibu Waziri, Wizara ya Madini, Mheshimiwa Doto Biteko.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Musukuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli anawapenda wachimbaji wadogo. Kwa kweli ametuelekeza tuwalee wachimbaji wadogo, tuwasimamie na tuwasaidie waweze kuchimba kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maeneo ambayo wameweza kupatiwa kwa ajili ya uchimbaji, ili tuweze kuwahalalisha ni lazima tuwapatie leseni. Naomba kutoa taarifa kwenye Bunge lako Tukufu kwamba ndani ya wiki hii tunayo maombi zaidi ya 8,000 ya uchimbaji mdogo tunaanza kutoa leseni. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alex Gashaza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi, ili niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa miongoni mwa *Retention License* zilizofutwa ni pamoja na *Retention License No. 0001/2009* ambayo ilikuwa inamilikiwa na *Kabanga Nikel Company Limited.* Kwa kuwa sababu zilizokuwa zimesababisha *Kabanga Nikel* wasiweze kuanza kuchimba ni kutokana na bei ya *nikel* kushuka lakini pia miundombinu ya usafirishaji kwa maana ya reli na Ngara kutokuwa na umeme wa uhakika. Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Tanzania na hususan wananchi wa Jimbo la Ngara, ambao walikuwa wanategemea mgodi huu kama ungeanza wangeweza kupata ajira na kuinua kipato chao?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Madini, Mheshimiwa Doto Biteko.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Alex Gashaza, Mbunge wa Ngara. Kabla sijajibu, niseme tu kwamba, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Alex Gashaza kwa ufuatiliaji wake kwenye mradi huu wa *Kabanga Nikel,* kwa kweli, amekuwa mtu ambaye kila mara anataka kujua nini kinchoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo jana Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Waziri walivyojibu, walieleza juu ya ufutwaji wa leseni zote za *retention.* Nataka niendelee kumwambia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba leseni hizi zote za *retention* zimefutwa kwa mujibu wa sheria na Serikali sasa inaangalia namna bora ya kuzisimamia leseni hizo ambazo zimerudishwa Serikalini.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali Na. 245, linaulizwa na Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga.

Na. 245

**Mradi wa Maji wa Kalenga – Tanangozi – Wilaya ya Iringa Vijijini**

**MHE. GODFREY W. MGIMWA** aliuliza:-

Mradi wa Maji wa Kalenga – Tanangozi ni wa muda mrefu na miundombinu yake imechakaa kabisa na hivyo kushindwa kukidhi mahitaji ya wananchi:-

Je, ni lini Serikali itaanza kurekebisha mradi huu ili wananchi wapate maji ya uhakika?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Naibu Waziri, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Oweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Kalenga – Tanangozi ni mradi uliojengwa kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Shirika la Kimataifa la Denmark *(DANIDA)* na kukamilika mwaka 1982. Mradi huo ni wa maji ya mtiririko ambao ulikuwa unahudumia vijiji 10 vyenye wakazi 12,000 kwa wakati huo. Aidha, kutokana na ongezeko la watu, taasisi mbalimbali na uchakavu wa miundombinu, maji ya mradi huo kwa sasa hayatoshelezi mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua adha ya maji ambayo wananchi wanaipata kutokana na kutotosheleza kwa maji katika mradi wa Kalenga – Tanangozi, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Iringa katika mwaka wa fedha 2017 imeweka mradi huo katika mpango wa ukarabati kwa kutumia fedha za *Payment By Result (PBR).* Ukarabati utahusisha sehemu zote korofi za mradi huo na hivyo kuwapunguzia adha ya maji wananchi wa Kalenga – Tanangozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda mrefu, Serikali inaendelea kutafuta raslimali fedha za kutosha ili kukarabati mradi huo kwa kuwasilisha andiko la mradi kwa wadau wa maendeleo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mgimwa.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naomba niseme kwamba mradi huu una zaidi ya miaka 35 na idadi ya watu ambao wapo katika eneo hili sasa hivi imeongezeka zaidi ya mara tatu na miundombinu yake imechakaa. Halmashauri imeomba fedha jumla ya shilingi milioni 276 lakini fedha zilizopelekwa ni shilingi milioni 59 tu, napenda kufahamu, hizi shilingi milioni 59 ambazo

zinagawanywa katika majimbo mawili katika wilaya moja zitawezaje kukamilisha mradi wenye idadi ya watu wengi kama huu ambao unategemewa na wananchi zaidi ya 36,000? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba, je, Naibu Waziri au Waziri wanaweza wakawa wako tayari kuungana na mimi ili twende Kalenga tukaone mradi huu ambao kwa kweli ukikamilika utakuwa unaleta tija kwa wananchi wangu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Waziri mwenyewe wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Eng. Isack Kamwelwe.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya Wabunge wote, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mgimwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa tumeshaweka utaratibu kwamba, hatukuletei fedha mpaka uzalishe. Kwa hiyo, hiyo shilingi milioni 59 imekuja kulingana na *certificate* uliyoleta. Ungeleta *certificate* ya shilingi milioni 200 basi tungekupa shilingi milioni 200. Hatuleti fedha ukae nayo, kwanza lazima uzalishe ndio tuweze kuleta fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili, nilishafika huko, lakini pia nitamruhusu Naibu Waziri wangu tukishamaliza Bunge ataambatana naye. Hata hivyo, niwape utulivu wananchi wa Kalenga kwamba ule mradi sasa ni mkubwa tunahitaji fedha nyingi siyo shilingi milioni 200 tena. Ndiyo maana katika jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri amesema tunataka tuufanyie usanifu kwa sababu utagharimu hela nyingi ili tuweze kutafuta fedha kwa wafadhili tuhakikishe kwamba maji yanawatosheleza wananchi wote wa eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa Ibofwe uko Mkoani Iringa ambao unahudumia vijiji 10. Nilikwishauliza swali la msingi nikajibiwa kwamba shilingi milioni 49 zitatolewa baada ya kutoka *certificate. Certificate* ilishatolewa pesa hazijapatikana toka mwaka jana, naomba kujua ni lini pesa hizo zitatolewa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, ni lini fedha hiyo itatolewa kwa mradi huo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii kumjibu Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa maji ni uhai na sisi kama Wizara ya Maji hatupo tayari kupoteza uhai wa wana Iringa, namuomba Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge tukae na wataalam wetu tuangalie namna ya kuzipeleka fedha hizo wananchi wapate maji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kunipa nafasi hii. Eneo la Mishamo ni eneo ambalo liliishi wakimbizi na sasa hivi ni Watanzania wapya ambao wamepewa uraia na Serikali. Eneo hili kupitia Shirika la *UNHCR* lilichimba visima karibu vijiji 16, vijiji hivyo kwa sasa havina maji kwani visima hivyo vilishaharibika. Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia kufufua visima hivyo ambavyo kimsingi vikifufuliwa na Serikali vitatatua kero ya maji katika maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake lakini kwa namna

bora ya kuhakikisha wananchi wake wanapata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara ya Maji tumekuwa na taratibu ya kufufua visima vyote ambavyo vimekufa kwa kuvirudisha katika hali yake ili wananchi waweze kupata maji. Nipo tayari kuongozana naye kwenda kuona hali halisi ili mwisho wa siku tupange namna gani tunaweza tukavifufua visima vile ili wananchi wake waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Willy Qambalo.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mradi wa Maji wa Kijiji cha Getamok, Namahaha na sasa Endonyoet katika Wilaya ya Karatu iliojengwa chini ya Mpango wa *WSDP I* haufanyi kazi kwa sababu ya kujengwa chini ya kiwango. Serikali ilituma wataalam wake kukagua tatizo hilo ili kubaini kiwango ambacho kingehitajika kufufua miradi hiyo. Je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha ili kurudisha huduma hiyo muhimu kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Waziri mwenyewe, Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Eng. Kamwelwe.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Qambalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeunda Tume maalum ya wataalam watakaohusisha sekta mbalimbali za Serikali. Tutachukua pamoja na hiyo ripoti ambayo anasema kwamba Serikali ilituma timu tuiangalie ili tukishabaini sasa ule upungufu tutatoa fedha na kukarabati mradi husika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali 246, linaulizwa na Mheshimiwa Mheshimiwa Omari Kigua, Mbunge wa Kilindi, kwa niaba yake Mheshimiwa Omari Kigoda.

Na. 246

**Mpango wa Kuvuna Maji ya Mvua - Wilaya ya Kilindi**

**MHE. OMARI A. KIGODA - (K.n.y. MHE. OMARI M. KIGUA)** aliuliza:-

Wilaya ya Kilindi ni miongoni mwa Wilaya chache zinazopata mvua nyingi nyakati za mvua lakini maji hayo yamekuwa yakipotea:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuweka utaratibu wa kuvuna maji hayo kwa kujenga mabwawa makubwa ya kuhifadhia maji hayo kwa matumizi ya binadamu?

(b) Je, Serikali imejipangaje kujenga mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na ufugaji wa samaki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Jimbo la Kilindi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wilaya ya Kilindi ni miongoni mwa wilaya zinazopata mvua nyingi hasa mvua za vuli. Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi inaendelea kujenga mabwawa ya kuhifadhi maji ambapo hadi sasa mabwawa matatu (3) katika vijiji vya Saunyi, Jungu na Kwinji/Muungano yamekamilika na hatua inayofuata ni kujenga miundombinu ya maji. Bwawa moja la Mafuleta miundombinu yake imekamilika na linatoa huduma ya maji. Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa mabwawa na miundombinu yake katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuvuna maji ya mvua.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, inaendelea kukamilisha mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa Mwaka 2002 ambapo masuala ya ujenzi wa mabwawa yamepewa kipaumbele. Mapitio haya yatabainisha maeneo mbalimbali yanayofaa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji kwa lengo la kukifanya kilimo cha umwagiliaji kuwa endelevu. Serikali katika mwaka wa fedha 2018/2019, itaendelea kutenga na kutoa fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa maeneo yanayofaa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kilimo cha umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Omari Kigoda.

**MHE. OMARI A. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya maji Handeni na Kilindi ipo kwa muda mrefu sana na sababu kubwa nyingi ni miradi ambayo imefanywa chini ya kiwango. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari baada ya Bunge twende wote tukakague miradi ile na Serikali iweze kuwatolea maamuzi kwa wahusika wote walioshiriki katika kutekeleza miradi hiyo? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Naibu Waziri, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Omari Kigua na kaka yangu Mheshimiwa Kigoda kwa namna ya kipekee wa ufuatiliaji wao wa maendeleo ya majimbo yao kwa wananchi wa Handeni pamoja na Kilindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa Serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi sana kutekeleza miradi ya maji lakini wapo baadhi ya wajanja wajanja kwa maana ya wakandarasi na

wahandisi wanahujumu fedha hizi za Serikali. Huruma hailei mwana. Sisi kama viongozi wa Wizara hatutomuonea haya mtu yeyote. Yapo maneno yanayosema kwamba eti huyu ni mtu wa kigogo tutamuonea haya, hata awe mtoto wa kigogo cha namna gani tutatumia *chainsaw* kulicharanga awe kuni wananchi waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngalawa na Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Wizara ya Maji ya mwaka 2016/2017 uliwekwa mpango wa kujenga bwawa la umwagiliaji la Bonde la Mto Ruhuhu ambalo linahusisha Wilaya ya Nyasa na Wilaya ya Ludewa. Je, mpango ule umefikia wapi kwa sababu kwenye bajeti ya mwaka huu hatujauona?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge lakini kikubwa tunatambua kabisa kilimo cha umwagiliaji ndiyo kitakachotoa Watanzania na kufikia azma ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa sisi kama Wizara tumeona kumekuwa na changamoto kubwa sana katika miradi ya umwagiliaji. Moja, miradi imekuwa mingi lakini haijakamilika na hata iliyokamilika imekuwa ikilima msimu mmoja tu kwa sababu hakuna chanzo cha maji. Kwa hiyo, tunapozungumzia umwagiliaji maana yake ni kilimo mbadala. Wizara kwa kupitia wahisani wetu wameona haja sasa ya kupitia miradi yote ya umwagiliaji ili tuwe na mpango

mahsusi utakaoweza kusaidia miradi michache lakini itakayokuwa na tija katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wananufaika na kilimo cha umwagiliaji. Baada ya mapitio hayo na katika eneo la Jimbo la Ludewa tutaangalia namna ya kuweza kusaidia jimbo hilo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Nassari.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba niiulize Serikali badala ya kutumia fedha nyingi kujenga mabwawa makubwa au yale ya kati kwa nini isiweze kununua mitambo yenye thamani hiyo hiyo ya bwawa ikaipa halmashauri husika ili baada ya kumaliza kuchimba hilo bwawa moja waweze kuendelea kuchimba mabwawa mengine mengi na thamani ya ile kazi itakuwa ni kubwa? Hii itakuwa ni njia moja ya kutumia *force account* vizuri sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali zuri sana la Mheshimiwa Mbunge Soni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo hayo ni mazuri lakini mara nyingi mabwawa Mheshimiwa Mbunge hatuchimbi, tunakinga ili tuweze ku-*retain* maji yaweze kufanya kazi. Mawazo yako naomba tukutane baada ya kikao hiki ili uweze kunieleza vizuri tuweze kuyafanyia kazi. Sisi kazi yetu kama Wizara tunasikiliza mawazo ya Waheshimiwa Wabunge, tunayapeleka kwa wataalam ili wakiyafanyia kazi vizuri basi tuweze kuyaingiza katika mfumo wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tatizo kama hili la maji ya mvua ambayo

yanapotea siyo tu kwamba liko huku Kilindi lakini hata kule kwetu Meru na siyo kupotea peke yake bali pia kusababisha maafa. Miaka ya 80 mwanzoni wakati Waziri Mkuu akiwa Marehemu Sokoine yalitokea maafa makubwa sana yaliyosababishwa na maji kwenye ukanda wa chini wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Iliundwa timu wakati ule ...

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga hoja tu ili waone umuhimu wa suala lenyewe tafadhali.

**MWENYEKITI:** Hujengi hoja hapa, uliza swali *please!*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba mwaka 2009, Ofisi ya Waziri Mkuu ilikuja Meru na walitengeneza *dossier* kubwa sana ambayo ilitoa mapendekezo ya kukinga maji ili yatumike kwa kilimo cha umwagiliaji kwenye Kata za Mbuguni, Shambaraiburuka pamoja na Makiba. Mapendekezo hayo hayakufanyiwa kazi na mwaka huu wananchi wana maafa makubwa. Hivi tunavyoongea sasa hivi wameshindwa kutembea mpaka Wizara ya Afya imepeleka *Mobile Services* kwa ajili ya kusaidia watu wa eneo lile. Namuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ni lini watatumia ile ripoti ili kuweza kukinga maji na kuokoa watu wa Kata za Mbuguni, Shambaraiburuka na Makiba?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Nassari kwa namna anavyowatetea wananchi wake lakini kubwa sisi tumepokea hayo aliyoyaeleza. Mimi kama Naibu Waziri tutakaa na wataalam wetu tuyapitie mapendekezo hayo tujue namna ya kufanya. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali 247, linaulizwa na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli.

Na. 247

**Ukarabati wa Mabwawa Kata ya Esilalei**

**MHE. JULIUS K. LAIZER** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya ukarabati wa mabwawa matatu katika Kata ya Esilalei ambayo aliahidi tangu mwaka 2015?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2016/2017 ilikamilisha usanifu kwa ajili ya ukarabati wa mabwawa ya Joshoni na Olkuro yaliyopo Halmashauri ya Monduli na kubaini kuwa shilingi bilioni 1.45 zinahitajika kwa ajili ya kazi hiyo. Serikali katika mwaka wa fedha 2018/2019 imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya Halmashauri ya Monduli kutekeleza miradi ya maji vijijini ikiwemo ukarabati wa mabwawa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji vya Lendikinya, Kata ya Sepeko ambao unatekelezwa kwa gharama ya shilingi milioni 868. Kazi imefanyika asilimia 75 na inatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba 2018 kwa kuzingatia mkataba. Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imeidhinisha shilingi milioni 639 kwa ajili ya ujenzi wa Mradi wa Maji katika Kijiji cha Nanja ambacho kipo Kata ya Lepurko

ambako utahudumia pia Shule ya Sekondari ya Nanja, Kata ya Sepeko. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Laizer.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, kwanza mradi wa Sepeko Lendikinya mwisho wake kwa mujibu wa mkataba ni Juni 2018. Kwa hiyo, ni muhimu Wizara ikachukua hatua ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize sasa maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, tatizo la maji katika Shule hii ya Nanja Sekondari limekuwa la muda mrefu na kusababisha adha ya wanafunzi kuacha masomo na kwenda kutafuta maji katika malambo upande wa pili wa barabara ambao ni hatari kwa usalama wao. Je, nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba fedha hizi ambazo Wizara imetenga mwaka huu na mpaka sasa haujaanza zinapelekwa ili mradi huu uweze kukamilika kwa haraka na wanafunzi wale waweze kupata maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa mradi huu wa mabwawa ni wa muda mrefu na utagharimu fedha nyingi shilingi bilioni 1.4, ni kwa nini sasa Serikali kupitia *DDCA* isichimbe visima vifupi katika Kata ya Makuyuni Esilalei ambako ni gharama nafuu na kwa haraka zaidi ili wananchi hao waondokane na adha ya maji ambayo imechukua muda mrefu sasa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maji na Umwagiliaji, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua changamoto kubwa ya maji baadhi ya maeneo mbalimbali, Serikali imekuwa ikitenga fedha katika kuhakikisha inatatua tatizo la maji. Nimwombe Mhandisi wa Maji wa Monduli asilale, Serikali imeshatenga fedha, ahakikishe ana-*raise certificate* ili wananchi wake

waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza pamoja na wanafunzi wa shule hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa ni kuhusu suala la uchimbaji visima *DDCA.* Nimuombe tu Mhandisi wa Maji aingie mkataba na watu wa *DDCA* na ile fedha aliyopangiwa ili watu wa *DDCA* waanze kazi ile mara moja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hussein Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri. Pamoja na kazi kubwa mnayofanya, je, mko tayari sasa kwenda katika Halmashauri ya Mji wa Nzega na kulifanyia tathmini bwawa ambalo limekuwa likitumika kwa ajili ya umwagiliaji katika Kijiji cha Idudumo ili kuweza kulirudisha katika hadhi yake na miundombinu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa kifupi Waziri mwenyewe wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Eng. Kamwelwe.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa yote ambayo utendaji wake unasuasua baada ya kukamilisha mpango kabambe, nia yetu ni kuhakikisha wananchi wanalima mara mbili, mara tatu kwa mwaka. Tutakwenda na tutalifanyia kazi vizuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kumueleza Mheshimiwa Waziri kuna bwawa katika Kata ya Urugu, Wilaya ya Iramba ambalo limekuwa na manufaa makubwa sana kwa muda mrefu kwa wananchi wanaoishi kwenye kata ile lakini sasa hivi linaelekea kupotea kwa sababu tope linajaa. Je, ni lini Serikali sasa itakwenda kusaidia wananchi wale ili tope lile liondolewe na shughuli zile ziendelee?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Maji na Umwagiliaji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mama yangu Mheshimiwa Martha Mlata kwa jinsi ambavyo anashughulikia Mkoa wa Singida kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilielekeza Idara yangu ya Umwagiliaji watengeneze teknolojia ya kuhakikisha kwamba inaondoa matope kwenye mabwawa kwa sababu mabwawa mengi yamejaa tope na leo wanakuja kunipa taarifa. Nipongeze sana Mkoa wa Singida, katika mikoa ambayo imeyatunza mabwawa na mifugo inapata maji kwa zaidi ya asilimia 60 ni Mkoa wa Singida. Kwa hiyo, Mheshimiwa Martha Mlata nalifanyia kazi, teknolojia ikishapatikana tunataka tuyaokoe mabwawa yote.

**MWENYEKITI:** Itapendeza sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu Bariadi mabwawa yote yamejaa tope, ahsante. *(Makofi)*

Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na swali la 248, linaulizwa na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua.

Na. 248

**Tatizo la Mawasiliano ya Simu – Wilaya ya Kaliua**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Maeneo mengi ya Wilaya ya Kaliua hayana mawasiliano ya simu ya uhakika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kupeleka mawasiliano ya simu katika Jimbo la Kaliua kwenye Vijiji vya Mpanda Mlohoka, Usimba, Mwamashimba, Usinga, Kakoko, Ibumba, Kombe, Shela, Mkuuyuni n.k.?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli maeneo mengi ya Wilaya ya Kaliua hayana mawasiliano ya simu ya uhakika na Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imekwishaviainisha vijiji vya Mpanda Mlohoka, Kakoko, Usinga, Kombe, Shela na Ushimba kwa kuangalia mahitaji halisi ya kufikisha huduma ya mawasiliano ikiwemo idadi ya wakazi, ukubwa wa eneo pamoja na jiografia ya vijiji husika. Baada ya kuviainisha vijiji hivyo, Mfuko wa Mawasiliano umeingiza mahitaji ya vijiji husika katika orodha ya vijiji vinavyotarajiwa kupatiwa huduma ya mawasiliano katika zabuni itakayotangazwa mwezi Juni, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Vijiji vya Mwamashimba, Ibumba na Mkuyuni vitaingizwa katika miradi kwa kadri ya upatikanaji wa fedha hususani kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia ya leo ya utandawazi mawasiliano ni uchumi, ni kilimo, ni kila kitu. Maeneo yote ambayo nimeyataja Mpanda Mlohoka, Usinga, Kombe, Shela, Mwamashimba, Ibumba, Mkuyuni na vingine vingi ni maeneo ambayo wanalima sana zao la tumbaku ambalo linaingiza kipato kikubwa. Serikali imekuwa na *speed* ndogo sana ya kupeleka mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jibu lake hapa la msingi anasema kwamba kuna baadhi ya maeneo...

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza swali, kwenye jibu la swali la msingi Mheshimiwa Waziri anasema maeneo mengine itategemea upatikanaji wa fedha, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali, kwa kuwa kuna makampuni ambayo pia yanapeleka mawasiliano maeneo ya Vijijini, wakati wanasubiri kupata fedha Serikali kwenye mpango wa Serikali wanaweza kuongea na haya makampuni ili baadhi yaanze kupeleka mawasiliano maeneo hayo kuliko kusubiri mpaka Serikali ipate fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kumekuwepo na migongano mikubwa kwenye masuala ya ulipaji wa minara ya simu kwenye maeneo mbalimbali ya vijijini, Serikali za Vijiji zikiona kwamba minara ile ni vipato kwa ajili ya Serikali lakini pia wananchi ambao wametoa yale maeneo wakiona ni haki yao wao kulipwa. Serikali inasemaje juu ya minara ambayo imewekwa vijijini ambapo imeleta migongano hawajui kwamba hela ziende wapi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditiye, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ni taasisi ya Serikali ambayo inahusika kupeleka mawasiliano katika vijiji vyote au sehemu zote ambazo hazina mvuto wa kibiashara. Haya makampuni ya simu yanafanya biashara, ili yaweze kuweka mnara sehemu mojawapo ni lazima pawe na mvuto wa kibiashara. Kuepuka hilo, ndiyo

maana Serikali ilianzisha Mfuko wa Mawasialiano kwa Wote kuhakikisha kwamba hata zile sehemu ambazo hazina mvuto wa kibiashara zinapata mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vijiji vya Mheshimiwa Sakaya, nashukuru sana kwamba kuna barua yake ambayo imeanisha vyote hivyo na nimeshaipokea pamoja na barua za Wabunge wengine wengi tu. Namuahidi baada ya kipindi cha Bunge hili la bajeti nitafanya ziara ya mwezi mzima na wataalam wangu kutoka *TCRA* na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kuhakikisha tunaanisha maeneo yote nchi nzima ambayo hayana mvuto wa kibiashara tutangaze tenda ili makampuni ya simu yaweze kuweka minara wananchi waweze kuwasiliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu malipo, kwanza kabisa kuna masuala kama mawili. Suala la kwanza ni malipo kwa mtu ambaye anatoa eneo lake mnara uwekwe, mara nyingi huwa ni mapatano kati ya mwenye ardhi na makampuni ambayo yanaweka mnara. Wakati mwingine tunashauri sana vijiji ndio viwe vinatoa maeneo kwa ajili ya kuweka mnara ili kuhakikisha kwamba pesa inarudi kwa wananchi lakini inapotokea kwamba ni mtu binafsi amepata hiyo fursa hatuwezi kumuingilia sana japo tunatamani sana halmashauri iweze kuwa inaingilia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Angalieni muda Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Waitara.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni kama alivyosema Naibu Waziri yanafanya biashara lakini kuna maeneo ambayo yana mahitaji makubwa na biashara ipo lakini hayajawahi kupata huduma za mawasiliano kwa muda mrefu. Naomba kujua ni lini Vijiji vya Nyangere, Nyaburundu, Nyabuzume, Tiling'ati, Tingilima na Kibara Ginnery zipata mawasiliano? Kwa mfano Kibara Ginnery ina kiwanda muda mrefu lakini hakuna mawasiliano, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Eng. Nditiye, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Getere na nimpongeze kwa jinsi ambavyo anafuatilia sana suala la mawasiliano hasa kwenye hii Kibara *Ginnery*. Vilevile nimshukuru kwamba ni mmoja kati ya Wabunge ambao wameleta maombi yao ofisini kwangu kwa ajili ya kwenda kuwekewa minara kwenye maeneo yote ambayo hayana mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niamuahidi kama nilivyozungumza wakati najibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sakaya kwamba baada ya Bunge hili nitafanya ziara karibu nchi nzima, *specifically* kwa wale Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameleta barua ofisini kuomba mawasiliano. Nitafanya ziara, tutaanisha maeneo, tutatangaza tenda kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, tutafungua tenda kabla ya mwezi Oktoba, minara itaanza kujengwa maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Jimbo la Ukonga lina kata 13 na kwa sasa mawasiliano yamekata kabisa hasa mawasiliano ya barabara nini kauli ya Serikali katika eneo hili?

**MWENYEKITI:** Unasemaje?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Jimbo la Ukonga lina Kata 13 ninavyozungumza mawasiliano ya barabara yamekatika kabisa ni jambo la dharura, nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Barabara na simu haviendani, tunaendelea na swali lingine. Mheshimiwa Masala. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo Kaliua linafanana na maeneo yangu ya Wilaya ya Nachingwea katika Kata za Kilimarondo, Mbondo, Mateko pamoja na Kiegei. Naomba kupata majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri nini mkakati wao juu ya kutatua tatizo hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Masala, *DC* wangu mstaafu wa Wilaya ya Kibondo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mheshimiwa Masala ni mmoja kati ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameleta barua zao za maombi ya minara kwa ajili ya mawasiliano kwenye eneo la Nachingwea. Vijiji vyote alivyovitaja, namuahidi kwamba nitakwenda kule na nitakapokuwa nakwenda kule nitamtafuta ili tuwe naye hata kama kuna maeneo mengine ambayo yana changamoto ya mawasiliano tuweze kuyaona na tuyafanyie kazi ili tuhakikishe kwamba inapofika mwishoni mwa mwaka huu Tanzania inawasiliana kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la 249, linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Joram Ismail Hongoli, Mbunge wa Lupembe.

Na. 249

## Umuhimu wa Somo la Ulipaji Kodi

**MHE. JORAM I. HONGOLI** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali isiingize kwenye mitaala ya elimu somo la umuhimu wa kulipa kodi ili lifundishwe kuanzia shule ya msingi ili wananchi wapate uelewa wa kodi na waweze kufurahia kulipa kodi kama ilivyo kwa nchi zilizoendelea?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa elimu ya mlipa kodi katika kumjengea mwananchi tabia, mwenendo na mazoea ya kulipa kodi kwa maendeleo ya Taifa letu. Wizara yangu kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania ndiyo yenye jukumu la kubuni, kuandaa na kuboresha mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeona umuhimu wa kuingiza elimu ya mlipa kodi kwenye mitaala ya elimu nchini ili kuwajengea Watanzania tabia, mwenendo na mazoea ya kuwa na utamaduni wa kulipa kodi. Katika somo la uraia na maadili kuanzia darasa la III na kuendelea, mtaala umelenga kumjengea na kumuandaa mwanafunzi kuwa mwajibikaji katika kutekeleza majukumu ya kila siku, kuiheshimu na kuithamini jamii yake na kuwa mwadilifu na mzalendo ikiwa ni pamoja na kutekeleza majukumu ya kitaifa ikiwemo kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kutokana na umuhimu wa kuwajengea vijana tabia kuhusu elimu ya mlipa kodi, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kushirikisha Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* itaendelea kuboresha elimu hii ili isisitizwe na kuwekewa mkazo katika mitaala ya elimu kuanzia elimu ya msingi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri kwa kujibu maswali vizuri lakini pia nina swali moja la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wengi hawana uelewa wa kulipa kodi, wanapoenda dukani kununua bidhaa wanalipa gharama ya zile bidhaa lakini pia wanalipa na *Value Added Tax (VAT)* asilimia 18 na wauzaji wakati mwingine hawawapi risiti na mwisho wa siku kodi hii ambayo wananchi wanalipa inapotoea. Je, ni lini sasa Wizara ya Elimu itaiagiza Taasisi ya Elimu *(TET)* kwa kushirikiana na *TRA* ili waanze kufanya kazi ya kuboresha mitaala hii ili Serikali isipoteze kodi kupitia wananchi kutokuwa na uelewa lakini pia na wauzaji wa hizi bidhaa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hongoli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa mlipa kodi, *TRA* kwa sasa wanaendesha zoezi hilo nchi nzima. Kwenye shule zetu nyingi wameanzisha *club* za kodi ambazo pamoja na mambo mengine wanafunzi wanaelezwa kuhusu umuhimu wa kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu ili kufanya sasa kodi iwe ni kitu ambacho kinafahamika zaidi, Wizara yangu iko tayari kushirikiana na *TRA* kuboresha mitaala iliyopo ili

kuendelea kuwajengea vijana wetu ufahamu na umuhimu wa kuwa wazalendo ikiwa ni pamoja na kulipa kodi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea swali letu la mwisho kwa leo ni 250 linaulizwa na Mheshimiwa Esther Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, linaelekezwa kwa Wizara hiyo hiyo.

Na. 250

**Sera ya Elimu Bure**

**MHE. ESTHER A. MAHAWE** aliuliza:-

Sera ya Elimu ya mwaka 2014 inaelekeza utoaji wa elimu bila malipo kuanzia ngazi ya chekechea hadi kidato cha nne ikiwemo kuondoa gharama za kulipia mitihani ya kitaifa katika shule za msingi na sekondari lakini wanafunzi wanaosoma katika shule zisizo za Serikali wanalipishwa gharama hizo wakati wazazi wao wanalipa kodi inayowezesha kutolewa elimu hiyo bila malipo:-

Je, ni lini Serikali itafuta ada hiyo ya mitihani kwa wanafunzi wanaosoma katika shule binafsi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali, naomba nitambue kwamba Mheshimiwa Esther Alexander Mahawe ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wamiliki wa Shule Binafsi Nchini. Lazima tu niseme kwamba katika kipindi cha uongozi wake Serikali imenufaika na ushirikiano mkubwa ambao umefanya Serikali iweze kuwahudumia sekta binafsi katika elimu, tunamshukuru sana Mheshimiwa Esther Mahawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na

Teknolojia, nijibu swali la Mheshimiwa Esther Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa sekta binafsi katika utoaji wa elimu nchini. Aidha, ili kuhakikisha mazingira rafiki katika utoaji wa elimu, Serikali imekuwa ikifanya majadiliano na sekta binafsi kwa lengo la kuondoa changamoto zinazowakabili. Hadi sasa Serikali imeweza kuondoa baadhi ya kodi na tozo mbalimbali ambazo awali walikuwa wakitozwa mawiliki wa shule binafsi. Mfano wa kodi hizo ni Kodi ya Mabango, Kodi ya Kuendeleza Ufundi Stadi *(Skills Development Levy),* tozo ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi *(OSHA)* pamoja na tozo ya zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Mpango wa Elimu bila Malipo, Serikali ilifuta ada na michango ya lazima katika shule za umma ngazi ya elimumsingi yaani elimu ya awali hadi kidato cha nne. Ada na michango hiyo iliyokuwa ikilipwa na wazazi au walezi kwa sasa hugharamiwa na Serikali. Mpango huu haukuzihusu shule binafsi pamoja na shule za umma ngazi za kidato cha tano na sita. Hivyo, shule hizo zitaendelea na utaratibu wa wazazi kuchangia gharama za uendeshaji wa elimu ikiwemo kulipa ada za mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya utoaji elimu nchini kadiri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mahawe.

**MHE. ESTHER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa bajeti ya Wizara ya Elimu inapopangwa inahusisha wanafunzi wote wanaotakiwa kuanza elimu yao ya msingi na sekondari na kwa kuwa wazazi wa hawa wanafunzi wanakuwa tayari wamechangia bajeti kuu ili kuweza kusomesha wanafunzi

hawa kwa kupitia elimu bure. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuendelea kuondoa kodi na tozo ambazo sio lazima kwa wazazi hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa moja ya malengo ya fedha za mitihani ni pamoja na kutafsiri mitihani kazi ambayo kimsingi ni jukumu la Baraza la Mitihani na siyo kwamba wazazi hawa wanaosomesha watoto katika shule ambazo sio za Serikali ni matajiri. Je, Serikali haioni kwamba kwa kuondoa tozo hizo watapata nafasi ya wanafunzi wengine wengi kusajiliwa katika shule hizo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Naibu Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Olenasha kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Mahawe, kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi kuboresha mazingira ya wao kuwekeza katika elimu. Tutaendelea kuboresha mazingira yaliyopo ili waweze kuwekeza kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niseme kwamba sekta binafasi wamekuwa walipaji wazuri wa kodi na wanatambua umuhimu wa kodi katika maendeleo ya Taifa. Kwa hiyo, pamoja na kwamba tupo tayari kujadiliana nao kuhusiana na namna ya kuweza kupunguza hizo kodi lakini bado tutaendelea kusisitiza kwamba ni vizuri wote tukashirikiana ili kuhakikisha kwamba baadhi ya gharama ambazo ni muhimu ziweze kulipwa na wale ambao wanaweza kuchangia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu ya 2014 ya Elimu Bila Malipo inaonekana kuwa ni sera ya ubaguzi ambayo inawabagua watoto wanaosoma kwenye shule binafsi. Mbali tu ya kuwalipisha ada za mitihani lakini sasa Serikali imekwenda mbali kwamba wanaosoma shule binafsi hawawezi hata kupata mikopo ya elimu ya juu. Hivi ni kigezo gani Serikali imekitumia cha kujiaminisha kwamba watoto wanaosoma shule binafsi ni watoto wa matajiri? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwaa Mtolea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba Sera ya Elimu Bure ni ya kibaguzi, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sio ya kibaguzi bali elimu bure tunazungumzia katika sekta ya umma. Kwa hiyo, lazima tutofautishe sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusiana na watoto ambao wamesoma shule binafsi kutoruhusiwa kupata mikopo ni suala tu la kuangalia kwamba kati ya mtu ambaye anaweza kulipa milioni mitatu au milioni nne kwenda shule ya msingi na sekondari na yule ambaye hawezi, ni yupi utamuangalia wakati wa kutoa mkopo? Ni suala la kuangalia nani mwenye mahitaji zaidi siyo suala la kibaguzi. Bajeti iliyopo ni kidogo na wahitaji ni wengi lazima tuchague na tunatoa zaidi kwa wale ambao wanahitaji zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa wanafunzi wale ambao wamepata bahati ya kusomeshwa labda na wafadhili, Serikali haiwanyimi mikopo, tunachotaka

ni ushahidi kwamba kweli wamefadhiliwa. Tutahitaji barua kutoka kwa mfadhili kuonyesha kwamba mwanafunzi amefadhiliwa. Kwa hiyo, sio ubaguzi ni suala tu la ni namna gani tunafanya kazi ili huduma hiyo ya elimu iweze kutolewa kwa wote kwa usawa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha lakini pia tumekula muda wetu kidogo.

Matangazo, nitaanza na wageni wa Mheshimiwa Spika ambao wapo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika ni Mr Clive Mather *(Chairperson of the Tear Fund)* akiambatana na mkewe Ann Mather pamoja na Ndugu Justine Nyamoga *Country Representative* wa Tanzania. Karibuni sana kwetu. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Spika ambaye ni Balozi wa Uswisi, Mheshimiwa Florence Mattli, ameambatana na Ndugu Sandrine Julia Denti, Afisa wa Ubalozi huo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tangazo lingine ni kwamba Mheshimiwa Spika anapenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge, tena msikilize vizuri sana hili, naombeni sana mnisikilize vizuri, huyu ni Spika anaongea. Napenda kuwaarifu kuwa katika Mkutano wa Bunge la Afrika *(PAP)* unaoendelea hivi sasa huko Midrand, Afrika ya Kusini, Mheshimiwa Mboni Mohamed Mhita, Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amechaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Vijana wa Bunge la Afrika *(President of the Youth Caucus of Pan African Parliament). (Makofi)*

Mheshimiwa Mboni Mhita, ameshinda nafasi hiyo katika uchaguzi uliofanyika jana tarehe 14 Mei, 2018 kwa kumshinda Mbunge mwenzake kutoka nchi ya Chad ambaye alikuwa anatetea nafasi yake. Mheshimiwa Mboni atatumikia nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia sasa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mboni Mhita kwa kuliletea sifa Bunge letu na Taifa kwa ujumla. Aidha, tunamtakia utekelezaji mwema wa majukumu yake katika nafasi hiyo aliyoipata. Tangu wiki iliyopita na wiki hii unaona Tanzania inavyozidi kunga'ara katika ngazi za Kimataifa. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni kwenye Jukwaa la Spika, tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Mbunge na Waziri wa Kilimo ambao ni Eng. Mathew Mtigumwe, Katibu Mkuu na Dkt. Thomas Kashilillah, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. Karibuni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Hatumwoni.

**MBUNGE FULANI:** Kashilillah yuko wapi?

**MBUNGE FULANI:** Asimame.

**MBUNGE FULANI:** Kashilillah asimame tumwone.

**MWENYEKITI:** Ahsanteni Waheshimiwa Wabunge. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Tumeku-*miss.*

**MWENYEKITI:** Imetosha Waheshimiwa Wabunge.

**MBUNGE FULANI:** Tumeku-*miss.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, inaeleweka.

**MBUNGE FULANI:** Mbona Kashilillah hayupo ?

**MWENYEKITI:** Makofi hayo Dkt. Kashilillah, hiyo ndiyo heshima Waheshimiwa Wabunge wamekupatia kwa kazi uliyofanya. *(Makofi/Vigelegele)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea. Tunao pia Wenyeviti wa Bodi mbalimbali

ambazo ziko chini ya Wizara hii, tukianza na Ndugu Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho. Mnakumbuka Mheshimiwa Anna Abdallah amekuwa kiongozi wa nchi hii kwa kipindi kirefu sana, amekuwa Mbunge na Waziri. Karibu sana mama yetu. *(Makofi)*

Wengine ni Dkt. Mshindo Msollah, Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mbolea; Dkt. Amiri Hamza, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Kahawa; Dkt. Joel Kabisa, Mwenyekiti wa Bodi ya Pamba; Ndg. Monica Mbega, Mwenyekiti wa Bodi ya Nafaka. Mheshimiwa Monica Mbega mnakumbuka amekuwa Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini. *(Makofi)*

Wengine ni *Eng.* Yustaki Kangole, Mwenyekiti wa Wakala wa Chakula. Pia wapo Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi na Wakuu wa Vitengo wa Wizara hiyo. *(Makofi)*

Wengine ni wageni kutoka Wabia wa Maendeleo tulionao hapa leo; Prof. Nuhu Khatibu, Mratibu Mkazi wa *AGRA* Tanzania; Ndg. Charles Tulahi, Mwakilishi Msaidizi wa *FAO* Tanzania; Prof. Marcelino Chojoringa, Mwakilishi wa *Bill and Melinda Gates Foundation.* Profesa, karibu sana. *(Makofi)*

Wengine ni Prof. Raphael Chibunda, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kilimo *(SUA);* Bw. Audax Lukonge, Mkurugenzi Mtendaji wa *ANSAF;* Ndg. Gesso Bujuta, Mkurugenzi Mtendaji wa *Bujuta International Company Ltd* na Bi. Jacqueline Mbuya, Mchumi Mkuu ambaye anaratibu shughuli zetu za wabia wa maendeleo. *(Makofi)*

Pia tunayo familia ya Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Tizeba, ambao ni Ndg. Kallist Phillip Tizeba, ambaye ni kaka yake na Mheshimiwa Waziri na Ndg. Hilda Tizeba, mtoto wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Pia tunao wageni watatu ambao ni wafanyakazi kutoka Bunge la Zambia, wamekuja kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na Bunge letu ambao ni Ndg. Ngowani Makasa, *Deputy Principal Clerk,* masuala ya huduma *from the Zambian Parliament;* Ndg. Millius Habukali, *Workshop*

*Foreman* na Ndg. Nicholas Kaite, *Transport Officer.* Karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tuna wageni 32 wa Mheshimiwa Eng. Atashasta Nditiye, Mbunge na Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, ambao ni viongozi watano wa CCM Wilaya ya Kibondo walioambatana na wanafunzi 20 na Walimu watano wa Shule ya Sekondari ya *Oliver Green* ya Wilayani Kibondo, Mkoani Kigoma. Karibuni sana ndugu zetu. *(Makofi)*

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Mary Chatanda, Mbunge, ambao ni Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wa Kata ya Manundu kutoka Muheza Korogwe, Mkoani Tanga.

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Mbunge, ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalum (CCM) na viongozi wa CCM kutoka Sumbawanga, Mkoani Rukwa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni tisa wa Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge, ambao ni Viongozi wa Umoja wa Madiwani wa CHADEMA kutoka Rukwa. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Alex Gashaza, Mbunge, ambao ni wachungaji kutoka Ngara Mkoani Kagera. Wachungaji wetu kutoka Ngara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 28 wa Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge, ambao ni Wachungaji, Wainjilisti na *New Jerusalem Worship Team* kutoka Kanisa la *Baptist Tanzania* wakiongozwa na Askofu Arnold Manase. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni 37 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge, ambao ni Wanamaombi na Wachungaji kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 25 wa Mheshimiwa Khadija Nassir, Mbunge, ambao ni Wajumbe wa Baraza la Vijana Mkoa wa Kusini Unguja, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Vijana Mkoa wa Kusini Unguja Ndg. Latifa Khamis. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 44 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge, ambao ni viongozi wa UWT katika Kata ya hapa Dodoma Mjini. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 27 wa Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mbunge, kutoka Mashirika ya *ACTION AID, FORUM MCC, ANSAF, TACOSODE* na *OXFAM* walioambatana na wakulima kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 36 wa Mheshimiwa Hussein Bashe, Mbunge, ambao ni Mapadri, Masista, Walimu na Wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari ya *Queen of Peace,* Mkoani Tabora. Karibuni sana. Tunafurahi kuwa nanyi hapa. *(Makofi)*

Tuna wageni kumi wa Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge, ambao ni Makatibu wa CCM kutoka Wilaya ya Kilolo Mkoani Iringa. *(Makofi)*

Tunao wageni 53 wa Mheshimiwa Destery Kiswaga, Mbunge, ambao ni wanafunzi na walimu kutoka *Ilungu Compassion* ya Jijini Mwanza. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kundi la tatu ni wageni waliotembelea Bungeni kwa ajili ya mafunzo. Ni wanafunzi na Walimu watano kutoka Shule ya *Dar es Salaam International* ya Jijini Dar es Salaam. Kwenye kundi hili napenda nitambue uwepo wa mtoto wa Mheshimiwa Bulembo miongoni mwa wanafunzi hao ambaye ni Zainab Abdallah Bulembo. Karibuni sana. Jifunzeni hayo mtakayopewa mkiwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Katika wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, tunaye pia Mwenyekiti, Mzee wetu Akasubi. Karibu sana. Mzee maarufu sana huyu. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa niwatangazie tena Waheshimiwa Wabunge wote walionunua fomu za kutaka kumilikishwa viwanja na Halmashauri ya Jiji la Dodoma katika maeneo ya Mtumba, wafike eneo walikochukulia fomu hizo ili waweze kupatiwa vocha kwa ajili ya kulipia umilikishwaji wa viwanja hivyo. Watumishi kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma wapo hapo kuwahudumia Waheshimiwa Wabunge.

Tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge wote Wakristo; mnatangaziwa kwamba leo tarehe 15 Mei, 2018, saa 7.00 mchana kutakuwa na ibada katika *Chapel* yetu pale Ukumbi wa Msekwa, Ghorofa ya pili. Aidha, katika ibada hiyo, tutakuwa na Mtumishi wa Mungu, Askofu Arnold Manase akihudumu pamoja na *New Jerusalem Worship Team* kutoka Kanisa la *Baptist* Tanzania kutoka Arusha. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa.

Mtaniwia radhi, matangazo yalikuwa mengi na marefu, nimejitahidi.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Ngoja niwachukue basi, siyo lazima niwachukue wote kwa sababu ya muda. Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Kikwembe ulikuwa umesimama kwa ajili ya mwongozo?

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Hapana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ngoja Mheshimiwa. Mwingine ni Mheshimiwa Waitara. Haya, Mheshimiwa Musukuma endelea.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) lakini naisoma na Kanuni ya 46(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge kuandaa maswali tunatumia muda mwingi sana kufanya mikutano na ziara kujua kero za wananchi wetu. Baadaye tunapokuwa tunapewa majibu yetu, tunawaandaa na wananchi wetu kisaikolojia kwamba leo majibu yenu yatasomwa mbele ya Bunge. Isipokuwa majibu ya Waheshimiwa Mawaziri yanakuwa na mizaha ambayo inasababisha wananchi wetu wasituelewe sisi wauliza maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni jana, liliulizwa swali kwa Wizara ya TAMISEMI, linasema, je, ni lini jina la Halmashauri litabadilishwa kuwa Halmashauri ya Uyui? Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI alipoenda pale, akazungumza mambo ya Simba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, aliulizwa Ofisi ya Mazingira akaenda kujibu Mheshimiwa Kangi Lugola, akazungumza mambo ya Simba. Swali la tatu likaulizwa kwa Wizara ya Afya, akaenda Mheshimiwa Dkt. Ndugulile akazungumza mambo ya Simba. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa humu ndani kuna *Hansard* na wewe mwenyewe jana ulikuwa hapo ulikuwa unasikiliza, wakizungumza mambo ya Simba watu wanapiga makele humu ndani. Kwa hiyo, *Hansard* za jana pamoja na wananchi waliotutuma kuuliza hayo maswali wameona tu mambo ya Simba, hata *Hansard* zenyewe zimechanganyikiwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako; kwa kuwa Mawaziri hawa ni Mawaziri wa Nchi, tunapouliza maswali, kwa nini wanaingiza masuala ya mizaha ya Simba wakati timu yenyewe imeshinda kombe siku moja tu?

Naomba mwongozo wako, Mawaziri wajikite kwenye maswali, masuala ya ushabiki waende nje pale. Kwa sababu kuna Timu ya Yanga, inashinda mara nyingi na hawajawahi kufanya haya mambo humu ndani. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Yanga ilishaletwa mara tatu humu Bungeni.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Wakati umenipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwenye swali mama Na. 248, nilieleza kwamba kwa hali ilivyo katika Jimbo la Ukonga au Dar es Salaam kwa ujumla, mvua zinanyesha siku mbili, tatu mfululizo. Mimi Jimbo langu la Ukonga lina Kata 13 na barabara zote zimekatika, hakuna mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na barabara ya kutoka Mvuti kwenda Mbagala, kama unatoka Kisarawe unaweza ukapita njia hiyo ukaenda Kusini mwa Dar es Salaam, sasa hivi haipitiki, imekatika, hakuna mawasiliano. Maana yake wanafunzi, Walimu, Madaktari na watumishi wengine pale hakuna mawasiliano. Njia pekee ya Ukonga ambayo unaweza kupita ni kutoka *TAZARA* inaishia Pugu. Barabara ya kutoka Banana – Msongora – Kivule, imekatika, wananchi hawawezi kutoka Kitunda kwenda Temeke kupitia Mzinga, barabara imekatika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kwa sababu jambo hili kimsingi ni jambo la dharura. Kama una watu zaidi ya 700,000, nusu yao hawana mawasiliano; watu hawawezi kwenda kazini, wagonjwa hawawezi kutibiwa na hospitali ambayo tunatumia kule Ukonga ni lazima uende Amana, Temeke au Mwananyamala. Kwa hiyo, kama kuna mgonjwa kule Mvuti au Dondwe, ina maana huyu mtu atafia nyumbani. Kwa hiyo,

naomba mwongozo wako kwa sababu Serikali ipo na hili ni jambo la dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeona kwenye *TV* kule Kivule imefikia mahali wananchi wa kawaida wametengeneza mitumbwi ya madumu ndiyo wanavusha watu. Jana kuna mtu amekufa katika eneo lile, kwa sababu ni mitumbwi ile ya maplastiki, wamebeba watu Sh.1,000, maji yanakuja mengi na magogo na vitu vyenye ncha kali, vimepiga ule mtumbwi, imezama na mtu amekufa. Mama wa watu amepoteza maisha pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kwa sababu jambo hili kwangu mimi kama Mbunge na wananchi wa Ukonga na Dar es Salaam kwa ujumla, ni jambo la dharura, ni jambo la fedheha, kazi zimesimama, uchumi hauendi, maisha yamekuwa magumu kweli kweli. Naomba busara yako ya Kiti, nisaidie katika jambo hili na viongozi wanasikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa hiyo miongozo miwili. Nitaanza na huu wa Mheshimiwa Waitara, Mbunge wetu wa Ukonga, siyo suala ambalo limetokea humu Bungeni. Katika swali lililoulizwa leo hapa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya lilihusu mawasiliano ya simu na ndiyo maana ulipochomekea barabara nikakuuliza Mheshimiwa unasema nini? Niliuliza hivyo ili nikusaidie kukurudisha kwenye reli, nikakuona bado hujanielewa.

Mwongozo wangu, unalalamikia kwa jibu ambalo limetolewa na Serikali, halikuwa swali lako, kama unataka majibu ya Serikali *(specific answer),* bado una muda wa kuuliza swali la msingi kwa Serikali. Hata hivyo, kwa hali hiyo uliyoielezea ya Jimbo lako la Ukonga na naamini na maeneo mengi ya Dar es Salaam kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, Serikali imekusikia na naamini Serikali kupitia vyombo vyake *TANROADS* na *TARURA* wataona uwezekano wa kuweza kurejesha mawasiliano ili maeneo ya Jimbo lako na mengine katika Dar es Salaam pamoja na maeneo

mengine nchini ambapo mvua zinaendelea kunyesha yaweze kupitika. Mwongozo wangu wa msingi ni kwamba ilikuwa ni mawasiliano ya simu ndiyo maana nilikuambia tusiende huko, uliza mawasiliano ya simu na siyo ya barabara.

Mheshimiwa Musukuma, nadhani sijakusoma vizuri, lakini kwa mbali nakuona wewe ni kama mtu wa Yanga. Tukio hilo ni la jana, halikutokea mapema leo. *(Kicheko/ Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nyumba hii ni ya Watanzania wote, Bunge tu limeweka utaratibu wa jinsi utavyoingia humu. Unaweza ukawa mgeni wa Spika, Mbunge au Waziri Mkuu, ndivyo taratibu zilivyo. Unaweza ukaja hapa kwa mafunzo.

Kwa hiyo, jana kwa sababu ya tukio hilo ilionekana timu hiyo ya Simba ifike hapa na ilifika kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, nakumbuka sana, Yanga wamewahi kuja hapa mara nyingi sana. Nadhani jana mlikuwa mnasawazisha tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mwongozo wangu, kwa sababu ya vyombo hivi, maana Mheshimiwa Waziri au Naibu anapojibu swali na ndiyo maana Kanuni ya 154 imewekwa kwa sababu hiyo, kutusaidia. Kama pongezi zikitolewa na Spika au na kiongozi mwingine ambaye yuko hapa, inatuambia usiyarudierudie tena hayo, maana pongezi zimeshatolewa. Wewe unapoenda kujibu swali pale, jizuie ile furaha ya Yanga au Simba, mimi hamjui ni timu gani. *(Makofi)*

Mwongozo wangu kwa hili ni kwamba tusilete sana ushabiki hapo lakini tunaposhangilia timu zinapokuja humu au wageni wengine tunafanya hiyo kwa staha, tufanye kwa staha. Huo ndiyo mwongozo wangu. Hata hivyo, mliwapongeza vizuri sana vijana hao jana kwa kazi nzuri. Naelewa Mheshimiwa Mwigulu na wengine hawakuwa na furaha sana lakini ndiyo hali halisi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Kilimo**

**MWENYEKITI:** Sasa namwita mtoa hoja, Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Tizeba. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba nitakayoitoa, naomba kuweka Mezani marekebisho ya hotuba ya bajeti ukurasa wa 76 hadi 78 kuhusu maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Mfuko wa Taifa wa Bembejeo za Kilimo na kiambatisho Na. 2 katika ukurasa wa 145 wa kitabu cha bajeti inayoelezea mikopo iliyotolewa na Mfuko wa Taifa wa Pembejeo hadi tarehe 30 Mei, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa Fedha wa 2018/2019. Hoja hii inawasilishwa kwa kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni mapema leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni waja wa Mwenyezi Mungu, hivyo, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema alizoturehemu kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa wazima wa afya njema na majaliwa ya amani kwa nchi yetu kwamba tunaweza kujadili bajeti hii inayolenga kusukuma mbele kasi ya maendeleo ya Watanzania, hususan wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo heshima ya kipekee kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uchungu alionao

kwa Watanzania na msukumo dhahiri anaoutoa katika kuendeleza Sekta ya Kilimo. Anafanya hivi kwa kuamini kwake kuwa sekta hii ina umuhimu wa kipekee katika mustakabali wa maisha ya Watanzania wengi kiuchumi na ushiriki wao katika ujenzi wa uchumi tarajiwa wa viwanda. Nakiri ameweka imani kubwa kwa kuweka dhamana hii kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faraja yangu ni namna anavyonipa shime na miongozo bayana kuhusu mabadiliko na maendeleo anayoyakusudia katika sekta hii. Uthibitisho wangu ni namna alivyotumia muda na umahiri wake mkubwa katika kuongoza Mkutano wa Baraza la Taifa la Biashara *(Tanzania National Business Council-TNBC)* uliofanyika jijini Dar es Salaam mnamo tarehe 19 Machi, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la mkutano huo ilikuwa kubaini namna tutakavyoweza kuboresha mazingira ya uwekezaji na uendeshaji wa biashara nchini. Kupitia mkutano huu aliweka bayana haja ya kuondoa utitiri wa kodi, tozo na ada kwa sekta za kilimo na shughuli nyingine zitokanazo kwa lengo la kumwezesha mkulima kupata manufaa stahiki kulingana na jasho lake na pia kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao kama vile mahindi, mpunga, sukari, korosho, chai, kahawa, pamba, tumbaku na mbegu za mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumwahidi Mheshimiwa Rais, Bunge lako Tukufu, wakulima na Watanzania wote kwamba sitawaangusha. Kwa kadri itakavyowezekana, nitatumia uwezo wangu wote, tena kwa unyenyekevu mkubwa, uaminifu na uadilifu mkubwa kuhakikisha kwamba rasilimali zinazotengwa kwa ajili ya maendeleo ya Sekta ya Kilimo zitatumika kwa ufanisi na kuwafikia walengwa hasa wakulima ili waongeze uzalishaji, tija na ubora wa mazao na kujipatia manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa ustawi wa kilimo ni upatikanaji wa soko la uhakika. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kulivalia njuga suala la kuwavutia

wawekezaji katika viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana kwa wingi nchini, hasa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya juhudi hizi yameanza kuonekana. Hivi karibuni tumeshuhudia akizindua viwanda katika mikoa mbalimbali nchini kama vile Kagera, Mwanza, Shinyanga, Singida, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam; na vingi kati ya viwanda hivyo vinatumia malighafi za kilimo, kudhihirisha kuwa tumeanza kupata muunganiko wa shughuli za viwanda na kilimo nchini, jambo ambalo lilishindikana kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, napenda kutambua na kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuhimiza utunzaji wa mazingira kwa ustawi endelevu wa uchumi na maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara zake mbalimbali nchini, moja ya ajenda yake kuu ni kutuasa juu ya kuendesha shughuli zetu huku tukizingatia hifadhi ya mazingira na kujenga uwezo wa kuhimili mabadiliko ya mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi. Maelekezo hayo yamezingatiwa katika utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu pia kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa muda wake mwingi anaotumia kuhamasisha na kutoa maelekezo muhimu yenye lengo la kuongeza uzalishaji na tija katika Sekta ya Kilimo, hususan mazao ya mkakati kama vile chai, kahawa, korosho, pamba na tumbaku. Sanjari na hili, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha muunganiko wenye tija wa shughuli za kilimo na masoko hasa ya ndani. Katika hili ameweka azma ya kweli ya kufufua na kuimarisha maendeleo ya Vyama vya Ushirika nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwa lengo la kuchochea mageuzi ya kilimo nchini, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliongoza Kikao Kazi cha Baraza la Mawaziri kilichojadili na kuridhia Utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(ASDP II),* programu ambayo inatarajiwa kuzinduliwa rasmi hivi karibuni Jijini Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake na pia Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa taarifa zake mbalimbali zilizotoa ufafanuzi kuhusu hali halisi ya uchumi kwa mwaka 2017, mwenendo na mwelekeo wa Sekta ya Kilimo kwa mwaka ujao, misingi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2018/2019, ambazo zimeweka msingi wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mnyimi wa fadhila ikiwa nitajisahau na hivyo kushindwa kutambua na kukupongeza wewe mwenyewe hapo kwenye kiti Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wengine wa Bunge kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge kwa umahiri mkubwa. Bunge letu hivi sasa limerejesha hadhi na heshima yake kwa wananchi na wanayo matarajio makubwa na mhimili huu. Aidha, natumia nafasi hii pia kuwapongeza Wabunge wote kwa umahiri wao mkubwa katika mijadala inayoendelea katika Bunge hili la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee pia napenda kutambua ushirikiano, maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Morogoro, Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nistakabadhi shukrani zetu za dhati kwa miongozo waliyotupatia wakati wote wa maandalizi ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/2019. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba

tutaendelea kuipatia Kamati ushirikiano, kwani kwa njia hii tutaweza kutekeleza lengo letu la kubadilisha kilimo nchini kufikia matarajio ya jamii na uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, niruhusu nitoe shukrani kwa wananchi wa Jimbo langu, familia yangu kwa ushirikiano na uvumilivu wanaoendelea kunipatia pale ninapokuwa mbali nao nikitakiwa kutekeleza dhamana yangu hii. Nawapongeza kwa ushirikiano na kuwapa shime kwa juhudi wanazofanya katika kujiletea maendeleo yao wenyewe na maendeleo ya Jimbo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru sana mke wangu mpendwa Furaha kwa uvumilivu mkubwa anaoendelea kuwa nao juu ya maisha haya ambayo ni ya kutumikia umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salaam na shukrani hizi, niruhusu sasa nitoe ufafanuzi kwa muhtasari wa hali ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Kilimo nchini imeendelea kuwa ni sehemu muhimu katika maendeleo ya uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla hususan wakati huu tunapojizatiti kufikia uchumi wa viwanda. Sekta hiyo imeendelea kuimarika na hivyo kuchangia asilimia 30.1 katika Pato la Taifa kwa mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 29.2 kwa mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa msimu wa 2016/2017 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2017/2018 iliyofanyika mwezi Juni, 2017 imebaini kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo uliopita ilifikia tani 15,900,864. Uzalishaji wa mazao ya nafaka ambayo ndiyo kipimo kikuu cha hali ya upatikanaji wa chakula ulifikia tani 9,388,772, ambapo mahindi yalikuwa tani 6,680,758 na mchele tani 1,593,609. Uzalishaji wa mazao mengine yasiyo ya nafaka ulifikia tani 6,512,092.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa chakula nchini ukilinganishwa na mahitaji umeendelea kuwa imara. Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2017/2018 ni tani 13,300,034 na kati ya hizo, mahitaji ya nafaka ni tani 8,457,558 na yasiyo nafaka ni tani 4,842,476. Kwa ujumla, kuna ziada ya tani 2,600,831. Kati ya hizo kwa nafaka kuna ziada ya tani 931,214 na kwa mazao mengine yasiyo ya nafaka ziada ni tani 1,669,617. Hali hii inalifanya Taifa liwe na kiwango cha utoshelevu wa chakula kwa asilimia 120 ukilinganisha na kiwango cha utoshelevu wa asilimia 123 kwa mwaka 2016/ 2017. Hivyo, kufuatia hali hii, Serikali imeruhusu mazao ya chakula, ikiwa pamoja na mahindi kuuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii pia imesaidia kushuka kwa mfumuko wa bei kufikia asilimia 6.2 ikilinganishwa na 7% mwezi Desemba, 2016. Ili kuboresha masoko kwa mazao ya chakula, hususan mahindi, Serikali itaanzisha utaratibu wa kutoa vibali mipakani kwa mfumo wa kielektroniki ambapo waombaji wataweza kupata huduma vibali vya kusafirisha nje bila kulazimika kwenda Makao Makuu ya Wizara ya Kilimo kuvifuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Taifa kujitosheleza kwa chakula, bado kuna Halmashauri ambazo zina maeneo yenye upungufu wa kujirudiarudia kila mwaka. Hali hii inapelekea kuwa na matatizo ya usalama wa chakula na lishe katika maeneo haya. Namna ya kukabiliana na changamoto hii, Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya tathmini kwa kipindi cha mwezi huu wa Mei hadi mwezi ujao kubaini mwelekeo wa hali ya uzalishaji kwa msimu wa 2017/ 2018 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ushirika nchini imeendelea kuimarika ambapo kufikia Desemba mwaka 2017 vyama vipya 394 vilisajiliwa na kufanya idadi ya vyama kufikia 10,990 kutoka 10,596 vilivyokuwepo Machi, 2017. Vyama hivi vinakadiriwa kutoa ajira mpya takribani 1,182 na katika kipindi hicho, wanachama wapya 385,295 walijiunga kufanya idadi ya wanachama kuongezeka kutoka 2,234,016 hadi 2,619,311.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, amana za *SACCOS* zimeongeza kufikia shilingi bilioni 53 mwaka 2017/2018 ikilinganishwa na shilingi bilioni 47 mwaka uliopita 2016/2017. Ufafanuzi wa mwenendo wa ushirika nchini umetolewa kutoka aya ya 18 hadi 24 za kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa Sekta ya Kilimo kufikia mwaka 2025 ni kuleta mageuzi *(transformation),* kutoka mtazamo wa kilimo cha kujikimu kuelekea katika mfumo wa kibiashara. Lengo la mageuzi haya ni kuhakikisha kuwa shughuli za kilimo zinakuwa na manufaa kwa nchi na wakulima; pia kuendana na dhamira ya kuwa uchumi wa viwanda wa hadhi ya kipato cha kati. Ili kuhakikisha malengo yetu ya kubadili kilimo yanafanikiwa, mazao makuu ya kilimo; pamba, kahawa, tumbaku, chai na korosho yatauzwa na kununuliwa kupitia Vyama vya Ushirika vya Wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ieleweke kwamba Vyama vya Ushirika siyo vitakavyonunua mazao haya, bali wafanyabiashara au wanunuzi ndiyo watakaonunua mazao ya wakulima kupitia vyama vyao. Ni marufuku Vyama Vikuu vya Ushirika au Vyama vya Msingi vya Ushirika kupeleka dhana kwa wananchi kwamba vyenyewe ndivyo vinanunua mazao ya wanachama wake. Kazi ya vyama ni kuleta kwa pamoja mazao ya wakulima ili wafanyabiashara wanunue au moja kwa moja au kwa njia ya mnada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Ushirika vya Kahawa vitakusanya na kupeleka kahawa mnadani. Vyama vya Ushirika vya Pamba, vitasimamia, kukusanya na kuhakiki ubora wa pamba ili wanunuzi waje kununua kutoka kwenye maghala ambayo ushirika utakuwa umeyaandaa. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo ya malengo ya Sekta ya Kilimo yanapatika katika aya za 25 hadi 28 za kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli kwa mwaka 2017/2018 na mipango ya mwaka 2018/

2019. Wizara ya Kilimo ina mafungu mawili; Fungu 43 - Wizara ya Kilimo na Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli katika mafungu mawili haya ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Mapato na Matumizi ya Fedha katika Kipindi cha mwaka 2017/2018, Fungu 43; Makusanyo ya Maduhuli. Wizara ya Kilimo kwa Fungu 43, katika mwaka 2017/2018 ilikadiria kukusanya mapato ya Sh.2,015,010,000/= kutokana na vyanzo mbalimbali. Kufikia tarehe 31 Machi, 2018, Wizara ilikusanya jumla ya Sh.1,708,724,841.68 sawa na asilimia 84.80 ya makadirio na Wizara bado inaendelea kukusanya maduhuli hadi tarehe 30 Juni, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Fungu 43, ilitengewa jumla ya Sh.214,815,759,000/=. Kati ya hizo, Sh.bilioni 64,562,759,000/= zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.150,253,000,000/= kwa shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Kufikia tarehe 31 Machi, 2018, jumla ya Sh.39,069,819,172/= kati ya Sh.64,562,759,000/= zilizopitishwa kwa Fungu 43 kwa mwaka wa fedha uliopita kwa matumizi ya kawaida zilikuwa zimetolewa na kupokelewa sawa na asilimia 55.87 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha zilizopokelewa, Sh.33,054,942,776.63 sawa na asilimia 91.64 zilikuwa zimetumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye matumizi ya maendeleo. Wizara ya Kilimo, Fungu 43, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ilitengewa jumla ya Sh.150,253,000,000/= kwa utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Kati ya fedha hizo, Sh.59,600,000,000/= zilikuwa fedha za ndani na Sh. 90,653,000,000/= za nje. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 Shilingi 27,231,305,232.69 zimetolewa sawa na asilimia 18 ya Fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Aidha, kufikia tarehe hiyo,

fedha zilizokuwa zimetolewa, zilikuwa zimetumika sawa na asilimia 100 ya fedha za maendeleo zilizopokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na mpango wa mwaka wa fedha 2018/2019. Wizara ya Kilimo kwa Fungu 43 katika mpango na bajeti wa mwaka 2017/ 2018, ina maeneo nane ya kipaumbele. Maeneo haya yanatekelezwa kupitia mipangokazi ya Idara, Vitengo, Asasi na Taasisi za Wizara kama inavyoelezwa kuanzia aya ya 34 hadi 194 za kitabu cha hotuba. Kwa muhtasari, utekelezaji wa maeneo haya ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusimamia matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo na maji. Wizara ikishirikiana na Wizara za Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Sekta Binafsi kwa mwaka 2017/2018 imewezesha kupatikana ardhi ya uwekezaji mkubwa katika mashamba ya miwa na uzalishaji wa sukari katika eneo la Mkulazi lenye hekta 60,000; Bagamoyo lenye hekta 10,000 na Mbigiri lenye ekari 12,000. Aidha, imeweza kuvutia wawekezaji, ambapo kwa shamba la Mkulazi ni Kampuni ya Mkulazi *Holding Company Limited;* Bagamoyo ni Kampuni ya *Bakhresa Group of Companies;* na kwa Mbigiri ni kampuni ya *Mkulazi Holding Company Limited* ikishirikiana na Jeshi la Magereza. Ili kuwanufaisha wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba la Mkulazi, Wizara kupitia ushirikiano wa kitaasisi imewezesha kutolewa hati za Hakimiliki 400 za Kimila kwa wananchi wa Kijiji cha Chanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili, Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imepanga kutekeleza mpango wa kujenga mabwawa ya kuvuna, kuhifadhi na kilimo cha umwagiliaji katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Aidha, Wizara itajenga bwawa la Kalege na miundombinu ya umwagiliaji kwa eneo la takribani hekta 11,700 na litahudumia Halmashauri za Bukoba Vijijini na Misenyi. Bwawa hilo litakuwa na uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo milioni 2,780,000

ambapo litasaidia upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo, ufugaji wa samaki na kuchangia kupunguza uharibifu wa vyanzo vya maji katika bonde la Mto Ngono Mkoani Kagera. Vilevile, bwawa hilo litatumika kwa ajili ya kuhifadhi maji kwa matumizi wakati wa kiangazi, kuboresha ustahimilivu wa mabadiliko ya tabia nchi, kuzuia athari za mafuriko katika eneo la takriban hekta 3,555 na uzalishaji wa megawati 2.46 za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018, Wizara ilijielekeza katika kuimarisha upatikanaji wa mbolea. Kufikia Aprili, 2018 tani 435,178 zilikuwa zimeingizwa na wafanyabiashara walioruhusiwa na kusambazwa katika mikoa mbalimbali nchini ukilinganisha na tani 332,000 kipindi cha mwezi Aprili, 2017. Kiasi hicho kilichoingizwa ni sawa na asilimia 89.73 ya wastani wa mahitaji ya tani 485,000 kwa mwaka. Kati ya kiasi hicho cha mbolea, tani 233.9 ziliagizwa kwa kutumia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja, zikiwa ni tani 88,945 za mbolea ya kupandia *(DAP)* na tani 145,034, mbolea ya kukuzia *(UREA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mafanikio yaliyopatikana, Wizara katika mwaka 2018/2019 itaendelea kutumia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja wa Mbolea *(Bulk Procurement System)* ambapo wafanyabiashara watakaopata zabuni za kuleta mbolea nchini wataingiza tani 300,000 za mbolea. Kati ya hizo, tayari tani 100,000 zimeagizwa na tani 32,000 zimekwishapokelewa, hali inayotoa uhakika wa upatikanaji wa mbolea kwa wakati msimu wote ujao. Ili kuimarisha usambazaji, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za Mikoa itahamasisha ushiriki wa sekta binafsi kujenga maghala makubwa kwa ajili ya kuhifadhi mbolea *(strategic storage facilities)* hasa katika maeneo yenye mahitaji makubwa. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia bei ili kuwalinda wakulima na kuongeza matumizi ya mbolea. Tunadhamiria pia kutumia Jeshi la Kujenga Taifa na Kampuni ya Mbolea ya Taifa *(TFC)* katika kuhakikisha kwamba mbolea inakuwepo katika Mikoa na Wilaya zote muda wote wa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msukumo pia umewekwa katika kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora na viuatilifu nchini. Katika mwaka 2017/2018 upatikanaji wa mbegu bora umefikia tani 51,700.51 ukilinganishwa na tani 28,278.2 za mwaka 2016/2017, ambapo tani 26,112.69 zilizalishwa nchini; tani 16,277.7 ziliagizwa kutoka nje na wafanyabiashara na tani 9,310.12 zikiwa ni bakaa ya msimu wa 2016/2017. Kati ya mbegu zilizozalishwa nchini, tani 18,500 ni za zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara itachangia upatikanaji wa tani 40,000 za mbegu bora mbalimbali; miche bora ya chai milioni 10 na miche bora ya kahawa milioni 12, kusambaza tani 8,600 na lita 9,800 za viuatilifu na ekapaki 7,000,000 za viuatilifu vya zao la pamba. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *"Bill and Melinda Gates Foundation"* itakamilisha Mfumo wa Taifa wa kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora. Mfumo huo utahusisha uboreshaji wa uzalishaji wa mbegu mama katika vituo vya utafiti, kuimarisha na kuboresha miundombinu ya mashamba ya *ASA* yanayozalisha mbegu zilizodhibitiwa, kujenga uwezo wa Taasisi ya Uthibiti wa Ubora wa Mbegu *(TOSCI)* na kuboresha mfumo wa menejimenti ya upatikanaji, usambazaji na matumizi ya mbegu bora nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 kiuatilifu aina ya *sulphur* pamoja na vifungashio vya korosho (magunia) havitatolewa kwa njia ya ruzuku kama ilivyokuwa msimu wa kilimo uliopita. Wakulima watauziwa kwa bei ambayo itatangazwa na Bodi ya Korosho ili wakulima na wadau wa korosho waweze kufahamu utaratibu wa kupata pembejeo hiyo pamoja na magunia kwa wakati na kwa bei itakayopitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia Bodi ya Korosho kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika wa Korosho na Benki ya *NMB* imekamilisha mchakato wa uagizaji wa pembejeo za korosho ikiwemo kuingia mikataba na wazabuni ambapo kwa ujumla wao wataleta *sulphur* ya

unga tani 35,000 na viuatilifu vya maji lita 520,000. Hadi leo tarehe 15 Mei, 2018 kiasi cha tani 6,299 za *sulphur* ziko nchini na tani 1,328 tayari zimekwishasambazwa kwa wakulima kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika. Kiasi cha tani 37,873 zimeagizwa ambapo tani 17,500 zinatarajiwa kufika nchini mwezi huu wa Mei. Tani 20,373 zitawasili nchini kati ya mwezi Juni na Julai na Serikali inasimamia upatikanaji wa magunia ya kuhifadhi korosho kupitia makubaliano kati ya Vyama vya Ushirika, Benki na wazalishaji wa magunia.

Mheshimiwa Mwenyekiyi, nizungumzie udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao. Hadi kufikia mwezi Aprili 2018, ndege waharibifu aina ya kweleakwelea walidhibitiwa katika Wilaya 11 nchini ambapo jumla ya lita 2,425 kati ya 6,000 za kiuatilifu aina ya *Fenthion 60% ULV* zilitumika kuangamiza ndege milioni 61.7. Hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na kufanya tathmini ili kubaini viwavijeshi vamizi *(Fall armyworm)* iliyofanyika katika Mikoa sita sanjari na tathmini ya kubaini uwepo wa nzige wekundu katika mbuga za mazalio, hususan maeneo ya Ziwa Rukwa, Iku-Katavi, Malagarasi, Wembere na Bahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kudhibiti visumbufu vya mazao na mimea kwa kufanya tathmini ili kudhibiti milipuko ya nzige, kweleakwelea, panya, viwavijeshi na magonjwa ya mimea. Hatua pia zitachukuliwa kuimarisha vituo vya ukaguzi vya mipakani na Kituo cha Kudhibiti Milipuko cha Kilimo Anga. Vilevile, kupitia Programu ya Maendeleo ya Kilimo Awamu ya II, Wizara itavijengea uwezo na kukarabati Vituo 36 vya Afya ya Mimea na Vituo nane vya Ukaguzi wa Mazao Mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti na utoaji wa matokeo ya utafiti kwa wadau. Katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Vituo vya Utafiti na kwa kushirikiana na taasisi binafsi za kilimo imegundua na kuidhinisha mbegu bora mpya 25 (Kiambatisho Na.1). Aidha, mbegu hizo zitaanza kuzalishwa

na Wakala wa Mbegu wa Taifa na makampuni binafsi na kusambazwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya mbegu bora zilizogunduliwa na watafiti na kusambazwa kwa wakulima wa korosho yameonesha kuongezeka kwa uzalishaji kutoka tani 127,956 mwaka 2012/2013 hadi tani 265,238 mwaka 2016/ 2017 ikiwa ni pamoja na kuzingatia kanuni bora za kilimo, udhibiti wa wadudu wenye magonjwa, pamoja na kuimarika kwa bei ya korosho. Mwaka huu mpaka sasa korosho iliyozalishwa na kuuzwa kupitia minada rasmi ni tani 319,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia vituo vyake vya utafiti itaendelea kuwezesha kugundua, kutathmini na kusambaza teknolojia bora za kilimo. Aidha, mbegu bora mama na mbegu za awali tani 10 zikiwemo nafaka na mikunde zenye sifa mbalimbali zitazalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Programu ya *ASDP II* itaboresha na kuimarisha miundombinu ya utafiti kwa kukarabati ofisi, maabara na nyumba katika vituo nane vya utafiti, Kituo cha Taifa cha Utunzaji Nasaba za Mimea *(National Plant Genetic Resource Centre)* pamoja na ujenzi na uboreshaji wa Makao Makuu ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo *(TARI).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itahakikisha kuwa matokeo ya utafiti yanawafikia wadau wa kilimo kwa njia ya mtandao, maonesho, mashamba ya mfano, taarifa na machapisho mbalimbali kama vile mabango, vipeperushi na vijarida. Aidha, itaratibu upatikanaji wa taarifa muhimu za utafiti kupitia majarida makubwa ya utafiti ulimwenguni kwa kushirikiana na Taasisi za Kimataifa ili kuongeza ubunifu wenye tija kwa maendeleo ya Sekta ya Kilimo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie huduma za ugani na kusambaza teknolojia za kilimo. Katika

mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kupeleka teknolojia za kilimo kwa wakulima kwa kutoa mafunzo ya matumizi sahihi ya viuatilifu vya zao la pamba kwa wakulima viongozi na wengineo 15,230 katika Halmashauri 14 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kwa ushirikiano na TAMISEMI, itaendelea kusimamia huduma za ugani na kuboresha usambazaji wa teknolojia bora kwa wakulima kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo utoaji wa ushauri wa kitaalam moja kwa moja na ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa kazi za ugani katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kupitia Programu ya Kilimo Awamu ya II, tutaendelea kuviimarisha vituo saba vya maonesho ya wakulima (Nane Nane) na kujenga kituo kimoja kipya cha maonesho cha Kanda ya Ziwa Mashariki katika Mkoa wa Simiyu ili kupeleka teknolojia za kilimo kwa wakulima wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa mazao baada ya mavuno, kuongeza thamani na upatikanaji wa masoko. Katika mwaka 2017/2018, sisi kwa kushirikiana na wadau kama vile *FAO, ANSAF* na *HELVETAS* tumekamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Mazao baada ya mavuno unaolenga kupunguza upotevu wa mazao ya chakula, kuongeza upatikanaji wa masoko na kipato kwa mzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeandaa andiko la Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu *(Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination)* ambao unalenga mazao ya mahindi na karanga na utatekelezwa katika mikoa ya Mwanza, Geita, Tabora, Simiyu, Kigoma, Dodoma, Morogoro, Manyara, Ruvuma, Songwe na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara itatekeleza Mradi wa *TANIPAC* ambapo itafanya usanifu wa ujenzi wa kituo cha mfano cha kusambaza teknolojia za usimamizi wa

mazao baada ya kuvuna *(Post-harvest Centre of Excellence),* Maabara ya mfano *(Central Agriculture Reference Laboratory for Aflatoxin and Fungal Testing)* kwa ajili ya vipimo vya maambukizi ya sumukuvu na aina nyingine za ukungu mkoani Dodoma. Aidha, katika kuimarisha soko la ufuta, kuanzia msimu wa mavuno wa mwaka 2017/2018, zao la ufuta litauzwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala hususan Mikoa ya Lindi, Ruvuma, Morogoro, Dodoma na Singida na maandalizi yamekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudhibiti matumizi ya vipimo vya mazao visivyo rasmi, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji na wadau wengine, itasimamia na kuhamasisha matumizi ya mizani na vifungashio sahihi ili kumsaidia mkulima kupata mapato stahiki kutokana na mauzo ya zao lake. Aidha, Serikali itasimamia utekelezaji wa Sheria ndogo ndogo ili kudhibiti matumizi ya vipimo visivyo rasmi na inaendelea kwa kadri inavyowezekana kuhimiza mazao yote yauzwe kwa uzito badala ya ujazo. Lumbesa ni tatizo la kujitakia. Tukiuza kwa uzito tatizo hili litapungua sana au litaisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusimamia uzalishaji kupitia Bodi za Mazao. Katika mwaka 2017/2018, tumeendelea kusimamia uzalishaji wa mazao kupitia Bodi za Mazao hayo. Uzalishaji kwa baadhi ya mazao makuu ya asili ya biashara umeongezeka kwa viwango tofauti kama inavyoonekana katika Jedwali Na.1. Ongezeko hilo limechangiwa na sababu mbalimbali zikiwemo matumizi ya teknolojia na mbinu bora za uzalishaji pamoja na ongezeko la bei ya mazao ya pamba, pareto, korosho, chai na tumbaku katika msimu uliopita. Hali kadhalika, *sulphur* iliyotolewa bure na Serikali kupitia fedha za *Export Levy* ilisaidia kuongeza mavuno katika zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018, uzalishaji wa mazao ya bustani na viungo *(horticulture)* umeongezeka kwa viwango tofauti kama inavyoonekana

katika Jedwali Na.2. Ongezeko hilo linatokana na wakulima kuhamasika kuzalisha mazao ya parachichi, matikiti na nyanya. Wizara inaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali kuhamasisha kilimo cha mazao ya bustani na viungo pamoja na ulaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara itahakikisha kuwa mpango wa bajeti unatekelezwa kwa kuzingatia vipaumbele na miongozo ya kitaifa ili kilimo kichangie kutoa malighafi za viwanda na kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Lengo letu ni kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa kati mwaka 2025. Mimi binafsi naamini kwamba endapo programu za kilimo zitatekelezwa kama tulivyojipanga, Tanzania itakuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo au kabla ya mwaka 2022, hili jambo linawezekana.

Mheshimwia Mwenyekiti, Wizara kupitia Programu ya Kilimo Awamu ya II inatekeleza mkakati wa maendeleo ya mazao ambao unaweka mfumo *(framework)* wa kuendeleza mazao ya kilimo kwa kushirikisha wadau na Wizara ikiwa na jukumu la uratibu wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwa ufupi sana taasisi za Wizara. Mwaka 2017/2018, kupitia taasisi za Wizara, tumeendelea kusimamia hifadhi ya chakula, kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya riba nafuu, uzalishaji wa mbegu bora na udhibiti wa ubora wa pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)*. Katika kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula nchini, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ulifanikiwa kununua tani 26,038.643 sawa na asilimia 143 ya lengo lake iliyokuwa tani 18,182 za mahindi. Wizara kupitia Wakala huu inatekeleza Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi Nafaka kwa kujenga maghala na vihenge vya kisasa katika maeneo nane nchini ambayo ni Dodoma, Songea, Makambako, Mbozi, Sumbawanga, Mpanda, Shinyanga na Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiwe la msingi la mradi huu liliwekwa Dodoma tarehe 21 Aprili, 2018 na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ujenzi umeshaanza, ambapo vihenge na maghala hayo yatakuwa na uwezo wa kuhifadhi tani 250,000. Katika mwaka 2018/ 2019, Wakala umepanga kununua tani 28,200 za nafaka na kuendelea kutekeleza Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi Nafaka unaolenga kutufikisha kwenye uhifadhi wa kwenye uhifadhi nafaka kufikia tani 700,000 ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo. Hadi Februari, 2018, Wizara kupitia Mfuko huu wa Taifa wa Pembejeo imetumia Sh.2,391,246,400/= kukopesha zana mbalimbali za kilimo, mifugo na uvuvi kama inavyooneshwa katika Kiambatisho Na. 2 na *addendum* ambayo nimeiwasilisha mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Mbegu za Kilimo *(ASA).* Wakala huu umezalisha tani 784.155 za mbegu bora, zikiwemo mbegu bora za nafaka, mikunde na mbegu za mafuta ambapo tani 650 wameuziwa wakulima. Aidha, miche bora ya kahawa 1,163,758 imezalishwa ambapo kati ya miche hiyo, 207,358 imezalishwa Lyamungo (Kilimanjaro), 132,900 Ugano (Ruvuma), 646,800 Maruku (Kagera), 71,000 Mwayaya (Kigoma), 100,000 Mbimba (Songwe) na 5,700 Tarime (Mara).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Wakala wa Mbegu imepanga kuzalisha mbegu bora za nafaka na mikunde tani 1,800. Kwa kushirikiana na sekta binafsi itazalisha tani 1,500 za mbegu bora katika shamba la Mbozi, vipando bora vya muhogo pingili 7,000,000 katika mashamba ya Mwele na Msimba na miche bora ya matunda 50,000 katika mashamba ya Bugaga, Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora Tanzania *(TFRA)*. Wizara kupitia *TFRA* imeendelea kudhibiti ubora wa mbolea nchini ambapo hadi mwezi Februari, 2018 imesajili wafanyabiashara wa mbolea 430 na kufikia idadi ya wafanyabiashara wa mbolea 2,045 kwa nchi nzima. Imetoa vibali 286 vya kuingiza mbolea nchini ambapo tani 310,673.7 zimeingizwa. Imefanya ukaguzi wa maghala na maduka ya wafanyabiashara wa mbolea kwenye mikoa 19 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia *TFRA* itaimarisha Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja kwa kuhamasisha makampuni ya mbolea kuagiza mbolea kwa kiasi kikubwa katika kipindi ambacho bei ya mbolea kwa Soko la Dunia iko chini ili kuepuka ongezeko la bei katika Soko la Dunia. Aidha, *TFRA* itatoa elimu juu ya mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja kwa wasambazaji *(Agro – Dealers)* wa mbolea katika Mikoa na Halmashauri, kusajili wafanyabiashara wa mbolea, kukagua na kutoa vibali vya kuingiza mbolea nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Taasisi ya Uthibiti Ubora wa Mbegu Nchini – *TOSCI*. Wizara kupitia *TOSCI* imekagua mashamba ya mbegu na katika msimu uliopita imekagua hekta 8,103 ambapo hekta 24.3 sawa na asilimia 0.3 hazikukidhi viwango vya ubora; imehakiki uhalisia, ubora na sifa za aina mpya 126 za mbegu kwa ajili ya usajili; imetoa vibali 860 vya kuingiza mbegu na vibali 11 vya kutoa mbegu nje ya nchi ambapo jumla ya tani 13,393 za mbegu zimeingizwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TOSCI* imefungua kituo kipya cha udhibiti wa ubora wa mbegu katika Kanda ya Kusini chenye Makao Makuu yake Mtwara ili kurahisisha utoaji huduma katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma. Aidha, *TOSCI* itahakiki upya uhalisia na sifa kwa aina 107 za mbegu mpya na kutoa *label* milioni 15 kwa ajili ya kuweka kwenye mifuko ya kuuzia mbegu ili kukabiliana na tatizo la mbegu zisizo na ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo. Katika mwaka 2017/2018, Wizara imetoa ufadhili kwa wanafunzi 1,956 kwenye mafunzo ya kilimo ngazi ya Astashahada na Stashahada katika Vyuo 14 vya Mafunzo ya Kilimo. Vilevile, Wizara imedahili wanafunzi 246 wanaojilipia wenyewe ngazi ya Astashahada na Stashahada. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itadahili wanafunzi 2,300 ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa ufadhili wa Serikali; itandaa mtaala wa Stashahada ya Matumizi Bora ya Ardhi katika mfumo wa moduli; itahuisha mtaala wa Stashahada ya mboga, maua na matunda; itakarabati miundombinu ya vyuo saba vya mafunzo ya kilimo na vituo vitano vya mafunzo kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuunda na kupitia sera za sekta ndogo za mazao. Katika mwaka 2017/2018, Serikali kupitia Wizara hii ilifuta ada na tozo za mazao 78 kati ya 139 zilizokuwa hazina tija kwa wakulima. Kufuatia hatua hiyo, Wizara ilifanya marekebisho ya kanuni na sheria zilizoanzisha tozo na ada husika ili kuwezesha utekelezaji wa marekebisho hayo. Serikali inasisitiza kuwa utekelezaji wa sheria na kanuni hizo uzingatiwe na kwamba hatua kali zitachukuliwa kwa wale wote wanakaokiuka maelekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha 2018/2019, Wizara imechambua na kubaini ada na tozo 21 ambazo bado ni kero kwa wakulima nchini na imezifuta. Lengo ni kubakiza ada na tozo ambazo zina mahusiano ya moja kwa moja na uendelezaji wa mazao husika kama vile uendelezaji wa utafiti wa mazao na kadhalika. Ada na tozo zilizofutwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu katika tasnia ya chai; tatu tasnia ya kahawa; mbili katika tasnia ya tumbaku; na tozo moja moja kwa tasnia za sukari na pamba. Aidha, kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa pembejeo, Serikali imefuta tozo tano kwenye uzalishaji wa mbegu. Vilevile, kwa ajili ya kuimarisha maendeleo ya ushirika nchini, tozo sita katika ngazi mbalimbali za ushirika nazo zimefutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imewasilisha Wizara ya Fedha na Mipango mapendekezo ya kuboresha mfumo wa kodi na tozo kwa ajili ya kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na uendeshaji wa biashara katika shughuli za kilimo. Mapendekezo hayo yanalenga kutoa unafuu wa kodi katika vifungashio vya mazao na mbegu za mazao ya kilimo, mabomba ya kunyunyuzia madawa *(knapsack sprayers),* mashine na mitambo ya usindikaji wa mazao, miundombinu ya uzalishaji na hifadhi ya mazao ya bustani na kulinda wazalishaji wa ndani dhidi ya ushindani usio sawa wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Mpango wa Wizara ni kuhakikisha kero zote zinazokwamisha maendeleo ya tasnia ya mazao ya kilimo zinashughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na tathmini katika sekta. Katika mwaka 2017/2018, Wizara imeandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Kilimo *(Annual Performance Report)* kwa mwaka wa fedha 2016/2017; imeboresha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za Kilimo *(Agriculture Routine Data System)*; imeandaa mfumo wa kupima matokeo ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(ASDP II Result Framework)* pamoja na viashiria vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Kuendeleza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(SAGCOT)*. Katika mwaka 2017/2018, Wizara yangu imeendelea kuratibu uwekezaji kwenye ukanda wa *SAGCOT*. Hadi sasa jumla ya Dola milioni 500 kati ya Dola bilioni 3.5 zilizopangwa kuwekezwa ifikapo mwaka 2030 zimewekezwa katika Kilimo kwenye ukanda huo. Kati ya uwekezaji huo, Dola bilioni 2.4 zitatokana na sekta binafsi. Aidha, wawekezaji wakubwa wameweza kuunganishwa na wakulima ili kuongeza tija, kipato, chakula na lishe kwenye kaya za wakulima wa soya, chai, viazi vitamu na mviringo, mpunga, mboga na matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na *SAGCOT* na wadau wa kilimo

itapanua uzoefu uliopatikana kutoka *SAGCOT* kuendeleza kilimo kwenye maeneo mengine nchini. Hivyo, Wizara inao mpango madhubuti wa kuendeleza kilimo kwenye Ukanda wa Ziwa hususan kujenga mabwawa yatakayotumika kwenye kilimo cha umwagiliaji. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na wabia wa maendeleo na wadau wengine wa sekta ya kilimo ili kufikia malengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha masuala mtambuka, ushiriki wa vijana katika masuala ya kilimo. Katika mwaka 2017/2018, tutashirikiana na *Farm Africa* kutekeleza mkakati wa kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali na uzalishaji wa mazao ya ufuta, mahindi, maharage, mpunga, uyoga na asali kwa vijana 96,365 kutoka mikoa mitano ambapo kati ya hao 56,805 ni wa kiume na 39,560 ni vijana wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa mkakati wa vijana kushiriki katika kilimo na kuongeza ajira kwa kushirikiana na Wizara za kisekta, wabia wa maendeleo na wadau wetu ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Katika kutekeleza Mpango wa Kilimo kinachohimili mabadiliko ya Tabianchi *(Agriculture Climate Resilient Plan)* mwaka 2014, Wizara kwa kushirikiana na Idara ya Kilimo ya Marekani *(United States Department of Agriculture - USDA),* inatekeleza mradi wa kujenga uwezo wa kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi kwa usalama wa chakula ambapo mashamba darasa mawili yameanzishwa katika Wilaya za Kongwa na Uyui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wakulima kupitia Mradi wa Kuongeza Uzalishaji na Tija kwa zao la Mpunga *(Expanded Rice Production Project)* imeandaa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii *(Environmental and Social Management Plans)* wa kutunza mazingira ya

Skimu za Umwagiliaji za Kigugu, Mbogo-komtonga, Mvumi, Msolwa Ujamaa na Njage. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itazijengea uwezo Halmashauri za Wilaya katika Mikoa ya Kagera, Mbeya, Iringa, Morogoro na Kilimanjaro wa kutambua umuhimu wa kujumuisha njia za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika bajeti na mipango ya maendeleo ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kutekeleza mpango wa Serikali wa kuhamia Dodoma. Mwaka huu Wizara imeendelea kutekeleza mpango agizo la Serikali wa kuhamia Dodoma katika awamu tatu, ambapo katika awamu hizo watumishi 316 waliokuwa Makao Makuu ya Wizara Dar es Salaam wamehamia Makao Makuu Dodoma. Katika mwaka ujao, Wizara itaendelea kuhamisha watumishi wake kuja Makao Makuu Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Fungu 24 - Vyama vya Ushirika. Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Fungu 24 – Vyama vya Ushirika, lilitengewa jumla ya Sh.6,293,857,760/= zikijumuisha Sh. 2,413,888,760/= za Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*). Kati ya fedha hizo, Sh.1,456,634,072/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo zikiwa ni Sh.942,577,072/= za Tume za Ushirika na Sh.514,057,000/= za *COASCO*. Jumla ya Sh.4,837,223,688/= zilitengwa kwa ajili ya mishahara na Sh.2,937,391,928/= zilikuwa ni mishahara ya Watumishi wa Tume na Sh.1,899,831,760/= ni kwa ajili ya Watumishi wa *COASCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotolewa katika bajeti ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2018, fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa kutoka Hazina zilikuwa ni Sh. 3,854,197,441.41 sawa na asilimia 61.24 ya kiasi kilichoidhinishwa. Hadi kufikia Machi, 2018 jumla ya Sh. 3,854,197,441.41, sawa na asilimia 100 ya fedha zilizopokelewa kwa Fungu 24 zilikuwa zimetumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018, Wizara chini ya Fungu 24 imeendelea kutekeleza majukumu yaliyopangwa. Kwa muhtasari majukumu yaliyotekelezwa na mpango kwa mwaka 2018/2019 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Tume, imekagua Vyama vya Ushirika 2,896 sawa na asilimia 55.7 ya lengo la kukagua vyama 5,200. Aidha, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika limekagua Vyama vya Ushirika 1,520 sawa na asilimia 18.91 ya lengo la kukagua vyama 8,040. Katika mwaka 2018/2019, Wizara inaendelea kuiwezesha *COASCO* kufanya ukaguzi katika Vyama vya Ushirika 8,040. Aidha, Wizara kupitia Tume itakagua Vyama Vikuu vya Ushirika 47, miradi ya pamoja na 34, Vyama vya Ushirika vya Msingi 10,909 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Tume imesimamia chaguzi za viongozi wa Vyama Vikuu vya Ushirika na Miradi ya Pamoja 12 sawa na asilimia 26.7 ya lengo la kusimamia vyama 45. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, imeratibu na kusimamia chaguzi za Vyama vya Msingi 5,599 sawa na asilimia 93.3 ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa itaratibu na kusimamia chaguzi za Vyama Vikuu na miradi ya pamoja 36 na Vyama vya Ushirika vya Msingi 5,000 pote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Licha ya ukweli kwamba Sekta ya Kilimo ni muhimu kwa maisha na ustawi wa uchumi kwa watu wengi hapa nchini, bado mchango wa sekta hii katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii hausadifu fursa kubwa tuliyonayo kama nchi. Kwa kiasi kikubwa hali hii inachangiwa na mambo ambayo yapo ndani ya uwezo wetu, hususan kuwa na mawazo mgando kuhusu uendeshaji wa kilimo na mapokeo ya maumbile asili ya dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumedhamiria kuondokana na mgando huu kwa kufanya mageuzi makubwa katika uendeshaji wa shughuli za kilimo kupitia *ASDP*-II na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Wizara imebaini maeneo manne ya kuongoza mageuzi hayo ambayo ni kama ifuatayo:-

(i) Kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo;

(ii) Kusimamia kikamilifu hifadhi na matumizi jadidifu ya maji, ardhi na mazingira sambamba na kuongeza miundombinu ya umwagiliaji;

(iii) Kuweka msukumo katika mabadiliko ya fikra na mazingira ya kibiashara kwa sekta ya kilimo; na

(iv) Kuweka mfumo mpya wa usimamizi wa kilimo kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi kwa uendeshaji kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira hii ya Serikali ni endelevu na ya kweli. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuanza utekelezaji wa hatua hii ya mageuzi kwa kuelekeza kuondoa kero na vikwazo walivyowekewa wakulima kwa miaka mingi. Anaposema wabebe gunia moja moja anamaanisha hili, nawaomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono katika mageuzi haya. Natambua ugumu uliopo hasa pale tunapogusa maslahi ya waliokuwa wananufaika na mifumo wa zamani. Mwanzo ni mgumu na wajibu wetu kama viongozi ni kutotetereka na kubaki tumejielekeza katika malengo ya tunayojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru na kuzishukuru nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Kwanza napenda kuzishukuru nchi za Japan, Marekani, Uingereza, Ireland, Malaysia, China, Indonesia, Korea ya Kusini, India, Misri, Israel, Ubelgiji, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil, Uholanzi, Vietnam na

Poland. Nayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa za Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF* na wengine wengi. Nalishukuru pia Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani, Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu, *Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust*, *Rockfeller Foundation, The Aga Khan Foundation, Unilever* na Asasi zisizo za Kiserikali nyingi ambazo siwezi kuzitaja zote hapa. Ushirikiano na misaada ya nchi na mashirika haya bado tunauhitaji ili tuweze kubadili kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za kipekee kabisa kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Napenda kumshukuru Naibu Waziri wangu wa Kilimo Mheshimiwa Dkt. Mary Machechu Mwanjelwa Mbunge, Katibu Mkuu, Mhandisi Mathew John Mtigumwe; Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Thomas Didimu Kashilillah; Wakurugenzi wa Idara na Wakuu wa Vitengo, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara, watumishi wote wa Wizara na wadau mbalimbali wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2017/2018 kama nilivyofafanua katika hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba, nitaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2018/2019. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha kitabu cha hotuba ya bajeti ya mwaka 2018/2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha. Katika mwaka 2018/2019 Wizara inaomba idhini ya kukusanya maduhuli ya jumla ya Sh.2,315,010,000. Maduhuli hayo yanatokana na faini mbalimbali na ada ya cheti cha afya ya mimea katika uingizaji wa mazao ya kilimo nchini na usafirishaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi. Katika mwaka 2018/2019, Wizara ya Kilimo inaomba jumla ya Sh.170,273,058,000 kupitia Fungu 43 na Fungu 24 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Sh.162,224,814,000 zinaombwa kupitia Fungu 43. Kati ya fedha hizo, Sh.98,119,516,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na Sh.64,105,298,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Sh.28,560,428,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara; Sh.14,346,253,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Bodi na Taasisi; Sh.12,727,150,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Wizara na Sh.8,471,467,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Bodi na Taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Sh.8,048,244,000 zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kupitia Fungu 24. Kati ya fedha hizo, Sh.2,199,700,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo; Sh. 4,013,370,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Tume na Sh.1,835,174,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono.

## HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI

### 1.1 UTANGULIZI

***1. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja mbele ya Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo Mifugo na Maji inayohusu Wizara ya Kilimo, sasa Bunge lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Matumizi

ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

**2. *Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa na afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania ambao wengi wao ni wakulima. Napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kutoa msukumo wa pekee katika kuendeleza Sekta ya Kilimo hususan kutambua umuhimu wa sekta hii katika kuendeleza uchumi wa viwanda. Aidha, namshukuru Mhe. Rais kwa kuendelea kuniamini. Napenda kutumia fursa hii kumuahidi Mhe. Rais, Waheshimiwa Wabunge, Wakulima na Watanzania wote kwamba nitatumia uwezo wangu wote kwa uaminifu na uadilifu kuhakikisha kwamba rasilimali zinazotengwa kwa ajili ya Sekta hii zinawafikia wakulima wetu ili wazalishe mazao na kupata manufaa stahiki kwa jasho lao.

***3. Mheshimiwa Spika,*** namshukuru pia Mhe. Rais kwa kuongoza Mkutano wa Baraza la Taifa la Biashara *(Tanzania National Business Council-TNBC)* uliofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 19 Mwezi Machi, 2018 na kushirikisha wafanyabiashara mbalimbali ikiwa ni pamoja na waliopo katika sekta ya kilimo. Mkutano huo ni muhimu sana ambapo jitihada hizo zilijikita katika kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na biashara katika tasnia mbalimbali kama sukari, korosho, pamba na mbegu za mafuta ya kula.

***4. Mheshimiwa Spika,*** Aidha, katika kuonesha umuhimu wa sekta ya kilimo katika maendeleo ya viwanda, Mhe. Rais Mwezi Machi, 2018 alizindua Kiwanda cha kusindika mafuta ya alizeti Mkoani Singida ambacho kinatumia teknolojia ya kisasa katika uzalishaji wa mafuta ya kula. Pia katika kipindi hicho, Mhe. Rais pia alizindua Kiwanda cha mafuta ya pamba, mkoani Shinyanga. Viwanda hivyo, vitasaidia kuwahakikishia wakulima upatikanaji wa masoko

ya mazao yao na kuchangia katika kukuza kipato na pato la Taifa kwa ujumla.

**5. Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza Makamu wa Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa akifanya ziara mikoani kuona shughuli za kilimo na maendeleo kwa ujumla na kutoa maelekezo mbalimbali ya namna ya kuendeleza kilimo. Katika ziara hizo, Mhe. Makamu wa Rais amekuwa akisisitiza umuhimu wa kilimo endelevu na kinachozingatia hifadhi ya mazingira na kinachohimili mabadiliko ya tabianchi. Maelekezo hayo yamezingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ili kuharakisha maendeleo ya kilimo nchini.

**6. Mheshimiwa Spika,** napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa kutumia muda wake mwingi kuhamasisha na kutoa maelekezo yenye lengo la kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo. Mhe. Waziri Mkuu amekuwa mstari wa mbele kuweka mkazo maalum wa kuyaendeleza mazao ya chai, kahawa, korosho, pamba na tumbaku ili kuongeza mapato ya wakulima, kuwa chanzo kikuu cha ajira, kuliingizia taifa fedha za kigeni na malighafi katika uchumi wa viwanda.

**7. Mheshimiwa Spika**, vilevile, ninampongeza Mh. Waziri Mkuu kwa kuchukua hatua na kutoa ushauri wa kuimarisha utawala bora kwenye vyama vya ushirika pamoja na kuhakikisha kwamba mauzo ya mazao hayo yanafanyika kwa uwazi na ushindani; na kuimarisha masoko kwa kuhamasisha mfumo wa stakabadhi ghalani ambapo mazao hayo yatauzwa kupitia vyama vya ushirika kwa njia ya minada. Aidha, Mhe. Waziri Mkuu aliongoza Kikao Kazi cha Baraza la Mawaziri kilichojadili na kuridhia Utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Programu hiyo itazinduliwa rasmi hivi karibuni na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jijini Mwanza.

***8. Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe mwenyewe, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge letu tukufu kwa umahiri mkubwa. Uongozi wenu ndio umetufikisha hapa ambapo hadi hivi sasa Bunge letu halina migogoro yoyote. Nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Wabunge wote wa Bunge lako tukufu kwa kuchangia kwa umahiri mkubwa mijadala inayoendelea ya bajeti za Wizara mbalimbali.

***9. Mheshimiwa Spika****,* napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Makamu Mwenyekiti Dkt. Christine G. Ishengoma (Mb) kwa maoni, ushauri na ushirikiano mkubwa walitupatia wakati wote wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2018/2019. Naishukuru Kamati kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Kilimo ya mwaka 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2018/2019 katika vikao vyake vilivyofanyika Dodoma tarehe 20 na 21 Machi, 2018. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa yamezingatiwa katika bajeti hii, na tunaahidi kuipatia Kamati ushirikiano wa kila namna ili kilimo nchini kiweze kubadilika kufikia malengo tuliyojiwekea.

**10. Mheshimiwa Spika,** natoa shukrani na pongezi za pekee kwa wananchi wa Jimbo langu la Buchosa kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Aidha, nawapongeza na kuwapa shime kwa juhudi wanazofanya katika kujiletea maendeleo wao wenyewe na maendeleo ya jimbo lao.

**11. Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kuwapongeza Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), na Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Philip Mpango (Mb) kwa hotuba zao zilizotoa ufafanuzi kuhusu hali ya uchumi kwa mwaka 2017, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2018/2019 ambazo

zimeelezea kwa muhtasari hali ya kilimo kilivyo hivi sasa na mwelekeo kwa mwaka ujao.

## 1.1 HALI YA KILIMO NCHINI

12. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Kilimo nchini imeendelea kuwa ni Sekta muhimu katika maendeleo ya uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla hususan katika wakati huu tunapojizatiti kufikia uchumi wa viwanda. Sekta hiyo imeendela kuimarika kwa kuchangia Pato la Taifa hadi asilimia 30.1 kwa mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 29.2 mwaka 2016. Mazao ya kilimo ni malighafi muhimu sana katika viwanda kwani huchangia asilimia 65 ya malighafi zinazohitajika viwandani. Kilimo kinaendelea kutoa fursa nyingi za ajira kuliko Sekta zote, ambapo asilimia 65.5 ya Watanzania wameajiriwa na kujiajiri katika Sekta hiyo. Aidha, inachangia zaidi ya asilimia 100 ya chakula kinachopatikana nchini na hivyo kusaidia kudhibiti mfumuko wa bei na kuimarisha ushindani wa uchumi.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini ya awali ya viashiria vya ukuaji wa Sekta ya Kilimo nchini kwa msimu wa kilimo 2017/2018, inaonesha kuendelea kuimarika ikilinganisha na msimu wa 2016/2017.

Katika kipindi cha nusu ya mwaka, kuanzia Julai hadi Desemba 2017, ukuaji wa Sekta ya Kilimo ulifikia asilimia 3.1 ukilinganisha na asilimia 2.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2016.

## 1.2 HALI YA UPATIKANAJI WA CHAKULA

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Tathmini ya Awali ya Uzalishaji wa Mazao ya Chakula nchini kwa msimu wa 2016/2017 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2017/2018 iliyofanyika mwezi Juni 2017 ilibaini kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2016/2017 ulifikia tani 15,900,864 ambapo uzalishaji wa nafaka utafikia tani 9,388,772 ikiwemo mahindi tani 6,680,758 na mchele tani

1,593,609. Uzalishaji wa mazao ya si nafaka ulifikia tani 6,512,092 kati ya hizo muhogo ni tani 1,341,755, viazi ni tani 2,007,972, mikunde tani 2,317,807 na ndizi tani 844,558.

***15. Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa chakula kwa msimu wa mwaka 2016/2017 ulipungua kwa kiasi cha tani 271,977 ukilinganishwa na tani 16,172,841 za mwaka 2015/ 2016. Upungufu huo ulitokana na uhaba wa mvua za vuli kwa mwaka 2016 pamoja na mtawanyiko mbaya wa mvua hizo katika maeneo yanayotegemea mvua za vuli. Aidha, mvua za msimu pamoja na mtawanyiko wake kwa mwaka 2017 pia haukuwa mzuri hivyo kupelekea mavuno kuwa hafifu.

***16. Mheshimiwa Spika,*** licha ya upungufu huo, upatikanaji wa chakula nchini umeendelea kuwa imara. Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2017/2018 ni tani 13,300,034 kati ya hizo, mahitaji ya nafaka ni tani 8,457,558 na yasiyo ya nafaka ni tani 4,842,476. Mahitaji hayo yakilinganishwa na uzalishaji yanaonesha uwepo wa ziada ya tani 2,600,831, ambapo kwa nafaka kuna ziada ya tani 931,214 na yasiyo ya nafaka tani 1,669,617. Hali hii inafanya Taifa kuwa na kiwango cha utoshelevu wa chakula cha asilimia 120 ikilinganishwa na kiwango cha utoshelevu cha asilimia 123 kwa mwaka 2016/2017. Kufuatia hali hii, mfumuko wa bei umepungua kufikia asilimia 6.2 ikilinganishwa na asilimia 7.0 uliokuwepo mwezi Desemba 2016. Hivyo, Serikali imeendelea kutoa vibali kwa wakulima na wafanyabiashara wanaosafirisha mazao ya chakula nje ya nchi, likiwamo zao la mahindi. Aidha, mazao yanayoharibika haraka (*perishables*) hayahitaji kupata kibali bali usafirishaji wa mazao hayo unatakiwa kufuata taratibu za kibiashara zilizopo kisheria. Ili kuboresha upatikanaji wa masoko ya mazao ya chakula, hususan mahindi, Serikali itaanzisha utaratibu wa kutoa vibali mipakani kwa mfumo wa kielektroniki na hivyo kuwezesha waombaji kupata huduma hiyo bila kulazimika kwenda Makao Makuu ya Wizara ya Kilimo.

***17. Mheshimiwa Spika,*** pamoja na Taifa kujitosheleza kwa chakula, bado kuna Halmashauri ambazo zina maeneo yenye upungufu wa chakula unaojirudia kila mwaka. Hali hii inapelekea kuwa na matatizo ya usalama wa chakula na lishe katika maeneo husika. Ili kukabiliana na changamoto hii, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – Idara ya Maafa, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa - FAO pamoja na wadau wengine wa masuala ya Usalama wa Chakula na Lishe imepanga kufanya Tathmini ya Kina ya Hali ya Usalama wa Chakula na Lishe katika maeneo yenye uhaba wa chakula mara kwa mara. Lengo ni kubaini sababu za msingi za tatizo hilo na kupendekeza hatua za kuchukuliwa katika kipindi cha muda wa kati na mrefu ili kukabiliana na matatizo hayo. Tathmini hiyo itafanyika katika kipindi cha mwezi Mei hadi Juni, 2018. Taarifa ya tathmini hii itatoa mwelekeo wa hali ya uzalishaji katika msimu wa 2017/2018 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2018/2019 hapa nchini. Hata hivyo, zipo dalili kuwa mavuno yatakuwa mazuri kwa maeneo mengi ya nchi licha ya kujitokeza kwa wadudu waharibifu, yaani viwavi jeshi vamizi (*American Fallarmy Worm*).

## 1.3 MAENDELEO YA USHIRIKA

***18. Mheshimiwa Spika,*** Ushirika ni Sekta mtambuka inayohusisha Sekta mbalimbali zikiwemo Kilimo, Ufugaji, Uvuvi, Madini, Viwanda, Nyumba na Fedha (Ushirika wa Akiba na Mikopo na Benki) ambazo zinagusa wananchi wengi zaidi. Kutokana na umuhimu wa Sekta hii, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeendelea kuwezesha na kuimarisha Ushirika ili wananchi wengi zaidi waweze kunufaika na fursa zinazopatikana kupitia Ushirika kwa lengo la kuchangia katika kuongeza kipato kwa wananchi wengi hususan waliopo vijijini.

***19. Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa mwaka 2017/2018 ulilenga kutatua changamoto zinazoikabili Sekta ya Ushirika. Maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2017/2018 yalikuwa ni kuhuisha Sera ya Maendeleo ya Ushirika; kujenga uwezo wa Tume

katika kutoa huduma kwa wadau; kuhimiza misingi ya utawala bora na uwajibikaji katika Vyama vya Ushirika; kufanya uhamasishaji kwa kushirikisha Wizara za kisekta, Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine; kuboresha mifumo ya upatikanaji na usimamizi wa rasilimali; na kujenga na kuimarisha uwezo wa kiuchumi katika Vyama vya Ushirika.

**20. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Tume imefanya uhamasishaji wa wananchi kujiunga au kuanzisha Vyama vya Ushirika ambapo hadi kufikia Desemba 2017 vyama vipya 394 vilisajiliwa na kufanya idadi ya vyama kufikia 10,990 kutoka 10,596 vilivyokuwepo Machi 2017. Vyama hivi vinakadiriwa kutoa ajira mpya kwa wananchi takribani 1,182. Katika kipindi hicho, wanachama wapya 385,295 walijiunga au kuanzisha Vyama vya Ushirika na kufanya idadi ya wanachama kuongezeka kutoka 2,234,016 hadi kufikia 2,619,311.

***21. Mheshimiwa Spika,*** Tume imeendelea kuvijengea na kuimarisha uwezo wa kiuchumi Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) ambapo jumla ya Shilingi bilioni 902 zilitolewa kwa wanachama kama mikopo kwa mwaka 2017 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 855.29, zilizotolewa mwaka 2016. Vilevile, SACCOS zimeweza kuongeza akiba za wanachama kufikia Shilingi bilioni 561 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 331 kwa mwaka 2016. Aidha, SACCOS zimeweza kuongeza amana hadi kufikia Shilingi bilioni 53 kwa mwaka 2017/18 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 47 zilizokuwepo mwaka 2016/2017.

***22. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho,Vyama vya Ushirika wa Mazao (*Agricultural Marketing Cooperative Sociteies – AMCOS*) vimeendelea kutoa huduma mbalimbali kwa wakulima ikiwemo huduma za ugani, usambazaji wa pembejeo, ukusanyaji na uuzaji wa mazao. Wizara kupitia Tume imeendelea kuhimiza ukusanyaji na uuzaji wa mazao makuu ya biashara kupitia Vyama vya Ushirika. Utaratibu huu umesaidia katika kuongeza kiasi cha makusanyo ya mazao kupitia Vyama vya Ushirika, uhakika wa soko na kuimarika kwa bei za mazao kupitia minada.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imeendelea kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika mazao mbalimbali yakiwemo pamba, kahawa, ufuta na kakao ili wakulima waweze kunufaika na bei kama ilivyo katika zao la korosho ambapo katika msimu wa 2017/2018, vyama viliuza korosho na kuwalipa wakulima jumla ya Shilingi bilioni 1,290.00 ikilinganishwa na malipo ya Shilingi bilioni 809.18 msimu wa 2016/2017.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Ushirika bado unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo ubadhirifu wa mali za vyama vya Ushirika unaofanywa na baadhi ya viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika wasio waaminifu na uelewa mdogo wa wanachama juu ya haki, wajibu na majukumu yao kama wamiliki wa vyama. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali inaimarisha usimamizi kwa kuongeza kasi ya ukaguzi wa vyama, kuwajengea uwezo viongozi na kutoa mafunzo kwa wanachama kuhusu haki na wajibu wao. Aidha, Serikali imeendelea kufuatilia ili kuzirudisha mali zote za vyama vya Ushirika zilizoporwa na watu binafsi au taasisi pamoja na kuwachukulia hatua za kinidhamu wahusika wa ubadhirifu.

## 1.4 MWELEKEO NA MALENGO YA SEKTA YA KILIMO

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Kilimo inatekeleza malengo yake kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Programu hii inatekeleza malengo ya Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Nchini (*Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan – TAFSIP*) ikiwa na lengo mahsusi la kuhakikisha kuwa Kilimo kinakua kwa asilimia 6 kwa mwaka kuendana na malengo ya Programu Kabambe ya Maendeleo ya Kilimo Barani Afrika (*Comprehensive Africa Agriculture Development Program – CAADP*).

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia haya, mwelekeo wa Sekta ya kilimo ambao Wizara itausimamia kwa dhati kuanzia sasa hadi mwaka 2025 ni kuleta mageuzi

(transformation) ya kilimo kutoka mtazamo uliopo wa kilimo cha kujikimu kufikia uendeshaji wa kilimo kwa mfumo wa kibiashara. Lengo la mageuzi haya ni kuhakikisha kuwa shughuli za kilimo zinakuwa na manufaa kwa nchi na wakulima kuendana na dhamira yetu ya kufikia uchumi wa kati na wa viwanda. Itakumbukwa kwamba sekta ya kilimo inaajiri zaidi ya asilimia 65 ya nguvu kazi nchini. Aidha, asilimia 80 ya Watanzania maskini wanaishi kwa kutegemea kipato na maisha yao kutokana na shughuli za kilimo.

***27.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mantiki hiyo, mageuzi tunayotaka kuyafanya ni ya kuondoa asilimia 80 ya Watanzania walio katika lindi la umaskini, au kiasi cha watu milioni 10 ifikapo 2025. Malengo mengine ya mageuzi haya ni pamoja na kuhakikisha tunajitosheleza kwa chakula ikiwa ni pamoja na kujenga mfumo imara wa hifadhi ya chakula kitaifa na ugavi ili kuruhusu ubobevu (specialization); kuongeza uzalishaji na tija ya kilimo hasa kwa mazao ya biashara na mazao ghafi kwa uzalishaji viwandani ili kuchochea uwekezaji katika mnyororo mzima wa thamani wa uzalishaji wa mazao hayo kuendeshwa kibashara. Pia, mageuzi hayo yatatusaidia kuongeza uwezo, kama nchi, wa kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi ambayo yamekuwa na athari sana kwenye kilimo nchini. Kuhusiana na hili, msukumo umewekwa katika kuongeza miundombinu ya uvunaji maji na hifadhi ya maji; umwagiliaji na elimu ya matumizi jadidifu ya maji na hifadhi ya ardhi.

***28.*** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba sasa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

## 2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2017/2018 NA MPANGO KWA MWAKA 2018/2019 (FUNGU 43)

### 2.1 Mapato na Matumizi ya Fedha katika Kipindi cha mwaka 2017/2018 (Fungu 43)

### 2.1.1 Makusanyo ya Maduhuli

***29.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Kilimo kwamwaka 2017/2018 ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi **2,015,010,000** kupitia Fungu 43 kutokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo tozo na ada za huduma za ukaguzi wa mazao ya kilimo yanayoingia na yanayosafirishwa nje ya nchi; tozo zinazotokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni; kodi za majengo ya ofisi; na makato ya mishahara ya

**21.** watumishi ambao wanakaa kwenye nyumba za serikali. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 Wizara ilikusanya jumla ya Shilingi **1,708,724,841.68** sawa na asilimia **84.80** ya makadirio na Wizara inaendelea kukusanya maduhuli hayo.

### 2.1.2 Fedha Zilizoidhinishwa

***30.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Kilimo kupitia Fungu 43 ilitengewa jumla ya Shilingi **214,815,759,000.** Kati ya Fedha hizo, Shilingi **64,562,759,000** ni Fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi **150,253,000,000** ni Fedha za maendeleo.

### 2.1.3 Matumizi ya Bajeti ya Kawaida

***31.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, fedha za matumizi ya kawaida zilizopitishwa kwa Fungu 43 ni Shilingi **64,562,759,000**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **29,868,879,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Wizara, Shilingi **15,199,054,000** ni mishahara ya watumishi wa Bodi na Taasisi na Shilingi **19,494,826,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, Kati ya fedha za matumizi mengineyo, Shilingi **7,889,038,800** Ruzuku kwa Mashirika ya ndani na Shilingi **11,605,787,130** ni kwa ajili ya matumizi ya Idara, Vitengo na Vituo vya Wizara.

***32.*** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 jumla ya Shilingi **36,069,819,172** za matumizi ya kawaida kati ya Shilingi **64,562,759,000** zilikuwa zimetolewa sawa na asilimia **55.87** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha zilizotolewa, Shilingi **26,417,055,451** ni mishahara na Shilingi

**9,652,763,721** ni za matumizi mengineyo. Aidha, fedha zilizotumika ni Shilingi **33,054,942,776.63** sawa na asilimia **91.64** ya fedha zilizotolewa.

#### 2.1.4 Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo

***33.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa 2017/2018, Wizara ya Kilimo ilitengewa jumla ya Shilingi **150,253,000,000** kupitia Fungu 43 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **59,600,000,000** ni Fedha za ndani na Shilingi **90,653,000,000** ni Fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 Shilingi **27,231,305,232.69** zimetolewa sawa na asilimia **18** ya Fedha zilizoidhinishwa. Matumizi ni Shilingi **27,231,305,232.69** sawa na asilimia **100.00** ya Fedha zilizotolewa. Kati ya Fedha hizo Shilingi **25,576,120,000** ni Fedha za ndani na Shilingi **1,655,185,232.69** ni Fedha za nje.

### 2.2 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2017/2018 na Mpango kwa Mwaka 2018/2019 (Fungu 43)

***34.*** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2017/2018, umezingatia malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021); Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals - SDGs*); *Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan (TAFSIP)*; na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020. Malengo hayo yalitekelezwa kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Program – ASDP II* ), na Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (*Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT*). Maeneo mengine yaliyozingatiwa ni pamoja na masuala mtambuka yakiwemo Jinsia, Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi, UKIMWI na Ajira ya Vijana katika Sekta ya Kilimo.

***35.*** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, kupitia Programu ya ASDP II, Sekta Binafsi ambayo ni nguzo muhimu katika maendeleo ya Sekta ya Kilimo imeshirikishwa kikamilifu katika

kuongeza uzalishaji na tija, uongezaji wa thamani wa mazao, upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo, masoko kwa ajili ya mazao na bidhaa za Kilimo na kutoa huduma mbalimbali ikiwemo huduma za utafiti, mafunzo na ugani.

***36. Mheshimiwa Spika,*** katika kufanikisha majukumu yake, Wizara imetekeleza Maeneo ya Kipaumbele nane (8) kupitia Fungu 43 katika Idara, Vitengo, Asasi na Taasisi za Wizara. Maeneo ya kipaumbele yaliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:

i. Kusimamia Matumizi Endelevu ya Ardhi ya Kilimo na Maji

ii. Kuongeza kilimo chenye tija kwa kuongeza upatikanaji na utumiaji wa pembejeo za kilimo (mbolea, mbegu bora, zana za kilimo na viuatilifu vya kudhibiti wadudu, magugu na magonjwa ya mimea) na kuboresha mfumo wa utafiti na utoaji wa matokeo ya utafiti kwa wadau, huduma za ugani na kusambaza teknolojia za kilimo juu ya uzalishaji wa mazao

iii. Kuimarisha usimamizi wa mazao kabla na baada ya mavuno na kuongeza thamani ya mazao na upatikanaji wa masoko kwa mazao yote ya wakulima

iv. Kuratibu utekelezaji wa Mikakati ya Maendeleo ya Mazao na kuimarisha huduma za udhibiti

v. Kuunda na kupitia Sera za Sekta ndogo ya Mazao na Sheria zake ili kuweka Mazingira mazuri ya Uwekezaji katika Kilimo

vi. Kuimarisha Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini ya Sekta

vii. Kuimarisha Masuala Mtambuka (Vijana katika Kilimo, Jinsia, Mazingira, Lishe na UKIMWI).

viii. Kuendelea kutekeleza Mpango wa Serikali kuhamia Dodoma

***37. Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka 2017/2018 na mpango kwa mwaka 2018/2019 kwa kuzingatia vipaumbele ni kama ifuatavyo;

### 2.2.1 Kusimamia Matumizi Endelevu ya Ardhi ya Kilimo na Maji

***38. Mheshimiwa Spika,*** Matumizi Endelevu ya Ardhi ya Kilimo na Maji ni pamoja na upimaji wa ardhi yote ya kilimo; usimamizi wa ubora wa ardhi na maji na hifadhi ya mazingira kwa ajili ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuandaa miongozo na kutoa elimu juu ya teknolojia za hifadhi ya udongo na maji mashambani.

***39. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Programu ya Kusaidia Umilikishaji wa Ardhi kwa Wananchi (*Land Tenure Support Programme*) ilishirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kuandaa Mipango ya Matumizi Bora ya vijiji vinavyotekeleza programu hiyo katika Halmashauri za Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi. Kazi hiyo iliwezesha kutolewa kwa Hati za Hakimiliki za Kimila 4,968 kwa wananchi.

***40. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji imeandaa taarifa ya migogoro ya ardhi yenye mapendekezo ya utatuzi wake; kutoa mafunzo kwa wakulima 8,800 wa Vijiji vya Sigara, Lumeji, Kasoli, na Ng'esha katika Wilaya ya Magu Mkoani Mwanza juu ya kilimo cha makinga maji; upandaji wa miti na kilimo cha matuta katika kudhibiti mmonyoko wa ardhi mashambani kupitia Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria (LVEMP II);

kuendelea na mradi wa Matumizi Endelevu ya Ardhi katika Lindimaji za Mito ya Ruvu na Zigi iliyo katika mikoa ya Morogoro na Tanga mtawalia kwa kufanya utambuzi wa wilaya ambazo wataalamu wa ugani watapewa mafunzo ya teknolojia za hifadhi ya udongo na maji mashambani; kupitia mwongozo wa Upangaji wa Mipango ya matumizi ya Ardhi ya Vijiji na kuandaa Mkakati wa kukabiliana na changamoto za Matumizi bora ya Ardhi nchini.

***41. Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeshirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Sekta binafsi kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji katika shamba la miwa la Mkulazi lenye hekta 60,000 ambalo kampuni ya Mkulazi Holding Company LTD imewekeza katika kuzalisha miwa na sukari. Ili kuwanufaisha wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba hilo Wizara imewezesha kutolewa kwa hati za Hakimiliki za Kimila 400 kwa wananchi wa Kijiji cha Chanyumbu. Aidha, Shamba la kilimo cha miwa la Bagamoyo lenye hekta 10,000 limetolewa kwa Kampuni ya Bakharesa Group of Companies kwa ajili ya kuwekeza katika kilimo cha zao la miwa na kuzalisha sukari. Shamba lingine ni Mbigiri lenye ekari 12,000 ambalo kampuni ya Mkulazi Holding Company LTD inashirikiana na Magereza katika kuliendeleza kwa kilimo cha miwa na kusindika sukari.

***42. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara itatekeleza mpango madhubuti wa kujenga Mabwawa katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Aidha, Wizara itajenga bwawa la Kalege na miundombinu ya umwagiliaji inayotarajiwa kumwagilia takriban hekta 11,700 na litahudumia Halmashauri za Bukoba Vijijini na Misenyi. Bwawa hilo litakuwa na uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo 2,780,000 ambapo litasaidia upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo, ufugaji wa samaki (*aquaculture*) na kuchangia kupunguza uharibifu wa vyanzo vya maji (*degraded sub-catchments*) katika bonde la Mto Ngono Mkoani Kagera. Vilevile, bwawa hilo litatumika kwa ajili ya uhifadhi wa maji wakati wa msimu wa kiangazi, kuboresha ustahimilivu wa

mabadiliko ya tabia nchi, kuzuia mafuriko ambayo yanaathiri jumla ya hekta 3,555 (hekta 2,901 mashamba makubwa na hekta 654 mashamba madogo) na uzalishaji wa megawati 2.46 za umeme.

**43. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia itaendelea kusimamia matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo na maji katika maeneo mbalimbali nchini kote kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine wa kilimo. Wizara itafanya tathmini ya ardhi ya kilimo na hali ya uchumi wa kijamii, utunzaji mazingira, na uandaaji wa mpangokina wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo ya kilimo yaliyopo kwenye pori tengefu la Loliondo na mashamba ya wakulima wadogo wanaozunguka mashamba saba ya uwekezaji ya Lukulilo, Mkulazi, Pangani, Kitengule, Muhoro,Tawi na Bagamoyo.

**44. Mheshimiwa Spika,** Vilevile Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kutambua maeneo mapya ya kilimo kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo cha kibiashara na kuwezesha Vijana kujiajiri katika kilimo. Mikoa itakayohusika katika kazi hii ni Rukwa, Katavi, Lindi, Ruvuma, Kigoma, Kagera, Mtwara, Geita, Tabora, Singida na Morogoro. Wizara pia itaendelea kuimarisha matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo kwa kuhimiza matumizi ya teknolojia za hifadhi ya udongo na maji mashambani katika lindimaji za mto Wami/Ruvu na Pangani na kueneza teknolojia mbalimbali za matumizi bora ya ardhi ya kilimo kupitia maonesho ya kitaifa NaneNane, Siku ya Chakula Duniani na Wiki ya Utumishi wa Umma.

**45. Mheshimiwa Spika,** Wizara itashirikiana na wadau mbalimbali kukamilisha rasimu ya Mpango Kabambe wa Matumizi Endelevu ya Ardhi ya Kilimo na kuboresha rasimu ya Sheria ya Rasilimali za Ardhi ya Kilimo ili ardhi ya kilimo iweze kutumika ipasavyo na kulindwa. Aidha, Wizara itashirikiana na wadau wengine katika kusuluhisha na kuandaa mikakati endelevu ya kuzuia migogoro baina ya wakulima na watumiaji wengine wa ardhi ikiwa ni pamoja

na kupima maeneo yaliyo chini yake kwa ajili ya kupata Hatimiliki.

### 2.2.2 Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo

***Mbolea***

***46.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa mbolea ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 tani 435,178 zimeingizwa nchini na kusambazwa katika mikoa mbalimbali kwa matumizi ya wakulima. Kiasi hicho kilichoingizwa ni sawa na asilimia 89.73 ya wastani wa mahitaji ya tani 485,000 kwa mwaka. Kati ya mbolea iliyoagizwa kutoka nje ya nchi, tani 233,979.16 ziliagizwa kwa Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja (BPS) ambapo tani 88,945 ni mbolea ya kupandia (DAP) na tani 145,034.16 ni mbolea ya kukuzia (UREA).

***47.*** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati wa utekelezaji wa mfumo wa BPS changamoto mbalimbali zilijitokeza na kusababisha upungufu au ukosefu wa mbolea kwenye baadhi ya maeneo kama vile mikoa ya Rukwa, Ruvuma (Songea) na Katavi. Changamoto hizo ni pamoja na baadhi ya wafanyabiashara wa mbolea kutoridhika na bei elekezi iliyotolewa na Serikali; mtaji mdogo wa wafanyabiashara; kupanda kwa gharama za usafirishaji wa mbolea kulikosababishwa na mvua zilizonyesha na hivyo kuathiri miundombinu ya barabara za vijijini; na utoroshwaji wa mbolea kwenda nchi jirani za Zambia na Malawi kulikosababishwa na kushuka kwa bei ya mbolea nchini.

***48.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuharakisha usambazaji wa mbolea katika maeneo yaliyokuwa na upungufu, Wizara ilichukua hatua ya dharura ya kusambaza mbolea kwa kutumia magari ya Jeshi la Wananchi Tanzania. Aidha, Wizara ilitoa ufafanuzi kwa Wakuu wote wa Mikoa na Wilaya kuangalia uhalisia wa gharama za usafirishaji na kuwaruhusu wafanyabiashara (wafanyabiashara wadogo wanaopeleka mbolea vijijini) kuongeza bei ya mbolea endapo ongezeko

la gharama ya usafiri litajitokeza ili mbolea ifike kwa wakulima kwa wakati. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara wa mbolea hususan walioko katika ngazi ya Halmashauri kuhusu utaratibu wa kupata mbolea na jinsi wanavyoweza kununua kwa pamoja kutoka kwa wasambazaji wakubwa ili kupunguza gharama mbalimbali za usafirishaji.

***49.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kutumia Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja *(Bulk Procurment system-BPS)* ambao utahakikisha upatikanaji wa mbolea kwa wingi na kwa bei nafuu. Kwa kutumia mfumo huo, Wizara itawezesha upatikanaji na matumizi ya tani 300,000 za mbolea. Kati ya hizo tani 100,000 ambayo tayari uagizaji na uingizaji wake umeanza kwa tani 32,000 na hivyo uhakika wa upatikanaji wake wakati wote wa msimu ujao wa kilimo ni mbolea ya kupandia (DAP) na tani 200,000 ni mbolea ya kukuzia (UREA). Aidha, Wizara itahamasisha wafanyabiashara wa mbolea kujenga maghala makubwa kwa ajili ya kuhifadhi mbolea *(strategic storage facilities*) hususan katika maeneo yenye mahitaji makubwa ili kuhakikisha wakulima wanapata mbolea kwa wakati wote. Vilevile, Wizara itashirikisha wadau wa maendeleo kama *African Fertilizer and Agribusiness Partnership (AFAP)* kuanzisha miradi yenye lengo la kusaidia ujenzi wa maghala.

### *Mbegu Bora na Viuatilifu*

***50.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018 upatikanaji wa mbegu bora umefikia tani 51,700.51 ikilinganishwa na tani 28,278.2 za mwaka 2016/2017. Kiasi hicho cha mbegu bora kinatokana na tani 26,112.69 zilizozalishwa hapa nchini, tani 16,277.7 zilizoingizwa nchini na tani 9,310.12 zikiwa ni bakaa ya msimu wa 2016/2017. Kati ya mbegu bora zilizozalishwa nchini tani 18,500 ni mbegu za Pamba.

***51.*** ***Mheshimiwa Spika*** Wizara kupitia Bodi ya Korosho imezalisha miche bora ya korosho 8,178,709 na kusambaza kwa wakulima wa mikoa ya Mtwara (1,559,407), Lindi (4,027,951), Ruvuma (819,370), Dodoma (753,662), Singida (956,419) na Tabora (610,900). Kati ya miche ya korosho iliyozalishwa miche iliyobebeshwa (*grafted*) ni 738,103 na miche isiyobebeshwa ni 7,440,606. Aidha, usambazaji wa miche ya korosho unaendelea katika mikoa ya Pwani, Tanga, Morogoro, Katavi, Njombe, Iringa, na Kilimanjaro. Vilevile, miche bora ya Chai 11,560,000 imezalishwa kupitia Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA) kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo. Miche bora ya kahawa 1,163,758 imezalishwa na kusambazwa kwa wakulima kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kahawa kupitia vituo vyake vidogo vya Lyamungu (Kilimanjaro), Ungani (Mbinga), Maruku (Kagera), Mwayaya (Kigoma), Mbimba (Mbozi) na Sirari (Tarime).

**52.** Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Pamba ilinunua na kusambaza kwa wakulima chupa milioni 7.3 za viuadudu vyenye thamani ya Shilingi bilioni 29.2 na vinyunyizi 16,500 vyenye thamani ya shilingi milioni 495 na kukarabati vinyunyizi 6,000 vilivyokuwa kwa wakulima.

***53.*** ***Mheshimiwa Spika***, Sekta Binafsi imeingiza kutoka nje kiasi cha tani 149.03 za mbegu za alizeti. Miongoni mwa aina hizo za mbegu za alizeti ni mbegu chotara; *NSFH 36, NSFH 145, AGUARA 4* na *HYSUN 33* zilizoidhinishwa nchini na Kamati ya Taifa ya Mbegu mwaka 2015 zikiwa na sifa ya utoaji mavuno ya tani kati ya 2.5-3.6 kwa hekta ukilinganisha na tani 1-2 kwa hekta kwa mbegu aina ya *Record* iliyoidhinishwa nchini zaidi ya miaka 30 iliyopita.

***54.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara itawezesha upatikanaji na matumizi ya tani 40,000 za mbegu bora; kuzalisha miche bora ya chai milioni 10 na miche bora ya kahawa milioni 12; kusambaza tani 8,600 na

lita 9,800 za viuatilifu; na ekapaki 7,000,000 za viuatilifu vya zao la pamba.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, Wizara kwa kushirikiana na *"Bill and Melinda Gates Foundation"* itakamilisha maandalizi ya Mfumo wa Taifa wa kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora. Mfumo huo utahusisha uboreshaji wa uzalishaji wa mbegu mama katika vituo vya utafiti; kuimarisha na kuboresha miundombinu ya mashamba ya ASA yanayozalisha mbegu zilizothibitishwa; kujenga uwezo wa Taasisi ya Uthibiti wa Ubora wa Mbegu (TOSCI); na kuboresha mfumo wa menejimenti ya upatikanaji, usambazaji na matumizi ya mbegu bora nchini. Aidha, Wizara itahakikisha sekta binafsi inashiriki kikamilifu katika Tasnia ya mbegu ili kuongeza upatikanaji wa mbegu bora nchini. Vilevile, Wizara itafuatilia na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi ya pembejeo za kilimo kwenye Mikoa na Halmashauri nchini. Wizara itafanya tathimini ya mahitaji halisi ya mbegu kwa mwaka nchini.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19 kiuatilifu aina ya Sulphur pamoja na Vifungashio vya korosho (magunia) havitatolewa kwa njia ya ruzuku kama ilivyokuwa msimu wa Kilimo 2017/18. Wakulima watauziwa kwa bei ambayo itatangazwa na Bodi ya Korosho ili wakulima na wadau wa Korosho waweze kufahamu utaratibu wa kupata pembejeo hiyo pamoja na magunia kwa wakati na kwa bei itakayopitishwa. Aidha, Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika wa Korosho na Benki ya NMB imekamilisha mchakato wa uagizaji wa pembejeo za korosho ikiwemo kuingia mikataba na wazabuni ambao kwa ujumla wao wataleta salfa ya unga tani 35,000 na viuatilifu vya maji lita 520,000. Hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Mei, 2018 kiasi cha pembejeo zinazohitajiwa zitakuwa zimeshapokelewa. Aidha, Serikali inasimamia upatikanaji wa magunia ya kuhifadhia Korosho kupitia makubaliano kati ya Vyama vya Ushirika, Benki na wazalishaji wa magunia.

### 2.2.3 Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea na Mazao

***Udhibiti wa visumbufu vya milipuko***

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya katika Mikoa kwa kununua jumla ya kilo 820 za kuua panya (Rodenticide), lita 6,000 za kuua kwelea kwelea (Fenthion 60% ULV), lita 10,000 za kuua kiwavijeshi vamizi (Duduba) na 500 za kivutia inzi wa matunda (Methyl eugenol) vyote vikiwa na thamani ya Shilingi milioni 700.

**58.** ***Mheshimiwa Spika***, Hadi kufikia mwezi April 2018, ndege waharibifu aina ya kwelea kwelea walidhibitiwa katika Wilaya za Mbarali, Moshi Vijijini, Arumeru, Simanjiro, Kishapu, Nzega, Igunga, Kahama, Msalala, Shinyanga vijijini, Sengerema na Manispaa ya Dodoma. Katika kufanikisha kazi hiyo, Jumla ya lita 2,425 kati ya 6,000 za kiuatilifu aina ya *Fenthion 60% ULV* zilitumika kuangamiza takriban kweleakwelea milioni 61.7.

**59.** ***Mheshimiwa Spika***, Savei ya kubaini kiwavijeshi vamizi (*Fall armyworm*) imefanyika katika Mikoa ya Morogoro, Rukwa, Mara, Songwe, Mbeya na Tanga. Jumla ya wataalam 350 kutoka Mikoa ya Njombe, Mbeya, Katavi, Rukwa, Pwani, Morogoro, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Arusha, Simiyu, Geita, Mwanza na Kagera walipatiwa mafunzo ya kutambua na kudhibiti viwavijeshi vamizi. Aidha, Wizara imepokea jumla ya mitego ya nondo wa kiwavijeshi vamizi 305, ambapo mitego 169 imesambazwa katika Mikoa ya Mbeya (34), Songwe (24), Shinyanga (6), Arusha (2), Dar es Salaam (25), Mwanza (4), Tabora (10), Iringa (10), Morogoro (10), Manyara (10), Kilimanjaro (10) na Rukwa (24). Mitego 136 iliyobaki inaendelea kusambazwa katika Mikoa kulingana na mahitaji. Vilevile, savei ya kubaini nzige wekundu ilifanyika katika mbuga za mazalio ya nzige hao katika maeneo ya Ziwa Rukwa, Iku/Katavi, Malagarasi, Wembere na Bahi.

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, Udhibiti wa panya umefanyika kwa kushirikiana na Wilaya za Mvomero, Chalinze/Bagamoyo, Handeni, Kilindi, Kilombero, Ulanga, Malinyi, Morogoro vijijini, Kilosa, Songwe na Korogwe. Jumla ya vijiji 221 na kaya 18,382 zilipewa kiuatilifu kilo 1,331 ya sumu ya panya. Kati ya hizo kilo 511 zilinunuliwa na Halmashauri za Wilaya

***Udhibiti wa visumbufu kibaiolojia.***

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao kibaiolojia umeendelea kufanyika ambapo wadudu 12,000 rafiki wa mkulima (*Fopius arisanus* na *Diachasmimorpha longicaudata)* wamezalishwa na kusambazwa katika maeneo ya Wilaya za Kibaha na Mkuranga Mkoani Pwani ili kudhibiti Inzi wa matunda. Aidha,Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha ICIPE - Kenya imetoa elimu kwa wakulima 100 na maafisa ugani 25 kutoka Wilaya za Kibaha, Bagamoyo na Mkuranga kuhusu udhibiti wa Inzi vamizi wa matunda na mboga ambapo wakulima waliopata mafunzo hayo walipewa mitego, chambo na kiuatilifu ili kudhibiti inzi vamizi katika maeneo yao.

**62.** ***Mheshimiwa Spika***, kituo cha kudhibiti visumbufu kibaiolojia killichopo Kibaha-Pwani kimezalisha na kutunza wadudu marafiki aina ya Mbawakavu (*Neochetina eichhoniae* na *Neochetina bruchi*) kwa ajili ya kudhibiti magugu maji pamoja na manyigu (*Apoanagyrus lopezi)* kudhibiti Kidung'ata wa muhogo (*Cassava mealybug*). Pia, Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Kimataifa cha ICIPE imetoa mafunzo ya matumizi ya Teknolojia ya mimea inayodhibiti funza wa mabua (*push pull*) na kiduha (*striga*) kwenye zao la Mahindi na Mtama kwa vijiji 7 katika Wilaya za Mvomero na Morogoro ambapo mashamba darasa 29 yameanzishwa. Wizara imetoa mafunzo ya udhibiti wa visumbufu vya Pamba kwa wakulima katika Halmashauri za Sengerema, Kwimba, Bunda, Igunga, Nzega,Chato, Musoma, Misungwi, Itilima, Busega, Bariadi, Meatu, Maswa, Geita, Bukombe, Mbogwe, Nyang'hwale, Kishapu na Maswa.

***Kueneza Elimu ya Udhibiti Husishi Nchini (Integrated Pest Management – IPM)***

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa mafunzo kuhusu Udhibiti Husishi ambapo Maafisa Kilimo 30 kutoka Mkoa wa Mbeya walipewa mafunzo juu ya Udhibiti Husishi (IPM). Aidha, wakulima wa Wilaya za Misungwi, Kwimba, Bariadi na Iramba wamepewa mafunzo ya Udhibiti Husishi kwa zao la pamba kupitia Mashamba Darasa *(Farmers Field School-FFS)*. Vilevile, uhamasishaji wa udhibiti wa mdudu mpya wa nyanya *(Tuta absoluta)* kwa njia ya IPM umefanyika kwenye Mikoa ya Kanda ya Kaskazini. Pia, Wizara kwa kushirikiana na FAO imechapisha vitabu 1,000 vya mwongozo wa Udhibiti Husishi kwa mazao ya nyanya, migomba na matikiti maji.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuviwezesha Vituo vya Kanda za Afya ya Mimea na Vituo Maalum vya Afya ya Mimea (*Kibaha Bio Control, Morogoro Rodent Control,* Kilimo Anga) ili vitoe huduma bora ya udhibiti wa visumbufu vya mazao na mimea. Vilevile, Wizara imethibitisha na kutoa vyeti vya uingizwaji na usafirishwaji wa mazao ya nafaka, bustani na mbegu za mafuta. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya vyeti 1,931 vya kuingiza mazao kutoka nje ya nchi na vyeti 3,287 vya usafi vya kusafirisha mazao nje ya nchi vimetolewa kwa wafanyabiashara wa mazao.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kudhibiti visumbufu vya mazao na mimea kwa kufanya tathmini ili kudhibiti milipuko ya nzige, kweleakwelea, panya, viwavijeshi na magonjwa ya mimea. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha vituo vya ukaguzi vya mipakani ili kudhibiti mazao yanayosafirishwa na yanayoingia nchini. Vilevile, kituo cha kudhibiti milipuko cha Kilimo Anga kitaendelea kuimarishwa ili kutoa huduma bora ya udhibiti wa milipuko ya visumbufu vya magonjwa ya mazao na mimea. Vilevile, kupitia ASDP II Wizara itavijengea uwezo na

kukarabati vituo 36 vya Afya ya Mimea na Vituo 8 vya Ukaguzi wa mazao mipakani.

***66.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kufanya udhibiti wa utoaji wa vyeti vya uingizwaji na usafirishwaji wa mazao ya nafaka, bustani na mbegu za mafuta. Aidha, Wizara itaendelea kuviwezesha Vituo vya Kanda za Afya ya Mimea na Vituo Maalum vya Afya ya Mimea (*Kibaha Bio Control, Morogoro Rodent Control, Kilimo Anga*) ili kutoa huduma bora ya udhibiti wa milipuko ya visumbufu vya magonjwa ya mimea na mazao. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa maafisa ugani na wakulima juu ya matumizi sahihi ya viuatilifu, kubaini milipuko, kudhibiti na itaendelea kuimarisha vituo vya ukaguzi vya mipakani ili kudhibiti mazao yanayosafirishwa na yanayoingia nchini.

***67.*** ***Mheshimiwa Spika***, ili kufanikisha udhibiti wa visumbufu vya milipuko hasa viwavi jeshi vamizi na panya, Wizara imezishauri Halmashauri za wilaya zote nchini kutenga bajeti kwa ajili ya udhibiti wa visumbufu hususan ununuzi wa viuatilifu. Aidha, Wizara itaendelea na jukumu la kutoa ushauri wa kitaalamu na mafunzo.

### 2.2.4 Zana za Kilimo

***68.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza matumizi ya zana bora za kilimo, Sekta binafsi imeingiza nchini zana bora za kilimo kwa lengo la kuongeza upatikanaji wake. Kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2017, jumla ya matrekta makubwa 1,604 na matrekta ya mkono 378 yaliingizwa nchini ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2016 ambapo jumla ya matrekta makubwa 900 na matrekta ya mkono 260 yaliingizwa nchini.

***69.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) wameunganisha matrekta makubwa 420 aina ya URSUS kati ya 822 katika kiwanda cha kuunganisha matrekta cha

TAMCO Kibaha. Matrekta hayo yataanza kuuzwa kwa wakulima kwa fedha taslimu. Aidha, Shirika linakusudia kusogeza huduma karibu na wakulima kwa kutumia *mobile services* kutoa huduma baada ya mauzo (vipuri, matengenezo na ushauri wa kiufundi).

**70.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushiriakana na Sekta Binafsi wametoa mafunzo ya uendeshaji, usimamizi na utunzaji wa mashine za kuvuna na usindikaji zao la mpunga kwa maopereta 150 na Maafisa Zana 12 kutoka kwenye skimu 14 za umwagiliaji. Mashine hizo zenye uwezo wa kusindika kati ya tani 10 hadi 30 kwa siku zitaongeza thamani na soko la zao la Mpunga katika skimu za Mombo (Korogwe), Kivulini (Mwanga), Mawemairo (Babati), Ipatagwa, Uturo na Mbuyuni (Mbarali), Lekitatu (Meru), Mkula (Kilombero), Musa Mwinjanga (Hai), Nakahuga (Songea), Magozi (Iringa vijijini), Kilangali (Kilosa), Mkindo (Mvomero) na BIDP (Bagamoyo).

**71.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itakamilisha Sheria ya Zana za Kilimo kwa ajili ya kulinda na kudhibiti ubora wa zana za kilimo, vipuri vinavyoingizwa na kuzalishwa nchini kwa kuzingatia mazingira. Vilevile, Wizara itafanya tathmini ya vituo vya zana za kilimo na mahitaji ya mashine na zana za kilimo katika Kanda 7 za Kilimo kwa ajili ya kuanzisha au kuhamasisha ukarabati wa vituo hivyo.

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia itasimamia na kufanya tathmini ya ufanisi wa mashine za kuvuna, kukata, kupura na kukoboa mpunga kwa matumizi endelevu katika skimu 14 ambazo ni: Mombo (Korogwe), Kivulini (Mwanga), Mawemairo (Babati), Ipatagwa, Uturo na Mbuyuni (Mbarali), Lekitatu (Meru), Mkula (Kilombero), Musa Mwinjanga (Hai), Nakahuga (Songea), Magozi (Iringa vijijini), Kilangali (Kilosa), Mkindo (Mvomero) na BIDP (Bagamoyo). Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) na Sekta Binafsi itabainisha, itatambua na kuhamasisha matumizi ya mashine za zana za kupanda, kupalilia na kuvuna mazao (viazi mviringo, mahindi na

muhogo) katika Kanda 2 za Kilimo. Vilevile, Wizara itahamasisha Sekta Binafsi kuanzisha viwanda vidogo na vya kati vya usindikaji muhogo katika Kanda 2 za Kilimo.

***73.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Sekta binafsi, itahamasisha uanzishwaji wa vituo viwili vya mfano vya kukodisha mashine za kilimo ili kuongeza huduma za zana za kilimo, kutengeneza ajira na kuongeza kipato katika Kanda 2 za Kilimo. Aidha, Wizara itafanya utambuzi, uanzishwaji na uhifadhi wa teknolojia sahihi za Kilimo Hifadhi katika Kanda ya Kati na Nyanda za Juu Kusini. Wizara pia kwa kushirikiana na Sekta binafsi itatoa mafunzo ya uendeshaji, utunzaji na usimamizi wa mashine na zana za kilimo kwa wamiliki ili kutoa huduma bora na zenye tija kwa wakulima wadogo.

### 2.2.5 Utafiti na Utoaji wa Matokeo ya Utafiti kwa Wadau

***74.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Vituo vya Utafiti na kwa kushirikiana na Taasisi Binafsi za kilimo imegundua na kuidhinisha mbegu bora mpya aina 25 (17 za Wizara na 8 za Taasisi Binafsi) za mazao ya pamba (2), maharage (9), mahindi (3), karanga (3), njugumawe (2), tumbaku (5) na mpunga (1) (**Kiambatisho Na.** 1). Aidha, mbegu hizo zilizoidhinishwa zitaanza kuzalishwa na ASA na Makampuni Binafsi kwa ajili ya kuzisambaza kwa wakulima.

***75.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imezalisha mbegu mama na mbegu za awali *(Breeder and Pre- basic seeds)* za mazao mbalimbali. Mbegu mama zilizozalishwa ni tani 5.2 ambazo ni pamba kilo 4,200 na mpunga kilo 1,050. Mbegu za awali zilizozalishwa ni tani 98.9 ambazo ni pamba kilo 23,240; viazi mviringo kilo 6,380; mpunga kilo 4,780; mahindi kilo 12,600; ulezi kilo 3,000, mtama kilo 1,300, soya kilo 2,200; maharage kilo 45,400; mazao mengine miche 5,150 ambayo ni migomba 1,750 na matunda 3,400; muhogo pingili 3,248,000 na viazi vitamu vipando 3,516,110.

**76.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia na CIMMYT inaendelea na utafiti wa ugunduzi wa mbegu za mahindi aina 6 zinazoonyesha kustahimili ugonjwa wa *Maize Lethal Necrosis Disease (MLND)*. Aidha, utafiti wa wadudu waharibifu wanaoshambulia zao la miwa umeendelea kwa kuzalisha wadudu marafiki wenye uwezo wa kudhibiti wadudu waharibifu, utafiti ukikamilika wadudu marafiki watasambazwa kwenye mashamba ya wakulima. Vilevile, utafiti wa magonjwa ya batobato na michirizi kahawia kwa zao la muhogo umeendelea kufanyika kwa njia ya baioteknolojia ili kupata aina za mbegu zinazostahimili ukame na magonjwa kwa mfano Mkuranga 1.

**77.** **Mheshimiwa Spika,** matokeo ya mbegu bora zilizogunduliwa na watafiti na kusambazwa kwa wakulima wa korosho yameonesha kuongezeka kwa uzalishaji kutoka tani 127,956 mwaka 2012/2013 hadi tani 265,238 mwaka 2016/2017 ikiwa ni pamoja na kuzingatia kanuni bora za kilimo, udhibiti wa wadudu na magonjwa, pamoja na kuimarika kwa bei ya korosho. Aidha, ulifanyika utafiti wa tathmini ya faida ya zao la nanasi Mkoani Pwani ambapo matokeo yameonesha kuwa mkulima akitumia mbegu na kanuni bora za kilimo cha nanasi hupata faida ya wastani wa Shilingi 15,000,000 kwa hekta kwa kuuzia shambani ambayo ni mara nne zaidi ya wakulima wasiolima kitaalam.

**78.** **Mheshimiwa Spika,** matokeo ya utafiti wa udongo uliofanyika katika kanda tano (5) za Ziwa, Mashariki, Magharibi, Nyanda za Juu Kusini na Kusini umefanikisha kutoa aina kuu mbili za mbolea mpya aina ya *Nitrogen Phospharus Sulphur* (NPS) na NPS Zinki ambazo zimesaidia kutoa mapendekezo sahihi ya matumizi bora ya mbolea kwenye maeneo yanayolima mazao ya mahindi, mpunga na maharage. Aidha, tathmini ya udongo kwa ajili ya kuzalisha zao la miwa imefanyika katika mashamba makubwa ya miwa ya Mkulazi (hekta 60,000), Mbigiri (hekta 12,000) na Bagamoyo (hekta 10,000) ambapo matokeo yameonyesha kuwa maeneo hayo yanafaa kwa kilimo cha miwa. Vilevile, Wizara imefanya mapitio ya ramani za udongo kwa

kutumia Mfumo wa Kijiografia (GIS) katika ukanda wa SAGCOT ili kurahisisha utambuzi wa maeneo yanayofaa kwa uwekezaji.

***79.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia vituo vyake vya utafiti itaendelea kugundua, kutathmini na kusambaza teknolojia bora za kilimo. Aidha, mbegu bora mama na mbegu za awali tani 10 zikiwemo nafaka na mikunde zenye sifa ya kutoa mazao mengi kwa kuzingatia mnyororo wa thamani; kiwango kikubwa cha virutubisho; ukinzani dhidi ya wadudu na magonjwa; zinazozalishwa kwa njia ya kawaida na kibiotekinolojia; zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi; na zenye ubora wa usindikaji viwandani zitazalishwa.

***80.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia itaendelea kugundua na kusambaza teknolojia bora kwa ajili ya kurutubisha na kuhifadhi udongo kwa mazao ya kipaumbele, itarekebisha mapendekezo ya matumizi bora ya mbolea yanayotumika sasa kwenye mazao mbalimbali yakiwemo mpunga na mahindi katika kilimo cha mvua. Aidha, Wizara itaendelea kuhakiki ramani katika mfumo wa kijiografia wa habari (GIS) kwa wilaya 5 katika ukanda wa SAGCOT zinazolenga maeneo ya uwekezaji.

***81.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia itaendelea na utafiti wa kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa katika mazao ya bustani, mahindi, muhogo, pamba, viazi mviringo, migomba na korosho kwa teknolojia zinazolinda mazingira. Aidha, Wizara itafanya utafiti wa uchumi jamii katika mnyororo wa thamani kwa mazao ya kipaumbele katika ikolojia za kilimo, masoko, uchambuzi wa aina ya wadau na mahitaji yao kwa kuzingatia jinsia. Vilevile, itaandaa mizania (*farm budgets*) na mpango biashara (*business plan*) kwa mazao ya chakula na biashara kufikia malengo mkakati ya uchumi wa viwanda.

***82.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Programu ya ASDP II itaboresha na kuimarisha miundombinu ya utafiti kwa kukarabati ofisi, maabara na nyumba katika vituo nane

(8) vya utafiti vya Ukiriguru, Ilonga, Uyole, Naliendele, Tumbi, Seliani, Makutopora na Kituo cha Taifa cha Utunzaji Nasaba za Mimea (*National Plant Genetic Resource Centre*) pamoja na ujenzi na uboreshaji wa Makao Makuu ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI).

***83.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itahakikisha kuwa matokeo ya utafiti yanawafikia wadau wa kilimo kwa njia ya mtandao, maonesho, mashamba ya mfano, taarifa na machapisho mbalimbali kama vile mabango, vipeperushi na vijarida. Aidha, itaratibu upatikanaji wa taarifa muhimu za utafiti kupitia majarida makubwa ya utafiti ulimwenguni kwa kushirikiana na Taasisi za Kimataifa ili kuongeza ubunifu wenye tija kwa maendeleo ya Sekta ya Kilimo nchini.

***84.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaboresha utafiti unaozingatia masuala mtambuka ya kijinsia (*gender mainstreaming*) kwa kuelimisha wataalamu na wakulima umuhimu wake katika miradi kwa manufaa ya wakulima wa jinsia zote na kuongeza upokeaji wa teknolojia kwa mazao 8 ya kipaumbele chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo- ASDP II.

### 2.2.6 Huduma za Ugani na Usambazaji wa Teknolojia za Kilimo

***85.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kupeleka teknolojia za kilimo kwa wakulima kwa kutoa mafunzo ya matumizi sahihi ya viuatilifu vya zao la pamba kwa wakulima viongozi na wengineo 15,230 katika Halmashauri za Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu (Simiyu); Kwimba, Sengerema na Buchosa (Mwanza); Igunga na Nzega (Tabora); Chato na Geita (Geita) na Bunda, Musoma Vijijini, Serengeti (Mara). Aidha, kupitia mradi wa ERPP mafunzo ya kilimo shadidi (*System for Rice Intensification -SRI*) cha mpunga yametolewa kwa wataalamu 48 kutoka katika skimu za umwagiliaji 17 kwenye Halmashauri za Kilombero, Mvomero, Kilosa, Ulanga na Morogoro. Vilevile, Mashamba Darasa 40 ya mpunga yenye jumla ya wakulima 1,200 yameanzishwa katika skimu za umwagiliaji 40 kwenye

Halmashauri za Ulanga, Malinyi, Kilombero, Kilosa, Mvomero na Morogoro. Kupitia maonesho ya Sikukuu ya Wakulima (NaneNane) wadau mbalimbali wakiwemo wakulima wapatao 515,172 wamejifunza teknolojia mbalimbali za uzalishaji na usindikaji wa bidhaa na mazao ya kilimo.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kusimamia huduma za ugani na kuboresha usambazaji wa teknolojia za kilimo bora kwa wakulima kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo utoaji wa ushauri wa kitaalam na ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa kazi za ugani katika Halmashauri zote nchini.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia ASDP II itaendelea kuviimarisha vituo vya maonesho ya wakulima (NaneNane) vilivyopo katika kanda za Kati (Nzuguni – Dodoma), Mashariki (J.K Nyerere – Morogoro), Kusini ( Ngongo – Lindi), Nyanda za juu Kusini (John Mwakangale – Mbeya), Magharibi (Fatma Mwasi – Tabora), Kaskazini (Themi – Arusha), Ziwa Magharibi (Nyamhongoro – Mwanza) na kujenga kituo kimoja kipya cha maonesho cha Kanda ya Ziwa Mashariki katika Mkoa wa Simiyu ili kupeleka teknolojia za kilimo kwa wakulima wengi zaidi. Hatua hizo ni sehemu ya mpango wa kuboresha maonesho hayo ambayo yana umuhimu mkubwa katika kuhakikisha teknolojia bora zinawafikia wakulima na kutangaza fursa za masoko ya mazao na bidhaa mbalimbali za kilimo. Aidha, kupitia mradi wa ERPP mashamba 300 ya mfano ya mpunga yenye jumla ya ekari 300 yataanzishwa ili kufundisha wakulima 1,200 juu ya matumizi bora ya pembejeo katika skimu 40 za umwagiliaji kwa kutumia kilimo shadidi (*System of Rice Intesification - SRI*). Pia itawezesha usambazaji wa pembejeo za kilimo (mbegu na mbolea) kwa wakulima 11,200 kwenye skimu 40 za umwagiliaji na mafunzo juu ya teknolojia ya SRI yatatolewa kwa wataalam 60 wa Ugani.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara itatoa elimu kwa wakulima 2000 wa ngano na wakulima wa mahindi 8000 katika kanda za Kaskazini na Ziwa

mtawalia. Mafunzo hayo yatahusu kanuni za kilimo bora cha ngano kwa kutumia mbinu shirikishi ya shamba darasa ikiwa ni pamoja na kusambaza pembejeo za kilimo za kutosha na kwa wakati. Pia, Wizara itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao yanayostahimili ukame yakiwemo mtama, muhogo na uwele hususan kwenye maeneo yenye ukame.Vilevile, elimu itatolewa kwa wakulima wa Kanda ya Ziwa na Mkoa wa Tabora kuhusu kilimo bora cha mpunga kwa kutumia mfumo wa shadidi ili kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa tani 2.5 kwa hekta hadi wastani wa tani 6 kwa hekta.

***89.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itafanya tathmini ili kubaini mahitaji ya mafunzo kwa maafisa ugani katika Halmashauri zote nchini kwa lengo la kuwajengea uwezo na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma bora kwa wakulima. Aidha, itaandaa mpango wa mafunzo rejea kwa maafisa ugani ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia za kilimo na ubobevu (*specialisation*) ya mazao kimaeneo. Kwa ujumlamgawanyo wa ujuzi wa maafisa ugani kwa sasa hauendani na mahitaji kimaeneo. Mfano ni mkoa wa Kagera wenye maafisa ugani 548, ambapo ni maafisa ugani na 32 tu ndio wenye ufahamu wa zao la Kahawa. Wizara itaandaa mwongozo wa uzalishaji kwa mazao muhimu yanayozalishwa katika kanda za kiekolojia.

### 2.2.7 Usimamizi wa mazao baada ya mavuno, kuongeza thamani na upatikanaji wa masoko

***90.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na wadau kama FAO, ANSAF na HELVETAS imekamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Mazao Baada ya Mavuno. Mkakati huo unalenga kupunguza upotevu wa mazao ya chakula katika mnyororo wa uzalishaji; kuongeza upatikanaji wa chakula na kipato kwa mzalishaji; kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya chakula kwa kuimarisha miundombinu ya masoko ikiwemo maghala kwa ajili ya hifadhi ya mazao ya chakula na vifaa vya usindikaji wa mazao hayo; kuimarisha mahusiano kati

ya wazalishaji, wasindikaji na masoko. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la HELVETAS imeandaa mwongozo kwa maafisa ugani kwa lengo la kuwaongoza katika kuandaa mafunzo kwa vitendo kwa wakulima kuhusu usimamizi wa mazao baada ya kuvuna.

***91.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) imetekeleza Mradi wa Udhibiti wa Sumukuvu katika mikoa ya Dodoma na Manyara. Kupitia mradi huu wakulima 10,023 (Me 6,799: Ke 3,224) wamefundishwa na kuhamasishwa kutumia mbinu za kilimo bora na utunzaji bora wa mazao wakati na baada ya kuvuna ili kudhibiti maambukizi ya sumukuvu katika zao la mahindi, kuzalisha chakula/mazao salama na kuwa na uhakika wa soko.

***92.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeandaa Mwongozo wa Udhibiti wa Sumukuvu, Kitabu cha Kufundishia, vipeperushi na mabango vinavyoelimisha wazalishaji na jamii kuhusu sumukuvu, madhara na udhibiti wake. Vilevile, Wizara imetoa semina kwa viongozi wa juu 28 wa Mikoa na Wilaya ambapo mradi huo unatekelezwa kwa lengo la kuwapatia uelewa kuhusu sumukuvu, umuhimu wa kuingiza masuala ya sumukuvu katika mipango yao na kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wake. Aidha, kupitia mradi huo, jumla ya mifuko maalum 1,000 isiyopitisha hewa na inayohifadhi nafaka pasipo kuweka viuatilifu (*Hemetic bags*) na maturubai 200 vilisambazwa katika Halmashauri za Wilaya za Chemba, Kondoa, Kongwa na Kiteto kwa ajili ya kukausha na kuhifadhi nafaka.

***93.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa andiko la Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu (*Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination – TANIPAC*) ambao unalenga mazao ya mahindi na karanga na utatekelezwa katika mikoa ya Mwanza, Geita, Tabora, Simiyu,Kigoma, Dodoma, Morogoro, Manyara, Ruvuma, Songwe na Mtwara.

***94.*** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi za Mazao imeendelea kuhamasisha upatikanaji wa masoko ya

kilimo ili kumnufaisha mkulima. Aidha, uhamasishaji wa uzalishaji wa zao la muhogo kibiashara umefanyika katika Kanda ya Mashariki (Tanga na Pwani) na Kusini (Lindi na Mtwara) kwa kuanisha maeneo ya uzalishaji, wafanyabiashara na wazalishaji wa mbegu. Pia Wizara inayo mikakati ya kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora za muhogo ili kutumia fursa ya soko la ndani na nje ya nchi hususan soko la China.

***95.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia ASDP II itaendelea kusimamia udhibiti wa maambukizi ya sumukuvu katika mazao ya chakula kwa lengo la kulinda ubora wa mazao, afya za walaji na kuwapatia wakulima soko la uhakika. Katika kutekeleza hilo, Wizara itajenga makaushio bora 18 kwa vikundi 18 vya wakulima katika Halmashauri za Wilaya za Sikonge, Chemba, Kondoa, Chamwino, Manispaa ya Dodoma na Kiteto kwa ajili ya ukaushaji wa mazao ya mahindi na karanga.

***96.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia itatekeleza Mradi wa *TANIPAC* ambapo itafanya usanifu wa ujenzi wa kituo cha mfano cha kusambaza teknolojia za usimamizi wa mazao baada ya kuvuna (*Post-harvest Centre of Excellence*), Maabara ya mfano (*Central Agriculture Reference Laboratory for Aflatoxin and Fungal Testing*) kwa ajili ya vipimo vya maambukizi ya sumukuvu na aina nyingine za ukungu mkoani Dodoma. Aidha, maghala 14 kwa ajili ya hifadhi ya mahindi katika Halmashauri za Wilaya za Ileje, Chemba, Babati, Kiteto, Nzega, Kibondo, Kasulu, Newala, Namtumbo, Buchosa, Bukombe, Itilima pamoja na kituo cha udhibiti wa maambukizi (*Quarantine*) na ukarabati wa maabara ya Taifa ya udhibiti wa kibaiolojia iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha.

***97.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia ASDP II itaendelea kuimarisha miundombinu ya masoko kwa lengo la kuimarisha usalama wa chakula na kutatua changamoto za masoko nchini. Katika mwaka 2018/2019 Wizara itajenga maghala 15 yenye uwezo tofauti kwa ajili ya hifadhi ya

mahindi. Maghala hayo yatajengwa katika mikoa ya Mwanza (3) (Buchosa (2) - tani 2,000 kila moja na Sengerema - tani 1,000); Manyara (1) (Kiteto - tani 5,000); Singida (2) (Mkalama - tani 1,000 na Ikungi - tani 1000); Kigoma (3) (Kasulu - tani 2,000, Uvinza -tani 2,000 na Kibondo tani 2000); Simiyu (2) (Meatu - tani 2000 na Itilima - tani 3000); Tanga (2) (Handeni 2000 kila moja) na Tabora (2) (Nzega - tani 2000 na Urambo tani 2000).

***98.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itakamilisha ukarabati wa maghala 33 kwa ajili ya hifadhi ya mahindi katika Halmashauri za wilaya za Mlele, Nsimbo, Songea na Njombe. Ujenzi na ukarabati wa maghala unalenga kuimarisha miundombinu ya hifadhi, upatikanaji wa chakula kwa mwaka mzima na kuwawezesha wakulima kuuza mazao yao wakati bei itakapokuwa nzuri. Aidha, Wizara itafanya ufuatiliaji wa miradi ya Usalama wa Chakula katika mikoa ya Ruvuma, Iringa, Mbeya, Songwe, Singida, Shinyanga na Tanga.

***99.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia mradi wa Kuongeza Uzalishaji na Tija ya Zao la Mpunga (ERPP) itajenga maghala matano (5) kwa ajili ya hifadhi ya zao la mpunga katika skimu za umwagiliaji za Njage, Msolwa Ujamaa, Kigugu, Mvumi na Mbogo Komtonga mkoani Morogoro. Aidha, itawajengea uwezo wakulima viongozi 250 katika skimu 40 za umwagiliaji kuhusu ushirika na ujasiriamali ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mpunga baada ya kuvuna, usindikaji, kupanga madaraja ili kuongeza thamani na ujuzi wa masoko.

***100.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia changamoto zilizojitokeza katika soko la nje kwa zao la mbaazi, Wizara itaendelea kuimarisha soko la ndani na kuhamasisha matumizi ya zao hili kuwa sehemu ya chakula nchini. Vilevile, Wizara itahamasisha wawekezaji kuanzisha viwanda vya kusindika mbaazi kwa ajili matumizi mbalimbali ikiwemo

utengenezaji wa vyakula vya mifugo na hivyo kuondokana na utegemezi wa soko la nje. Aidha, katika kuimarisha soko la ufuta, kuanzia msimu wa mavuno wa mwaka 2017/2018, zao la ufuta litauzwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala hususan mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ambapo mfumo huo unatumika kwa zao la korosho.

***101.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo itawatambua na kuwahamasisha wazalishaji na wasindikaji wa zao la muhogo kutumia teknolojia bora za usindikaji wa zao hilo katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Mwanza, Geita, Kagera na Mara kwa lengo la kupata bidhaa bora na hatimaye kuongeza kipato.

***102.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaanzisha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za mazao ya chakula na mazao yanayosindikwa viwandani kwa lengo la kubaini upotevu katika mnyororo wa thamani na kutengeneza mikakati ya kuboresha viwanda, kupunguza upotevu na hatimaye kutengeneza ajira na kipato. Aidha, Wizara itaandaa mfumo mwingine wa kukusanya takwimu za maghala yanayotumika kuhifadhi mazao ya chakula hususan nafaka na mikunde. Lengo la mfumo huo ni kutaka kujua idadi, hali na uwezo wa hifadhi wa maghala nchini ili kubuni mikakati ya kuimarisha hifadhi ya mazao ikiwa ni pamoja na kukarabati/kujenga maghala mapya. Pia, kuwajengea uwezo wakulima juu ya hifadhi bora ili kuwa na uhakika wa chakula katika kaya, masoko na kipato kizuri.

***103.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kudhibiti matumizi ya vipimo vya mazao visivyo rasmi**,** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji na wadau wengine, itasimamia na kuhamasisha matumizi ya mizani na vifungashio sahihi ili kumsaidia mkulima kupata mapato stahiki kutokana na mauzo ya mazao yake. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji itasimamia utekelezaji wa Sheria ndogo ndogo ili kudhibiti matumizi ya

vipimo visivyo rasmi. Serikali inaelekeza kwa kadri inavyowezekana mazao yote yauzwe kwa uzito badala ya ujazo.

### 2.2.8 Kusimamia Uzalishaji Kupitia Bodi za Mazao

***104. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kusimamia uzalishaji wa mazao kupitia bodi zake ambazo ni Bodi ya Pamba, Chai, Pareto, Korosho, Mkonge, Sukari, Kahawa na Tumbaku. Uzalishaji kwa baadhi ya mazao makuu ya asili ya biashara umeongezeka kwa viwango tofauti kama inavyoonekana katika Jedwali namba 1. Ongezeko hilo limechangiwa na sababu mbalimbali zikiwemo matumizi ya teknolojia na mbinu bora za uzalishaji pamoja na ongezeko la bei ya mazao ya pamba, pareto, korosho, chai na tumbaku katika msimu uliopita. Vilevile, kuhusiana na zao la Korosho, Serikali ilitoa Sulphur bure kupitia fedha za *export levy* ili kuhamasisha uzalishaji wa korosho.

***105. Mheshimiwa Spika,*** Aidha, Uzalishaji wa mazao ya mkonge, sukari na kahawa umepungua kwa viwango tofauti ikilinganishwa na mwaka 2016/2017. Uzalishaji wa zao la kahawa umeshuka kutokana na baadhi ya mashamba ya kahawa kubadilishwa kuwa makazi ya watu hususan katika Kanda ya Kaskazini na upungufu wa maji ya umwagiliaji. Aidha, uzalishaji wa sukari kwa msimu wa 2017/2018 umeshuka ukilinganishwa na msimu wa 2016/2017 kutokana na ukosefu wa mvua za kutosha mwanzoni mwa msimu kutokana na hali ya hewa iliyoathiri ukuaji wa miwa na kupelekea kudumaa kwa zao hilo hasa kwa wakulima wadogo *"outgrowers"* na kusababisha kiwango cha sukari katika miwa kupungua. Vile vile, kiwanda cha Mtibwa kilichelewa kuanza msimu wa uzalishaji wa sukari kutokana na ukarabati wa kiwanda uliochukua muda mrefu kukamilika na kiwanda hicho kuendelea kuwa na matengenezo ya mara kwa mara.

**Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa mazao ya asili ya biashara (tani)**

| Zao | 2015/2016 | 2016/2017 | 2017/2018* | 2018/2019** |
|---|---|---|---|---|
| Pamba | 149,445 | 121,639 | 133,000 | 600,000 |
| Chai | 32,629 | 26,975 | 31,814 | 35,000 |
| Pareto | 2,011 | 2,150 | 2,400 | 3,000 |
| Korosho | 155,416 | 265,238 | 311,899 | 350,000 |
| Mkonge | 42,314 | 36,533 | 26,498 | 43,127 |
| Sukari | 293,075 | 330,843 | 307,431 | 358,600 |
| Kahawa | 60,921 | 48,329 | 38,414 | 60,000 |
| Tumbaku | 60,691 | 58,639 | 63,800 | 70,000 |

***Chanzo:****Wizara ya Kilimo, 2018*
**Uzalishaji unaendelea ** Matarajio ya uzalishaji*

***106. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imenunua jumla ya tani 2,504.09 za mahindi kutoka kwenye vikundi vya wakulima wa mikoa ya Iringa na Ruvuma kwa kutumia jumla ya Shilingi bilioni 1.25. Aidha, hadi kufikia mwezi Desemba 2017 Bodi imesagisha tani 146.5 ambapo zimepatikana tani 112.7 za unga wa mahindi na tani 33.8 za pumba. Usagishaji unaendelea na mauzo yanaendelea katika mikoa ya Iringa, Dodoma, Dar es Salaam na Mwanza.

***107. Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza uwezo, Bodi imepokea mkopo wa Shilingi 3,668,268,829 kutoka Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kununua mashine yenye uwezo wa kusagisha tani 60 za mahindi kwa siku na mashine yenye uwezo wa kukamua tani 20 za mbegu za alizeti kwa siku zitakazofungwa katika eneo la Kizota mjini Dodoma. Aidha, Mashine hizo zitakapoanza kufanya kazi Bodi itaweza kununua tani 17,000 za mahindi na tani 6,000 za mbegu za alizeti kutoka kwa wakulima kwa mwaka. Mzabuni wa kufunga mashine hizo kampuni ya UGUR ya Uturuki inatarajia kukamilisha ufungaji wa mashine kabla mwezi Julai, 2018.

***108. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko itaongeza kununua idadi ya mazao. Mazao yatayoongezwa

ni pamoja na jamii ya mikunde (mbaazi, choroko na dengu), mbegu za mafuta (ufuta, alizeti na karanga), nafaka (mtama, ulezi na uwele), mizizi (muhogo) na kakao.

***109.*** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea na uhamasishaji wa uanzishwaji wa kilimo cha mkataba na kibishara kwa zao la muhogo katika kanda za Mashariki na Kusini. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Mikoa ya Lindi, Mtwara, Manyara, Singida na Morogoro itaendelea kutekeleza Programu ya *Supporting Indian Trade and Investiment in Africa - SITA* kwa kutumia mfumo wa kilimo cha mkataba kuzalisha mazao ya mikunde na mafuta kibiashara. Aidha, Wizara itaendelea kuwahamasisha wakulima kuzalisha kibiashara mazao jamii ya mikunde, mazao ya bustani na mbegu za mafuta kwa ajili ya soko la ndani na nje.

### 2.2.9 Uzalishaji wa mazao ya bustani na mbegu za mafuta

***110.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, uzalishaji wa mazao ya bustani ambayo ni matunda, mboga, maua na viungo umeongezeka kwa viwango tofauti kama inavyoonekana katika Jedwali namba 2. Ongezeko hilo linatokana na wakulima kuhamasika kuzalisha mazao ya parachichi, matikiti na nyanya. Wizara imeendelea kushirikiana na Taasisi mbalimbali ili kuhamasisha kilimo cha matunda, mboga, maua na viungo pamoja na ulaji wake.

**Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani)**

| Zao | 2016/2017 | 2017/2018* | 2018/2019** |
|---|---|---|---|
| Matunda | 4,946,550 | 5,243,343 | 5,610,377 |
| Mboga | 1,236,560 | 1,298,388 | 1,376,291 |
| Maua | 11,615 | 11,847 | 12,003 |
| Viungo | 21,420 | 22,062 | 22,834 |

***Chanzo:****Wizara ya Kilimo, 2018 * Uzalishaji unaendelea, ** matarajio ya uzalishaji*

***111. Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta za alizeti, karanga, ufuta, mawese na soya umeongezeka kwa viwango tofauti kama inavyoonekana katika Jedwali namba 3. Kuongezeka kwa uzalishaji kumechangiwa na kuongezeka kwa hamasa kwa wakulima kutokana na uwepo wa soko la uhakika, ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi pamoja na uwekezaji katika viwanda vidogo na vya kati vya kusindika mazao hayo katika mikoa ya Manyara, Singida, Dodoma, Mbeya, Katavi, Lindi, Mtwara, Iringa, Njombe, Rukwa na Kigoma. Katika kuhamasisha uwekezaji katika mazao ya mafuta, Serikali itaongeza kodi kwenye mafuta ghafi yanayoingizwa nchini toka asilimia 10 hadi asilimia 25 ambapo ongezeko hilo litatumika kuendeleza uzalishaji wa mbegu za mafuta.

**Jedwali Na. 3: Uzalishaji wa Mbegu za Mafuta (Tani)**

| Zao | 2016/2017 | 2017/2018* | 2018/2019** |
|---|---|---|---|
| Alizeti | 3,112,500 | 3,229,220 | 3,334,394 |
| Karanga | 2,215,257 | 2,281,710 | 2,396,962 |
| Ufuta | 1,291,724 | 1,343,390 | 1,393,474 |
| Mawese | 42,277 | 43,120 | 43,658 |
| Soya | 6,135 | 6,380 | 6,535 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo, 2018*
** Uzalishaji bado unaendelea ** Matarajio ya uzalishaji*

***112. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kusimamia uendelezaji wa mazao nchini na kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati wa mazao ya bustani.

### 2.2.10 Mikakati ya uzalishaji wa mazao

***113. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara itahakikisha kuwa Mpango wa bajeti unatekelezwa kwa kuzingatia vipaumbele na miongozo ya Kitaifa ili kuhakikisha kuwa kilimo kinachangia kutoa malighafi za

viwanda ili kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Wizara kupitia ASDP II itatekeleza mkakati wa maendeleo ya mazao ambao unaweka mfumo (*framework*) wa kuendeleza mazao ya kilimo kwa kushirikisha wadau mbalimbali na Wizara ikiwa na jukumu la uratibu wa utekelezaji.

***114. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa Mwongozo wa Uzalishaji Mazao kulingana na kanda za kilimo za kiekolojia ambao ukitumika sambamba na Mwongozo wa Kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi, kanuni za kilimo bora na mazingira wezeshi kwa wakulima kuzalisha mazao kwa tija na gharama nafuu na utawavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Aidha, katika kuhakikisha uzalishaji wa mazao unaongezeka, Wizara inaandaa utaratibu mpya wa uuzaji wa mazao ndani na nje ya nchi. Chini ya utaratibu huo, vibali vya kuuza nje vitapatikana mipakani ingawa vitatolewa na Wizara kwa njia ya kielektroniki. Hakutakuwa na haja ya mwananchi kupeleka maombi Wizarani.

***Mahindi***

***115. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inalenga kuongeza uzalishaji wa mahindi kutoka tani 6,680,758 mwaka 2016/2017 hadi kufikia tani 8,000,000 ifikapo mwaka 2021/2022. Lengo hilo linatarajiwa kufikiwa kwa kupeleka teknolojia za kilimo kwa wakulima ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati zikiwemo mbegu bora, mbolea na madawa na kuwaelimisha wakulima kuhusu matumizi sahihi ya pembejeo. Vilevile, itaimarisha udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao hususan viwavijeshi vamizi (*fall armyworms*) pamoja na udhibiti wa magonjwa. Pia, masoko ya zao la mahindi yataimarishwa kwa kujenga miundombinu ya masoko hususan maghala kwa lengo la kupata bei nzuri na kuongeza thamani.

***116. Mheshimiwa spika,*** Ili kuboresha upatikanaji wa masoko ya mazao ya chakula hususan mahindi, Wizara imeondoa zuio la kuuza mazao hayo nje ya nchi (*Export Ban*). Aidha, Wizara kwa kushirikiana AGRA na wadau wengine

itafanya utafiti utakaosaidia kuweka mfumo mbadala utakaoboresha biashara endelevu ya mazao hayo ndani na nje ya nchi. Mfumo huo utaratibu upatikanaji wa takwimu sahihi za uzalishaji, mahitaji na ziada ya chakula nchini pamoja na ufuatiliaji wa mwenendo wa masoko ndani na nje ya nchi bila kuathiri hali ya usalama wa chakula nchini. Sambamba na mfumo huu, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itaandaa Mkakati wa Kitaifa wa Usalama wa Chakula (National Food Security Strategy) ili kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na usalama wa chakula endelevu.

***Mpunga***

***117. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaongeza uzalishaji wa mpunga kutoka tani 3,000,000 za sasa hadi kufikia tani 5,000,000 ifikapo mwaka 2021/2022. Ili kufikia lengo hilo Wizara itatoa elimu kwa wakulima kwa mfumo wa shadidi ambao utamsaidia mkulima kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa tani 2.5 hadi kufikia tani 6.5 kwa hekta. Vilevile, elimu itatolewa kwa wakulima wawezeshaji kwenye skimu za umwagiliaji kwa kutumia mbinu shirikishi za shamba darasa; kuanzisha mashamba ya mfano; kuhamasisha matumizi ya mbegu bora za mpunga; kuboresha miundombinu ikiwemo barabara za mashambani; ujenzi wa maghala pamoja na mitambo ya usindikaji. Upanuzi wa miundombinu ya umwagiliaji utafanyika, ambapo jumla ya hekta 8,182 zitajengwa na kukarabatiwa kote nchini.

***Ngano***

***118. Mheshimiwa Spika,*** mahitaji ya ngano hapa nchini ni takribani tani 250,000, hata hivyo uzalishaji kwa sasa ni wastani wa tani 76,400. Aidha, Wizara inalenga kuhamasiha kuongeza uzalishaji kutoka tani 76,400 za sasa hadi kufikia tani 100,000 ifikapo mwaka 2021/2022. Katika kuhakikisha lengo hilo linafikiwa, Wizara itahamasisha kilimo cha ngano katika Ukanda wa Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini; na itahamasisha matumizi ya mbegu bora na kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora za ngano. Wakulima katika mashamba ya Basutu na Songwe watashauriwa kulima

ngano na waagizaji wa ngano kushauriwa kununua kutoka soko la ndani kwanza.

***Muhogo***

***119. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inalenga kuhamasisha uzalishaji wa muhogo kutoka tani 1,341,755 za muhogo mkavu (makopa) kwa mwaka 2016/2017 na kufikia tani 4,500,000 ifikapo 2021/2022. Ili kufikia lengo hilo Wizara kwa kutumia Vituo vya Utafiti na kwa kushirikiana na Sekta Binafsi inaendelea na uzalishaji wa mbegu ili kufikia pingili 25,000,000 kwa mwaka; kuongeza udhibiti wa milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao na magonjwa; uboreshaji wa mfumo wa uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za muhogo; na uhamasishaji wa matumizi ya mbegu bora. Utekelezaji wa mkakati huo utaleta mageuzi katika mnyororo wa thamani wa zao la muhogo kwa kuhamasisha wakulima kuzalisha kibiashara, kuongeza tija, uzalishaji na usindikaji wa bidhaa za muhogo zenye viwango vya kimataifa ili kukidhi soko la ndani na nje hususan soko la China.

***Mtama***

***120. Mheshimiwa Spika,*** zao la mtama ni muhimu katika maeneo ambayo yanapata mvua kidogo. Kwa sasa uzalishaji wa mtama ni wastani wa tani 1,000,000 wakati mahitaji ni wastani wa tani 1,800,000. Lengo la Wizara ni kuongeza uzalishaji kutoka tani 1,000, 000 za sasa hadi kufikia tani 3,000,000 ifikapo mwaka 2021/2022. Lengo hilo litafikiwa kwa kuongeza uzalishaji na matumizi ya mbegu bora na udhibiti wa visumbufu. Wizara pia itaendelea kuhamasisha kilimo cha zao la mtama kama njia mojawapo ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Ili kuwahakikishia upatikanaji wa masoko ya kuaminika wakulima wa mtama, Serikali haitatoa tena vibali vya kuingiza mtama kutoka nje mpaka iwe na ushahidi wa kutosha kwamba hakuna mtama katika soko la ndani.

***Alizeti***

***121. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inalenga kuhamasisha uzalishaji wa alizeti kutoka tani 3,112,500 kwa mwaka 2016/2017 hadi kufikia tani 9,337,500 ifikapo mwaka

2021/2022 na kuongeza tija kutoka tani 1.5 hadi tani 3 kwa hekta. Vilevile Wizara itahamasisha uzalishaji, usambazaji na matumizi ya mbegu bora hususan zinazotoa mafuta mengi na kuongeza upatikanaji wa pembejeo kwa wakati. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itawahamasisha wasindikaji wa zao la alizeti kuongeza ubora wa bidhaa za alizeti ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje.

***Korosho***

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019 Wizara kupitia Bodi ya korosho imepanga kuongeza uzalishaji wa korosho kutoka tani 311,899 mwaka 2017/2018 hadi kufikia tani 600,000 ifikapo 2021/2022. Ili kufikia lengo hilo Wizara imepanga kuhamasisha uzalishaji wa korosho katika mikoa mipya 18 inayofaa kwa kilimo cha zao la korosho kwa kuimarisha utafiti ili kupata aina bora za korosho; kuzalisha miche na kupanda mbegu bora za korosho katika maeneo mapya ya uzalishaji; kuhamasisha wakulima kufufua mashamba ya korosho yaliyotelekezwa na kuongeza upatikanaji na matumizi ya madawa hususani salfa. Aidha, Wizara haitatoa Sulphur bure, ila Serikali kupitia Bodi ya Korosho na Vyama Vikuu vya Ushirika wa Korosho imeingia Mikataba na Makampuni ya kuleta Sulphur ambayo itauzwa kwa bei nafuu na hatua hii imechukuliwa ili kuzuia upandaji bei kiholela.

***Pareto***

***123.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Pareto Tanzania imepanga kuongeza uzalishaji wa m a u a ya pareto kutoka tani 2,400 kwa sasa hadi kufikia tani takribani 3,000 ifikapo mwaka 2021/2022. Ili kufikia lengo hilo Bodi itashirikiana na makampuni yanayochakata pareto nchini hususan katika maeneo ya utafiti; kuimarisha huduma za ugani kwa wakulima na wataalamu wa zao la pareto; kuongeza upatikanaji wa mbegu bora pamoja na kujenga vikaushio; kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza kwenye viwanda vya kusafisha (*refinery*) ili kusaidia wakulima kuwa na uhakika wa soko la pareto.

***Sukari***

***124. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Sukari Tanzania inatekeleza Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Tasnia ya Sukari. Lengo la mkakati huu ni kuongeza uzalishaji kutoka tani 307,431.14 mwaka 2017/2018 hadi tani 495,000 ifikapo mwaka 2021/2022 kuwezesha Taifa lijitosheleze kwa mahitaji ya sukari. Lengo hili litafikiwa kwa kuongeza mashamba mapya ya miwa na kupanua yaliyopo (**Jedwali Na. 4**). Kwa kushirikiana na wadau, hatua mbalimbali za kimkakati zinachukuliwa ili kuongeza tija katika uzalishaji wa miwa kwenye mashamba ya wenye viwanda na wakulima wadogo; usindikaji wa miwa viwandani pamoja na uimarishaji wa huduma za udhibiti; utafiti; mafunzo na ugani. Pia, hatua zaidi zinachukuliwa ili kulinda uzalishaji wa wazalishaji wa viwanda vya ndani sambamba na kuweka mazingira bora kwa ajili ya kuvutia uwekezaji katika viwanda vipya vya sukari nchini. Serikali imeratibu uanzishwaji wa mashamba mapya ya miwa ya Mkulazi I (Ngerengere), Mkulazi II (Mbigiri) na Shamba la Bakhresa - *Bagamoyo Sugar* (Makurunge).

**Jedwali Na. 4: Matarajio ya uzalishaji wa sukari (Tani)**

| **Kiwanda** | **2017/20** | **2018/201** | **2019/202** | **2020/202** | **2021/202** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kilombero Sugar C | 118,511 | 121,600 | 126,900 | 131,100 | 145,000 |
| TPC Ltd | 91,487 | 107,000 | 114,000 | 117,000 | 117,000 |
| Kagera Sugar Ltd | 75,568.85 | 84,000 | 99,000 | 117,000 | 135,000 |
| Mtibwa Sugar Ltd | 18,185 | 40,000 | 52,000 | 65,000 | 85,000 |
| Manyar a | 3,679.29 | 6,000 | 10,000 | 12,500 | 13,000 |
| **JUMLA** | **307,431.** | **358,600** | **401,900** | **442,600** | **495,000** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo, 2018*
*** Matarajio ya uzalishaji*

### *Kahawa*

***125. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Kahawa inatekeleza mkakati wa miaka kumi (2011/2021) wa kuzalisha tani 100,000 ifikapo msimu wa 2021/2022 kutoka wastani wa sasa wa tani 50,000. Kiasi hiki kinatarajiwa kuingiza kipato cha Dola milioni 300 kwa hali ya soko ya sasa. Ili kufikia lengo hilo, mpango kabambe wa uzalishaji na ugawaji wa miche ipatayo milioni 10 kwa mwaka kwa wakulima sambamba na kuwa na mfumo wa utoaji pembejeo utatekelezwa na Serikali kupitia Bodi ya Kahawa. Aidha, ili kuhakikisha kuwa mkulima anapata bei inayoendana na ubora wa kahawa, Serikali imeelekeza kuwa kuanzia msimu wa kahawa 2018/2019 unaotarajiwa kuanza Mei 2018 kahawa katika soko la awali itakusanywa kutoka kwa wakulima na vyama vya Msingi (AMCOS) pekee ambavyo ndio vitakuwa na jukumu la kuipeleka kwenye viwanda vya kukobolea kahawa na baadae kwenye mnada wa kahawa. Wanunuzi wote (Makampuni Binafsi) watatakiwa kununua kahawa kwenye mnada wa kahawa. Sambamba na miche bora na soko, pia kuimarisha huduma za ugani na utafiti ambapo sasa TaCRI itakuwa chini ya Wizara moja kwa moja.

### *Mkonge*

***126. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania inatekeleza Mpango wa miaka 10 wa Maendeleo wa Sekta ya Mkonge kwa mwaka 2012/2021. Mpango huo unalenga kuongeza uzalishaji wa Mkonge kutoka tani 34,589 hadi tani 100,000; kuongeza tija kutoka tani 0.8 kwa hektatani 1.8 kwa hekta; kuongeza uzalishaji wa bidhaa za Mkonge (kamba, mazulia, vikapu, magunia) kutoka tani 9,759 hadi tani 21,996; kuongeza matumizi ya zao la Mkonge kutoka asilimia 2 ya sasa hadi asilimia 50; kuongeza mauzo ya bidhaa za mkonge badala ya singa ghafi kutoka tani 5,257 hadi tani 13,756 na kuongeza ushiriki wa wakulima wadogo wa mkonge nchini kutoka 5,828 hadi 16,500 kuanzia mwaka 2011/2012 hadi ifikapo mwaka 2020/2021.

***127.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Uzalishaji wa zao la mkonge unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo tija ndogo, ubora wa chini wa bidhaa zinazotokana na zao hilo na ushindani wa bidhaa mbadala zinazoingizwa nchini. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara itaimarisha uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora za mkonge kwa wingi kwa njia ya maabara (*Meristematic Tissue Culture*); kushirikiana na Taasisi za Utafiti kufanya utafiti kwa lengo la kupata tiba ya ugonjwa wa mabaka ya majani Korogwe (*Korogwe Leaf Spot*) ili kuimarisha ubora wa singa zinazozalishwa na bidhaa zingine. Vilevile, Wizara itafanya utafiti wa masoko mapya ya mkonge na bidhaa za mkonge hususan kwenye nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC. Msisitizo utawekwa katika kuongeza thamani kwa kuzalisha mazao ya mkonge ambayo ni pamoja na singa, Kamba, mazulia, magunia, kitambaa msasa, mbolea, *biogas*, chakula cha mifugo, karatasi nk ili kulinda soko la ndani. Wizara pia itashauri uwezekano wa ongezeko la kodi kwa bidhaa mbadala zinazoingizwa nchini ili kulinda viwanda vya ndani vya bidhaa za mkonge.

***Pamba***

***128.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina mkakati wa kuongeza uzalishaji wa zao la pamba kutoka tani 121,639 mwaka 2016/2017 hadi kufikia tani 1,000,000 ifikapo mwaka 2020. Lengo hilo litafikiwa kwa kuongeza matumizi bora ya mbegu ambapo katika msimu 2018/2019 Bodi itazalisha tani 40,000 za mbegu aina ya UKM08 ambayo ni zaidi ya mahitaji ya tani 25,000. Pia, kuongeza uzalishaji wa mbegu mpya aina mbili zilizothibitishwa kwa ajili ya kuzipeleka kwa wakulima; kutenga maeneo maalum ya kuzalisha mbegu bora; kuhamasisha Makampuni Binafsi kuzalisha mbegu za pamba; kutoa elimu kwa mkulima juu ya kanuni bora za uzalishaji wa pamba ili kuongeza tija; kutoa vitendea kazi vitakavyorahisisha utendaji na kuhamasisha uzalishaji katika mikoa ya Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Pwani na Iringa. Serikali imedhamiria kuwa zao la pamba lichangie katika ukuaji wa sekta ya viwanda kwa kuwa na viwanda vyenye uwezo wa kutumia malighafi zitokanazo na pamba

ikiwemo utengenezaji wa nyuzi, nguo, mafuta ya kula na vyakula vya mifugo. Ili kutekeleza azma hiyo, Serikali inatekeleza Mkakati wa kuongeza thamani kwenye pamba (Cotton *to Clothing Strategy* 2016 – 2020).

***Tumbaku***

***129. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina lengo la kuongeza uzalishaji na ubora wa zao la tumbaku kutoka tani 58,639 mwaka 2016/2017 hadi kufikia tani 120,000 ifikapo mwaka 2021/2022. Lengo hilo litafikiwa kwa kutekeleza yafuatayo: kutambua na kupanda aina mpya za tumbaku ambazo zinapendwa na wanunuzi wengi wakubwa katika soko la dunia; kubaini maeneo yanayoweza kupandwa mbegu mpya zenye tija na kusajili wanunuzi wapya kutoka nje na ndani ya nchi; uwepo wa kampuni mpya ya PT Far East Leaf Tobacco Company ya Indonesia iliyoonesha nia ya kununua tani mia sita (600) za tumbaku ya Tanzania. Makampuni mengine yaliyoonesha nia ni kutoka nchi za Irani, Misri na Vietnam. Aidha, Wizara itaimarisha utendaji wa kiwanda kinachokarabatiwa mjini Songea kinachomilikiwa kwa ubia kati ya mwekezaji na chama kikuu cha Ushirika cha Songea (SONAMCU).

***Chai***

***130. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Chai itashirikiana na wadau wengine kutekeleza mpango mkakati wa miaka 10 unaolenga kuongeza uzalishaji wa zao la chai kutoka tani 35,000 hadi kufikia tani 50,000 ifikapo mwaka 2022/2023. Mikakati ya kufikia lengo hilo ni pamoja na: kutoa elimu kwa wakulima wa chai juu ya kilimo bora; kujazia mapengo kwenye mashamba ambayo yana nafasi kubwa; kuwekeza kwenye umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wakati wa kiangazi; kuimarisha matumizi ya vipando bora vya chai; kuongeza tija kwa eneo kwa maeneo yaliyopo;

kuongeza uwekezaji katika viwanda vya kusindika chai na ukarabati wa mashamba ya chai yaliyotelekezwa. Aidha, uanzishwaji wa viwanda vipya vya kuchanganya na kufunga chai kwenye vikasha; kusajili viwanda vinne ambavyo ni Chai leo Ltd, Rift Valley Tea Solutions, Tea plus Investment na TEAZANIA kutachangia kuongeza uzalishaji, thamani ya chai inayozalishwa na kutoa ajira kwa watanzania zaidi ya 2,000.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Bodi za Mazao itaendelea kufuatilia, kusimamia na kutoa ushauri wa kitalaam kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji na tija pamoja na kuimarisha soko la mazao. Vilevile, Wizara kupitia ASDP II itaendelea kutoa ushauri wa kitaalam kupitia Bodi za Pamba; Korosho; Kahawa; Tumbaku, Nafaka na Mazao Mchanganyiko; Mkonge na Sukari ili kuongeza soko kwa mazao husika.

### 2.2.11 Taasisi za Wizara

***132.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Taasisi zake imeendelea kusimamia hifadhi ya chakula, kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya riba nafuu, uzalishaji wa mbegu bora na udhibiti wa ubora wa pembejeo za kilimo.

#### *Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula - NFRA*

***133.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula nchini, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ulilenga kununua tani 18,182.00 za mahindi kwa kutumia vituo vya Ununuzi na vikundi/vyama vya wakulima na ulifanikiwa kununua tani 26,038.643 sawa na asilimia 143.2 ya lengo. Mchanganuo wa malengo unaonekana katika **Jedwali Na. 4**

**Jedwali Na. 5: Malengo ya Ununuzi na Utekelezaji**

| Kanda | Lengo (tani) | Utekelezaji (tani) |
|---|---|---|
| Arusha | 1,500 | 1,000 |
| Dodoma | 1,000 | 1,500 |
| Makambako | 6,500 | 8,961.52 |
| Songea | 6,182 | 11,557.529 |
| Sumbawanga | 3,000 | 3,019.594 |
| **Jumla** | **18,182** | **26,038.643** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo, 2018*

***134.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) inatekeleza Mikataba ya Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi Nafaka tangu tarehe 9 Desemba, 2017. Utaratibu wa kupata vibali vya ujenzi, usanifu na uandaaji wa michoro ya maghala na vihenge (*silos*) tayari umekamilika, jiwe la msingi liliwekwa tarehe 21 Aprili 2018 na ujenzi umeanza. Pamoja na kuongeza uwezo wa Wakala wa kuhifadhi chakula, mradi huu utaongeza soko la wakulima wa nafaka hususan mahindi.

***135.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wakala umepanga kununua jumla ya tani 28,200 za nafaka kupitia vituo vya ununuzi na vikundi/vyama vya wakulima. Aidha, Wakala utaendelea kutekeleza Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi Nafaka ambao unalenga kuongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka kutoka tani 251,000 za sasa hadi kufikia tani 700,000 ifikapo mwaka 2025. Kupitia mradi huo, ujenzi wa vihenge vya kisasa, maghala mapya, ofisi na ukarabati wa baadhi ya maghala utafanyika.

***136.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huo utatekelezwa kwa awamu mbili ambapo katika awamu ya kwanza mradi utaongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka kwa tani 250,000 hivyo

kufanya Wakala kuweza kuhifadhi 501,000 ifikapo 2020. Mradi huo utekelezwa katika kanda za Arusha (Babati - tani 40,000), Shinyanga (Shinyanga - tani 30,000), Songea (Songea - tani 55,000), Makambako (Makambako - tani 40,000 na Mbozi - tani 20,000), Sumbawanga (Sumbawanga - tani 20,000 na Mpanda tani 25,000) na Dodoma (Dodoma - tani 20,000). Aidha, Mradi huu ni jitihada za Serikali ambazo zitapelekea ukuaji wa uchumi nchini na kuchangia kuwezesha Tanzania ya viwanda. Kuongezeka kwa uwezo wa kuhifadhi kutawezesha maghala ya Wakala kuweza kuhifadhi akiba ya chakula ambayo itaendana na mahitaji halisi ya dharura kulinganisha na ongezeko la watu nchini.

### *Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo - AGITF*

***137. Mheshimiwa Spika,*** hadi mwezi Februari, 2018 Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (*Agricultural Inputs Trust Fund* -AGITF)imetumia Shilingi 2,391,246,400 kukopesha matrekta mapya 28, matrekta 3 madogo ya mkono (*power tiller*), mikopo 11 kwa ajili ya pembejeo za kilimo na mifugo, mikopo mitano (5) kwa ajili ya miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi, mikopo miwili (2) kwa ajili ya mifugo na uvuvi kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na 2.**

***138. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara kupitia AGITF imeendelea kufuatilia marejesho ya mikopo kwa mafanikio kama ifuatavyo; mwaka 2015/2016 lengo lilikuwa kurejesha Shilingi 5,764,141,824.00 na kiasi kilichorejeshwa ni Shilingi 5,009,547,428.00 sawa na asilimia 87; mwaka 2016/ 2017 lengo lilikuwa kurejesha Shilingi 6,749,151,392.00 kiasi kilichorejeshwa ni Shilingi 3,244,119,751.00 sawa na asilimia 48.1; mwaka 2017/2018 lengo lilikuwa kurejesha Shilingi 8,793,639,412.00 na hadi 3 Mei, 2018 kiasi kilichorejeshwa ni Shilingi 3,656,998,256.62 sawa na asilimia 42. Sababu za kuendelea kushuka kwa marejesho ni kutokana na hali ya hewa, hali ya uchumi na mapingamizi mahakamani. Kutokana na uzalishaji kuathiriwa na hali ya hewa, wakopaji walishindwa kupata mavuno ya kukidhi urejeshaji wa mikopo.

Aidha, kutokana na hali ya uchumi, dhamana zilizowekwa zimekuwa haziuziki kutokana na wanunuzi kuja na bei ndogo sana isiyokidhi thamani ya mkopo. Pia, kumekuwa na mapingamizi mengi mahakamani yanayosababisha kuwekwa kwa zuio lakuuza dhamana hata kwa wale wenye uwezo.

***139. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) imepanga kutoa mikopo ya mitambo ya mashambani (matrekta mapya) 57; mikopo 34 kwa ajili ya pembejeo za kilimo na mifugo; mikopo tisa (9) kwa ajili ya ukarabati wa zana za kilimo; mikopo mitatu (3) kwa ajili ya miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi; mikopo 16 kwa ajli ya fedha za kuendeshea kazi za shamba; mikopo miwili (2) kwa ajili ya kununua ardhi kwa ajili ya kilimo, mifugo na ufugaji samaki; mikopo saba (7) kwa ajili ya zana unganishi; na mikopo 10 kwa ajili ya zana za kusindika na vifungashio vya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Mpango huo ni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na 3.**

***Wakala wa Mbegu za Kilimo - ASA***

***140. Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) umezalisha tani 784.155 za mbegu bora zikiwemo mbegu bora za nafaka, mikunde na mbegu za mafuta ambapo kati ya hizo tani 650.045 wameuziwa wakulima. Aidha, miche bora ya Kahawa 1,163,758 imezalishwa ambapo kati ya miche hiyo, 207,358 imezalishwa Lyamungo (Kilimanjaro), 132,900 Ugano (Ruvuma), 646,800 Maruku (Kagera),71,000 Mwayaya (Kigoma), 100,000 Mbimba (Songwe) na 5,700 Tarime (Mara).

***141. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019 Wizara kupitia ASA imepanga kuzalisha mbegu bora za nafaka na mikunde tani 1,800. Aidha, kwa kushirikiana na Sekta binafsi itazalisha tani 1,500 katika shamba la Mbozi. Vilevile, itazalisha vipando bora vya Muhogo pingili 7,000,000 katika mashamba ya Mwele na Msimba na miche bora ya matunda 50,000 katika mashamba ya Bugaga na Arusha.

***Mamlaka ya Udhibitiwa Ubora wa Mbolea Tanzania- TFRA***

***142. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora wa Mbolea Tanzania *(Tanzania Fertilizer Regulatory Authority- TFRA*) imeendelea kudhibiti ubora wa mbolea nchini ambapo hadi mwezi Februari 2018, imesajili wafanyabiashara wa mbolea 430 na kufikia idadi ya wafanyabiashara wa mbolea 2,045 kwa nchi nzima. Aidha, TFRA imetoa vibali 286 vya kuingiza mbolea nchini ambapo tani 310,673.703 zimeingizwa. Vilevile, TFRA imefanya ukaguzi wa maghala na maduka ya wafanyabiashara wa mbolea kwenye Mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa, Kigoma, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Ruvuma, Geita, Mwanza, Mara, Simiyu, Shinyanga, Singida na Kigoma.

***143. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuanzishwa kwa Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja, Wizara kupitia TFRA imetoa bei elekezi ya mbolea kuanzia mwezi Septemba 2017 ambayo ilikuwa tofauti kutoka sehemu moja hadi nyingine kulingana na umbali na gharama za usafirishaji. Aidha, bei elekezi ilikuwa kati ya Shilingi 33,500 na 47,500 kwa mfuko wa kilo 50 wa mbolea ya kukuzia (UREA), mbolea ya kupandia (DAP) ilikuwa kati ya Shilingi 45,000 na 57,000. Bei hizo zilikuwa pungufu kwa wastani wa asilimia 11 hadi 40 ukilinganisha na bei ya mbolea aina ya DAP iliyokuwa ikiuzwa kati ya Shilingi 60,000 na 100,000 kwa mfuko wa kilo 50. Vilevile, TFRA ilitoa elimu kwa wadau wa mbolea juu ya Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja kupitia vikao kazi vya wadau, maonesho ya Nane Nane, vyombo vya habari hususan magazeti, redio, runinga na mitandao ya kijamii.

***144. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia TFRA itaimarisha Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa pamoja kwa kuhamasisha makampuni ya mbolea kuagiza mbolea kwa kiasi kikubwa katika kipindi ambacho bei ya mbolea kwa soko la dunia iko chini ili kuepuka ongezeko la bei katika soko la dunia. Aidha, TFRA itatoa elimu juu ya mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja kwa

wasambazaji (*agro – dealers*) wa mbolea katika Mikoa na Halmashauri; kusajili wafanyabiashara wa mbolea; kukagua na kutoa vibali vya kuingiza mbolea nchini.

### *Taasisi ya Uthibiti Ubora wa Mbegu - TOSCI*

***145. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Uthibiti Ubora wa Mbegu *(Tanzania Official Seed Certification Instiute-TOSCI)* imekagua mashamba ya mbegu hekta 8,103.08 ambapo hekta 24.3 sawa na asilimia 0.3 hazikukidhi viwango vya ubora. Aidha, TOSCI imefanya uhakiki wa uhalisia, ubora na sifa za aina mpya 126 za mbegu kwa ajili ya usajili. Vilevile, TOSCI imechukua sampuli 2,038 za mbegu za mazao mbalimbali na kupima ubora wake wa usafi, uotaji na afya ya mbegu ambapo asilimia 98 zilikidhi viwango vya ubora. Pia, maduka 893 ya wafanyabiashara wa mbegu yamekaguliwa na kuhakiki ubora ambapo asilimia 95 ya sampuli za mbegu zilizokaguliwa zilikidhi viwango vya uotaji. TOSCI pia imetoa vibali 860 vya kuingiza mbegu na vibali 11 vya kutoa mbegu nje ya nchi ambapo jumla ya tani 13,393 za mbegu zimeingizwa nchini.

***146. Mheshimiwa Spika,*** TOSCI imesajili wafanyabiashara 446 wa mbegu na kutoa lebo za mbegu 4,000,000 ambazo zinawekwa kwenye mifuko yote inayotumika kuuzia mbegu. Matumizi ya lebo hizo yamesaidia kupunguza tatizo la uuzwaji wa mbegu zisizo na ubora. Aidha, TOSCI imefungua kituo kipya cha udhibiti wa ubora wa mbegu katika Kanda ya Kusini chenye makao makuu yake Mtwara ili kurahisisha utoaji huduma katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma.

***147. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wakulima ili kuzitambua lebo za ubora zinazobandikwa na TOSCI. Pia, Wizara kupitia TOSCI itakagua hekta 20,000 za wakulima wa mbegu, itachukua sampuli 2,700 za mbegu na kupima ubora wake; itakagua maduka 1,500 ya wafanyabiashara wa mbegu na kusajili wafanyabiashara wa mbegu na kutoa vibali 1,500 vya kuingiza mbegu nchini. Aidha, TOSCI itahakiki upya,

uhalisia na sifa kwa aina 107 za mbegu mpya na kutoa lebo 15,000,000 kwa ajili ya kuweka kwenye mifuko ya kuuzia mbegu ili kukabiliana na tatizo la mbegu zisizo na ubora (feki). Mafunzo yatatolewa kwa wakaguzi wa mbegu 50 walioidhinishwa (*Authorised Seed Inspectors*). Pia TOSCI itafungua kituo cha udhibiti wa ubora wa mbegu katika mkoa wa Tabora kitakachotoa huduma kwenye mikoa ya Nyanda ya Magharibi. Vilevile, kupitia Mradi wa Kuongeza Uzalishaji wa Mpunga (ERPP), TOSCI itaimarisha ukaguzi wa mbegu bora za mpunga kabla na baada ya mavuno.

***Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu vya Kitropiki – TPRI***

***148. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia TPRI imekagua wafanyabiashara wa viuatilifu na kutoa mafunzo kwa wakufunzi juu ya matumizi ya kisheria ya viuatilifu. Hadi kufikia mwezi Machi 2018, jumla ya maduka 699 ya wafanyabiashara wa viuatilifu katika Mikoa ya Mwanza, Mtwara, Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Katavi, Rukwa, Morogoro, Kigoma, Tabora, Shinyanga, Simiyu, Manyara na Arusha yamekaguliwa ambapo maduka 75 yaliyokosa vigezo yalifungwa. Jumla ya makampuni 1,455 yalipewa vibali vya kuendesha biashara mbalimbali za viuatilifu wakiwemo, wafukizaji (213), waagizaji wa viuatilifu (1128), wauzaji rejareja na jumla (93), wachanganyaji viuatilifu(21). Aidha, mafunzo juu ya matumizi sahihi ya viuatilifu yametolewa kwa wakufunzi (ToT) 188 wakiwemo maafisa ugani, wauzaji wa viuatilifu na wakulima wawezeshaji kutoka katika Mikoa ya Kagera, Mwanza, Singida na Ruvuma.

***149. Mheshimiwa Spika,*** vilevile TPRI imefuatilia madhara ya viuatilifu kwa viumbe hai na mazingira kwa wafanyabiashara wadogo 19 wanaojihusisha na biashara ya viuatilifu. Jumla ya viuatilifu 292 vilijaribiwa na idadi ya watu 57 walibainika kuwa katika hatari ya kupata madhara. Aidha, TPRI ilipima madhara ya viuatilifu kwa wafanyakazi 481katika mashamba ya maua, kahawa, chai na viazi katika mikoa ya Iringa, Songwe, Manyara, Arusha na Kilimanjaro na waathirika walipewa ushauri stahiki. Wizara pia

imewaelimisha waathiriki kuhusu madhara ya sumu iliyomo kwenye viuatilifu na namna ya kujikinga na sumu hiyo ikiwemo kutumia vifaa vya kujikinga na kuepuka kutumia vifungashio bandia.

**150.** Aidha, TPRI iliendesha mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa wadau 1,016 katika mikoa ya Mwanza, Singida, Mtwara, Shinyanga, Ruvuma, Tanga, Simiyu na Lindi. Vilevile, TPRI ilitoa mafunzo ya viuatilifu sahihi na matumizi sahihi ya kudhibiti viwavijeshi vamizi (*Fall army warms*), Kantangaze (*Tuta absoluta*) na gugu karoti katika mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Iringa, Kagera, Dodoma, Tanga, Morogoro na Dar-es-salaam.

***151.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019 TPRI itatoa leseni na kukagua wafanyabiashara wa viuatilifu; itapima na kuangalia mabaki ya viuatilifu kwenye mazao yanayosafirishwa nje ya nchi; itaendesha mafunzo kwa maofisa ugani, wakulima na wafanyabiashara wa viuatilifu kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu hususan katika mazao ya korosho, pamba na mboga; itafanya uchunguzi wa viwango vya madhara ya viuatilifu kwa wakulima; itadhibiti visumbufu katika mazao yanayoingizwa nchini; itafanya utafiti wa kina katika visumbufu vya mimea, mifugo, binadamu vikiwepo vile vya mlipuko; na itakusanya, itatambua na kuhifadhi nasaba za mimea kwa ajili ya matumizi endelevu ya kilimo.

### 2.2.12 Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo

***152.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara imetoa mafunzo kwa ufadhili wa Serikali kwa wanafunzi 1,956 kwenye mafunzo ya kilimo ngazi ya Astashahada na Stashahada katika Vyuo vya Ilonga, Mlingano, Mtwara, Tumbi, Ukiriguru, Uyole, HORTI Tengeru, Mubondo, Maruku, KATC Moshi, Igurusi, KATRIN, Chuo cha Sukari Kidatu na Inyala. Vilevile, Wizara imedahili wanafunzi 246 wanaojilipia wenyewe ngazi ya Astashahada na Stashahada. Wanafunzi wa mwaka wa pili wa ngazi ya Stashahada ni 779 na ngazi ya Astashahada ni 332 ambao

wanategemea kuhitimu masomo yao mwezi Juni 2018. Kozi wanazosomea ni Astashahada na Stashahada ya Kilimo mseto, Stashahada ya Umwagiliaji, Matumizi Bora ya Ardhi, Uzalishaji Chakula na Lishe, Matumizi ya Zana za Kilimo, Uzalishaji wa Mazao, Mboga, Maua na Matunda.

***153. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imewezesha kikao cha kamati ya pamoja (*Joint Coordinating Committee*) kati ya Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) na kujadili utekelezaji wa Mradi wa TANRICE 2-*Project for supporting Rice Industry Development in Tanzania).* Aidha, katika mwaka 2017/2018 kupitia mradi wa TANRICE 2 vyuo sita vya mafunzo ya kilimo vya KATC, Mtwara, Ukiriguru, Igurusi, Ilonga na Tumbi vimetoa mafunzo kwa wananchi kuhusu mbinu bora za uzalishaji mpunga kwa njia ya umwagiliaji kwa wakulima 4,354 (me=2,266 na ke=2,091) katika skimu 25 za Mlenge (Iringa), Msufini (Kilombero), Itete (Malinyi), Lukenge (Mvomero), Mkomazi (Korogwe), Mandera (Korogwe), Kimbande (Nyasa), Sangamabuni (Mbinga), Budushi (Nzega), Lwenge (Geita), Kyota (Muleba) , Cheju (Zanzibar), Ng'ongo (Sumbawanga), Lwafi (Nkasi), Budagachi (Kilombero), Mlali (Mvomero), Matekwe (Nachingwea), Mtawatawa (Liwale), Namahoka (Namtumbo), Kiurio (Same), Igigwa (Sikonge), Miswaki (Uyui), Miyobwezi (Ukerewe) na Dobi na Tibirizi (Chakechake

***154. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia mradi wa TANRICE 2 imeendelea kutoa Mafunzo yaliyohusu menejimenti ya skimu za umwagiliaji, jinsia katika kilimo cha mpunga, masoko ya mpunga, teknolojia baada ya uvunaji na uendeshaji na menejimenti ya zana na mashine za kilimo. Wakulima 350 katika skimu za Madaba, Gonja Maya, Nyatwali na Bumbwisudi walipatiwa mafunzo ya jinsia katika kilimo na wakulima 120 walipatiwa mafunzo ya masoko ya mpunga katika skimu 4 za umwagiliaji za Likunja, Lipalwe, Ilonga na Mvumi.

***155. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya kilimo cha mpunga unaotegemea mvua kwa wakulima 1,174 wa kilimo cha mpunga wa mabondeni na wakulima 855 wa kilimo cha mpunga wa nchi kavu (NERICA)

katika Wilaya za Mkuranga, Ulanga, Micheweni, Kilwa, Mtwara Vijijini, Nzega, Kigoma Vijijini, Chato, Biharamulo, Korogwe, Muheza na Busokelo. Aidha, kupitia mradi wa TANRICE 2 wakulima wamejifunza mbinu na teknolojia mbalimbali zinazohusu kilimo cha mpunga ambazo zimewawezesha kuinua uzalishaji na vipato vyao. Kwa mfano katika skimu ya Lukenge (Kilombero) uzalishaji umeongezeka kutoka tani 2 hadi 4.9 kwa hekta; Mkomazi (Korogwe) tani 1.4 hadi 4.6 kwa hekta; Kimbande (Nyasa) tani 2.5 hadi 5.9 kwa hekta; na Namahoka (Namtumbo) tani 2.3 hadi 7.5 kwa hekta.

***156. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara itadahili wanafunzi 2,300 ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa ufadhili wa Serikali. Aidha, Wizara itandaa mtaala wa Stashahada ya Matumizi Bora ya Ardhi (*Diploma in Land Use Planning*) katika mfumo wa moduli; itahuisha mtaala wa Stashahada ya mboga, maua na matunda (*Diploma in Horticulture*); na itakarabati miundombinu ya vyuo vya mafunzo ya kilimo vya Mlingano, KATC, HORTI Tengeru, Tumbi, Maruku, Mubondo na Ukiriguru yakiwemo madarasa, ofisi, mabweni, maktaba, bwalo la chakula na nyumba za watumishi.Vilevile, Vituo vitano (5) vya wakulima vya Mkindo, Ichenga, Bihawana, Themi na Inyala vitafanyiwa ukarabati na kupatiwa vitendeakazi.

### 2.2.13 Kuunda na kupitia Sera na Sheria za Sekta ndogo ya Mazao

***157. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Alliance for Green Revolution in Africa (AGRA) kupitia Mradi wa MIRA ilifundisha maafisa 19 wa Wizara kuhusu stadi za uchambuzi wa Sera na taratibu za maandalizi ya nyaraka za Baraza la Mawaziri. Mpango wa Wizara ni kujenga uelewa wa watumishi wake ili kuhakikisha kuwa, maamuzi yote ya Kisera yanafanywa kwa kuzingatia uwepo wa ushahidi kutoka kwenye uchambuzi wa kitafiti.

***158. Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kwamba kwa mwaka 2017/2018, Wizara ilifanya maboresho ya Kisera,

Kisheria, Kanuni na Mikakati mbalimbali ya kilimo ili kuweka mazingira mazuri ya uendeshaji na uwekezaji katika Sekta ya Kilimo nchini. Katika jitihada hizo, Serikali ilifuta ada na tozo za mazao 78 kati ya 139 zilizokuwa hazina tija kwa wakulima. Kufuatia hatua hiyo, Wizara ilifanya marekebisho ya kanuni na sheria zilizoanzisha tozo na ada husika ili kuwezesha utekelezaji wa marekebisho hayo. Serikali inasisitiza kuwa utekelezaji wa sheria na kanuni hizo uzingatiwe na kwamba hatua kali zitachukuliwa kwa wale wote watakaokiuka.

***159. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuchambua na kubaini ada na tozo ambazo bado ni kero kwa wakulima nchini na kuzifuta. Lengo ni kubakiza ada na tozo ambazo zina mahusiano ya moja kwa moja na uendelezaji wa mazao husika, kama vile uendelezaji wa utafiti wa mazao. Kwa msingi huo, Wizara inapendekeza kufuta ada na tozo 21 **(Kiambatisho Na. 4)** ambazo kwa mwaka 2017/18 zimeonekana ama kuwa kero kwa wakulima au vikwazo kwa maendeleo ya sekta ya kilimo. Ada na tozo zinazopendekezwa kufutwa ni 3 katika tasnia ya chai, 3 tasnia ya kahawa, 2 tasnia ya tumbaku na tozo moja moja kwa tasnia ya sukari na pamba. Aidha, kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa pembejeo, inapendekezwa kufuta tozo 5 kwenye uzalishaji wa mbegu. Vile vile, kwa ajili ya kuimarisha maendeleo ya ushirika nchini, inapendekezwa tozo 6 katika ngazi mbali mbali za ushirika zifutwe.

***160. Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imewasilisha Wizara ya Fedha na Mipango mapendekezo ya kuboresha mfumo wa kodi na tozo kwa lengo la kuboresha mazingira wezeshi ya uwekezaji na uendeshaji biashara katika shughuli za kilimo. Mapendekezo hayo, hususan yanalenga kutoa unafuu wa kodi katika vifungashio vya mazao na mbegu za mazao ya kilimo, mabomba ya kunyunyuzia madawa *(Knapsack Sprayers),* mashine na mitambo ya usindikaji wa mazao, miundombinu ya uzalishaji na hifadhi ya mazao ya bustani na kulinda wazalishaji wa ndani dhidi ya ushindani usio sawa wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Mpango wa Wizara

ni kuhakikisha kero zote zinazokwamisha maendeleo ya tasnia ya mazao ya kilimo zinashughulikiwa.

***161.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia itakamilisha taratibu za kujiunga na Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika ya Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa aina Mpya za Mbegu za Mimea [*The Protocol for Protection of New Varieties of Plants (Plant Breeders' Rights) in The Southern African Development Community-SADC*]. Itifaki hiyo inalenga kuwezesha nchi wanachama wa Jumuiya ya SADC kutoa Hakimiliki kwa Wagunduzi wa mbegu na kuhamasisha utafiti na ugunduzi wa mbegu bora zinazoendana na mabadiliko ya tabianchi.

***162.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itakamilisha utaratibu wa kupata ithibati ya Shirika la Kimataifa la Udhibiti wa Mbegu (*International Seeds Testing Association-ISTA*) ya maabara ya uthibiti wa ubora wa mbegu (TOSCI) ili kurahisha biashara ya mbegu na hivyo kuongeza upatikanaji na matumizi ya mbegu bora nchini. Katika hatua nyingine, Wizara itakamilisha marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Mimea ya mwaka 1997, Sheria ya Mbegu ya mwaka 2003 na Sheria mbalimbali za mazao (*Crop laws).* Aidha, Wizara itakamilisha mapendekezo ya kutunga Sheria mpya ambazo ni pamoja na Sheria ya Kilimo cha Mkataba; Sheria ya Zana za Kilimo, Sheria ya Huduma za Ugani; na Sheria ya Kulinda Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula.

### 2.2.14 Kuimarisha Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini ya Sekta

***163.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Kilimo (*Annual Performance Report*) kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Wizara pia iliboresha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za Kilimo (*Agriculture Routine Data System - ARDS*) kwa kuongeza vipengele muhimu kwa ajili ya kuainisha na kurahisisha uingizaji wa takwimu. Wizara pia imeandaa mfumo wa kupima matokeo ya Programu ya Kuendeleza

Sekta ya Kilimo awamu ya pili (ASDP II *Result Framework*) pamoja na viashiria.

***164.*** **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na FAO inatekeleza mradi wa uboreshaji na uhakika wa takwimu za utabiri wa uzalishaji wa mazao ya chakula nchini. Mradi huu unafanyika kwa majaribio (pilot)katika mikoa ya Morogoro,Tanga na Kagera ambapo uainishji wa pointi za sampuli katika mikoa hiyo na nyenzo (madodoso, GPS, Mizani na Tablets) za kufanyia utafiti kwa misimu ya msimu na vuli zimeandaliwa. Aidha, mafunzo kwa maafisa ugani kuhusu matumizi ya nyenzo hizo kwa njia ya kitaalam ya survey solution yalifanyika.

***165.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara itafanya Sensa ya Kilimo (*National Sample Census of Agriculture - NSCA*) kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo Mifugo Maliasili na Uvuvi – Zanzibar, Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Aidha, Wizara itaandaa Taarifa ya Utekelezaji (*Annual performance report*) pamoja na kufanya tathmini ya usambazaji na matumizi bora ya mbolea kwa wakulima kupita mfumo wa ununuzi wa pamoja (*bulk procurement*). Wizara itaendelea kuboresha mfumo wa ARDS ili kuufanya uwe rahisi zaidi kwa wadau.

***166.*** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeratibu na kushiriki kwenye Mikutano ya Mabaraza ya Mawaziri wa Kilimo kwa kushirikisha ngazi zote ambapo mikakati ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi na wa Usalama wa Chakula ilijadiliwa na kupitishwa. Aidha, andiko la maridhiano ya Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo kwa upande wa Afrika Mashariki (EAC- CAADP Compact) limekamilika na kuridhiwa na Mawaziri.

***167.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia, imeratibu na kuhudhuria Mikutano ya Baraza la Mawaziri wa Kilimo kwa Nchi za jumuiya ya Kusini mwa Afrika (SADC) kwa ngazi zote, ambapo rasimu ya fursa na changamoto zilizopo katika Sekta

ya Kilimo imeandaliwa. Vilevile, Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo wa SADC (SADC *Agriculture Development Fund*) umeridhiwa na umeainisha idadi ya miradi, vikundi vya wakulima, Sekta Binafsi na jamii ambazo zitapatiwa mikopo kwenye mfuko huo.

***168. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kuhudhuria mikutano ya FAO, IFAD, EU, Umoja wa Mataifa (UN) kwa ngazi ya wataalam waandamizi ambapo bajeti na miradi mbalimbali ya kikanda na nchi wanachama imepitishwa ikiwemo, miradi ya kiufundi ya kuimarisha masoko katika kilimo na kudhibiti magonjwa na visumbufu vya mimea kama sumu kuvu na viwavijeshi.

***169. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki kwenye mikutano ya nchi wahisani ambapo ilikutana na Mabalozi na wataalam wa nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, India, Norway, Israel, Korea ya Kusini, Iran, Saud Arabia, Uholanzi na Japan kuzungumzia mashirikiano yanayoendelea na ya baadaye katika Sekta ya Kilimo na taarifa za maeneo yaliyokubaliwa zimeandaliwa, ambapo Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Sekta ya Kilimo Tanzania na Misri imesainiwa. Wizara pia imeratibu na kupitia upya rasimu ya Hati ya Makubaliano ya ushirikiano kati ya Sekta ya Kilimo Tanzania, Iran na India.

***170. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa na kuratibu wadau wa Sekta ya Kilimo kushiriki katika makongamano ya biashara na uwekezaji katika Sekta ya Kilimo yaliyofanyika Vietnam, Madagasca, China na India. Wadau wa Sekta ya Kilimo walishiriki na kuweka mikakati ya ushirikiano (joint *venture*). Wizara imeratibu na kuhudhuria kikao cha kamati cha kuwezesha biashara *Trade Facilitation Agreements* ili kukidhi matakwa ya Shirika la Biashara la Kimataifa (*World Trade Organization* - WTO). Rasimu tano (5) za miradi ya kuwezesha mazingira mazuri ya kufanya biashara zimeandaliwa na kupitishwa. Rasimu hizo ni *Publication; Enquire Points; Test Procedures; Perishable Goods;* na *Border Agency Cooperation.*

**171. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuainisha, kuandaa na kutekeleza mashirikiano ya Kikanda na Kimataifa. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu, kupitia na kuandaa Hati ya Makubaliano, Mikataba na Maandiko kwa ajili ya majadiliano na Mashirika/nchi wahisani. Vilevile, Wizara itawezesha na kushiriki mikutano mbalimbali na kuandaa taarifa kuhusu masuala ya biashara za Kimataifa, kama WTO, EPA na AGOA.

### 2.2.15 Mpango wa Kuendeleza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania - SAGCOT

**172. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kuratibu uwekezaji kwenye Mpango wa Kuendeleza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT). Hadi sasa jumla ya Dola Milioni 500 zimewekezwa katika Kilimo kwenye ukanda wa SAGCOT kati ya Dola Bilioni 3.5 zilizopangwa kuwekezwa ifikapo mwaka 2030. Kati ya uwekezaji huo Dola Bilioni 2.4 zitatokana na Sekta Binafsi. Aidha, wawekezaji wakubwa binafsi wameweza kuunganishwa na wakulima ili kuongeza tija, kipato, chakula na lishe kwenye kaya za wakulima wa soya, chai, viazi vitamu na mviringo, mpunga, mboga na matunda.

**173. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Kituo cha SAGCOT imewezesha kufanyika kikao cha wadau wa Sekta ya kifedha na kutia saini Hati ya Makubaliano (MoU) ya kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wakulima wadogo. Wadau waliohusishwa ni pamoja na *Financial Sector Deepening Trust* (FSDT), SAGCOT Centre Ltd, *Agriculture Market Development Trust* (AMDT) and SAGCOT *Catalytic Trust Fund* (CTF). Dhumuni la MoU hiyo ni kuanzisha uratibu wa huduma maalum kwa wakulima wadogo katika mnyororo wa thamani wa mazao.

**174. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia kituo cha SAGCOT kwa kushirikiana na Baraza la Nafaka la Afrika Mashariki (*Eastern Africa Grain Council* - EAGC) waliandaa mdahalo uliowakutanisha wafanyabiashara na wakulima wa zao la Soya kwa lengo la kupata soko la uhakika. Matokeo

ya kongamano hilo umewezesha Kampuni ya NASSAD *Animal Feeds* kusaini mkataba wa kununua Soya ya ujazo wa Tani 4,000 kwa bei ya Shilingi 1,000 kwa kilo. Kabla ya kongamano Kampuni ya Silverlands ilinunua soya kiasi cha Tani 2,500 kutoka kwa wakulima wadogo Wilayani Songea kwa thamani ya Shilingi bilioni 2.5.

***175.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia mradi wa mbegu ya viazi mviringo Mkoani Njombe kwa ufadhili wa AGRA, Kituo cha SAGCOT na wadau wengine wakiwemo Yara, Syngenta, Mtanga Foods Ltd, Halmashauri za Njombe Mji, Njombe Vijijini na Wang'ingombe na wakulima wadogo walifanikiwa kuongeza uzalishaji wa viazi mviringo kutoka wastani wa tani 7 kwa hekta mwaka 2015 hadi kufikia tani 31 kwa hekta mwaka 2017.

***176.*** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, wakulima waliweza kupata mbegu bora za viazi mviringo kiasi cha tani 2,325 na takriban wakulima wapatao 9,305 walipata mafunzo ya kilimo bora cha viazi kupitia vipindi vya mafunzo kwa wakulima vilivyohusu teknolojia za kisasa. Zaidi ya wakulima 2,351 wanatumia mbegu bora za viazi mviringo, teknolojia mbalimbali za utunzaji wa shamba na uvunaji wa viazi mviringo. Aidha, kilianzishwa Chama cha Ushirika chenye wanachama 280 na kusajiliwa pamoja na kujenga maghala nane (8) kwa ajili ya kuhifadhia viazi mviringo.

***177.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuwepo kwa ubia wa zao la viazi mviringo, kampuni mpya ya kusindika viazi mviringo inayoitwa Tanzanice Ltd imesajiliwa. Kampuni hiyo imejikita katika kuzalisha viazi mviringo na kusafirisha matunda ya parachichi kwenda nchi za Ulaya. Uwepo wa Kampuni ya Tanzanice imeongeza idadi ya wadau katika kutatua changamoto ya zao la viazi mviringo katika mnyororo wa thamani.

***178.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa kilimo itapanua uzoefu uliopatikana kutoka SAGCOT kuendeleza kilimo kwenye maeneo mengine nchini. Hivyo, Wizara inao mpango

madhubuti wa kuendeleza kilimo kwenye Ukanda wa Ziwa hususan kujenga mabwawa yatakayotumika kwenye kilimo cha umwagiliaji. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Wabia wa Maendeleo na Wadau wengine wa Sekta ya Kilimo ili kufikia malengo ya Sekta.

### 2.2.16 Kuimarisha Masuala Mtambuka

***Ushiriki wa Vijana katika Kilimo***

***179. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kuongeza Ushiriki wa Vijana Katika kilimo kwa kuwajengea uwezo wa kujiajiri kwenye Sekta ya Kilimo ili kutatua tatizo la ajira nchini. Wizara kwa kushirikiana na *Farm Africa* wamewezesha mafunzo ya uzalishaji na ujasiriamali wa mazao ya kilimo kwa vijana 96,365 ambapo kati ya hao 56,805 ni wa kiume na 39,560 ni wa kike. Juhudi hizo zilifanyika katika mikoa ya Manyara, Shinyanga, Singida, Dodoma na Morogoro ambapo mafunzo hayo yalihusu mazao ya ufuta, mahindi, maharage, mpunga, uyoga na asali.

***180. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *Aga Khan Foundation* (AKF) katika mikoa ya Pwani, Lindi, na Mtwara kupitia mradi wa *Coastal Rural Support Program Tanzania* (CRSPT) imewezesha vijana 29,700 kwa kapata mafunzo ya kilimo biashara, ujasiriamali, kuweka na kukopa katika mikoa hiyo. Wizara pia kwa kushirikiana na *Sokoine University Graduate Enterprenuer Cooperatives* (SUGECO) wametoa mafunzo mbalimbali kwa vijana wapatao 540 wakiwemo wakike 227 na wakiume 313 katika kituo cha Mkongo kilichokuwa kinasimamiwa na RUBADA. Mafunzo hayo yalihusu uzalishaji kupitia mashamba darasa na kilimo biashara na mnyororo wa thamani wa mazao ya kitalu nyumba (*Green Houses*).

***181. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Vijana Kushiriki katika Kilimo na Kuongeza ajira kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta. Aidha, Wizara kwa

kushirikiana na Wadau wa maendeleo FAO, *Aga Khan Foundation*, *Heifer International*, SUGECO na *Farm Africa* wataendelea kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo vijana katika masuala ya ujasiliamali, kilimo biashara kwa mazao mbalimbali ili kuongeza thamani na kutoa ajira kwa vijana wengi nchini.

***VVU na UKIMWI***

***182.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI mahali pa kazi, Wizara imeendelea kuwahamasisha watumishi kupima afya ili kutambua hali zao. Katika mwaka 2017/2018 Wizara imeendelea kuwahudumia watumishi 15 wanaoishi na VVU kulingana na miongozo ya Serikali.

***183.*** ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari na kuendelea kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na VVU na wanaougua UKIMWI.

***Jinsia***

***184.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imehusisha masuala ya jinsia katika utafiti wa kilimo (*Gender Mainstreaming*) kupitia mradi wa *"Sweet potato Fast Truck*" uliofanyika Wilaya za Mkuranga (Pwani), Bukoba na Misenye (Kagera) ikiwa na lengo la kutathmini ushirikishwaji wa jinsia katika kilimo cha Viazi vitamu. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa mamlaka ya kuuza mazao yenye kipato, kudhibiti na kutoa maamuzi yanamilikiwa na wanaume kwa asilimia 70 na wanawake kwa asilimia 30. Baada ya tathmini, mafunzo yalitolewa kwa watafiti, maafisa ugani na waalimu wa kilimo 35, kati ya hao wanawake ni 19 na wanaume ni 16 kutoka Kanda ya Ziwa, Kaskazini na Zanzibar. Pia kwa maafisa ugani, walimu wa kilimo wa shule za msingi na viongozi wa vijiji 93, kati ya hao wanawake ni 28 na wanaume ni 65. Mafunzo yalihusu kuhamasisha jamii, tathmini na matumizi ya mbinu husishi ya nyenzo zinazozingatia jinsia katika kilimo.

**185. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuelimisha watafiti umuhimu wa kuhusisha jinsia katika miradi ya kilimo kwa manufaa ya wakulima wa jinsia zote. Kuandaa mwongozo wa kilimo na jinsia (*pocket guide*) wa maafisa ugani kwa ajili ya kufundishia wakulima na kijarida mkeka (*comic series*) kwa watoto wa shule za msingi waliopokea mbegu za viazi vitamu kwa ajili ya uelewa wa kilimo na jinsia kwa wilaya za Mkuranga, Bukoba na Misenyi.

***Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi***

**186. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na FAO na CARE International imetoa mafunzo na kusambaza Mwongozo wa Kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi kwa Wakuu wa Mikoa yote, Wakuu wa Wilaya zote, na kwa maafisa Mipango, maafisa Kilimo na Mazingira, maafisa Ugani na wawakilishi wa asasi zisizo za kiserikali kutoka Halmashauri za Wilaya 36 za Mikoa ya Morogoro, Iringa, Mbeya, Songwe, Mwanza, Dodoma, Tabora, Arusha, Mtwara, Lindi, Singida, Kigoma, Manyara, Rukwa, Ruvuma na Kagera.

**187. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wakulima kupitia Mradi wa Kuongeza Uzalishaji na Tija kwa zao la Mpunga (*Expanded Rice Production Project – ERPP*) imeandaa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii (*Environmental and Social Management Plans - ESMPs*) kwa ajili ya utekelezaji ili kutunza mazingira ya skimu za umwagiliaji za Kigugu, Mbogo-komtonga, Mvumi, Msolwa Ujamaa na Njage, pia maandalizi ya Mwongozo wa Hifadhi ya Mazingira na Mpango shirikishi wa kudhibiti visumbufu vya mimea na matumizi sahihi ya viuatilifu katika skimu hizo unaendelea.

**188. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya ufuatiliaji wa ujumuishwaji wa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya Halmashauri za Wilaya za Mikoa ya Morogoro (Mvomero), Iringa (Iringa DC), Mbeya (Rungwe), Dodoma (Dodoma MC), Singida (Singida DC) na Arusha (Arumeru) ambapo tathmini hiyo imeonesha ujumuishwaji wa masuala ya mazingira na mabadiliko ya

tabianchi katika mipango ya Halmashauri bado yana changamoto kama ufinyu wa bajeti na uelewa mdogo kwa viongozi na wataalamu wa wilaya juu ya athari za mabadiliko ya tabianchi katika uchumi wa halmashauri zao . Kwa hali hiyo, Wizara inaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa kazi ya kuwajengea uelewa wakulima kuhusu masuala ya mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi na jinsi ya kukabiliana nazo. Pia wakulima wapatao 160 wa Wilaya za Igunga, Manyoni, Mbinga, Mbozi na Mpanda pia walipatiwa mafunzo juu ya teknolojia na mbinu za utunzaji wa mazingira katika uzalishaji wa Tumbaku.

***189.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na wadau wa SAGCOT waliweza kuandaa mwongozo na mfumo wa kutathimni jinsi wawekezaji na wadau wa SAGCOT wanavyotekeleza uhifadhi wa mazingira na masuala ya kijamii katika kongani ya Ihemi. Mfumo huu uliweza kutathimi wawekezaji 15 katika kongani hiyo na mkoa wa njombe. Mfumo huu ulionyesha wengi wa wawekezaji wanajitahidi katika kuhifadhi mazingira na kujumuisha jamii, ingawa gharama za kufanya tathimini ya hifadhi ya mazingira pamoja, kukatika kwa umeme, wingi wa kodi na uelewa juu ya masuala ya tabianchi na vipaumbele vya nchi ni bado unahitajika.

***190.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kutekeleza Mpango wa miaka mitano wa Kilimo kinachohimili mabadiliko ya Tabianchi (Agriculture Climate Resilient Plan) wa mwaka 2014, wizara kwa kushirikiana na Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA) inatekeleza mradi wa kujenge uwezo wa kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi kwa usalama wa chakula. Mpaka sasa mashamba darasa katika mikoa ya Dodoma (Kongwa), Tabora(Uyui) yameshaanzishwa kwaajili ya kuonyesha na kufundishia wakulima mbinu na teknolojia za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi, pia wakulima wanafundishwa jinsi yakutafsiri na kutumia taarifa za hali ya hewa katika kilimo kwa mikoa hiyo.

***191.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya kilimo pia imefanikiwa kujenga uwezo kwa wadau wa kilimo katika

kongano ya Ihemi juu ya dhana ya uchumi wa Kijani "Green Economy" kwa kushirikiana na Mpango wa Kuhifadhi Mazingira wa Umoja wa Mataifa "UNEP" na SAGCOT Centre Limited. Katika mradi huu wizara iliweza pia kuleta pamoja taarifa mbali mbali zinazohusu uhifadhi wa mazingira na kilimo endelevu katika kongani ya Ihemi. Wizara pia iliweza kutengengeza mpango shirikishi wa matumizi bora ya ardhi kwa kongani hiyo ya Ihemi kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia taarifa juu ya njia bora za uhifadhi wa maji kwa ajili ya kuhifadhi ardhi oevu na vyanzo vya maji katika kongani ya Ihemi pia ilifanyika. Matumizi ya umwagiliaji kwa njia ya matone umeonekana kuwa ni njia bora ya kuhifadhi maji na kuleta kilimo chenye tija hasa kwa wakulima wa nyanya katika mkoa wa Iringa.

***192. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kufuatilia ujumuishaji wa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi katika Halmashauri za Wilaya za Mikoa ya Mtwara na Lindi. Vilevile, Wizara itaandaa, itachapisha na kusambaza mwongozo wa Hifadhi ya Mazingira na Mpango Shirikishi wa udhibiti visumbufu vya mimea na matumizi sahihi ya viuatilifu katika lugha ya Kiswahili. Aidha, Wizara itazijengea uwezo Halmashauri za Wilaya katika Mikoa ya Kagera, Mbeya, Iringa, Morogoro na Kilimanjaro wa kutambua umuhimu wa kujumuisha njia za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika bajeti na mipango ya maendeleo ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo.

### 2.2.17 Kuendelea kutekeleza Mpango wa Serikali kuhamia Dodoma

***193. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kutekeleza agizo la Serikali la kuhamia Dodoma katika awamu tatu, ambapo katika awamu hizo watumishi 316 waliokuwa Makao Makuu ya Wizara Dar es salaam wamehamia Makao Makuu Dodoma.

***194. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuhamisha watumishi wake kuja Makao Makuu Dodoma.

## 3.0 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2017/2018 na Mpango kwa Mwaka 2018/2019 (Fungu 24)

### 3.1 Mapato na Matumizi ya Fedha katika Kipindi cha mwaka 2017/2018 (Fungu 24)

***195. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Wizara chini ya Fungu 24 ilitengewa jumla ya Shilingi 6,293,857,760 zikijumuisha Shilingi 2,413,888,760 za Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO). Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,456,634,072 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo zikiwa ni Shilingi 942,577,072 za Tume na Shilingi 514,057,000 za COASCO. Jumla ya Shilingi 4,837,223,688 zilitengwa kwa ajili ya mishahara ambapo Shilingi 2,937,391,928 zilikuwa ni mishahara ya watumishi wa Tume na Shilingi 1,899,831,760 ni kwa ajili ya watumishi wa COASCO. Aidha, Katika mwaka huo, Fungu 24 halikutengewa fedha za bajeti ya matumizi ya maendeleo.

### 3.2 Fedha zilizotolewa katika Bajeti ya Kawaida

***196. Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi 2018, fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa kutoka Hazina zilikuwa ni Shilingi 3,854,197,441.41 sawa na asilimia 61.24 ya kiasi kilichoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, jumla ya Shilingi 2,745,882,013.41 zilikuwa kwa ajili ya shughuli za Tume, ambapo shilingi 2,239,309,730 zilikuwa ni mishahara ya watumishi wa Tume na Shilingi 506,072,283.41 matumizi mengineyo. Aidha, jumla ya Shilingi 1,108,815,428 zilikuwa ni kwa ajili ya shughuli za COASCO, ambapo Shilingi 971,733,828 zilikuwa ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi na Shilingi 137,081,600 Matumizi mengineyo.

### 3.3 Matumizi

***197.*** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi, 2018, Wizara chini ya Fungu 24 imetumia jumla ya Shilingi 3,854,197,441.41 sawa na asilimia **100** ya fedha zilizopokelewa. Kati ya kiasi hicho, Shilingi 2,745,382,013.41 zilitumika kulipa Mishahara ya watumishi wa Tume na Matumizi mengineyo. Aidha, Shilingi 971,733,828 zilitumika kulipa Mishahara ya watumishi wa COASCO na Shilingi 137,081,600 Matumizi mengineyo.

***198.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/2018, Wizara chini ya Fungu 24 imeendelea kutekeleza majukumu yake ya **Uhamasishaji, Usimamizi na Udhibiti** ili kufikia malengo ya kijamii na kiuchumi na kupunguza umasikini nchini kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kupitia Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025), Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Maelekezo ya Serikali ya mwaka 2017/2018, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020 na Mpango Mkakati wa Tume wa mwaka 2017/2018 pamoja na mapitio ya Bajeti ya mwaka 2016/2017.

### 3.4 Ukaguzi na Uchunguzi

***199.*** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi, 2018, Wizara imefanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa vyama vya ushirika 2,896 sawa na asilimia 55.7 ya lengo la kukagua vyama 5,200 katika mwaka 2017/18. Aidha, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) limefanya ukaguzi wa mwisho kwa vyama vya ushirika 1,520 sawa na asilimia 18.91 ya lengo la kukagua vyama 8,040. Katika kaguzi hizi, Wizara ilibaini mapungufu mbalimbali yakiwemo ukosefu wa Kanuni na Será mbalimbali, Utunzaji wa kumbukumbu usioridhisha, uingiaji wa mikataba usiokidhi matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika, watendaji wa vyama wasiokuwa na sifa stahiki, vyama kuwa na madeni sugu, viongozi na watendaji kutokuwa na elimu ya ushirika pamoja na ubadhirifu unaofanywa na viongozi pamoja na watendaji.

***200. Mheshimiwa Spika***, kutokana na mapungufu yaliyobainika wakati wa ukaguzi, Wizara imechukua hatua mbalimbali za utatuzi ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa viongozi na watendaji, kuwajengea uwezo katika kuandaa Será na Kanuni za vyama kwa mujibu wa Sheria na kuchukua hatua pale inapobainika ubadhirifu ikiwemo kuondoa Bodi za Uongozi na watendaji na kuweka bodi za muda kama vile bodi za SCCULT Ltd, TFC, MAMCU Ltd, NCU na WETCU.

***201. Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya uchunguzi maalum katika Vyama vya Ushirika 8 visivyo vya kifedha vya Matendo AMCOS, Luponde AMCOS, MBIFACU AMCOS Ltd, Lupembe AMCOS Ltd, SUDI AMCOS, Lihimalyao AMCOS, RIVACU Ltd na MAMCU Ltd. Matokeo ya uchunguzi huo yalibaini uwepo wa ubadhirifu na ukiukwaji wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 kwenye vyama vya MBIFACU Ltd na MAMCU Ltd uliosababishwa na usimamizi na utendaji mbovu wa viongozi na watendaji. Watuhumiwa wamefikishwa katika mamlaka husika kwa hatua zaidi za kisheria.

***202. Mheshimiwa Spika***, watuhumiwa mbalimbali walihojiwa kutokana na dosari zilizobainishwa kwenye taarifa za uchunguzi ili kuweza kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria ikiwa ni pamoja na kutoa hati za madai. Viongozi pamoja na watendaji wa vyama vya Ushirika vya Muhimbili SACCOS, Mlimani SACCOS, BOT SACCOS, Mbinga SACCOS, Kurugenzi Mbinga SACCOS, Ayalabe SACCOS, Madibila SACCOS, Wazalendo SACCOS na Arusha Kurugenzi SACCOS walihojiwa na Hati za madai zimeandaliwa kwa watuhumiwa 57 wa ubadhirifu wa kiasi cha Shilingi Bilioni 5.95 katika vyama saba. Aidha, watuhumiwa wanne wa ubadhirifu katika chama cha Wazalendo wamefikishwa mahakamani na rufaa zilizokatwa na watuhumumiwa wengine sita kuzipinga hati za madai zinashughulikiwa.

***203. Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha usimamizi wa SACCOS, Wizara imeingia makubaliano na Taasisi ya Dun & Bradstreet Credit Bureau Tanzania Ltd ya kutengeneza mfumo wa kielektroniki wa usimamizi (*SACCOS*

*Supervision Software)* ambapo kwa sasa upo kwenye majaribio. Mfumo huu utawezesha kupatikana kwa taarifa za mara kwa mara juu ya maendeleo ya SACCOS ikiwa ni pamoja na kufanya usimamizi kwa ufanisi na urahisi zaidi. Aidha, jumla ya nyaraka 10 za makubaliano (MoU) kati ya Wizara na wadau wengine wa Ushirika zimeandaliwa na kusainiwa

***204. Mheshimiwa Spika***, Wizara imepitia, kuchambua na kushauri juu ya uandaaji wa Kanuni za Kiutumishi za vyama vikuu vya NJORECU Ltd, MBIFACU Ltd, SONAMCU Ltd, CHUTCU Ltd, WETCU Ltd, RUNALI Ltd, RIVACU Ltd, TANECU Ltd, MAMCU Ltd na TAMCU Ltd ambazo zitasaidia vyama kuwa na Nyaraka ambazo zinatoa mwongozo wa utendaji kazi na stahili mbalimbali za viongozi.

***205. Mheshimiwa Spika***, katika msimu wa korosho wa 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Leseni za Ghala, Bodi ya Korosho, Vyama Vikuu vya Ushirika, TAMISEMI pamoja na mamlaka nyingine imeweza kusimamia minada zaidi ya 57 na uendeshwaji wa biashara ya zao la korosho kupitia Vyama vya Ushirika chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani, Tanga na Ruvuma. Usimamizi huo umepelekea kupanda kwa bei ya korosho ghafi kutoka wastani wa Shilingi 4,000.00 kwa kilo msimu wa 2016/2017 hadi kufikia Shilingi 4,128.00 kwa kilo msimu wa 2017/2018.

***206. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuliwezesha Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) kufanya ukaguzi wa nje wa hesabu za Vyama vya Ushirika 8,040. Aidha, Wizara kupitia Tume itafanya ukaguzi wa mara kwa mara na usimamizi wa karibu wa uendeshaji wa vyama vya Ushirika nchini. Wizara itakagua Vyama Vikuu vya Ushirika 47, Miradi ya Pamoja na 34, Vyama vya Ushirika vya Msingi 10,909 nchini. Vilevile, Wizara itawezesha kuandaliwa kwa Kanuni za kiutumishi na uendeshaji na mfumo wa usimamizi wa nyaraka kwa vyama vya Ushirika nchini.

### 3.5 Mapitio ya Mikataba katika Vyama vya Ushirika

**207.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imepitia na kufanya upekuzi wa mikataba katika vyama vya Ushirika na kuifanyia marekebisho, ikiwemo mkataba wa mbolea, madawa na vifungashio kati ya Chama Kikuu cha Ushirika Songea Namtumbo (SONAMCU Ltd) na kampuni ya PRIME, Mkataba wa kilimo cha viazi kati ya RIVACU Ltd na Crop Biosciences Solution Ltd, Mkataba wa Pango kati ya TFC na Kampuni ya Interstar Mining Ltd, Mkataba wa ukusanyaji wa madeni kati ya TUR SACCOS na Chimbuko VICOBA, Mkataba wa usambazaji wa magunia ya korosho kwenye Chama Kikuu cha TANECU Ltd, Mikataba ya usambazaji mbolea katika vyama vya vikuu vya WETCU Ltd, LATCU Ltd, KTCU Ltd na CHUTCU Ltd, Mikataba ya chai, Mikataba ya ajira ya NJORECU Ltd na mkataba wa kununua kahawa kati ya Kaderes Peasant Development PLC na Magate AMCOS Ltd.

**208.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kusimamia na kutoa ushauri kuhusu mikataba inayoingiwa na vyama vya ushirika nchini ili kudhibiti na kupunguza migogoro katika vyama vya ushirika.

### 3.6 Usimamizi wa Chaguzi za Viongozi wa Bodi za Vyama

**209.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha Utawala Bora, Wizara imesimamia chaguzi za viongozi wa Vyama Vikuu vya Ushirika na Miradi ya Pamoja 12 sawa na asilimia 26.7 ya lengo la kusimamia vyama 45 kwa mwaka 2017/18. Aidha, Wizara kwa kushirikana na Mamlaka za Serikali za Mitaa iliratibu na kusimamia chaguzi za vyama vya msingi vya kifedha na visivyo vya kifedha 5,599 sawa na asilimia 93.3 ya lengo la kusimamia chaguzi za vyama 6,000 kwa mwaka 2017/2018.

**210.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa

itaratibu na kusimamia chaguzi za Vyama Vikuu na Miradi ya Pamoja 36 na vyama vya ushirika vya msingi 5,000 nchini.

### 3.7 Utatuzi wa Migogoro na Malalamiko katika Vyama vya Ushirika

***211.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/2018, Wizara imetatua migogoro mbalimbali ikiwemo mgogoro kati ya Chama kikuu cha Ushirika Njombe (NJORECU LTD) na kampuni ya Njombe Filling Station, mgogoro kati ya Chama cha Ushirika cha Wakulima wadogo wa Kilimo cha Mpunga-Dakawa Morogoro (UWAWAKUDA) na wanachama wake, mgogoro kati ya Chama cha Ushirika cha Wakulima wa Mpunga katika skimu ya Ruvu (CHAURU) na Mwekezaji, mgogoro kati ya Chama cha Ushirika cha Viwanda vidogo Dar- es-salaam (DASICO) na wanachama walioachishwa uanachama, mgogoro kati ya Chama cha Ushirika cha Mshikamano Baraza SACCOS cha Mpwapwa na benki ya TIB, mgogoro kati ya SHIRECU Ltd na wafanyakazi wake, mgogoro kati ya baadhi ya SACCOS za Mkoa wa Morogoro na Chimbuko vikoba ambaye ni mtoa huduma ya ukusanyaji madeni na mgogoro kati ya TIB na baadhi ya SACCOS za Mkoani Manyara.

***212.*** ***Mheshimiwa Spika***, Vilevile, Wizara imeshughulikia malalamiko mbalimbali ya wanachama wa vyama vya Ushirika ikiwa ni pamoja na kutoa msaada wa kisheria kwenye jumla ya mashauri 14 katika vyama vya Ushirika vya Mikoa ya Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Dodoma, Mwanza, Morogoro, Dar es salaam na Iringa.

***213.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara itasimamia ili kuimarisha misingi ya utawala bora na uwajibikaji katika vyama vya ushirika ili kupunguza au kuondoa kabisa migogoro na malalamiko yasiyo ya lazima katika vyama vya ushirika nchini. Wizara itaendelea kutatua migogoro na malalamiko yaliyopo katika vyama vya ushirika nchini.

### 3.8 Usajili wa Masharti ya Vyama vya Ushirika

***214.*** ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2017/2018, Wizara ilipitia masharti na nyaraka mbalimbali za vyama na kusajili Masharti ya vyama 121 vikiwemo vyama vikuu vya Biharamulo (BCU LTD), Chama Kikuu cha Ushirika cha Nyanza (NCU), Chama Kikuu cha Ushirika Lake Tanganyika Tobacco Growers (LATCU Ltd), Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL),Kigoma Tobacco Cooperative Union KTCU Ltd, Chunya Tobacco Cooperative Union (CHUTCU Ltd), Rift Valley Cooperative Union (RIVACU), Western Tobacco Cooperative Union (WETCU Ltd), Tunduru Agricultural Cooperative Union (TAMCU Ltd) na Arusha Cooperative Union (ACU Ltd). Pia, Tume imetoa usajili wa kudumu kwa vyama vikuu vya Lindi Mwambao na RUNALI vya Lindi. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea na usajili wa Masharti na Nyaraka mbalimbali zitakazowezesha uendeshaji wa shughuli katika vyama vya ushirika unaofuata Sheria, Kanuni na taratibu za ushirika.

### 3.9 Uhamasishaji kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na Wadau wengine

***215.*** ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kuhamasisha umma hususan vijana, wanawake na vikundi vyenye mwelekeo wa Ushirika kujiunga au kuanzisha Vyama vya Ushirika. Kufuatia uhamasishaji huo, vyama vya Ushirika vipya 394 vilianzishwa na kusajiliwa vikiwemo chama cha Ushirika cha Mradi wa pamoja wa Wakulima wa miwa Magole cha Kilosa, Chama cha Ushirika cha Mradi wa pamoja wa Chai Njombe (NJOTCOJE LTD), vyama vya Msingi vitatu vinavyojihusisha na kilimo cha chai vya Itabaha, Pamwanga na Uwiluma vya Mkoani Njombe, vyama vya Msingi 18 vinavyojihusha na kilimo cha miwa vya Mkoani Morogoro na vyama vya Ushirika vya walaji 12 vya Ngorongoro Arusha. Aidha, jumla ya wanachama wapya takribani 385,295 walijiunga na ushirika, vyama hivi vinakadiriwa kutoa ajira mpya kwa wananchi takribani 1,182. Sambamba na hilo, Tume imeandaa Rasimu ya Mwongozo wa Uhamasishaji utakaotumika na timu za uhamasishaji.

**216.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa ushirika nchini imeratibu na kuwezesha kufanyika kwa majukwaa ya ushirika kwa mikoa 23 ya Manyara, Pwani, Arusha, Tanga, Njombe, Mbeya, Katavi, Rukwa, Lindi, Mwanza, Kagera, Singida, Tabora, Kigoma, Songwe, Iringa, Shinyanga, Simiyu, Ruvuma, Dar es salaam, Mara na Geita pamoja na Jukwaa la Ushirika la kitaifa lililofanyika mkoani Dodoma. Lengo la majukwaa haya lilikuwa ni kuwakutanisha wanaushirika na Wadau ili kujadili fursa, changamoto pamoja na kutafuta njia za utatuzi. Pia, jitihada zimefanyika na kuwezesha kuundwa au kufufuliwa kwa Kamati za Elimu ya Ushirika za Mikoa husika zinazosimamia shughuli za Ushirika na kuimarisha ushirikiano wa Wadau.

**217.** **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi hicho, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa ushirika ikiwemo SCCULT na TFC imeratibu na kufanikisha kufanyika kwa maadhimisho ya Siku ya Ushirika wa Akiba na Mikopo Duniani (ICUD), Siku ya Ushirika Duniani (SUD) na kushiriki katika maonesho ya siku ya wakulima NaneNane. Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na washiriki takribani 1,083 ambao ni pamoja na viongozi wa serikali, maafisa Ushirika, wanachama wa vyama vya Ushirika, wananchi na Wadau mbalimbali wa Ushirika. Katika maadhimisho hayo, vyama vilipata fursa ya kuonesha bidhaa zao na kujitangaza. Aidha, masuala ya maendeleo ya ushirika na utatuzi wa changamoto zinazokabili vyama vya Ushirika yalijadiliwa kwa pamoja na kutafutiwa ufumbuzi. Wizara iliandaa na kutangaza vipindi vinane vya televisheni na makala mbili za masuala ya Ushirika ziliandaliwa na kutangazwa katika vyombo mbalimbali vya habari.

**218.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Tume kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) imehamasisha wanachama 9,188 wa Vyama Vikuu vya Lindi Mwambao, RUNALI Ltd, TANECU Ltd na MAMCU Ltd kwenye Mikoa ya Lindi na Mtwara kujiunga na fao la Bima ya Afya lijulikanalo kama Ushirika Afya.

**219.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa GEPF imehamasisha

wanachama wa vyama vya ushirika katika mikoa ya Lindi na Mtwara kujiunga na huduma za hifadhi ya jamii ambapo jumla ya wanachama 650 wa mikoa hiyo wamejiunga na Mfuko kwenye fao lijulikanalo kama **Ushirika na Akiba** na uhamasishaji unaendelea.

***220.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019 Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wadau mbalimbali itaendelea kuhamasisha umma hususan vijana, wanawake na vikundi vyenye mwelekeo wa Ushirika kujiunga na au kuanzisha Vyama vya Ushirika ili kuongeza idadi ya vyama vya Ushirika na wanachama nchini lengo likiwa ni kufika wanachama 5,000,000 ifikapo Juni 2019. Aidha, Wizara itaendelea kufufua na kuimarisha vyama vya Ushirika hususan vya pamba katika Mikoa ya kanda ya ziwa, magharibi na kati ili kufufua uzalishaji wa zao la pamba.

***221.*** ***Mheshimiwa Spika*** Vile vile, Wizara itaendelea kuratibu na kutoa elimu ya ushirika kwa umma, Viongozi wa kisiasa na watendaji wa Taasisi mbalimbali na Vyama vya Ushirika (Wajumbe wa bodi, Watendaji wa Vyama na Wanachama) kupitia maonesho ya Kilimo (Nane nane), Siku ya Chakula Duniani, ICUD na Siku ya Ushirika Duniani kwa lengo la kuimarisha maendeleo ya vyama vya ushirika. Wizara itandaa na kuwezesha kurushwa kwa matangazo kupitia vyombo mbalimbali vya habari kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya ushirika. Vilevile, Wizara itafanya mikutano ya uhamasishaji kuhusu ushirika katika vyuo 7 vya elimu ya juu nchini. Aidha Wizara itaendelea kuhamasisha na kuunganisha Vyama Vya Ushirika 600 na mifuko ya hifadhi ya kijamii na taasisi za kifedha nchini.

### 3.10 Kujenga na Kuimarisha Uwezo wa Kiuchumi katika Vyama vya Ushirika

***222.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kujenga na kuimarisha uwezo wa kiuchumi katika vyama vya Ushirika, Wizara imeandaa Rasimu ya Hati ya Makubaliano (MoU) kati yake na BRITEN inayohusu uongezaji thamani ya mazao ya

vyama vya Ushirika nchini. Vilevile, Rasimu za Miongozo ya Masoko na Uwekezaji imeandaliwa ili iweze kutumika na vyama vya Ushirika katika kuimarisha upatikanaji wa masoko na uwekezaji. Aidha, Tume imevikutanisha vyama vya Ushirika vya walina asali vipatavyo 46 katika Mikoa ya Singida, Tabora na Kigoma na kujadili changamoto za soko la asali kwa lengo la kuzitatua.

**223. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/ 2019, Wizara itaendelea kuhamasisha na kuvijengea uwezo vyama vya Ushirika kuanza na kuendelea kuuza mazao yao kupitia mifumo rasmi ya masoko na yenye tija, pamoja na kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara itaendelea kuvijengea uwezo vyama vya Ushirika kuzalisha mazao ya biashara ya kimkakati (Korosho, Kahawa, Tumbaku, Pamba, na Chai) na mazao mengine pamoja na kutambua mapato ya wakulima yanayopatikana kupitia vyama vya Ushirika. Wizara itaendelaea kufuatilia mikopo inayotolewa kwa wanaushirika na mafanikio yake, ikiwa ni pamoja na kutambua thamani ya uwekezaji wa mtaji wa Ushirika katika Taasisi mbalimbali za kifedha.

***224. Mheshimiwa Spika***, Vile vile, Wizara itaendelea kuvijengea uwezo vyama vya Ushirika kutafuta Wabia na Wadau wengine kuanzisha au kufufua viwanda vya kuongeza thamani za mazao ya biashara yanayokusanywa na vyama husika kwa lengo la kuinua kipato cha mwanachama mmoja mmoja. Wizara itahamasisha na kuviunganisha Vyama Vya Ushirika 600 na wadau wa maendeleo wa uongezaji thamani mazao ya biashara pamoja na kuwezesha uandaaji na utekelezaji wa mipango ya uwekezaji katika Vyama hivyo. Aidha, Wizara itawezesha uandaaji wa Mipango Mikakati na Biashara kwa Vyama vya Vikuu vya Ushirika 50 nchini.

### 3.11 Kujenga uwezo wa Tume katika kutoa Huduma kwa Wadau

***225. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/2018, Wizara imekamilisha uteuzi wa Mwenyekiti na Makamishna

10 wa Tume, ambapo vikao viwili kikiwemo cha mafunzo ya kuwajengea uwezo wa masuala ya utawala na uongozi vilifanyika. Tume imeratibu vikao viwili vya watumishi wote na vikao viwili vya Warajis Wasaidizi wa Mikoa kwa lengo la kukumbushana wajibu na majukumu pamoja na kutathmini utendaji kazi wa Tume kwa mwaka mmoja.

***226.*** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuboresha Ofisi zake Mikoani kwa kuanzisha Mfumo wa Utunzaji Kumbumbuku katika ofisi za Warajis Wasaidizi wa Mikoa ya Mwanza, Dar es Salaam, Dodoma, Kagera, Manyara na Shinyanga. Aidha, taratibu za maandalizi ya ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu zipo katika hatua ya kukamilisha malipo ya ununuzi wa kiwanja ambapo hadi kufikia Machi, 2018 kiasi cha shilingi 30,000,000 zimeshalipwa sawa na asilimia 38.6 ya jumla ya shilingi 77,622,300 zinazohitajika kulipwa.

***227.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019 Wizara itaendelea kuboresha Ofisi zake Mikoani kwa kuanzisha Mfumo wa Utunzaji Kumbumbuku katika ofisi za Warajis Wasaidizi wa Mikoa 19 iliyobaki. Vilevile, Wizara itaendelea na taratibu za maandalizi ya ujenzi wa ofisi ya Tume Makao Makuu, Dodoma. Aidha, Wizara itaendelea kuibua, kuimarisha na kusimamia vyanzo vya mapato vya ndani ili kuimarisha usimamizi wa vyama vya Ushirika nchini.

### 3.12 Maendeleo ya Watumishi

***228.*** ***Mheshimiwa Spika***, Katika kuwajengea uwezo watumishi wake, Katika mwaka 2017/2018, Wizara imewezesha kutolewa kwa mafunzo ya usimamizi wa utunzaji kumbukumbu kwa maafisa wawili na mafunzo ya muda mfupi kwa wahasibu wanne yaliyotolewa na Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi. Vilevile, katika kipindi hicho, Mafunzo ya Menejimenti ya Viashiria hatarishi yametolewa kwa watumishi 35 wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

***229.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuajiri na kuhamisha watumishi kulingana

na mahitaji na kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu kwa ufanisi, kutoa stahili na motisha kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu za kiutumishi.

### 3.13 Utafiti na Mafunzo

***230.*** ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2017/2018, Wizara imefanya tafiti nne katika kuendeleza sekta ya Ushirika nchini. Tafiti mbili zimefanyika katika Mikoa ya Kilimanjaro na Kigoma zikilenga kubaini changamoto zinazowakabili wanachama wa vyama vinavyojihusisha na uzalishaji wa zao la kahawa. Kutokana na matokeo ya tafiti hizi, Tume kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali imeendelea na uhamasishaji wa matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika zao la kahawa kupitia vyama vya Ushirika badala ya kupitia kwenye vikundi na wanunuzi binafsi wanaowanyonya wakulima.

***231.*** ***Mheshimiwa Spika***, Utafiti mwingine ulilenga kubaini changamoto za Ukaguzi na Usimamizi wa vyama vya Ushirika nchini. Kutokana na utafiti huu, Wizara imeendelea kuimarisha Ukaguzi na Usimamizi wa vyama vya Ushirika nchini.

***232.*** ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi hicho, Wizara pia imefanya utafiti wa kubaini mahitaji ya mafunzo (upembuzi yakinifu) kwenye vyama vya ushirika vinavyojishughulisha na mazao ya kahawa na korosho katika mikoa ya Kigoma, Mtwara na Lindi. Utafiti huu umeiwezesha Tume kuandaa programu ya mafunzo katika mikoa hiyo na kutoa mafunzo kwa viongozi na watendaji 46 wa vyama vikuu na miradi ya pamoja.

***233.*** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia watoa huduma kwenye vyama vya ushirika ambapo watoa huduma 57 wamesajiliwa na kupewa vibali vya kutoa huduma za mafunzo, ukaguzi wa nje, TEHAMA na ukusanyaji madeni. Katika kuratibu na kusimamia watoa huduma hao, Tume imeandaa mwongozo wa watoa huduma kwenye vyama vya ushirika.

**234.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuratibu na kufuatilia mafunzo yatolewa na watoa huduma kwenye Vyama vya Ushirika 40 nchini. Wizara itaendelea kufanya tafiti mbalimbali kuhusu maendeleo ya Ushirika na mchango wa vyama vya Ushirika katika shughuli za kijamii na ukuaji wa pato la taifa.

**235.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa viongozi na watendaji kutoka vyama 15 vya akiba na mikopo, vilevile katika kutekeleza matakwa ya kisheria yanayoelekeza SACCOS kuwa katika makundi mawili SACCOS zenye Leseni na zisizokuwa na Leseni, kwa kuzingatia takwa hili la kisheria Wizara imetoa mafunzo kwa wajumbe wa Bodi pamoja na watendaji juu ya utoaji wa leseni na Usimamizi wa SACCOS zenye leseni kwa washiriki 378 kutoka kwenye vyama 189. Tume imepokea maombi ya leseni kutoka kwenye vyama 15 kati ya 50 na uchambuzi yakinifu unaendelea juu ya maombi hayo. Aidha, yametolewa mafunzo ya usimamizi wa nje na mahala pa chama (off-site & on-site supervision) kwa viongozi 413 kutoka kwenye SACCOS 196

**236.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuwezesha, kuratibu na kufanya mafunzo ya uongozi na utawala bora kwa viongozi, wanachama na watendaji 500 wa vyama vya ushirika nchini. Vilevile itaratibu na kutoa mafunzo kwa wakaguzi 192 katika usimamizi na uendeshaji wa vyama vya ushirika nchini. Wizara itachapisha na kusambaza nakala 7000 za Sheria ya Vyama vya ushirika na Kanuni 1000 za vyama vya Ushirika.

**237.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara imefanya kazi ya kuzitambua mali za Vyama Vikuu vya Ushirika 37, Miradi ya Pamoja 7 na Benki za Ushirika 2 ili kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi ziweze kurasimishwa

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuvijengea uwezo vyama vya Ushirika katika kuzitambua na kurasimisha mali za vyama vya ushirika kwa ajili ya uwekezaji. Wizara itawezesha uanzishwaji na

utekelezaji wa mpango wa uwekezaji kwa vyama vya ushirika 600 nchini. Aidha, Wizara itafanya uhakiki wa hali ya Vyama vya Ushirika katika Mikoa 16 ya Tanzania Bara pamoja na kusimamia ukusanyaji wa takwimu za Vyama vya Ushirika nchini.

## 4.0 HITIMISHO NA SHUKRANI

### 4.1 Hitimisho

***238.*** ***Mheshimiwa Spika***, sekta na shughuli za kilimo hapa nchini ni muhimu kwa maisha na ustawi wa uchumi kwa watu wengi hapa nchini. Kimsingi, kilimo ni nyenzo muhimu katika mapambano dhidi ya umaskini, kupanua fursa za ajira, kushirikisha wananchi wengi katika mnyororo wa thamani na biashara kimataifa, na ni msingi wa mageuzi tarajiwa kuelekea uchumi wa viwanda na kipato cha kati. Hata hivyo, mchango wa sekta hii katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii hausadifu fursa kubwa tuliyonayo kama nchi. Kwa kiasi kikubwa hali hii inachangiwa na mambo ambayo yapo ndani ya uwezo wetu, hususan kuwa na mawazo mgando kuhusu uendeshaji wa kilimo na mapokeo ya maumbile asili ya dunia.

***239.*** ***Mheshimiwa Spika,*** tumedhamiria kuondokana na mgando huu kwa kufanya mageuzi makubwa katika uendeshaji wa shughuli za kilimo. Chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP-II) na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano tumebaini maeneo manne ya kuongoza mageuzi ya kilimo na maisha ya wakulima nchini ikiwa ni pamoja na:

(i) Kuongeza uzalishaji na tija katika shughuli za wakulima;

(ii) Kusimamia kikamilifu hifadhi na matumizi jadidifu ya maji, ardhi na mazingira sambamba na kuongeza miundombinu ya umwagiliaji;

(iii) Kuweka msukumo katika mabadiliko ya fikra na mazingira ya kibiashara kwa sekta ya kilimo kwa lengo la kubadili mtazamo wa uendeshaji kilimo kama shughuli ya kujikimu na badala yake iendeshwe kibiashara kwa faida ya nchi na wakulima; na

(iv) Kuweka mfumo mpya wa usimamizi wa kilimo kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi kwa uendeshaji kibiashara na kuwezesha wakulima kuwa na sauti katika uendeshaji na biashara ya mazao yao.

***240. Mheshimiwa Spika,*** dhamira hii ya Serikali ni endelevu na ya kweli. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuanza utekelezaji wa hatua hii ya mageuzi kwa ari na mifano ya dhati. Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo ya kuondoa kero na vikwazo visivyostahili walivyowekewa wakulima kwa miaka mingi. Kwa maelekezo hayo mimi sioni sababu za kusita kuchukua yanayostahiki. Nawaomba waheshimiwa Wabunge waniunge mkono katika mageuzi haya.

## 4.2 Shukrani

***241. Mheshimiwa Spika***, naomba nitumie nafasi hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Kwanza napenda kuzishukuru nchi za Japan, Marekani, Uingereza, Ireland, Malaysia, China, Indonesia, Korea ya Kusini, India, Misri, Israel, Ubelgiji, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil, Uholanzi, Vietnam na Poland. Nayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, ILRI, CABI, CFC, AVRDC, AGRA, CIP, UNEP, WARDA, Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani (DLCO-EA), HELVETAS, Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu (IRLCO-CSA), *Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust*, *Rockfeller Foundation, Aga Khan Foundation, Unilever* na Asasi zisizo za kiserikali nyingi ambazo hatuwezi kuzitaja zote hapa.

Ushirikiano na misaada ya nchi na mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini.

***242. Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa (Mb); Katibu Mkuu Mhandisi Mathew John Mtigumwe; Naibu Katibu Mkuu Dkt. Thomas Didimu Kashilila; Wakurugenzi wa Idara na Wakuu wa Vitengo; Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara; watumishi wote wa Wizara; na wadau mbalimbali wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2017/2018 kama nilivyofafanua katika hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba, nitaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2018/2019. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha kitabu cha hotuba ya bajeti ya mwaka 2018/2019.

## 5.0 MAOMBI YA FEDHA MWAKA 2018/2019

***243. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19 Wizara inaomba idhini ya kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi **2,315,010,000**. Maduhuli hayo yanatokana na faini mbalimbali na ada ya cheti cha afya ya mimea katika uingizaji wa mazao ya kilimo nchini na usafirishaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi.

***244. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara ya Kilimo inaomba jumla ya **Shilingi 170,273,058,000** kupitia fungu 43 na fungu 24 kama ifuatavyo;

***FUNGU 43***

***245. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi 162,224,814,000** zinaombwa kupitia Fungu 43. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 98,119,516,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo na **Shilingi 64,105,298,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 28,560,428,000** ni kwa

ajili ya Mishahara ya Wizara, **Shilingi 14,346,253,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Bodi na Taasisi, **Shilingi 12,727,150,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara na **Shilingi 8,471,467,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Bodi na Taasisi.

***FUNGU 24***

***246. Mheshimiwa Spika***, jumla ya **Shilingi 8,048,244,000** zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kupitia Fungu 24. Kati ya fedha hizo, Shilingi **2,199,700,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), Shilingi **4,013,370,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Tume na **Shilingi 1,835,174,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Taasisi

***247. Mheshimiwa Spika,*** **NAOMBA KUTOA HOJA**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho lako. Sasa namuita Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA (MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa afya hii kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, naomba kuisoma hii taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na majukumu mengine jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara ya Kilimo. Vilevile Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, inataka Kamati kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo inajumuisha mafungu mawili ambayo ni Fungu 43 -Wizara ya Kilimo na Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Aidha, taarifa hii inaeleza masuala makubwa matano yafuatayo:-

(a) Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/ 2018;

(b) Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018;

(c) Mapitio ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018;

(d) Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019; na

(e) Maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipochambua maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo takribani kumi na moja (11), kama ilivyoorodheshwa katika kipengele (a) mpaka (k) kwenye kitabu mlichopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati haujatekelezwa kutokana na mtiririko wa fedha usioridhisha. Baadhi ya shughuli zilizoshindwa kutekelezwa kikamilifu ni kama zilivyoorodheshwa katika kipengele (a) mpaka (d) katika kitabu mlichopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha fedha kilichoidhinishwa. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ya Kilimo, kwa Fungu 43, liliidhinishiwa jumla ya Sh.214,815,759,000. Kati ya fedha hizo, Sh.64,562,759,000 ni fedha za matumizi ya kawaida na Sh.150,253,000,000 ni fedha za maendeleo, ambapo Sh.59,600,000,000 ni fedha la ndani na Sh.90,653,000,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa utoaji fedha zilizoidhinishwa. Hadi kufikia Machi, 2018, fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa ni jumla ya Sh.36,069,819,172 ambayo ni asilimilia 55.87 ya kiasi kilichoidhinishwa. Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo fedha zilizotolewa zilikuwa Sh.27,231,305,232.69 sawa na asilimia 18 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizotolewa Sh.25,576,120,000 ni fedha za ndani na Sh.1,655,185,232. 60 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Kilimo Fungu 43 ilikadiria kukusanya mapato ya Sh.2,015,010,000. Hadi kufikia Machi 2018, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Sh.1,708,724,841.68 ambayo ni sawa na asilimia 84.80 ya malengo ya ukusanyaji. Kamati inaitaka Wizara kuongeza jitihada kukusanya mapato zaidi kadri ya makadirio kwani sekta ya kilimo ina fursa nyingi na za uhakika za kuwezesha Serikali kupata mapato zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na kutolewa kwenye Fungu 24. Fungu hili liliidhinishwa jumla ya Sh.6,293,857,760 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, Fungu hili halikutengewa fedha za maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2018 kiasi cha Sh.3,216,391,509.45 zilitolewa ambayo ni sawa na asilimia 51.1 ya kiasi kilichoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni kuhusu mwenendo na utoaji wa fedha. Kwa miaka mitatu mfululizo, fedha zinazoidhinishwa na Bunge hazikutolewa kama zilivyoidhinishwa hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo

yaliyopangwa ikiwa ni pamoja na kutofanyiwa kazi ushauri wa Kamati katika maeneo mengi kama ilivyoelezwa hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa uchambuzi unaonesha kupanda kwa asilimia ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo kutoka asilimia 3.31 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi asilimia 18 kwa mwaka wa fedha 2017/2018, bado ongezeko la mtiririko wa kiasi cha fedha zinazotengwa na kutolewa katika bajeti ya kilimo haiwiani na mahitaji halisi ya sekta ya kilimo. Aidha, Fungu 24 kutotengewa fedha ya maendeleo kwa miaka mitatu mfululizo kwa maelezo kwamba fedha za maendeleo kwa ajili ya Tume zinakasimiwa kupitia Fungu 43 inaleta ugumu kwa Tume kuweza kupanga na kutekeleza mipango yake ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2018, Fungu 43 lilikuwa limepokea Sh.27,231,305,232.69 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Fedha hizo ni sawa na asilimia 18 ya kiasi kilichoidhinishwa cha Sh.150,253,000,000. Kamati haikuweza kukagua miradi ya mendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2017/2018 kwa kuwa fedha zilizotolewa zilitumika katika hatua za awali za uratibu wa kutekeleza miradi iliyopangwa. Hivyo, hakukuwa na miradi iliyotekelezwa kwa namna ya kuweza kukagua katika maeneo ambayo Kamati ilifanya ziara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hiyo, Kamati ilikagua mradi wa umwagiliaji wa *DADPS* katika Halmashauri ya Kigoma uliotekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na wahisani wa maendeleo ambao ulipelekewa fedha katika bajeti za miaka ya nyuma wakati kanuni zinaitaka Kamati kukagua miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha husika. Taarifa ya ukaguzi wa mradi huo pamoja na ushauri wa Kamati imefafanuliwa kwa kirefu katika taarifa ya Kamati mliogawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea na kuchambua mpango wa bajeti wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo

uchambuzi wa bajeti hii ya Wizara ya Kilimo ilihusu mafungu mawili ambayo ni Fungu 43 - Wizara ya kilimo na Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Wizara ya Kilimo kupitia mafungu yote mawili inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.170,273,048,972. Kati ya fedha hizo, Fungu 43 linaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.162,224,814,000 kati ya fedha hizo Sh.64,105,298,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.98,119,516,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa upande wa Tume ya Ushirika - Fungu 24, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.8,048,234,972. Kiasi kinachoombwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli. Wizara kupitia mafungu yake inatarajia kukusanya jumla ya maduhuli kiasi cha Sh.2,315,010,000 fedha ambazo zitapatikana kutoka vyanzo mbalimbali vilivyoainishwa kwenye taarifa ya Kamati. Fedha zinazoombwa zinapangwa kutekeleza malengo mbalimbali ya Wizara ambayo yameainishwa kama inavyoonekana katika taarifa ya Kamati mliyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepitia kuchambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika mipango ya bajeti ya mwaka 2018/2019 na kuridhishwa nayo. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa malengo na vipaumbele vilivyoainishwa vimekuwa vikijirudia kila mwaka kutokana na kasi ndogo ya utekelezaji wake unaosababishwa na kiasi kidogo cha fedha kinachotengwa na kutolewa kila mwaka. Pamoja na umuhimu wa sekta ya kilimo kama inavyoelezwa kupitia mipango, sera na mikakati mbalimbali ya Serikali bado sekta hii imekuwa haipewi msukumo wa kutosha kama kipaumbele cha uhai na ustawi wa sekta zingine za uzalishaji mali kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kushuka kwa bajeti inayotengwa na kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati katika uchambuzi wake, imebaini kuendelea kushuka kwa bajeti, inayotengwa na kutolewa kwa ajili ya Sekta ya Kilimo kila mwaka. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 bajeti ya kilimo ilikuwa ni asilimia 7.8 ya bajeti yote ya Serikali, mwaka wa fedha 2011/2012 ilikuwa ni asilimia 6.9 ya bajeti yote ya Serikali, mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali ilitenga asilimia 4.9 tu ya bajeti yote ya Serikali kwa ajili ya sekta ya kilimo na mwaka wa fedha 2017/2018 ilitenga asilimia 4.8 ya pato lake kwa ajili ya Kilimo. Ni dhahiri kwamba mwenendo huu wa uwekezaji mdogo kwenye sekta ya kilimo, unakinzana na dhana ya uchumi wa viwanda ambao malighafi ya viwanda kwa kiasi kikubwa inatokana na bidhaa zitokanazo na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi umebaini pia kuwa Tanzania ni ya mwisho katika Ukanda wa Afrika Mashariki kwa kupata asilimia 3.1 kati ya 10 katika utekelezaji wa Azimio la Malabo. Nchi nyingine za Afrika Mashariki zinaelekea kutenga asilimia kubwa ya pato lake la mwaka kwa ajili ya kilimo na hivyo kuwa kichocheo cha sekta ya kilimo kukua na kuongeza tija katika uzalishaji ukilinganisha na Tanzania. Nchi zilizofanya vizuri ni pamoja na Rwanda, Kenya, Burundi na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji mdogo unaofanywa na Serikali kwenye kilimo unaathiri pato na ustawi wa wananchi walio wengi ambao wanategemea kilimo kama njia kuu ya uzalishaji mali. Kamati inatahadharisha kuwa, endapo hatua madhubuti hazitachukuliwa katika kuinua sekta ya kilimo ni dhahiri kuwa mdororo wa uchumi na mnyororo wa umaskini utaendelea kuwa wimbo mahali pengi nchini. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutambua umuhimu wa kutekeleza kwa vitendo Mkataba wa Azimio la Maputo na Malabo ambao unazitaka nchi wanachama kutenga asilimia 10 ya pato ghafi kwa ajili ya sekta ya kilimo kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa bajeti ya maendeleo iliyotengwa kwa miaka miwili ya mwaka 2017/2018 na 2018/2019 katika

mafungu ya sekta ya kilimo na kubaini kuwa jumla ya fedha za maendeleo zilizotengwa kwa Fungu 43 kwa mwaka 2018/2019 ni pungufu kwa asilimia 34.7 ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Tume ya Maendeleo ya Ushirika - Fungu 24 haijatengea fedha za maendeleo. Hata hivyo, Kamati imefahamishwa kuwa, kwa sasa fedha za miradi ya maendeleo kwa Fungu 24 zimekasimiwa kupitia miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo kupitia mradi wa *Agricultural Support Developemnt Program(ASDP)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati. Naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo 14 ya Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Mtiririko usioridhisha wa fedha za miradi ya maendeleo. Upo udhaifu mkubwa katika kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za Kilimo. Kupungua kwa kiasi cha fedha kinachotengwa na mtiririko usioridhisha wa fedha za miradi ya maendeleo ni dhahiri kutaendelea kusababisha kasi ndogo ya ukuaji wa sekta ya kilimo kama inavyodhihirisha katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya kilimo kutoka asilimia 4.8 ya sasa hadi kufikia asilimia 10 ya Pato la Taifa kwa ajili ya kilimo, kama ilivyoelezwa katika Azimio la Maputo na Malabo ili kuweza kuwa na ukuaji wa sekta ya kilimo kwa asilimia Sita ifikapo 2025.

(ii) Upatikanaji wa uhakika wa mbolea nchini. Pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa mbolea nchini ikiwa ni pamoja na kutekeleza mfumo wa Ununuaji wa Mbolea kwa Pamoja (*Ferterlizer Bulk Procurement*), bado upatikanaji wake katika maeneo mbalimbali haukidhi mahitaji. Mfumo wa ununuzi

wa mbolea kwa pamoja unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(a) Bei ya mbolea bado ni ghali ikilinganishwa na matarajio ya Serikali ya kuanzisha mfumo huu;
(b) Mbolea iliyonunuliwa kupitia mfumo huu haifiki kwa wakulima kwa wakati;
(c) Kutozingatiwa kikamilifu kwa bei elekezi; na
(d) Uhaba wa mawakala/wasambazaji wa mbolea katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kufanyia kazi changamoto hizo hasa kwa kutambua kuwa Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja ni mkakati ya muda mfupi ya kuhakikisha kunakuwepo na upatikanaji wa mbolea katika vipindi vyote vya msimu wa kilimo. Aidha, ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha Taifa linakuwa na suluhisho la kudumu la upatikanaji wa mbolea kwa bei nafuu na kwa wakati ili kuondokana na uagizaji wa mbolea kutoka nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kutekeleza kwa vitendo azma yake ya kuzalisha mbolea hapa nchini, kwa kujenga viwanda vya kuzalisha mbolea pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya kuwezesha sekta binafsi kushiriki na kuwekeza katika tasnia ya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inaendelea na juhudi za ujenzi wa viwanda vya mbolea ili kupunguza adha ya ukosefu wa mbolea, Kamati inashauri kuwa ni vema Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa pamoja ukafanyika mara tatu (3) kwa mwaka ili mbolea iwe inapatikana muda wote kwa mwaka mzima tofauti na sasa ambapo uagizaji hufanywa mara moja, wakati baadhi ya mazao ya kilimo yanalimwa kwa zaidi ya mara moja kwa mwaka kupitia kilimo cha umwagiliaji.

(iii) Kuongeza uzalishaji na usalama wa chakula. Serikali imekuwa ikihamasisha wakulima kulima kilimo cha biashara ambacho kitainua kipato cha wakulima pamoja na kuhakikisha nchi inakuwa na usalama wa chakula. Kufuatia maelekezo hayo, wakulima wamehamasika na

kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali ambayo imepelekea ziada katika uzalishaji wa mahindi na mbaazi, hivyo kuwalazimu wakulima kujitafutia masoko nje ya nchi. Jitihada ambazo kwa kiasi fulani zimekwamishwa na Serikali kwa madai kwamba, uuzaji wa mazao hayo nje ya nchi utapelekea nchi kuwa na upungufu wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kwa Serikali kuongeza uratibu na usimamizi kwa kutekeleza mikakati madhubuti ya kupata takwimu sahihi na kwa muda unaostahili kuhusu kiwango cha uzalishaji wa mazao mbalimbali. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kukosekana kwa takwimu sahihi kuhusu mahitaji ya chakula nchini kumepelekea Serikali kushindwa kufanya maamuzi sahihi kuhusu mwenendo wa biashara ya ndani na nje ya mipaka hususan kwa mazao na nafaka na hivyo kusababisha hasara kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na uhakika wa usalama wa chakula ni muhimu kwa Serikali kuitengea Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* fedha za kukidhi utekelezaji wa majukumu yake ambayo ni pamoja na ununuzi na uhifadhi wa akiba ya chakula. Kwa kutambua umuhimu huu, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa maghala na vihenge vya kisasa katika Kanda Nane (8) vitakavyoongeza uwezo wa *NFRA* kuhifadhi nafaka kutoka tani 250,000 za sasa hadi tani 501,000. Kamati inapongeza hatua hii kwani itaongeza ufanisi na kuchangia jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano ya kufikia Tanzania ya Viwanda kwa kupunguza upotevu wa mazao.

(iv) Kuimarisha kilimo cha biashara kwa mazao mbalimbali. Katika miaka ya hivi karibuni mazao ya biashara aina ya pamba, tumbaku, kahawa, pareto, korosho na katani yanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufanisi mdogo wa vyama vya ushirika; ukosefu wa teknolojia za kisasa; pembejeo; masoko ya uhakika;

kukosekana kwa ruzuku ya Serikali pamoja na kukosekana mipango thabiti ya kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao yao. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inatoa ushauri kwa Serikali juu ya hatua za kuchukua katika kila zao kama inavyooneka katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa kwenu.

(v) Upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa wakulima nchini. Ukosefu wa mikopo ya uhakika na yenye riba nafuu kwa wakulima walio wengi ni kikwazo kwa wakulima kutoweza kukopa na kufanya kilimo cha kisasa na chenye tija. Uchambuzi wa Kamati umeibaini kuwa mikopo ya kibiashara katika taasisi mbalimbali za fedha ina riba ya juu ya kati asilimia 16 na 18 mikopo ambayo ni dhahiri kuwa wakulima hawawezi kumudu kukopa na kurejesha kwa tija. Kamati inaishauri Serikali kuongeza mtaji katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ili iweze kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wakulima. Aidha, kuwezeshwa kwa Benki ya Wakulima kutasaidia kuwafikia wakulima wengi zaidi katika maeneo ya vijijini.

(vi) Mipango ya dharura kukabiliana na milipuko ya wadudu waharibifu wa mazao mbalimbali. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2017/2018 kumekuwepo na mlipuko wa wadudu waharibifu wa mazao, wakiwemo wadudu waharibifu wa zao la pamba, viwavijeshi na panya ambapo Serikali ilichukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto hiyo. Pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali, bado athari zilijidhihirisha kutokana na kasi ndogo ya kushughulikia tahadhari hizi. Ufuatiliaji wa Kamati juu ya hatua zilizochukuliwa, ulibaini kutochukuliwa kwa hatua za haraka kulitokana na ukosefu wa fedha kwa ajili ya dharura. Hivyo, ni muhimu kwa Serikali kuwa na utaratibu madhubuti wa kuwezesha upatikanaji wa fedha za dharura kwa haraka maana dharura haisubiri.

(vii) Suluhisho la migogoro litokanalo na matumizi ya ardhi ya kilimo. Migogoro baina ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi imeendelea kuwepo na

kuathiri uzalishaji katika sekta mbalimbali za kilimo kutokana na hofu, uvunjifu wa amani, vifo na uharibifu wa mali na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa migogoro ya matumizi ya ardhi ni mtambuka na hivyo suluhu yake inaweza kupatikana kupitia jitihada za pamoja miongoni mwa sekta husika. Kwa kutambua hivyo na kuzingatia malalamiko ambayo yamekuwa yakitolewa na Wabunge Bungeni ambao kimsingi ndiyo wawakilishi wa wananchi, yalipelekea Serikali kuunda Tume inayohusisha Wizara tano zinazohusika na ardhi. Kufuatia kazi nzuri iliyofanywa na Tume hiyo, Kamati inashauri kuwa ni vema taarifa ya Tume iliyoundwa ikawasilishwa Bungeni ili Bunge liweze kutekeleza wajibu wake wa kuishauri Serikali. *(Makofi)*

(viii) Kuweka mazingira bora kuwezesha sekta ya binafsi kushiriki kuwekeza kikamilifu katika tasnia ya kilimo. Sekta binafsi ina mchango mkubwa katika kuwezesha uzalishaji wenye tija katika kilimo nchini. Ili kuweza kuwa na mapinduzi ya kilimo kupitia uzalishaji wenye tija, kuongeza thamani ya mazao na kuimarisha mnyororo wa thamani ya mazao ya kilimo, Serikali imekuwa ikishirikiana na sekta binafsi kama mdau muhuimu kwa maslahi mapa na Taifa. Hii ni kutokana na kwamba sekta hii ndiyo mzalishaji wa moja kwa moja na ndiyo mwekezaji kwa kupitia mitaji, teknolojia, tafiti, uchakataji na masoko. Pia kwa upande wake Serikali inawajibika kuweka mazingira rafiki kwa sekta hii kuweza kuwa na tija kuzalisha kwa faida.

(ix) Kukamilisha miradi inayoendelea kabla ya kuanza kutekelezwa kwa miradi mpya. Kwa ujumla miradi mbalimbali ya maendeleo inayoombewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa kiasi kikubwa ni muendelezo wa utekelezaji wa miradi ya mwaka 2016/2017 na 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya kuendelea miradi ya miaka iliyopita ambayo mingine inatekelezwa katika programmu tofauti ni kutokamilika utekelezaji wa

miradi hiyo kwa wakati uliopangwa na hivyo kuisababishia Serikali hasara. Kwa muktadha huu, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha miradi iliyopo kabla ya kuanzisha miradi mipya. Ushauri huu ukitekelezwa utasaidia kupunguza mzigo kwa Serikali kwa kuwa na miradi mingi isiyokamilika.

(x) Upatikananji wa uhakika wa mbegu bora nchini. Matumizi ya mbegu bora huchangia takribani asilimia 40 ya mavuno ya zao husika. Pamoja na ukweli huu, uwezo wa uzalishaji mbegu ni asilimia 36 na upungufu ni asilimia 64 ambazo huagizwa kutoka nje ya nchi na huuzwa kwa gharama kubwa ambazo wakulima wengi hawamudu na hivyo kuzorotesha kilimo. Kwa kutambua changamoto hii, Serikali imehasisha sekta binafsi kushiriki katika uzalishaji mbegu. Hata hivyo, sekta binafsi haijaweza kushiriki kikamilifu katika uzalishaji wa mbegu kutokana na kodi na tozo nyingi zinazoambatana na teknolojia za uzalishaji mbegu, ghararma kubwa za mashamba na ushindani wa soko la mbegu zinazotoka nje. Ili sekta binafsi ishiriki kikamilifu kwenye uzalishaji mbegu, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kufanya tathmini na kupunguza tozo zinazoambata na uzalishaji wa mbegu.

(xi) Changamoto ya upungufu wa mafuta ya kula nchini. Tafiti mbalimbali zinaonyesha uwezo wetu wa kuzalisha mafuta ya kula ni asilimia 30, ambapo kwa kiasi kikubwa huzalishwa kutokana na pamba, alizeti, ufuta na karanga. Sehemu kubwa ya mafuta ambayo ni asilimia 70 huagizwa kutoka nje ya nchi na hugharimu takribani shilingi bilioni 413 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini changamoto hii ya mahitaji ya upungufu wa mafuta ya kula ni asilimia 70 ni fursa kwa wakulima. Kamati inaishauri Wizara kuchukua hatua za makusudi na kutumia fursa ya soko la ndani la mafuta kula kwa kuweka mipango na mikakati ya kuwawezesha wakulima kuongeza uzalishaji na kujenga

viwanda vya kukamulia alizeti. Hatua hii ikitekelezwa itapunguza na kuokoa fedha nyingi zinazoagiza mafuta kutoka nje na hivyo kuwezesha nchi kunufaika na mnyororo wa thamani katika tasnia ya mafuta.

(xii) Umuhimu wa barabara za vijijini na uhusiano wake kwenye kilimo. Takwimu zinaonesha kwamba asilimia 65.5 ya Watanzania wanajishusha na kilimo. Pamoja na idadi kubwa ya wananchi wanaojihusisha na kilimo bado...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa malizia tu muda umeisha.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA (MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa sukari nchini, naomba uchukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu deni la mawakala, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda haupo, nenda mwishoni tumalize.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA (MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba madeni ya mawakala yaangaliwe na waweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuwasilisha taarifa yangu na naomba yale machache yaliyobakia yaweze kuingia kwenye *Hansard* na nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioshiriki katika Kamati ya Bunge na Wizara yote kwa ujumla kwa kufanikisha maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa taarifa ya Kamati.

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na majukumu mengine jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara ya Kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inataka Kamati kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo inajumuisha mafungu mawili (2) ambayo ni Fungu 43 -Wizara ya Kilimo na Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Aidha Taarifa hii inaeleza masuala makubwa matano yafuatayo:-

a) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

b) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018;

c) Mapitio ya Ukaguzi wa Miradi ya Mandeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na

e) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

## SEHEMU YA PILI

---

## 2.0 UCHAMBUZI WA MASUALA MBALIMBALI

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inabainisha masuala muhimu yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Kamati kwa kuzingatia masuala yaliyoorodheshwa katika Kipengele 1.5 cha Sehemu ya Kwanza.

## 2.1 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipochambua maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo takribani kumi na moja (11). Maeneo hayo yanajumuisha ushauri kuhusu:-

(a) Uwekezaji mdogo katika sekta za kilimo;
(b) Mtiririko wa fedha za miradi ya maendeleo usioridhisha;
(c) Mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja (*fertilizer bulk procurement);*
(d) Umuhimu wa kukamilisha miradi inayoendelea kutekelezwa kabla ya kuanza kutekelezwa kwa miradi mipya;

(e) Upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu itakayoongeza tija katika sekta ya kilimo;

(f) Umuhimu wa kuchukua hatua kushughulikia kero ya muingiliano wa shughuli zinazofanywa na Mamlaka za udhibiti;

(g) Umuhimu wa kukabiliana na migogoro ya ardhi nchini na athari zake;

(h) Umuhimu wa ujenzi wa maghala kwa ajili ya hifadhi ya nafaka na usalama wa chakula.

(i) Kuongeza Wigo wa Tume ya maendeleo ya ushirika nchini.

(j) Umuhimu wa kutenga Kanda maalum kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

(k) Katazo la kuuza chakula nje ya nchi.

**2.1.1 Mheshimiwa Spika,** kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati haujatekelezwa kutokana na mtiririko wa fedha usioridhisha. Baadhi ya shughuli zilizoshindwa kutekelezwa kikamilifu ni pamoja na:-

a) Upatikanaji wa uhakika na usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa bei nafuu na kwa kuzingatia msimu wa kilimo wa eneo husika;

b) Mikakati ya Serikali kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi ili kuendeleza kilimo hususan ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji;

c) Serikali kuiongezea mtaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili kutoa mikopo nafuu kwa wakulima wengi ikiwa ni pamoja na kufungua matawi nchini kote ili kurahisisha utoaji wa mikopo kwa wananchi kwa ujumla;

d) Kushindwa kupima maeneo ya kilimo na kuyapatia hatimiliki hivyo kusababisha kuendelea kuwepo kwa migogoro ya wakulima na wafugaji;

## 2.2 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 2.2.1 SEKTA YA KILIMO - FUNGU 43

#### a) Kiasi cha fedha kilichoidhinishwa

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara ya Kilimo, kwa **Fungu 43**, liliidhinishiwa jumla ya shilingi **214,815,759,000** kati ya fedha hizo shilingi **64,562,759,000** ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi **150,253,000,000** ni fedha za maendeleo, ambapo **59,600,000,000** ni fedha ndani na **90,653,000,000** ni fedha za nje.

#### b) Mwenendo wa utoaji fedha zilizoidhinishwa

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2018 fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa ni Jumla ya shilingi **36,069,819,172** ambayo ni **asilimilia 55.87%** ya kiasi kilichoidhinishwa. Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo fedha zilizotolewa zilikuwa shilingi **27,231,305,232.69** sawa na **asilimia 18%** ya fedha zilizoidhinishwa**.** Kati ya fedha hizo zilizotolewa shilingi **25,576,120,000** ni fedha za ndani na **1,655,185,232. 69** ni fedha za nje.

#### c) Makusanyo ya maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Kilimo Fungu 43 ilikadiria kukusanya mapato ya shilingi **2,015,010,000**. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **1,708,724,841.68** ambayo ni sawa na **asilimia 84.*80%*** ya malengo ya ukusanyaji. Hata hivyo, Kamati inaipongeza Wizara kwa kufanikiwa kukusanya kiasi hicho cha maduhuli, Aidha, Kamati inaitaka Wizara kuongeza jitihada kukusanya mapato zaidi kadiri ya makadirio kwani, Sekta ya kilimo ina fursa nyingi na za uhakika za kuwezesha Serikali kupata mapato zaidi.

### 2.2.2 TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA - FUNGU 24

**a) Kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na kutolewa**

**Mheshimiwa Spika,** fungu 24 liliidhinishwa jumla ya shilingi **6,293,857,760** kwa ajili ya matumizi ya kawaida, fungu hili halikutengewa fedha za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 kiasi cha shilingi **3,216,391,509.45** zilitolewa ambayo ni sawa na **asilimia 51.1%** ya kiasi kilichoidhinishwa.

**b) Maoni kuhusu mwenendo na utoaji wa fedha**

**Mheshimiwa Spika,** kwa miaka mitatu mfulilizo, fedha zinazoidhinishwa na Bunge hazitolewi kama zilivyoidhinishwa hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa, ikiwa ni pamoja na kutofanyiwa kazi ushauri wa Kamati katika maeneo mengi kama ilivyoelezwa hapo awali.

**JEDWALI NA.1: Linaonyesha mlinganisho wa fedha za maendeleo zilizotengwa na kutolewa kwa mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2017/2018**

| Bajeti ya mwaka | Fungu | Bajeti ya maendeleo iliyotengwa | Bajeti ya maendeleo iliyotolewa | % fedha iliyotolewa |
|---|---|---|---|---|
| 2015/2016 | 43 | 32,713,073,000 | 5,192,797,589 | 16 % |
| | 24 | 00 | 00 | 00 % |
| 2016/2017 | 43 | 101,527,497,000 | 3,369,416,666 | 3.31% |
| | 24 | 00 | 00 | 00 % |
| 2017/2018 | 43 | 150,253,000,000 | 27,231,305,232.69 | 18.00 |
| | 24 | 00 | 00 | 00 |

**Chanzo: Randama ya Wizara ya Kilimo, 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Jedwali Na.1 linaonyesha, kuongezeka kwa kiasi cha jumla ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge na kutolewa na Serikali kwa bajeti

ya Kilimo kupitia Fungu 43 kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2016/2017, ambapo kwa fungu 43, linaonyesha kupanda kwa asilimia ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo kutoka **asilimia 3.31%** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 hadi **asilimia 18.00%** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Hata hivyo hakuna bajeti yeyote ya maendeleo iliyotengwa kwa fungu 24, kwa miaka mitatu mfulilizo kwa maelezo kwamba Fedha za maendeleo kwa ajili ya Tume zinakasimiwa kupitia fungu 43 jambo ambalo linaikosesha Tume uwezo wa kupanga na kutekeleza mipango yake ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo unaojidhihirisha wa mtirirko wa kiasi cha fedha zinazotengwa na kutolewa katika Bajeti ya Kilimo, hauwiani na mahitaji halisi ya sekta ya kilimo ambapo asilimia **65.5 %** ya wananchi waishio vijijini wanategemea kilimo na kuchangia takribani asilimia **30%** ya pato la Taifa na asilimia **65 %** ya malighafi kwa ajili ya viwanda. Mwenendo huu unadhihirisha kukosekana kwa dhamira ya dhati ya uwekezaji katika miradi ya kilimo na ni kikwazo katika ukuaji wa kilimo na kupunguza umaskini.

| Bajeti ya mwaka | Fungu | Bajeti ya maendeleo iliyotengwa | Bajeti ya maendeleo iliyotolewa | % fedha iliyotolewa |
|---|---|---|---|---|
| 2015/2016 | 43 | 32,713,073,000 | 5,192,797,589 | 16 % |
| | 24 | 00 | 00 | 00 % |
| 2016/2017 | 43 | 101,527,497,000 | 3,369,416,666 | 3.31% |
| | 24 | 00 | 00 | 00 % |
| 2017/2018 | 43 | 150,253,000,000 | 27,231,305,232.69 | 18.00 |
| | 24 | 00 | 00 | 00 |

### *2.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018*

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Kamati kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni kufanya ukaguzi wa tathmini halisi ya fedha iliyotumika (Value for Money). Aidha, msingi wa kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni kuiwezesha Kamati kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha unaofuata katika sekta za Kilimo.

**Mheshimwia Spika,** Kamati haikuweza kutekeleza ipasavyo matakwa ya Kanuni ya 98(1) ambayo inaitaka Kamati kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka unaomalizika ambao ni 2017/2018 kutokana na miradi ya sekta ya kilimo kutopelekewa fedha yeyote na

kushindwa kutekelezwa. Aidha, kwa baadhi ya miradi iliyopata kiasi kidogo cha fedha zilitumika katika hatua za awali za uratibu wa kutekeleza miradi iliyopangwa, hivyo hakukuwa na miradi iliyotekelezwa kwa namna ya kuweza kukaguliwa.

**2.3.1 Fedha iliyotengwa na kutolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo - fungu 43**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2018 fungu 43 ilikuwa imepokea shilingi **27,231,305,232.69 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, Fedha hizo ni** sawa na **asilimia 18** ya kiasi kilichoidhinishwa, cha shilingi **150,253,000,000.** Baadhi ya miradi iliyokwishaanza kutekelezwa katika hatua za awali za kiuratibu ni pamoja na;

- Programu ya kuendeleza sekta ya kilimo ASDP;
- Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzani (SAGCOT);
- *Expanded Rice Production Project* (ERPP)na
- *Catalysing the Future Agri-food System of* Tanzania (CFAST).

**2.3.2** Malengo ya wizara yaliyoathiriwa na mtitiriko wa fedha usioridhisha

**Mheshimiwa Spika,** mtiririko wa fedha usioridhisha umechangia kutofikiwa kwa malengo ya Wizara yaliyopangwa kutekelezwa katika 2017/2018 katika programu mbalimbali za kuendeleza sekta ya kilimo. Maeneo yaliyoathirika ni pamoja na:-

a) Kusimamia matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo na maji;

b) Kuongeza kilimo chenye tija kwa kuongeza upatikanaji na utumiaji wa pembejeo za kilimo (mbolea,

mbegu, zana za kilimo na viuatilifu vya kudhibiti wadudu, magugu na magonjwa ya mimea na kuboresha mfumo wa utoaji wa matokeo ya utafiti kwa wadau, huduma za ugani na kusambaza teknolojia za kilimo juu ya uzalishaji wa mazao);

c) Kuimarisha usimamizi wa mazao kabla na baada ya mavuno na kuongeza thamani ya mazao na upatikanaji wa masoko na mazao yote ya wakulima na

d) Kuunda na kupitia sera ndogo ya mazao na sheria zake ili kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kutotolewa fedha za kuwezesha kuanza kutekeleza miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa sekta ya Kilimo, ililazimu Kamati kukagua mradi wa umwagiliaji wa DADPS Halmashauri ya Kigoma, uliotekelezwa kwa ushirikiano kati Serikali na wahisani wa maendeleo ambao ulipelekewa fedha katika bajeti za miaka ya nyuma wakati kanuni zinaitaka Kamati kukagua miradi iliyotengewa fedha kwa mwka ea fedha husika.

### 2.3.3 Mradi wa umwagiliaji wa DADPS Halmashauri ya Kigoma

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa utekelezaji wa mradi huu ulitekelezwa kupitia Mpango wa DADPS katika Halmashauri ya Kigoma Vijijini. Na kwamba Mradi huu ulipangwa kutekelezwa kwa awamu tofauti kwa ushirikiano kati ya Halmashauri na Wizara ya Kilimo na wahisani wa maendeleo. Katika utekelezaji wa mradi huu, awamu ya mwisho ilitekelezwa mwaka 2016/2017 ambapo ilipangwa kutumia shilingi **milioni 600**. Kamati ilielezwa kuwa katika utekelezaji wa mradi huu kumekuwapo na kutoshirikishwa Halmashauri na wananchi ipasavyo, hali iliyopelekea malalamiko ya kuwepo matumizi mabaya ya fedha hizo,

kutokana na mradi kutokamilika na kutokuwa na tija iliyokusudiwa.

Kufuatia malalamiko ya wananchi kuhusu mradi kujengwa chini ya kiwango na matumizi yasiyoelezeka ya fedha kiasi cha shilingi **milioni 600**, Kamati ilitaka maelezo kutoka Halmashauri ya Kigoma pamoja na Wizara ya Kilimo ambayo ilihusika wakati wa ujenzi wa mradi. Na kwamba hapakuwepo na majibu kutokana na Halmashauri na Wizara kutokuwa na Taarifa zozote kuhusu mradi huo kwa maelezo kuwa mradi uliratibiwa na kusimamiwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kanda ya magharibi. Aidha katika ukaguzi uliofanywa na Kamati katika eneo la mradi, wajumbe hawakuridhishwa na mradi baada ya kushuhudia mradi ukiwa katika hali ya kutelekezwa pamoja na kupokea malalamiko mengi ya wananchi kuhusu namna mradi unavyoendeshwa, mradi kukosa usimamizi makini na kupelekea wananchi kutonufaika nao kikamilifu. Kamati ilishauri;

a) Wizara na Halmashauri zifanye mawasiliano ili kupata taarifa sahihi kuhusu namna mradi ulivyotekelezwa, pamoja na kufuatilia fedha kiasi cha shilingi **million 600**, ambazo maelezo yake ya namna zilivyotumika hayaeleweki.Kamati ilishauri kuwa uchunguzi ufanyike ili kubaini matumizi ya fedha kiasi cha shilingi **milioni 600** zilivyotumika.

b) Halmashauri isimamie ipasavyo miradi inayotekelezwa katika Halmashauri, ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za kitaalamu kuhusu ushiriki wa wananchi katika miradi pamoja na huduma za ugani kwa wakulima.

c) Kamati imebaini dosari ya namna miradi ya DADPS inavyotekelezwa kwani ushiriki wa wanachi na Halmashauri ambako miradi inatekelezwa haukidhi. Hivyo inashauri Serikali kuweka miongozo madhubuti itakayowezesha kuimarisha udhibiti na ushiriki wa wadau, kama njia ya kuifanya miradi kuwa na tija na endelevu.

## *2.4 MPANGO WA BAJETI NA UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 tarehe 20 - 21 Machi, 2018. Mpango ambao umeandaliwa kwa kuzingatia Sera na Mikakati ya Kitaifa na Kisekta katika kuandaa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/2019, Mpango wa maendeleo ya sekta ya kilimo, Mpango wa Taifa wa uwekezaji katika kilimo na usalama wa chakula na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Taifa 2025.

### 2.4.1 Umuhimu wa Sekta ya Kilimo

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, unabainisha kuwa, kilimo kimeendelea kuwa sekta muhimu katika maendeleo ya uchumi hususan uchumi wa viwanda kwa kutoa malighafi za viwanda. Kilimo kimeendelea kuwa sekta inayotoa ajira zaidi kuliko sekta zote nchini ambapo zaidi ya **asilimia 65.5%** ya watanzania wamejiajiri katika sekta ya kilimo na inachangia zaidi ya **asilimia 100%** ya chakula kinachopatikana nchini kwenye kipindi chenye mvua za kutosha[1]. Aidha Utoshelezi wa chakula (*Food Self Sufficient Ratio*) mwaka 2017 ni asilimia 120 ikionyesha nchi inajitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada ya **asilimia 20%.** Aidha, kutokana na asilimia kubwa ya wananchi kushiriki katika shughuli za kilimo, kilimo kinachangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza umaskini na kuongeza kipato. Mfano Sekta ya Kilimo imechangia **asilimia 28** ya pato la Taifa kwa mwaka 2014 na kupanda kufikia **asilimia 29** mwaka 2015.[2]

---

[1] Randama ya Wizara ya Kilimo 2017/2018

[2] Taarifa ya Baraza la Kilimo Tanzania kuhusu mchango wa sekta ya Kilimo katika pato la Taifa

Kwa mwaka 2017/2018 kilimo kimechangia **asilimia 30%** ya pato la taifa kwa takriban dola **bilioni 13.9.** Vile vile Sera na Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa vinatambua Kilimo kama sekta muhimu katika Uchumi wa Tanzania.

### 2.4.2 Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013

**Mheshimiwa Spika,** sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013, kwa kutambua umuhimu wa kilimo inasisitiza juu ya kila kijiji kuwa na afisa ugani mmoja na kuweka uwiano wa kati ya afisa ugani na wakulima kuwa **1:600,** kuongeza kilimo chenye tija kwa kuongeza upatikanaji wa huduma za ugani, utumiaji pembejeo za kilimo na kusambaza teknolojia za kilimo juu ya uzalishaji wa mazao, kuimarisha usimamizi wa mazao kabla na baada ya mavuno na kuongeza thamani ya mazao na upatikanaji wa masoko kwa mazao yote ya wakulima, kuratibu utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya mazao na kuimarisha huduma za udhibiti,utafiti na takwimu kwa ujumla.

### 2.4.3 Mikakati ya Serikali kuendeleza kilimo

Aidha, mikakati na kauli mbiu za Serikali katika nyakati tofauti zinadhihirisha umuhimu wa kilimo kama ajenda ya Taifa. Baadhi ya kaulimbiu amabazo zimekua zikilenga kuharakisha mapinduzi ya kilimo na kukuza viwanda nchini ni pamoja na;

a) Azimio la Arusha- 1967;
b) Siasa ni kilimo-1974;
c) Azimio la Iringa-1974; na
d) Kilimo Kwanza -2009.

Hata hivyo, pamoja na mikakati na kaui mbiu hizi kilimo nchini kinakabiliwa na changamoto nyingi, ambazo zimekua sababu ya tija ndogo katika sekta.

### 2.4.4 Azimio la Maputo na Malabo la kutenga asimilia 10 ya pato la Taifa kwa ajili ya kilimo

**Mheshimiwa Spika,** Kimataifa Tanzania imeridhia na kuendelea kutekeleza Mipango na Mikataba mbalimbali kwa lengo la kuongeza kasi ya uwekezaji katika kilimo na ukuaji uchumi. Mathalan Mpango kabambe wa kuendeleza kilimo Africa (CAADP/AUC NEPAD) wa mwaka 2003 Maputo-Msumbiji ambao pia ulirejewa mwaka 2014 Malabo-Guinea Bissau uliweka maazimio ya nguzo saba za kuendeleza kilimo, mojawapo ikiwa ni kuhakikisha kuwa kila nchi inatenga asilimia 10% ya bajeti ya Taifa kwa ajili ya sekta ya kilimo ili kuchochea ukuaji kwa **asilimia 6%.**

### *2.5 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Kilimo, unajumuisha mafungu mawili ambayo ni:-

(i) Fungu 43 – Wizara ya Kilimo na
(ii) Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2018/ 2019, Wizara ya Kilimo, kupitia Fungu 43 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **162,224,814,000.** Aidha, Fungu 24 inaomba kuidhinishiwa shilingi **8,048,234,972**. Kwa ujumla Wizara ya Kilimo, kupitia mafungu yote mawili fungu 43 na fungu 24 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **170,273,048,972.** Aidha Wizara kupitia mafungu yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/ 2019 inatarajia kukusanya jumla ya maduhuli kiasi cha **shilingi 2,315,010,000.**

### 2.5.1 Wizara ya Kilimo- Fungu 43

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/ 2019 Fungu 43 linaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **162,224,814,000** Kati ya fedha hizo, shilingi **64,105,298,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **98,119,516,000** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara

kupitia Fungu 43 imepanga kukusanya jumla ya **shilingi 2,315,010,000**

### 2.5.2 Tume ya Maendeleo ya Ushirika- Fungu 24

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara kupitia Fungu 24 linaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **8,048,234,972.** Kiasi kinachoombwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 hakuna fedha yeyote iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kamati inasikitishwa na hatua ya Serikali kuendelea kutoitengea fedha ya maendeleo Tume ya Ushirika.

### *2.6 MALENGO YA UTEKELEZAJI NA VIPAUMBELE*

**Mheshimiwa Spika**, fedha zinazoombwa zimepanga kutekeleza malengo mbalimballi ya Wizara, malengo hayo ni pamoja na:-

a) Kusimamia matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo na maji;

b) Kuongeza kilimo chenye tija kwa kuongeza upatikanaji wa huduma za ugani, utumiaji pembejeo za kilimo na kusambaza teknolojia za kilimo juu ya uzalishaji wa mazao

c) Kudhibiti upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno na kuongeza thamani ya mazao na upatikanaji wa masoko kwa mazao yote ya wakulima;

d) Kuratibu utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya mazao na kuimarisha huduma za udhibiti;

e) Kuunda na kupitia sera za sekta ndogo za mazao na sheria zake ili kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika kilimo;

f) Kuimarisha uratibu,takwimu,ufuatiliaji na tathmini ya sekta ya mazao;

g) Kuimarisha masuala mtambuka yanayohusu vijana katika kilimo, jinsia, mazingira, lishe na UKIMWI;

h) Kuimarisha mafunzo ya kilimo na kuboresha miundombinu katika Vyuo vya mafunzo ya Kilimo;

i) Kuboresha mfumo wa utafiti, ugunduzi wa mbegu mpya na utoaji wa matokeo ya utafiti kwa wadau.

### *2.7 TATHIMINI YA MALENGO KWA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/2019*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2018/2019 na kuridhishwa nayo. Hata hivyo uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, malengo na vipaumbele vilivyoainishwa vimekuwa vikijirudia kila mwaka kutokana na kasi ndogo ya utekelezaji wake unaosabishwa na kiasi kidogo cha fedha kinachotengwa na kutolewa kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na umuhimu wa sekta za kilimo kama unavyoelezewa kupitia Mipango, Sera na Mikakati mbalimbali ya Serikali, bado sekta hii imekuwa haipewi msukumo wa kutosha kama kipaumbele cha uhai na ustawi wa sekta zingine za uzalishaji mali.

#### 2.7.1 Kushuka kwa bajeti inayotengwa na kutolewa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati katika uchambuzi wake, imebaini kuendelea kushuka kwa bajeti inayotengwa na kutolewa kwa ajili ya Sekta ya Kilimo kila mwaka. Kwa mfano: kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 bajeti ya kilimo ilikua ni **asilimia 7.8%** ya bajeti yote ya Serikali, Mwaka wa Fedha 2011/2012 ilikua ni **asilimoa 6.9%** ya bajeti yote ya Serikali, Mwaka wa Fedha 2016/2017 Serikali ilitenga **asilimia 4.9%** tu ya bajeti yote ya Serikali kwa ajili ya Sekta za kilimo na Mwaka wa Fedha 2017/2018 ilitenga asilimia **4.8 %** ya pato lake kwa ajili ya Kilimo.

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kwamba mwenendo huu wa uwekezaji mdogo kwenye sekta ya kilimo, unakinzana na dhana ya uchumi wa viwanda ambao malighafi ya viwanda kwa kiasi kukubwa yatatokana na bidhaa zitokanazo na kilimo. Uchambuzi umebaini pia kuwa Tanzania ni ya mwisho katika ukanda wa Afrika mashariki kwa kupata alama 3.1 kati ya 10 katika utekelezaji wa Azimio la Malabo[3]. Nchi nyingine za Afrika mashariki zinaelekea kutenga asilimia kubwa ya pato lake la mwaka kwa ajili ya kilimo na hivyo kuwa kichocheo cha sekta ya kilimo kukua na kuongeza tija katika uzalishaji ukilinganisha na Tnzania. Kwa mfano Rwanda imepata alama **6.1,** Kenya **4.8,** Burundi **4.7** na Uganda **4.4**.

Tafsiri ya mwenendo huu ni kuwa uwekezaji katika sekta ya kilimo una tija ya moja kwa moja katika kuchochea kilimo, kuongeza uzalishaji na kuchochea uchumi wa viwanda. Hivyo ili Tanzania iweze kumudu ushindani wa kikanda katika kukua uchumi haina budi kuongeza uwekezaji katika kilimo kufikia asilimia 10% ya pato lake la jumla kwa mwaka ifikapo 2025.

**Jedwali: Muhtasari wa matokeo ya tathmini ya Tume ya Umoja wa Afrika wa Utendaji wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mshariki ya Mpango Kabambe wa Kilimo-Afrika.**

[3] Taarifa ya Tume ya Umoja wa Africa wa Utendaji wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Africa Mashariki juu ya Mpango Kabambe wa Kuendeleza Kilimo-Africa,2017

**Mchanganuo:-**

**A-**Dhamira juu ya mkataba wa CAADP.
**B-**Kuongeza fedha za uwekezaji katika kilimo.
**C-**Kutokomeza njaa ifikapo 2025.
**D-**Kupunguza umaskini kwa 50% ifikapo 20125.
**E-**Kukuza biashara za mazao ya kilimo baina ya nchi Africa.
**F-**Kuongeza urahisi kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.
**G-**Uwajibikaji wa pamoja kwa ajili ya mipango na matokeo.
**H**- Alama (juu ya 10).

**Mheshimiwa Spika,** uwekezaji mdogo unaofanywa na Serikali kwenye kilimo unaathiri pato na ustawi wa wananchi walio wengi ambao wanategemea kilimo kama njia kuu ya uzalishaji mali. Kamati inatahadharisha kuwa, endapo hatua madhubuti hazitachukuliwa katika kuinua Sekta ya kilimo, ni dhahiri kuwa mdororo wa uchumi na mnyororo ya umaskini utaendelea kuwa wimbo mahala pengi nchini. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutambua umuhimu wa kutekeleza kwa vitendo mkataba wa Azimio la Maputo na Malaba ambayo yanazitaka nchi wana chama kutenga **asilimia 10** ya pato ghafi kwa ajili ya stka ya kilimo kila mwaka.

### 2.7.2 Kasi ndogo ya ukuaji sekta ya kilimo

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati pia umebaini kuwa tathmini ya awali ya viashiria vya ukuaji wa sekta ya kilimo nchini kwa msimu wa kilimo 2017/2018 inaonyesha kuendelea kukua na kuimarika kwa sekta ya kilimo ukilinganisha na msimu wa 2016/2017, ambapo katika kipindi cha nusu ya mwaka 2017 ukuaji wa sekta ya kilimo ulikua kwa asilimia **3.1%** ukilinganisha na asilimia **2.7%** kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2016. Na kwamba mfumko wa bei kwa mazao ya chakula na vinywaji visivyo vya kilevi umeendelea kuimarika ukilinganisha na mwaka 2016 ambapo hadi kufikia mwishoni mwa mwezi disemba 2017

mfumko wa bei ulifikia **asilimia 6.2%** ukilinganisha na **asilimia 7.0%** iliyofikiwa mwezi Disemba 2016.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwepo viashiria vya ukuaji katika sekta ya kilimo,uzalishaji na utoshelezi wa chakula na kupungua kwa mfumko wa bei, ni dhahiri kuwa kasi hii ya ukuaji ni ndogo ikilinganishwa na makusudio ya ukuaji wa **asilimia 6%** inayotarajiwa ifikapo mwaka 2025. Uchambuzi wa Kamati umebaini pia kuwa kasi ndogo ya ukuaji sekta unahusishwa kwa kiasi kikubwa na uwekezaji usiokidhi katika sekta ya kilimo ambao hauendani na mipango ya kukuza sekta kwa kiwango kinachotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto zilizoonekana za kushuka kwa bajeti inayotengwa na kutolewa ambayo imepelekea kasi ndogo ya ukuaji sekta ya kilimo na kuwa na athari hasi katika kufikia malengo na vipaumbele vinavyoainishwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 katika maeneo yafuatavyo:-

**a) Uhaba wa Maafisa Ugani**

Takwimu zinaonyesha kuwa kuna upungufu wa zaidi ya asilimia 40 ya maafisa ugani wanaohitajika kitaifa. Aidha, hata maafisa ugani waliopo wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na baadhi yao hupangiwa kazi nje ya taaluma na weledi wao, kufanya kazi katika mazingira magumu, kukosa vitendea kazi, changamoto hizi zimekuwa zikisababisha kukosekana utaalamu bora kwenye kilimo na kuchangia kushuka kwa maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.

**b) Uhaba wa Pembejeo na kukosekana kwa mbegu zenye ubora**

Pembejeo ni moja ya eneo muhimu katika kuchangia uzalishaji kwenye kilimo. Takwimu zinaonyesha kuwa mbegu bora pekee huchangia takribani **asilimia 40%** ya mavuno ya zao husika. Takwimu za Serikali zinaonyesha matumizi ya mbegu bora nchini zikiwemo mbegu za nafaka, mikunde na

mafuta ni **asilimia 86.2%** ya mahitaji halisi. Takwimu hizi zinatia shaka na hasa ikizingatiwa kuwa wakulima wengi wamekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuhusu upatikanaji wa mbegu usiokuwa wa uhakika, matumizi ya mbegu zisizo na ubora na bei kubwa ya mbegu ambavyo vimekuwa vikikwamisha ustawi wa kilimo. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kujenga viwanda vya ndani kwa ajili ya kuzalisha mbolea, mbegu na viuatilifu kulingana na mahitaji ya soko.

**c) Matumizi ya mbolea bora na inayopatikana kwa wakati**

Matumizi ya mbolea bora na inayopatikana kwa wakati ina tija katika uzalisha wa kilimo. Kwa kutambua umuhimu huu katika msimu wa 2017/2018 Serikali imeanzisha mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja ambapo kiasi cha mbolea kilichoingizwa kupitia mfumo huu ni asilimia **48%** ya mahitaji na hivyo kuwepo kwa upungufu wa asilimia **52%.** Taarifa ya Benki ya Dunia ambayo inaeleza kuwa, ili kuwa na kilimo chenye tija, wastani wa matumizi ya mbolea ni kilo **119.9** kwa hekta. Hapa nchini matumizi ya mbolea ni wastani wa kilo **10** za mbolea kwa hekta moja, kiwango ambacho ni chini sana ya viwango stahiki kuweza kuleta tija inayokusudiwa katika uzalishaji.

**d) Changamoto ya uhakika wa masoko ya mazao na upangaji bei ya mazao**

Masoko ya mazao na upangaji bei imekua changamoto ya kudumu kwa wakulima nchini. Kamati imebaini kuwa pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali za kuhamasisha wakulima kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani na kuimarisha usimamizi wa ushirika ili kuwawezesha wakulima kuuza mazao yao kwa bei nzuri na kupata masoko ya uhakika kwa mazao mbalimbali, bado wakulima wengi wanakabiliwa na changamoto ya uhakika wa masoko kwa mazao yaliyo mengi kama ilivyo kwa mazao ya mbaazi na mahindi. Hali hii imekuwa ikikatisha tamaa wakulima wengi

na kutokana na kutopata manufaa ya kilimo ikilinganishwa na gharama kubwa za uzalishaji wanazotumia.

**e) Umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji katika kuongeza uzalishaji**

Kilimo cha umwagiliaji kimeendelea kutopewa msukumo wa kutosha na hivyo kutoonyesha dhamira ya dhati ya Serikali kuinua sekta ya Kilimo kupitia umwagiliaji na kuepukana na kilimo cha kutegemea mvua ambacho kwa kiasi kikubwa kinaathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi. Takwimu zinaonesha kuwa Tanzania ina eneo lenye ukubwa wa **hekta 29.4** milioni zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji hata hivyo hadi sasa ni **hekta 461,326** tu ambazo ni sawa na **asilimia 1.6** ndio linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Kamati inaitaka Serikali kutambua fursa ya eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kuchukua hatua za makusudi ili kuimarisha kilimo cha umwagiliaji.

***2.8 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa Bajeti ya Maendeleo iliyotengwa kwa miaka miwili, 2017/2018 na 2018/2019 katika mafungu ya sekta za kilimo kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo.

**JEDWALI NA. 3: ULINGANISHO WA BAJETI YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MIAKA MIWILI 2017/2018 NA 2018/2019.**

| Fungu | Bajeti ya Mwaka 2017/2018 | Bajeti ya Mwaka 2018/2019 | % ongezeko |
|---|---|---|---|
| 43 | 150,253,000,000 | 98,119,516,000 | -34.7 % |
| 24 | 00 | 00 | 00 % |

**Chanzo cha Taarifa: Randama ya Wizara ya Kilimo 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ulinganisho wa bajeti ya maendeleo iliyotengwa kwa miaka miwili mfululizo kwa mafungu yote ya Wizara. Kamati imebaini kuwa, jumla

ya fedha za maendeleo zilizotengwa kwa fungu 43 kwa mwaka 2018/2019 ni pungufu kwa **asilimia 34.7 %** ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa Mwaka 2017/2018. Kati ya fedha hizi, fedha za ndani zikiwa ni **asilimia 83.57%**. Kamati inatahadharisha athari hasi zinazoweza kutokana na kushuka kwa kiasi kinachotengwa kwa ajili ya kilimo, wakati kilimo kikiendelea kuonekana kama njia kuu ya uzalizaji malighafi za viwanda, ajira na chakula kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Tume ya Maendeleo ya Ushirika - Fungu 24 haijatengea fedha za maendeleo, hata hivyo Kamati imefahamishwa kuwa kwa sasa fedha za miradi ya maendeleo kwa fungu hilo hukasimiwa kupitia miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo kupitia mradi wa *Agricultural Support Developemnt Programs* (ASDP).

## SEHEMU YA TATU

---

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/ 2019, Naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo kumi na nne (14) kama ifuatavyo:-

1. **Mtiririko usioridhisha wa fedha za miradi ya maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** upo udhaifu mkubwa katika kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za Kilimo. Kwa mfano: katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Fungu 43 ilipelekewa shilingi **16,520,540,444** sawa na **asilimia 11% tu** ya fedha zilizotengwa. Aidha, jumla ya fedha za maendeleo zilizotengwa kwa fungu 43 kwa mwaka 2018/2019 ni pungufu kwa **asilimia 34.7 %** ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa

Mwaka 2017/2018. Kupungua kwa kiasi cha fedha kinachotengwa na mtiririko usioridhisha wa fedha za miradi ya maendeleo ni dhahiri kutaendelea kusababisha kasi ndogo ya ukuaji wa sekta ya kilimo,kama inavyojidhihirisha katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo ukuaji wa sekta ya kilimo ulikua kwa asilimia **3.1%** ukilinganisha na asilimia **2.7%** ya mwaka 2016/2017. Ukuaji huu hauakisi malengo na vipaumbele vya sekta ambavyo vinalenga sekta ya kilimo kukua kwa **asilimia 6%** ifikapo mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya Kilimo kutoka **asilimia 4.8%** ya sasa hadi kufikia **asilimia 10%** ya pato la Taifa kwa ajili ya kilimo, kama ilivyoelezwa katika Azimio la Maputo na Malabo ili kuweza kuwa na ukuaji wa sekta ya kilimo kwa asilimia **6%** ifikapo 2025.

**Mheshimiwa Spika,** endapo pendekezo hili litatekelezwa litasaidia kuchochea tija katika uzalishaji kilimo, kuwa na uhakika wa usalama wa chakula, kuongeza ajira, maligafi kwa ajili ya viwanda, kuongeza pato na ustawi wa wakulima, pamoja na kuongeza pato la Taifa kwa ujumla na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi.

2. **Upatikanaji wa uhakika wa mbolea nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa mbolea nchini ikiwa ni pamoja na kutekeleza mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja (*Ferterlizer Bulk Procument*), bado upatikanaji wake katika maeneo mbalimbali haukidhi mahitaji. Mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

a) Bei ya mbolea bado ni ghali ikilinganishwa na matarajio ya Serikali ya kuanzisha mfumo huu;

b) Mbolea iliyonunuliwa kupitia mfumo huu haifiki kwa wakulima kwa wakati;

c) Kutozingatiwa kikamilifu kwa bei elekezi; na

d) Uhaba wa mawakala/wasambazaji wa mbolea katika maeneo mengi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kufanyia kazi changamoto hizo hasa kwa kutambua kuwa mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja ni mikakati ya muda mfupi ya kuhakikisha kunakuwepo na upatikanaji wa mbolea katika vipindi vyote vya msimu wa kilimo. Ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha Taifa linakuwa na suluhisho la kudumu la upatikanaji wa mbolea kwa bei nafuu na kwa wakati ili kuondokana na uagizaji wa mbolea kutoka nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kutekeleza kwa vitendo adhma yake ya kuzalisha mbolea hapa nchini kwa kujenga viwanda vya kuzalisha mbolea pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya kuwezesha sekta binafsi kushiriki na kuwekeza katika tasnia ya mbolea.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Serikali inaendelea na juhudi za ujenzi wa viwanda vya mbolea, ili kupunguza adha ya ukosefu wa mbolea, Kamati inashauri kuwa, ni vema mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja ukafanyika mara tatu (3) kwa mwaka ili mbolea iwe inapatikana muda wote kwa mwaka mzima tofauti na sasa ambapo uagizaji hufanywa mara moja wakati baadhi ya mazao ya kilimo yanalimwa kwa zaidi ya mara moja kwa mwaka kupitia kilimo cha umwagiliaji.

3. **Kuongeza uzalishaji na usalama wa chakula.**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikihamasisha wakulima kulima kilimo cha biashara ambacho kitainua kipato cha wakulima pamoja na kuhakikisha nchi inakuwa na usalama wa chakula. Kufuatia maelekezo hayo, wakulima wamehamasika na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali ambayo umepelekea ziada katika uzalishaji wa mahindi na mbaazi na hivyo kuwalazimu wakulima kujitafutia masoko nje ya nchi jitihada ambazo kwa kiasi flani zimekwamishwa na Serikali

kwa madai kwamba uuzaji wa mazao hayo nje ya nchi utapelekea nchi kuwa na upungufu wa chakula.

**Mheshimiwa Spika,** Ni muhimu kwa Serikali kuongeza uratibu na usimamizi kwa kutekeleza mikakati madhubuti ya kupata takwimu sahihi na kwa muda unaostahili kuhusu kiwango cha uzalishaji wa mazao mbalimbali. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kukosekana kwa takwimu sahihi kuhusu mahitaji ya chakula nchini kumepelekea Serikali kushindwa kufanya maamuzi sahihi kuhusu mwenendo wa biashara ya ndani na nje ya mipaka hususan kwa mazao ya nafaka na hivyo kusababisha hasara kwa wakulima.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuwa na uhakika wa usalama wa chakula, ni muhimu kwa Serikali kuitengea Walaka wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) fedha za kukidhi utekelezaji wa majukumu yake ambayo ni pamoja na ununuzi na uhifadhi wa akiba ya chakula. Kwa kutambua umuhimu huu, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa maghala na vihenge vya kisasa katika kanda nane (8) vitakavyo ongeza uwezo wa NFRA kuhifadhi nafaka kutoka **tani 250,000** za sasa hadi **tani 501,000**. Kamati inapongeza hatua hii kwani itaongeza ufanisi na kuchangia jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano ya kufikia Tanzania ya Viwanda kwa kupunguza upotevu wa mazao.

4. **Kuimarisha kilimo cha biashara kwa mazao mbalimbali**

**Mheshimiwa Spika,** katika miaka ya hivi karibuni mazao ya biashara aina ya pamba, tubaku, kahawa, pareto, korosho na katani yanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufanisi mdogo wa vyama vya ushirika, ukosefu wa teknolojia za kisasa, pembejeo, masoko ya uhakika, kukosekana kwa ruzuku ya Serikali pamoja na kukosekana mipango dhabiti ya kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kukabiliana na changamoto hizo Kamati inatoa ushauri kwa Serikali juu ya hatua za kuchukua katika kila zao kama ifuatavyo:-

a) **Zao la Pamba**

Endapo zao la pamba litapewa msukumo unaostahili ikiwemo uzingatiaji wa mbegu bora, upatikanaji wa mbolea na madawa kwa uhakika, mikopo yenye riba nafuu pamoja na kuwa na soko la ndani la pamba kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya nyuzi na nguo itaongeza tija kwa zao hilo na hivyo kuwanufaisha wakulima wa pamba.

b) **Zao la Tumbaku**

Zao la Tumbaku linakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa uhakika wa soko na bei nzuri kwa wakulima kutoka na kampuni chache za kimaitafa kuhodhi soko. Ni vema Serikali ikaratibu upatikanaji wa masoko ya ndani kwa kuhamasisha ujenzi wa viwanda hatua ambayo itasaidia kuepukana na ukiritimba uliopo katika kutafuta bei nzuri na masoko ya nje.

c) **Zao la Kahawa**

Zao la kahawa pamoja na changamoto zingine zinazolikabili, changamoto kubwa ni ukosefu wa minada ya kutosha kukidhi ushindani wa soko. Kwa kuwa Serikali imetoa utaratibu mpya wa uendeshaji wa masoko ya Kahawa kwa kuelekeza kahawa zote kuuzwa kwa njia ya mnada, Kamati inashauri kuwa ni vema minada ya zao la kahawa ikaongezwa ili kuwa na wigo wa kutosha na hivyo kuwezesha upatikanaji wa soko la uhakika.

d) **Zao la Pareto**

Zao la Pareto ni zao la biashara ambalo nchini Tanzania halipajewa msukumo unaostahili, kwani takwimu zinaonyesha uzalishaji wa na ndani ni **tani 2,000** kwa mwaka ikilinganishwa na mahitaji ya **tani 6,000** ambayo upatikanaji

wake ungewezesha uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata zao hilo. Uzalishaji mdogo wa zao hilo umekuwa ni kikwazo na hivyo kupelekea uchakataji wa zao hilo kufanyika nje ya nchi na kuikosesha Serikali mapato ya moja kwa moja na fursa ya ajira kwa watanzania.

Kufuatia hali hiyo, Kamati inashauri Serikali kuongeza kasi ya kuhamasisha ulimaji wa pareto ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya kilimo biashara kuhusu zao hilo, kwa kufanya hivyo kutawezesha kufikia malengo ya uzalishaji yatakayopelekea kuanzisha viwanda hapa nchini. Aidha Kamati inapongeza uamuzi wa Serikali wa kuendelea na utaratibu wa kutotoza tozo ya asilimia mbili kwa pareto inayosafirishwa nje ya nchi (*export levy*) kama njia ya kuongeza fedha za kigeni na hivyo kuhamasisha kilimo cha pareto kabla ya kuanza uchakataji wa zao hili nchini.

e) **Katani**

Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua inazochukua kuhakikisha kuwa zao la katani limeanza kulimwa na kuzalishwa kama awali. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati kuona kuwa zao la katani linachakatwa na bidhaa zake, kama magunia kutumika nchini, hivyo kuongeza soko la zao lakini pia kuepusha kuagiza mifuko ya kubebea mazao mbalimbali kutoka nje ya nchi amayo inaligharimu Taifa fedha nyingi za kigeni.

f) **Korosho**

Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua inazochukua kuimarisha tija katika uzalishaji wa zao la korosho. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inashauri Serikali kuweka na kusimamia taratibu na misingi zitakazowezesha kuepukana na changamoto ya ukosefu wa salfa ya kutosha kwa wakati kama ilivyobainika katika msimu uliopita pamoja na vitendo vya udanganyifu unaofanywa na watu ambao sio waaminifu kwa kuchanganya mawe na korosho, jambo ambalo linaharibu sifa nzuri ya korosho ya Tanzania katika biashara ya kimataifa.

5. **Upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa wakulima nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Ukosefu wa mikopo ya uhakika na yenye riba nafuu kwa wakulima walio wengi ni kikwazo kwa wakulima kutoweza kukopa na kufanya kilimo cha kisasa na chenye tija. Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa, mikopo ya kibiashara katika taasisi mbalimbali za fedha zina riba ya juu ya kati ya asilima 16% na 18%. Mikopo ambayo ni dhahiri kuwa wakulima hawawezi kuimudu kukopana kuirejesha kwa tija. Aidha wakulima wengi wadogo nchini hawakopesheki kutokana na mikipo ya kibiashara kuwa na mashart magumu ambayo wakulima wanashindwa kufikia vigezo stahiki. Taarifa ya Shirika la Chakula Duniani (FAO) inaeleza kuwa wakulima wanaopata mikopo nchini ni chini ya **asilimia 2%.** Hali hii ni kikwazo katika kufikia uzalishaji wa kilimo chenye tija. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Benki ya Kilimo (TADB), hadi mwezi disemba, 2017 ilikua na mtaji wa kiasI cha shilingi **66,785,790,739.00.** Aidha kiasi cha mtaji kilichoombwa ni shilingi bilioni **800.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuongeza mtaji katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ili ibebe jukumu hili la kutoa mikopo kwa wakulima wengi zaidi katika maeneo mbalimbai nchini. Aidha ili kufikia adhma hii Kamati inasisitiza kuwepo uwiano wa mtawanyiko wa huduma zitakazotolewa na benki hii katika maeneo ya uzalishaji vijijini sambamba na kutoa elimu na kuhamasisha utoaji mikopo ya kilimo cha biashara badala ya ilivyo sasa ambapo inaendesha shughuli zake katika maeneo machache ya mjini, ambayo si wakulima wote wanaweza kuzifikia.

6. **Mipango ya dharura kukabiliana na milipuko ya wadudu waharibifu wa mazao mbalimbali nchini.**

**Mheshimiwa Spika**, Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2017/2018 kumekuwepo na mlipuko wa wadudu waharibifu wa mazao wakiwemo wadudu waharibifu wa zao la pamba, viwavi jeshi na panya. Na kwamba Serikali

ilichukua hatua kukabiliana na dharura iliyojitokeza ili kunusuru mazao katika maeneo yaliyoshambuliwa na kuepusha hasara. Pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali, bado athari zilijidhihirisha kutokana na kasi ndogo ya kushughulikia tahadhari hizi. Ufuatiliaji wa Kamati juu ya hatua zilizochukuliwa ulibaini kutochukuliwa hatua kwa haraka kulitokana na ukosefu wa fedha kwa ajili ya dharura ya milipuko. Na kwamba Wizara ililazimika kuanza taratibu za kutafuta fedha kutoka hazina, kutafuta au kuwezesha upatikanaji wa mikopo kutoka katika Benki pamoja na kuomba fedha kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa ili kupata msaada wa fedha kwa ajili ya kukabiliana na dharura ya viwavijeshi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na dharura ya mlipuko wa wadudu waharibifu wa mazao, Kamati haijaridhishwa na kasi ndogo ya upatikanaji wa fedha katika kukamilisha taratibu za kupata fedha inayohitajika. Kamati inasisitiza kuwa pamoja na kwamba milipuko ya wadudu waharibifu ni dharura, ni lazima kukaandaliwa utaratibu madhubuti wa kuwezesha upatikanaji wa fedha za dharura kwa haraka, maana dharura haisubiri. Hii itasaidia kuepusha hasara inayoweza kupatikana kutokana na kuchelewa kuchukuliwa hatua kukabiliana na dharura kwa maelezo ya kukamilisha taratibu za kupata fedha.

### 7. Suluhisho la migogoro itokanayo na matumizi ya ardhi ya kilimo nchini

**Mheshimiwa Spika**, migogoro baina ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi imeendelea kuwepo na kuathiri uzalishaji katika sekta mbalimbali za kilimo kutokana na hofu, uvunjifu wa amani, vifo na uharibifu wa mali na mazingira. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, migogoro ya matumizi ya ardhi ni mtambuka na hivyo suluhu yake inaweza kupatikana kupitia jitihada za pamoja miongoni mwa sekta husika, kwa kutambua hivyo na kuzingatia malalamiko ambayo yamekuwa yakiliyotolewa na Wabunge Bungeni ambao kimsingi ndio wawakilishi wa

wananchi, yalipelekea Serikali kuunda Tume inayohusisha Wizara tano zinazohusika na ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa ni vyema taarifa ya Tume hiyo ikawasilishwa Bungeni ili Bunge liweze kutekeleza wajibu wake wa kuishauri Serikali. Aidha Serikali iongeze kasi ya kutekeleza kwa vitendo Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999, pamoja na kuhuisha sheria zingine zinazosimamia matumizi, umiliki, uhifadhi ili kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu ardhi.

8. **Kuweka mazingira bora kuwezesha sekta binafsi kushiriki kuwekeza kikamilifu katika tasnia za kilimo**

**Mheshimiwa Spika,** Sekta binafsi ina mchango mkubwa katika kuwezesha uzalishaji wenye tija katika kilimo nchini. Ili kuweza kuwa na mapinduzi ya kilimo kupitia uzalishaji wenye tija, kuongeza thamani ya mazao na kuimarisha mnyororo wa thamani ya mazao ya kilimo, Serikali imekua ikishirikiana na Sekta binafsi kama mdau muhimu kwa maslahi mapana ya Taifa.Hii ni kutokana na kwamba sekta hii ndio mzalishaji wa moja kwa moja na ndio muwekezaji kupitia mitaji, teknolojia, tafiti, uchakataji na masoko. Lakini pia kwa upande wake Serikali inawajibika kuweka mazingira rafiki kwa sekta hii kuweza kuwa na tija kwa kuzalisha kwa faida.

9. **Kukamilisha miradi inayoendelea kabla ya kuanza kutekelezwa kwa miradi mipya**

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla miradi mbalimbali ya maendeleo inayoombewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa kiasi kikubwa ni muendelezo wa utekelezaji wa miradi ya Mwaka wa Fedha 2017/208 na 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** sababu kubwa ya kuendelea na miradi ya Miaka iliyopita, ambayo mingine inatekelezwa katika program tofauti ni kutokamilika utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati uliopangwa. Kutokamilika kwa miradi hii

pamoja na athari zingine kunapelekea kuongeza gharama za utekelezaji miradi kutokana na kupanda kwa bei ya gharama za manunuzi ya vifaa vya mradi pamoja na wakati mwingine uchakavu wa miradi inayoendelea kutekelezwa kutokana na miradi kuchukua muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii ya kutokamilika miradi kwa muda uliopangwa sio tu kuwa kunasababisha hasara ya fedha kutokana na uchakavu wa sehemu ya mradi iliyokwisha tekelezwa, lakini pia kunanyima wanachi fursa ya kunufaika na miradi hiyo, jambo ambalo linadumaza ukuaji wa sekta. Kwa muktadha huu, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha miradi iliyopo kabla ya kuanzisha miradi mipya. Ushauri huu ukitekelezwa utasaidia kupunguza mzigo kwa Serikali wa kuwa na miradi mingi isiyokamilika.

10. **Upatikanaji wa uhakika wa mbegu bora nchini**

**Mheshimiwa Spika,** utafiti unaonyesha kuwa ni takribani **asilimia 25** ya wakulima nchini hutumia mbegu bora. Aidha, matumizi ya mbegu bora huchangia takribani **asilimia 40%** ya mavuno ya zao husika. Pamoja na ukweli huu, uwezo wa uzalishaji mbegu ni **asilimia 36** na upungufu ni **asilimia 64** ambazo huagizwa kutoka nje ya nchi na huuzwa kwa gharama kubwa ambazo wakulima wengi hawamudu na hivyo kuzorotesha kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na changamoto hiyo ya uhaba wa mbegu Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013 imeweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kushiriki katika uzalishaji wa mbegu. Pamoja na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika uzalishaji wa mbegu, sekta binafsi haijaweza kushiriki kikamilifu katika uzalishaji wa mbegu kutokana na kodi na tozo nyingi zinazoambatana na teknolojia ya uzalishaji mbegu, gharama kubwa za mashamba na ushindani wa soko la mbegu zinazotoka nje.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuwa na kilimo chenye tija ni wazi kuwa upatikanaji wa uhakika wa mbegu bora ni jambo la kipaumbele. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuendelea kufanya tathimini na kupunguza tozo zinazoambatana na uzalishaji wa mbegu pamoja na kutambua na kushughulikia kero zingine zinazokwamisha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika uzalishaji wa mbegu.

11. **Changamoto ya upungufu wa mafuta ya kula nchini**

**Mheshimiwa Spika,** tafiti mbalimbali zinaonyesha uwezo wetu wa kuzalisha mafuta ya kula ni **asilimia 30** ambayo kwa kiasi kikubwa huzalishwa kutokana na pamba, alizeti, ufuta na karanga. Sehemu kubwa ya mafuta ambayo ni asilimia 70 huagizwa kutoka nje ya nchi na hugharimu takribani **shilingi bilioni 413 kwa mwaka**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini changamoto hii ya mahitaji ya upungufu wa mafuta ya kula kwa asilimia 70 ni fursa kwa wakulima, kwa mfano: zao la alizeti pekee ambalo husifika kwa kuhimili ukame, halishambuliwi na wadudu kirahisi, uzalishaji wake ni rahisi na hauhitaji gharama kubwa na mafuta yake yamethibitika kuwa na manufaa kiafya. Kutokana na manufaa hayo, wakulima wengi wamehamasika na kujihusisha na kilimo cha alizeti ambapo takwimu zinaonyesha Tanzania ina takribani wakulima **milioni1.6** ambao hukabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa uhakika wa mbegu bora, ukosefu wa masoko, huduma za ugani, teknolojia duni, kukosekana kwa mitaji, kero na kodi na ushindani wa mafuta yanayoagizwa kutoka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huu, Kamati inaishauri Wizara kuchukua hatua za makusudi na kutumia fursa ya soko la ndani la mafuta ya kula, kwa kuweka mipango na mikakati ya kuwawezesha wakulima kuongeza uzalishaji na kujenga viwanda vya kukamua alizeti. Hatua hii ikitekelezwa itapunguza na kuoka fedha nyingi

zinazoagiza mafuta kutoka nje na hivyo kuwezesha nchi kunufaika na mnyororo wa thamani katika tasnia ya mafuta.

### 12. Umuhimu wa Barabara za Vijijini na uhusiano wake kwenye Kilimo

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonyesha kwamba **asilimia 80** ya Watanzania wanaishi vijijini kati ya hao **asilimia 65.5** wanajihusisha na kilimo. Pamoja na idadi kubwa ya wananchi wanaojihusisha na kilimo, bado kilimo cha Tanzania hakimnufaishi mkulima wa Tanzania kutokana na sababu mbalimbli ikiwa ni pamoja *na* ubovu wa miundombinu ya barabara za vijijini ambao unaopelekea ugumu wa wakulima kufikisha bidhaa katika masoko au viwanda kwa muda unaostahili na wakati mwingine kusababisha kuharibika kwa mazao baada ya kuvunwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua changamoto hii Serikali imechukua hatua na kuanzisha wakala wa barabara za vijijini na mijini ili kuhakikisha barabara hizo zinapitika muda wote na hivyo kuwezesha wananchi kufanya shughuli zao za uzalishaji na kujiongezea kipato na hatimae kupunguza umaskini. Kwa msingi huu, ni muhimu kwa Serikali kuiwezesha TARURA kujenga barabara za vijijini kama njia ya kuchochea kilimo na hivyo kuinua pato la wakulima na Taifa kwa ujumla.

### 13. Upungufu wa sukari nchini

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa sukari ya uhakikia ni changamoto ya muda mrefu inayochangiwa na uzalishaji mdogo wa ndani usiotosheleza mahitaji. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imekua ikihamasisha uwekezaji katika mashamba makubwa ili kuongeza uzalishaji, hata hivyo bado hatua zinazochukuliwa hazijaweza kukidhi mahitaji. Kamati inaishauri kuwa pamoja na mikakati ya Serikali kuhamasisha uwekezaji katika Mashamba makubwa ni vema kuwa na mkakati wa kuwezesha wakulima wadogo wa miwa kuzalisha miwa katika maeneo yao na

kuwezeshwa kujenga viwanda vidogo vigogo ambavyo vitaongeza upatikanaji wa sukari na hivyo kukabiliana na upungufu uliopo.

Aidha, Kamati inasisitiza ni muhimu kwa Serikali kuwa na Mkakati wa makusudi wa kuviwezesha na kuvilinda viwanda vya ndani ili viweze kuzalisha sukari ya kutosha na kuondokana na uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi.

### 14. Deni la Mawakala

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua ya kuhakiki madeni ya Mawakala kwa lengo la kuzuia matumizi mabaya ya fedha za umma. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Serikali ni vyema ikatoa matokeo ya uhakiki iliyofanya ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua watu wote waliothibitika kuhusukika na udanganyifu huo ili iwe fundisho kwa wengine.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Kilimo, Mhe. Charles Tizeba, (Mb), Naibu Waziri Mhe. Mary Mwanjelwa (Mb), Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Mhandisi. Mathew Mtigumwe, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Thomas Kashililah pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati Kamati ikichambua na kujadili bajeti ya Wizara ya Kilimo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao walioyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi

kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mahmoud H. Mgimwa Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb | " |
| 5. | Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani, Mb | " |
| 6. | Mhe. Katani Ahmad Katani Mb | " |
| 7. | Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb | " |
| 8. | Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb | " |
| 9. | Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb | " |
| 10. | Mhe. Mattar Ali Salum, Mb | " |
| 11. | Mhe. Lucy Simon Magereli, | " |
| 12. | Mhe. Justine Joseph Monko | " |
| 13. | Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb | " |
| 14. | Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb | " |
| 15. | Mhe. Pascal Yohana Haonga | " |
| 16. | Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb | " |
| 17. | Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb | " |
| 18. | Mhe. Devotha Methew Minja, Mb | " |
| 19. | Mhe. Haji Ameir Haji, Mb | " |
| 20. | Mhe. Haji Khatib Kai, Mb | " |
| 21. | Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb | " |
| 22. | Mhe. Juma Ali Juma, Mb | " |
| 23. | Mhe. Emmanuel Papian John, Mb | " |
| 24. | Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb | " |
| 25. | Mhe. Anthony Calist Komu, Mb | " |

**Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai pamoja na Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Rachel Nyega, Ndg. Virgil Mtui, Ndg. Martha Chassama na Ndg. Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa

Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa katika hoja ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mahmoud Hassan Mgimwa, (Mb)

**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,**
**MIFUGO NA MAJI**

15 MEI, 2018

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea kwa maana ya ninyi kuanza kuijadili hotuba hii, ninayo matangazo mawili.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni pia wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine *(SUA)* na vijana wajasiriamali kutoka SUGECO karibuni sana.

Kuna tangazo la Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wabunge Waislamu, Mheshimiwa Mbaraka Dau, anawatangazia Wabunge wote Waislamu kuwa leo kuna kikao kitakachofanyika katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 7.00 mchana baada ya shughuli za Bunge kusitishwa. Wabunge wote Waislamu mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyokuwa nayo, sasa tunaanza mjadala, hoja hii ina siku mbili, leo na kesho lakini idadi ya wachangiaji kwa uwiano wetu tuna 17 - CCM, 3-*CUF* na 4 - CHADEMA, kwa mpangilio huo. Sasa mimi huwa naanza na wale wengi ndiyo haki. Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndassa na Mheshimiwa Mashimba Ndaki ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi ya kwanza kuwa mchangiaji wa Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri kwa wasilisho la Wizara hii ya Kilimo lakini nimpongeze kwa jitihada ambazo alizifanya kwenye Mkoa wa Katavi, kuwaruhusu wananchi wa Mkoa ule waweze kulima zao la pamba. Tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwenye zao la tumbaku. Zao la tumbaku lilikuwa linachangia pato kubwa sana la Taifa na wakulima wa zao hilo kupata fedha nyingi ambazo zilisaidia jamii kwenye maeneo yanayozalisha zao la tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matatizo ambayo yamelikumba zao hili la tumbaku. Tatizo la kwanza ni mabadiliko yaliyosimamiwa na Serikali ya kubadilisha mfumo wa kuuza tumbaku badala ya kuuza kwa dola sasa inauzwa kwa shilingi ya Kitanzania. Maamuzi hayo tuliyoyatoa yamewapa umaskini wakulima wa zao la tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mjadala wa bei ulipokuwa unajadiliwa kilo moja ya tumbaku wastani wa dola ulikuwa Sh.2,246 leo hii dola moja ni sawa na Sh.2,289. Mkulima huyo atapoteza kwa kila kilo Sh.43 ukizidisha kwa kilo ambazo zitazalishwa kilo milioni 63, mkulima wa zao la tumbaku atapoteza karibu shilingi bilioni 4.77. Naamini ukifika mwisho wa msimu mkulima huyu anaweza akawa amepoteza shilingi bilioni 5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, maamuzi mengine ambayo tunayafanya na Serikali tunayabariki, yanaleta umaskini kwa wakulima wa nchi hii. Ifike mahali Waziri ashuke chini akasikilize kilio cha wakulima wa zao la tumbaku, akaangalie mapato ambayo yanapotezwa kwa sababu ya maamuzi mabovu. Naomba

hili mlifanyie kazi. Kima nilichowatajia cha shilingi bilioni 4 mpaka shilingi bilioni 5, tunakipoteza kwa sababu ya kushindwa kuwa na usimamizi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine kwenye zao la tumbaku ni juu ya mfumo wa uagizaji wa pembejeo. Zao la tumbaku lina kalenda yake. Haiwezekani unaagiza pembejeo kwa kuchelewa ukitegemea kwamba utawasaidia wakulima hawa. Nia nzuri ya Serikali ya kuagiza kwa pamoja, mfumo huo kwa wakulima wa zao la tumbaku haukuwasaidia wakulima, ndiyo maana kila eneo wana bei yake tofauti na ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda Kahama mfuko mmoja unauzwa kwa Sh.74,00, Chunya Sh.96,000, Mpanda Sh.96,000, Tabora na maeneo mengine mpaka Sh.98,000 lakini walipokuwa na chombo kimoja, wakulima wa zao la tumbaku walikuwa wana uwezo wa kutumia bei moja kwa nchi nzima. Naomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa ana-*wind up* hotuba ya Wizara hii, watafute majibu ya suluhu ya kuwatafutia chombo ambacho kitawasimamia wakulima wa zao la tumbaku ili waweze kusimamia zao lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni zao la pamba. Serikali imefanya kazi nzuri ya kuhamasisha wakulima wa zao la pamba katika nchi yetu. Karibu maeneo yote wamelima na wameitikia wito wa Serikali. Niwaombe sana Serikali iangalie ni jinsi gani wakulima hawa wa zao la pamba watapata soko lao vizuri. Niwaombe sana mliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yangu ya Tanganyika ambayo ndiyo imeanza kulima zao la pamba hawajajipanga vizuri juu ya kuweka msimamo wa kununua zao la pamba kupitia kwenye ushirika, watanunua vipi ile pamba? Naomba Waziri atupe majibu. Mfumo uliopo wamelima bila kupitia kwenye ushirika na ushirika haukuandaliwa, naomba na hili mlifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni zao la mahindi. Wakulima wa mahindi, mpunga, mbaazi na mazao mengine wamekuwa watumwa katika nchi yao. Mkulima wa mahindi ndiye pekee katika nchi hii anayeonewa, anapangiwa bei ya kuuza mazao yake hapewi nafasi ya kuyauza mazao mahali ambapo anahitaji kuyauza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba muwaonee huruma wakulima wa mazao ya tumbaku na mpunga. Hawa wakulima ndiyo wamekuwa watu ambao wanalinda mfumuko wa bei, kitu ambacho siyo sahihi. Mkulima wa zao la mahindi ama mpunga asipewe mzigo wa kulinda mfumuko wa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii sukari inauzwa Sh.3,000 mpaka Sh.2,800, kwa hiyo mkulima wa kijijini akitaka kununua sukari ya kilo 10 lazima abebe gunia mbili ndiyo anunue kilo 10. Haiwezekani! Fikeni mahali mbadili mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Waziri waimarishe Kitengo cha Ununuzi wa Mazao. Kwenye bajeti nimeangalia, mmetenga shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kununua mazao, ambapo uhalisia mnahitaji shilingi bilioni 86 kwa mujibu wa Kamati ya Kilimo. Niombe mfuate maelekezo ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani, mwananchi tajiri awe anapata unafuu kwa mwananchi kutoka kijijini. Mwananchi wa kati analishwa na mwananchi wa kijijini, mwananchi mzururaji wa nchi hii analishwa na mwanakijiji ambaye yuko kule kijijini, haiwezekani! Naomba Waziri aje na majibu ya msingi, wawaruhusu wakulima wauze mazao yao mahali popote wanapotaka. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mfumo wa pembejeo, Serikali ilikuja na nia njema lakini haijawasaidia wananchi. Pembejeo hazikufika kwa wakati na kulikuwa na urasimu mkubwa. Naomba Waziri aje na majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwenye ushirika. Serikali mmesema kwamba mtaanzisha Tume ya Ushirika, kwenye Tume ya Ushirika hamna kitu chochote kilichofanyika. Vyama vya Ushirika vinasimamiwa na Tume hii ya Ushirika, hampeleki fedha watajiendesha vipi? Katika wafanyakazi ambao wanashida nchi hii ni wanaushirika. Maafisa Ushirika wamebaki na jina tu kuitwa Maafisa Ushirika lakini uhalisia hakuna kitu chochote kinachofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umeisha.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Mashimba Ndaki ajiandae.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba ni siasa lakini pamba ni uchumi. Nitamke wazi kuwa siungi mkono bajeti hii kwa sababu moja kubwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu alihamasisha sana Wakuu wa Mikoa, mikoa 10 na wilaya 46 zinazolima pamba, wananchi wakajitokeza kwa wingi wakalima kweli, kitu cha kushangaza ni kwamba matarajio ya wakulima hawa kwa bei ya mwaka jana kwa kilo moja ilikuwa Sh.1,200, lakini bila aibu mkulima huyu amejitolea kweli kweli, bei ya sasa kwa kilo moja ni Sh.1,100. Hivi mkulima huyu tunamsaidia namna gani? Kila mwaka msimu unapoanza, kelele ya bei ni kwa zao la pamba peke yake, hivi tatizo huwa ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kupitia bei ya soko. Bei ya soko ni senti 76, ukikokotoa utakuta thamani ya

pamba nyuzi ni Sh.1,357 thamani ya mbegu ni Sh.281, ukijumlisha kwa kilo moja unapata Sh.1,638. Gharama za uendeshaji na uchambuaji kwa yote hayo ni Sh.405, ukitoa kwenye hiyo Sh.1,600 utabaki na Sh.1,233. Ni bora basi huyu mkulima ambaye amehangaika usiku na mchana kulima mngemuachia bei yake iwe kwa kilo Sh.1,200, Sh.100 mnamnyang'anya, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, eti wanasema hiyo ni kwa sababu mkulima huyu anatakiwa kulipia deni la viuadudu la shilingi bilioni 29, mkulima huyu alipie mabomba ya kupulizia shilingi milioni 525 lakini mkulima huyu alipie deni la mbegu shilingi bilioni 1.2, mkulima huyu alipie deni la shilingi bilioni 27.7, mkulima huyu huyu, lakini alipie na deni la miaka ya nyuma shilingi bilioni 3. Hivi wakati haya madeni mnayatengeneza mkulima huyu alikuwepo? Hakuwepo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi jinsi mkulima huyu wa pamba anavyoonewa, analazimishwa kukatwa ile Sh.100 ili kusudi alipie mbegu kabla hata ya kulima, akatwe shilingi bilioni 16 lakini anunue chupa milioni tano shilingi bilioni 20, pia alipie mabomba shilingi bilioni 2. Hivi mkulima huyu hata kabla hajalima mnaanza kumkata kwenye hii Sh.100, huyu mkulima amekosea nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, kwenye kitabu chake ukurasa wa 148, kwenye pamba, unasema kwamba mchango kwa ajili ya maendeleo ya zao la pamba fedha ambazo huwekwa kwenye Mfuko wa Pembejeo wa Zao la Pamba kwa ajili ya kusaidia kutoa mbegu na dawa za pamba, Sh.30 kwa kilo zinaondolewa. Unasema unaondoa Sh.30, unamuongezea Sh.100 utakuwa umepunguza au umeongeza? Kwa sababu huku unasema umeondoa Sh.30 lakini unakwenda unamuongezea Sh.100 huko, utakuwa umepunguza au umeongeza matatizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mfuko kwa jinsi ulivyo, tunaiomba Serikali ukafanyiwe ukaguzi na *CAG* kwa sababu hiki ni kichaka cha watu kupata fedha za wakulima. Siku zote mifuko hii imekuwa ikiwanufaisha wao wala siyo wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina ugomvi hata kidogo na Mheshimiwa Waziri Tizeba, hata kidogo, ni mdogo wangu, ugomvi wangu uko kwa wakulima wa bei ya Sh.1,200, hii Sh.100 irudisheni kwa wakulima. Mnataka tutoke tani 122,000 twende kwenye tani 1,000,000 za pamba, mtafikaje huko kama mnawanyima *incentive* hawa wakulima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wale wote wanaotoka kwenye mikoa wanayolima pamba, tusiunge mkono mpaka tupate maelezo ya kina kuhusu hii Sh.100. Sisi tunakubali kama ni Sh.1,200 lakini siyo kwa Sh.1,100. Mheshimiwa Tizeba mwakani kuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa, tutawaambia nini wale wananchi? Kama nilivyosema, pamba ni uchumi, pamba ni siasa, lazima tufike mahali tuwasaidie wananchi wetu, wamejitolea mno kulima na Waziri anafahamu jinsi walivyohangaika, kuna wadudu na matatizo mengine yamejitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi na hili naomba Waziri aje alifafanue vizuri zaidi, anasema ushirika kazi yake ni kukusanya, sijui unakusanya kutoka kwa nani? Yaani huyu mkulima achukue pamba yake ampelekee huyu ushirika, ushirika ambao tunaujua sote pamoja na Waziri, hii pamba yangu au yake? Halafu baada ya hapo aje mnunuzi, pamba yangu iende ikakae siku tatu, nimezoea nikuchukua pamba yangu naipeleka sokoni, napima kilo shilingi ngapi, nachukua hela yangu, sasa mkulima huyu aende akakopwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo jema kuimarisha ushirika lakini twende basi taratibu. Ukishasema kwamba kazi yao hawa ni kukusanya, je, anakusanya kwa siku ngapi? Kwa siku nne au tano yaani huyu mkulima apeleke pamba yake

ikasubirie pale, Mheshimiwa Tizeba mdogo wangu nawe unatoka kwenye pamba...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndassa kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Mashimba Ndaki, atafuatiwa na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami pia niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri iliyo mbele yetu. Nianze kwa kusema kwamba siungi mkono hoja ikiwa suala la bei ya pamba halitakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu vizuri kazi ya kulima inakuwaje. Kama kazi ya kulima zawadi yake ndiyo hii tunayoipata kutoka Serikalini basi nadhani tuhamasishe watu wetu waache kulima. Mwaka jana bei ya pamba ilikuwa Sh.1,200, mwaka huu kama alivyosema ndugu yangu ni Sh.1,100 sababu hazieleweki, haijajulikana kwa nini bei imeshuka? Kuna mambo mengi hapa ambayo yanasikika, moja ni kwamba Sh.33 zinabaki sijui ushirika, Sh.12 zinaenda kuimarisha sijui Chama Kikuu cha Ushirika, Sh.55 zinaenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofika kwenye masuala yanayogusa watu wengi ni muhimu sana Serikali iwe sikivu sana. Ni vuzuri tuelewane hapa, bei ya pamba kama ilivyotajwa na ndugu yangu Mheshimiwa Ndassa ndivyo ilivyo kwa nini kuondoa Sh.100 kwa wakulima? Si ingebaki angalau Sh.1,200 kama ilivyokuwa mwaka jana, kwa nini tumeiondoa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutataka majibu yaliyo sahihi, lakini jibu lililo sahihi ni kurudisha Sh.100 kwa wakulima wa pamba. Majibu mengine mbali na hayo hayataeleweka na hayaeleweki. Ndugu yangu Mheshimiwa Ndassa amesema vizuri, mazao haya makuu ya pamba, korosho na mazao mengine ni siasa kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema juu ya ununuzi wa pamba mwaka huu. Msimu wa pamba umekwisha kuanza tarehe 1 Mei, 2018 lakini hakuna tone la pamba iliyonunuliwa mpaka sasa. Kwenye Jimbo na Wilaya yangu hakuna pamba iliyonunuliwa na sababu ni kwamba, umekuja utaratibu mpya wa kununua kupitia ushirika. Ushirika ni mzuri, lakini ulifanya vibaya siku za nyuma na watu hawauamini tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa badala ya Serikali kuhangaika na mafunzo na kuwajengea uwezo watu wetu na ushirika wenyewe ili waelewe dhana mpya ya ushirika kwamba itawasaidiaje wananchi wetu, wamekuja moja kwa moja na kuiweka kwenye utekelezaji. Nadhani ni kosa kwa sababu kama watu walishauona ushirika ni mbaya unapotaka kuanzishwa upya ni muhimu sana kuwaelimisha wananchi waweze kuelewa. Kwa hali ilivyo mimi sijui tutaishia wapi msimu huu wa pamba kwa sababu kama pamba haijanunuliwa, haijaenda kwenye ghala la ushirika, sasa sijui itaenda lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo hayo utaratibu uko hivi, pamba ikusanywe kwenye ghala la ushirika, ghala lenyewe la ushirika kwenye kijiji liko moja na kijiji kina vitongoji zaidi ya kimoja, vitatu, vinne hadi vitano na vingine viko mbali, lakini wakati wa ununuzi wa watu binafsi pamba ilikuwa inanunuliwa mahali karibu na mwenye pamba, maghala yalikuwa mengi. Sasa safari hii ghala liko moja na mahali pengine maghala hayo ya ushirika yaliyopo yamechakaa hayana hadhi ya kuhifadhi pamba, sijui tutafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo lingine kuna utaratibu wa wakulima kulipwa pesa yao kupitia benki. Kwa nini iwe ni lazima? Nafikiri suala la kulipwa kupitia benki ni zuri kama ni kwa hiyari, kwa sababu hii pesa ni ya mkulima. Mimi nauza pamba yangu leo, nina mgonjwa, nina matatizo mtoto wangu hajaenda shule sijanunua *uniform* za shule, halafu nipeleke pamba yangu nisubiri siku mbili, tatu, nne bado sijalipwa. Halafu ikilipwa niende benki iliyo Makao Makuu ya Wilaya kilometa mia moja na kitu, saa ngapi nakamilisha mahitaji yangu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linapaswa kuangaliwa vizuri. Halafu ushirika unafanyika kama wakala, wao wanakusanya pamba ya mkulima halafu mnunuzi anakuja pale na pesa yake au pesa yake anawapa watu wa ushirika. Hivi kuna mnunuzi gani binafsi atapeleka pamba yake kwa mshirika ambaye anajulikana alikuwa …

**TAARIFA**

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndaki, kuna taarifa, ngoja nimsikilize kama ina maana.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa mzungumzaji anayendelea kwamba kuna baadhi ya Vyama vya Ushirika vimechagua viongozi wasiokuwa na *credibility* katika maeneo hayo, hawaaminiki na wana historia mbaya, kule wanaitwa ‘magalagaja’. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naikubali kabisa taarifa yake. Kwa sababu hao viongozi waliochaguliwa nina habari wengine wametoa rushwa sijui kwa kutarajia kupata kitu gani. Kwa hiyo, ni walewale

waliokuwa wameharibu ushirika kule nyuma ndiyo wamerudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini pamba haijapelekwa sokoni mpaka leo ni kwa sababu wanunuzi na wenyewe wamerudisha mikono nyuma kwa sababu hawana imani na watu wa ushirika waliopewa dhamana ya kuchukua pamba na pesa kwa wanunuzi. Mnunuzi huyu atamwaminije mtu ambaye hajamchagua? Atamwaminije ampe bulungutu la mamilioni ya pesa eti amnunulie pamba wakati hamjui? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utaratibu wa kununua uko hivyo basi wanunuzi binafsi wapeleke watu wao kwenye gulio pamba ilipo, muuzaji aje pale auze pamba yake alipwe hela yake aondoke lakini mtu atakayekuwepo pale ni yule aliyeaminiwa na mnunuzi wa pamba. Vinginevyo ushirika tuendelee kuujenga upya bado haujapokelewa vizuri kwa sababu ya historia yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya pamba kuwa chini inasababishwa na vitu vingi mojawapo ni soko la hapa ndani ni dogo sana. Takwimu zinaonesha asilimia 20 mpaka asilimia 30 ndiyo tunaweza kutumia hapa ndani. Viwanda vyetu vya pamba vinashindwa kushindana kwa sababu ya ushindani usio haki wa nguo nyingi kutoka Uchina, Malaysia, Uturuki na mahali pengine. Sasa tutapandishaje mazao ya wakulima wetu nchi hii kama hatulindi viwanda vilivyoko kwenye nchi hii? Viwanda vya nchi hii havilindwi vinaachwa tu na wakati mwingine vinashindanishwa na mtu ambaye ana nguvu kuliko yeye, lazima vitakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu zao la pamba limelimwa kwa wingi sana. Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu hata Mheshimiwa Waziri wa Kilimo mweyewe kwa kuhamasisha hivyo, lakini wakulima wetu wamelima pamba hii kwa taabu sana na ndiyo maana nasema kama bei ya pamba hairudi Sh.1,200 siwezi kuunga mkono hoja hii kwa sababu ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mashimba. Tunaendelea na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenan kwa dakika tano.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba pamoja na dada yangu Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Juzi kwenye hotuba yetu ya maji tulizungumza sana tatizo la Maafisa Ugani kwenye eneo la maji, siku ya pili akalitolea maagizo kwamba Maafisa Ugani sasa hivi wawajibike *direct* kwenye Wizara ya Maji pamoja na Ardhi. Tunamuomba tena Mheshimiwa Rais Maafisa Ugani hawa kwenye eneo la kilimo tunaomba wawajibike *direct* kwa Katibu Mkuu ili kusudi wawe na *control* moja kwa moja kutoka Wizarani *otherwise* tatizo litaendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 75 ya Watanzania ni wakulima wamejiajiri katika sekta hii. Kwa masikitiko makubwa sana bado hatuitendei haki hii asilimia 75. Ukiangalia kwenye bajeti yetu na ukiangalia kwenye makubaliano yetu na nchi za Afrika Mashariki na zile za Kusini Mashariki za *SADC* na sisi Watanzania tulisaini Maputo na Malabo *Agreement* kwamba asilimia 10 ya bajeti kuu itengwe kwenye sekta ya kilimo, lakini ukliangalia kwenye *analysis* mpaka sasa Tanzania ndiyo nchi ya mwisho tuna asilimia 3.1, hii ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo ambalo tunaajiri Watanzania wengi hakika tunatakiwa tupeleke bajeti ya kutosha. Kwenye eneo hili tunategemea kutengeneza ajira ya kutosha na ndiko itakakopatikana *raw material* ya kutosha kwa ajili ya viwanda vyetu. Tumekusudia kwenda kwenye uchumi wa viwanda, tunaendaje kwenye uchumi wa viwanda kama hatuna uhakika wa kupata *raw material* ya kutosha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu tunaiomba Serikali iangalie upya kwenye eneo hili. Hata kama hatuwezi kufika asilimia 10 ya bajeti kuu tufike hata 6 au 7 tulingane na wenzetu wa Uganda na Kenya, lakini kuendelea kuwa kwenye mstari wa mwisho kwa asilimia 3.1 haifurahishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Tulipokuwa tunatamka kwamba tunataka tuanzishe Benki ya Maendeleo ya Kilimo tulikuwa tunaamini kabisa benki hii itakuja kwa ajili ya manufaa ya wakulima, lakini ukiangalia *structuring* yake utakuta kwanza yenyewe haipo kwenye *site* ya wakulima, makao makuu yako Dar-es-Salaam, haya tujiulize Dar-es-Salaam kuna mashamba makubwa kiasi gani? Taratibu za kumsaidia mtu apate mkopo kama ana shida ya kupata mkopo aende Dar-es-Salaam akatafute mkopo mtu kutoka Mufindi au Njombe? Kwa hiyo, Serikali iangalie upya itengeneze matawi nchi nzima na ilenge wakulima kwenye *site*, tunataka tupate matawi ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika *analysis* mpaka sasa hivi mtaji walionao Benki ya Kilimo ni shilingi bilioni 67 na mahitaji ya Watanzania ni shilingi bilioni 800, tofauti ni kubwa sana. Kwa hiyo, naomba sana Serikali tuongeze mtaji kwenye benki hii ili kusudi tupate uhakika wa kuajiri Watanzania walio wengi kwenye eneo hili na ambako inapatikana *raw material* ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa lazima niliseme jambo hili tena. *NFRA* ambao ndiyo wanahakikisha usalama wa mazao yetu na chakula chetu hapa nchini waliomba shilingi bilioni 86, lakini kwenye bajeti tumewatengea shilingi bilioni 15. Mgogoro mkubwa wa wakulima wa mahindi unaanzia hapa na kwenye eneo hili kama Mheshimiwa Waziri hatakuja kuonesha kwamba ataongeza hela nitakuwa mtu wa kwanza kushika shilingi hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tumepata tatizo kubwa sana kwenye eneo la mahindi. Kwa mfano, sasa hivi kwetu Mufindi debe la mahindi ni Sh.3,000 ambalo lina kilo 20, kilo moja ya sukari ni Sh.3,000 wapi na wapi? Kwa hiyo, mtu akitaka sukari kilo moja ni lazima auze debe moja la mahindi, itafika sehemu tutakata tamaa kulima mahindi. Serikali isipotamka kupagusa hapa kwenye *NFRA* nitawashawishi Wabunge wenzangu tunaotoka Mufindi na maeneo mengine kwamba tunapigwa. Hatuna jambo la kujivunia katika Mikoa ya Iringa, Njombe na Mikoa yote ya Kusini kama mahindi yetu tuliyokuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali imeamua kujenga maghala na vihenge ya kisasa kabisa katika Kanda Nane, sasa kwa shilingi bilioni 15 tutaweka nini humu? Tumejenga majengo ambayo yanagharimu fedha nyingi lakini hela za kuweka hayo mahindi kwenye maeneo haya, hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusiendelee kuwaonea watu wa Mufindi na wa maeneo mengine kwenye eneo hili, mimi sipo tayari. Waziri ni rafiki yangu tumekua wote na mimi ndiye Mwenyekiti wake wa Kamati lakini leo nasema najivua Uenyekiti wa Kamati, nabaki kama Mbunge wa Mufindi Kaskazini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali, kulikuwa kuna jambo la madeni ya mawakala Serikali

ikasema lazima ihakiki. Haya Serikali mmehakiki baada ya kuhakiki *what next?* Kwa nini tusiseme mawakala hawa wanadai, hawa hawadai, kusudi Serikali iwalipe ambao wanadai? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie. Hawa mawakala wengine wanakufa, wanauziwa majumba yao, wana hali mbaya kwenye maeneo mbalimbali. Ifike wakati Serikali itoe tamko mawakala wanaodai ni hawa na hawa hawadai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Maofisa wa Serikali ambao wameshiriki kwenye utapeli, kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria? Tunaenda kushughulika tu na mawakala? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka niseme tu kwamba naunga mkono hoja lakini...

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini nasema hivi Mheshimiwa Waziri asipokuja na majibu kuhusu kuongeza hela *NFRA* nitashika shilingi yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Khenani dakika tano.

**MHE. AIDA J. KHENAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa aliyemaliza amesema anaunga mkono hoja lakini amezungumzia suala la mahindi, mimi nasema mapema kwamba siwezi kuunga mkono hoja wakati wananchi wangu mahindi yanaoza yako nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbolea, tumezungumza suala la Mfumo wa Pamoja wa Kununua Mbolea, nataka nimwaambie Waziri na Wizara kwa ujumla kwamba, mfumo huu ume-*fail,* haujafanikiwa hata kidogo. Mkafanye tathmini upya juu ya ugawaji wa mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa Mkoa wangu wa Rukwa, juzi tulikuwa kwenye semina mkazungumzia Minjingu, yaani kwetu Minjingu tunaichukia kama ugonjwa wa UKIMWI. Imeleta umaskini kwa wakulima na imeleta shida kwa wakulima wetu. Kwa hiyo, kama lengo la Serikali ni kujenga viwanda, waiteni wawekezaji waje kuzalisha *urea,* waiteni wawekezaji ambao watakuja kuangalia hitaji la wakulima wanataka nini, Minjingu Mkoa wa Rukwa hatuihitaji, labda kama mtarudi kufanya maboresho ya mbolea hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la bei elekezi. Bei elekezi ni kizungumkuti tu. Mkoa wetu wa Rukwa mbolea imekuja kwa bei tofauti na ile ambayo ilikuwa imepangwa. Kwa hiyo, niseme tu kabla hamjatoa tamko lolote au kuzungumzia bei elekezi kama hamna uhakika muache kwanza mkafanye tafiti badala ya kuwaletea ugomvi wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi tamko la Serikali linatoka hapa la kuzuia kuuza mazao nje ya nchi, Sumbawanga Mjini bei ya gunia ilikuwa Sh.70,000, hivi ninavyozungumza leo gunia la mahindi Mkoa wa Rukwa ni Sh.18,000 mpaka Sh.24,000. Naomba niwaambie tu Serikali ya Chama cha Mapinduzi kama mmeamua kwamba zao la mahindi halifai njooni na zao mbadala badala ya

kuwafanya wakulima wawe maskini. Kama hamna zao mbadala muwaambie kwamba wao ni Watanzania au wanatoka nchi gani? Mbolea mnaleta kwa kuchelewa, yaani wakati tunahitaji mbolea za kupandia hamleti, wakati tunahitaji mazao yakue ndiyo mnaleta mbolea ya kupandia kwa hiyo mnakwenda *vice versa* tena kwa bei tofauti na ile ambayo mlikuwa mmepanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niiambie Serikali, kama nia yetu ni kujenga viwanda, kama mnavyosema kauli mbiu ni kujenga viwanda, mambo yanayotendeka na Wizara ya Kilimo ni tofauti na kauli mbiu. Huwezi kujenga viwanda umeshindwa kutengeneza mazao ambayo unajua ndiyo ambayo yanakwenda kuzalisha hivyo viwanda vyenu mnavyovizungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo yanasikitisha sana. Leo unapozungumzia kilimo ambacho kinaajiri watu wengi kwenye Taifa hili ndiyo mmepeleka asilimia 18. Tunaomba Waziri utakapokuja hapa utuambie nini kilitokea mpaka mkapewa asilimia 18. Mkumbuke kwa kuwa, ninyi ndio mlizuia wananchi wasiuze mazao yao nje ya nchi yale mazao yao ya mwaka jana kwa sababu tunaenda kwenye msimu mwingine wa mavuno, ambayo ninyi ndio mlisababisha wao wakashindwa kuuza, mnayafanyaje? Mnayanunua au mnawaruhusu wapeleke sehemu nyingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kizungumkuti kidogo kwenye suala la mawakala. Bajeti ya 2015/2016 ilikuwa ni shilingi bilioni 35, kwenye chombo chao cha mawakala wanazungumza kwamba hilo ndiyo deni, lakini watu wenu kwenye Wizara wanasema ni shilingi bilioni 67 na ndiyo maana mpaka sasa hivi hamjawalipa mnaendelea kuhakiki. Sasa tunata Waziri atakapokuja atuambie ipi ni sahihi? Kwa sababu, kama bajeti ilikuwa shilingi bilioni 35 hiyo shilingi bilioni 67 imetoka wapi na hizo vocha zilitengenezwa kwa

pesa gani? Zile vocha zilizorudi zimerudi kwa nani na kwa utaratibu gani? Waziri atakapokuja hapa atuambie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kutengeneza vocha zaidi ya bajeti ilivyotengwa, lazima uendane na bajeti. Kwa hiyo, kama kweli mna hakika mnashughulikia mafisadi tunataka uwazi wa jambo hili, ni kipi kati ya shilingi bilioni 35 na shilingi bilioni 67? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khenani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumejitahidi kidogo, huo ndiyo muda wetu kwa asubuhi hii. Nina tangazo moja tu tena kwenu, tusikilizane basi. Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wenye shughuli za uvuvi katika majimbo yao ama wanakusudia au wana matamanio na shughuli za uvuvi, anaomba mkutane kule nyuma ya Ukumbi wa Msekwa kwenye chumba tulichokuwa tunatumia zamani kama zahanati. Kwa hiyo, mara tu baada ya shughuli za Bunge kusitishwa, yeye ni mtaalam wa masuala ya uvuvi labda ana habari njema kwetu lakini wasiishie tu na shughuli za uvuvi tunataka na ufugaji wa samaki kwenye malambo na madimbwi.

Waheshimiwa Wabunge, majina ya Wabunge ambao tutaanzanao saa 11.00 niwataje watatu wa kwanza wa dakika 10 hawa ni Mheshimiwa Hassan Masala, Mheshimiwa Mariam Ditopile na Mheshimiwa Richard Mbogo, *then* tutaona namna ya kwenda mbele.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Niliwataja Waheshimiwa Wabunge watatu wa kwanza ambao ni Mheshimiwa Hassan Masala, Mheshimiwa Mariam Ditopile na Mheshimiwa Richard Mbogo, hawa ni wa dakika kumi, kumi. Tuanze na Mheshimiwa Masala.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza jioni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipitia na kuisoma vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri na maombi ya fedha ambayo anaomba. Pamoja na yote ambayo yamewasilishwa nina mambo kadhaa ambayo napenda kwa niaba ya wananchi ambao tunawawakilisha hapa Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atupatie maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni uendelezaji wa zao la korosho. Ziko jitihada kubwa sana ambazo zimefanywa na Serikali yetu lakini pia iko kazi kubwa sana ambayo sisi Wabunge pamoja na Serikali tumeifanya katika kutoa tozo zile ambazo zilikuwa kandamizi kwa wakulima wetu na hii imepelekea angalau kuona tija kidogo. Hata hivyo, yako mambo ambayo naona ni busara sasa tuweze kuelekezana na pia tupeane ufafanuzi ili tuweze kuona namna bora ambavyo tutaliendeleza zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na Mfuko wa Pembejeo ambao kazi yake kubwa ilikuwa ni kuendeleza zao la korosho. Kwa msimu wa 2016/2017, ziko fedha nyingi sana (*export levy)* ambazo wakulima wa korosho wamekatwa. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kusimama atueleze kwa mwaka nilioutaja 2016/2017 ni kiasi gani cha fedha zao la korosho limechangia lakini pia Serikali itueleze ni kiasi gani imerejesha kwa ajili ya uendelezaji wa zao hili la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena Mheshimiwa Tizeba kila Mbunge aliyesimama kutoka Mkoa wa Lindi na Mtwara jambo hili amelizungumzia na mimi naomba kwa heshima na taadhima utakapokuja kusimama utuambie fedha ya *export levy* ambayo tulipaswa turudishiwe kwa ajili ya kununua pembejeo mpaka sasa hivi tunavyozungumza iko wapi na imetumika kufanya kazi gani? Kwa sababu utaratibu ambao sasa hivi unaendelea ni kinyume na makubaliano yetu ya awali na namna hata mfuko unavyotaka katika uendelezaji wa zao letu la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo pia naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni nia haswa ambayo wenzetu wa Wizara wameanza kuionyesha. Kabla sijasema naomba kidogo niwakumbushe wale waliosoma historia. Kipindi cha ukoloni nchi hii iligawanywa katika kanda, yako maeneo ambayo yalikuwa yanalima mazao kutokana na hali ya hewa jinsi ilivyo. Leo hii ukienda Mwanza utakuta pamba, Kusini mwa Tanzania utakuta korosho na ndiko inakostawi na ndiko inakotoka korosho bora na ukienda Kaskazini huko utapata kahawa na chai. Leo hii sijajua ni tamaa kiasi gani imetuingia tunataka tulihamishe zao la korosho kutoka Kusini ambako lilikuwa linalimwa tulifanye kuwa zao la Tanzania nzima. Siyo jambo baya, kama tumeamua kuweka mkakati huo basi si vibaya Mheshimiwa Waziri atuambie ni kiasi gani cha fedha ya kahawa anaenda kutuletea watu wa Lindi na Mtwara ili na sisi tukaanze kulima mazao haya ya biashara ambayo yatakwenda kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kinachofanyika nafahamu kina nia njema kwa wakulima na Watanzania na hii ni kwa sababu tayari tumeshaanza kuona faida kubwa ambayo inapatikana kwenye zao la korosho. Ukichukua mathalani Dodoma leo hii tunakuja kupanda korosho, mikorosho ambayo mmeisambaza mwaka uliopita mpaka sasa hivi iko majumbani inakauka tu, hamna mtu yeyote ambaye anaishughulikia na anaifanyia kazi. Wakati mikorosho hii tungeweza kuisambaza Tandahimba, Mauta,

Nachingwea na Liwale ambako hali ya hewa inaruhusu ingeweza kuleta tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba Mheshimiwa Waziri atuambie hasa anachokusudia kukifanya ni nini. Kama lengo ni kutawanya keki hii basi si vibaya na sisi watuletee fedha za pamba, kahawa na chai ili na sisi tuweze kulima katika maeneo yetu kwa sababu ardhi yetu nayo pia inaweza kuhimili na kupokea mazao hayo kama ambavyo maeneo mengine wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kupata ufafanuzi kupitia watu wa Wizara. Ukisoma Ripoti ya *CAG,* ukurasa wa 148 – 151, umeeleza ubadhirifu mkubwa sana ambao umejitokeza katika uzalishaji wa zao la korosho. Ziko hatua ambazo tulitamani kuziona zinachukuliwa na zitatusaidia sana kuendeleza zao la korosho kama ambavyo Serikali na watu wa Wizara wamekusudia. Najua uko wakati ambao tutajadili ripoti ya *CAG* lakini ni vizuri wakati tunaenda kujadili bajeti ya Wizara hii lazima tuone hatua na dhamira gani watu wa Wizara wamekuwa nazo kwa ajili ya kuhakikisha ubadhirifu ambao umeendelea kujitokeza kwenye zao la korosho unadhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ukisoma utaona kupitia Mfuko wa Hisani wa Kuendeleza Zao la Korosho iko fedha ambayo ilipaswa tayari iwe imeshakatwa kutoka kwa watu wa vyama Sh.4,085,000,000. Mpaka mwaka huu wa fedha ambao tunaenda kuumaliza fedha hii haieleweki ipo kwa watu wa vyama vya ushirika kwa maana kwenye akaunti zao au ilitakiwa iwe wapi kwa sababu wako watu ambao wamekatwa na hawa ni wakulima ambao sisi tunawawakilisha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba sana, haya siyo maneno yangu ni ripoti ya *CAG* ukiisoma vizuri inabainisha na inataka watu wanaohusika na eneo hili watueleze fedha hii shilingi bilioni 4 iko wapi mpaka sasa hivi ili tuweze kuwarudishia wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine katika ripoti hii ya *CAG* ukiiangalia vizuri utaona wako watu ambao

wamepewa fedha kwa ajili ya ubanguaji wa korosho. Iko Kampuni moja inaitwa *Jumbo Cashewnuts* na kikundi cha akina mama wanaonekana wamechukua fedha zaidi ya shilingi milioni 500, fedha hii haijarejeshwa mpaka leo tunavyozungumza. Wako viongozi wa Bodi ya Korosho wamechukuliwa hatua lakini hatuamini kwamba wale wachache waliochukuliwa hatua ndiyo pekee ambao wamehusika na upotevu wa fedha za wakulima. Tunaomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na timu yake watuambie wote wanaowasaidia viongozi wote wa Bodi ya Korosho ni hatua gani watakwenda kuchukuliwa kwa usumbufu na hasara kubwa ambayo wamewasababishia wakulima wetu ambao kimsingi mpaka sasa uendelezaji wake unasuasua. Wale wanaopaswa kukopeshwa hizi fedha bado hawajakopeshwa kwa sababu tu kuna watu ambao makampuni yao yamechukua fedha na hawajazirejesha kwa wakulima ili tuweze kuingiza katika mzunguko ambao utatusaidia kuwakomboa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka nilizungumze ni suala zima la uchelewaji wa malipo. Yako makampuni leo tunazungumza mwezi wa tano takribani miezi sita imepita toka tumefunga minada bado hawajalipa wakulima fedha zao. Hili ni jambo la hatari na la kukatisha tamaa sana. Wakulima wetu walio wengi sasa hivi wanapata shida ya kuendesha maisha yao kwa sababu fedha zao kuna makampuni wamezikalia. Ziko sheria ambazo zinataka wale waliochukua fedha hizi kuchukuliwa hatua lakini mpaka sasa hivi kesi nyingi ziko polisi na wakulima wanaopaswa kulipwa hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri alishafika katika maeneo yetu na hasa aliishia Masasi lakini naomba niwape taarifa, walichokiona Masasi ni sehemu tu bado maeneo ya Nachingwea ukienda Liwale kuna wananchi mpaka leo napozungumza, mkihitaji ushahidi wa haya nitakuja niwaambie hawajalipwa fedha zao na wanaendelea kuzungushwa. Kesi zinaenda polisi hazifikishwi Mahakamani, hatujui sababu za kesi hizi kutofikishwa

Mahakamani ni nini wakati wakulima walishatoa korosho zao kwenye makampuni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauri makampuni yanayoshindwa kulipa yaondolewe katika ununuzi wa korosho za wakulima. Jambo hili huu sasa mwaka wa pili halijafanyika na makampuni haya yanaendelea kushiriki kwenye ununuzi wa korosho. Sasa hii kidogo inatupa shida kujua dhamira yetu haswa ipo katika eneo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka nichangie ni zao la mbaazi. Mheshimiwa Waziri Mzee Tizeba kila tunaposimama hapa tunazungumza suala la mbaazi, uchungu wake ni kama bado haujawafikia lakini kwa sisi tunaokaa na hawa wakulima hili jambo tutapaza sauti kila tutakapopata nafasi ya kusimama hapa mpaka Serikali itakaposhtuka. Wakulima wetu bado wanaendelea kuzalisha mbaazi lakini hakuna mikakati yoyote ambayo itaenda kumkomboa mkulima anayelima mbaazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako majibu hapa tumepewa kwamba tulime mbaazi na ikiwezekana tule kama mboga haina shida, hizo sisi tunakula kama mboga lakini bado tunaomba majibu ya kina. Nimeisoma hotuba vizuri sana inaeleza kwamba Serikali itaendelea kuimarisha soko la ndani lakini pia itaendelea kuhamasisha viwanda ambavyo vitafunguliwa kwa ajili ya kuendeleza au kununua zao hili. Tunaomba kupitia Kitengo cha Utafiti watuambie bado tuna mahitaji ya mbaazi? Kama hatuna mahitaji tuwaambie wakulima wetu wasiingie hasara ya kulima mashamba makubwa ambayo tija yake mpaka sasa hivi bado haijaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha naomba jambo hili alipe kipaumbele, tunaomba *statement,* tunaomba kauli yake vinginevyo mwezi wa saba, wa nane tutakuja hapa kumlaumu kwamba kwa nini mbaazi haijanunuliwa wakati hili jambo siyo lake yeye ni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Masala kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Mariam Ditopile, Mheshimiwa Richard Mbogo na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi wajiandae.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kutoa mchango wangu. Natangulia kwa kusema kauli inayosema nitasema ukweli daima fitina kwangu mwiko. Naenda kuchangia ukweli siyo fitina wala majungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kuwapongeza viongozi wetu wakuu wawili: Rais wa nchi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Waziri Mkuu, wameonekana namna gani wana dhamira ya dhati kuwasaidia Watanzania. Katika ziara zake zote Mheshimiwa Rais lazima atatue matatizo ya wakulima, hata Waziri Mkuu tumeona akihangaika kwenye kahawa, korosho, tumbaku kwa kweli hawa viongozi wetu kwenye hili wanapaswa kupongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Dkt. Tizeba ni swahiba wangu lakini leo naomba nimwambie uswahiba baina yangu mimi na yeye haujazidi uswahiba niliokuwa nao na wakulima wa nchi hii. Najua jasho wanalolitoa, najua jinsi gani wanavyojikwamua na mazingira magumu lakini wanataka kupatia uchumi wetu kipato kikubwa. Kwa hiyo, leo hii nasimama kwa niaba ya wakulima wangu wa Chubi, Chamwino, Dodoma Mjini, Kondoa, Chemba, Soya, kote naomba niongelee machungu yanayowapata na naongea kwa *facts*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na zao la mahindi. Tanzania ilishatoka kwenye kilimo cha *subsistence,* hatulimi mahindi kwa ajili ya chakula, tunalima mahindi kwa ajili ya biashara na chakula. Leo hii ripoti yake yeye mwenyewe inamsuta amesema tumezalisha zaidi ya asilimia

120, kwa hiyo, suala la yeye kulinda *food security* asiende kuwaumiza watu ambao tunawaambia walime kwa ajili ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe ni kijana ambaye ni mkulima, nina mwaka wa saba kwenye kilimo lakini *I regret to say* ni mwaka wa kwanza sijalima. Nina gunia 6,500 juzi nimetoka kuzitupa zimeoza, tunaelekea wapi? *It is very simple,* Mheshimiwa Tizeba anakwenda kushauri viongozi wetu wakuu anawalisha matangopori kwa nini? Leo hii tayari tuna ziada na kiada ya mahindi anaenda kuweka zuio la ku-*export* mahindi lakini anaruhusu mahindi yaingie basi si angeacha tuminyane wenyewe ndani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima hajaomba mbegu hasa sisi wa Kanda ya Kati, Dodoma tunalima katika hali ngumu, anasema ili kwa Mheshimiwa Musukuma wasife njaa atuumize sisi. Musukuma ana madini, ana ziwa kule anavua samaki, sisi tunategemea kilimo, kilimo chenyewe ni cha machungu kweli kweli hatupati lolote kutoka Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mahindi yameoza hali ni mbaya, anajibu majibu kirahisi oh hao wachuuzi, kwani wachuuzi wanaenda kununua na mawe yale mahindi? Mkulima kitu chochote akishavuna, amekaa miezi saba anasubiria kitu chini ya ardhi hajui hatma yake, anavuna mahindi yeye anachotaka apate hela aendelee na maisha, alipie watoto ada, aweze kula, aweze kujitibu anasema *simply* wachuuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mkiwasema wachuuzi ndiyo vijana wangu wengi wa hapa Dodoma wamejiajiri katika sekta hiyo na hawa ndiyo wa kuwasaidia. Hebu tutathmini leo hii *exporters* wangapi wana asili ya Kitanzania? Sasa kama hatutowashika hawa mkono kuwapandisha tutazidi tu kuwa na wale wageni ambao ndiyo wanapeleka mazao nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni-*regret* sana kwenye mahindi kwa kweli basi angalau ungesema tunakataza kutoa nje lakini tusiingize kutoka nje ya nchi. Leo hii Zambia wameingiza mahindi mengi Mtwara, Lindi mpaka Himo, mahindi yetu yamekwama hakuna soko, huo ndio ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye tumbaku, kwa sababu anajitetea sana Mheshimiwa Waziri. Uongozi una vitu viwili, sawa bajeti anapelekewa ndogo lakini kuna utashi, Waziri ana utashi gani, hapa umesoma hotuba yako hata hatujasisimkwa sisi kama wakulima. Bajeti ya kwanza aliongea Mheshimiwa Mwigulu hapa kila mtu alisisimka kama mkulima alisema kabisa sasa hivi yale mageti hakuna kuzuia magunia ya wakulima muwaache. Aliendа kutatua kero ambayo inamgusa mkulima wa kawaida*, but now nothing my friend, nothing*. Sawa Waziri anapelekewa bajeti ndogo lakini utashi, ameaminiwa na Mheshimiwa Rais apeleke kilimo kwa ajili ya kuleta uchumi wa viwanda lakini ndiye yeye anavuruga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *world market price* ya tumbaku, *Cost, Insurance and Freight* mpaka Vietnam ilikuwa kilo moja ni dola 2.20. Wanunuzi wetu hapa walikuwa tayari kwa sababu ununuzi wa tumbaku ni *pre-order*, walikuwa tayari kununua zaidi ya *order* waliyotaka lakini wakaomba wanunue kwa dola 1.3 lakini Mheshimiwa Waziri akakataa huku akijinadi kwamba ana wanunuzi. Akaenda nasema tena tangopori akamlisha Mkuu, akamlisha Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini Wabunge wa Tabora huku walichachamaa wakasema mbona wanunuzi wanazuiwa kununua na tumbaku zinakaa muda mrefu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe inavyosemekana Waziri alisema kwamba wanataka kununua kwenye 0.8 lakini ilikuwa wanataka kununua kwa 1.3. Kilichotokea mvua imenyesha, hawana vihenge wale, hawana sehemu ya kuhifadhia, wanalima ili wauze waweze kuendelea na maisha mengine, tumbaku zimeharibika, zimeshuka thamani, mwisho wa siku wameuza kwa *0.8 USD*. Kwa hiyo, zile pesa

walizopata wameenda kulipa tu madeni hakuna chochote yaani kwa kweli wenzangu Wabunge wa Tabora watakuja kusema hali halisi, mimi ni Mbunge wa nchi nzima kwa hiyo lazima niliongelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye korosho. Picha tunayoipata kwenye korosho kwa kweli niwaambieni siyo juhudi za Wizara, ni kudra ya Mwenyezi Mungu. Tuna *advantage* kwamba msimu unapoanza sisi ndiyo nchi ya kwanza ya kuvuna korosho, kwa hiyo, tunakuta makampuni mengi yanahitaji ile korosho. Ndiyo maana mpaka leo korosho ina bei ya juu tunapoona kwenye minada. Vilevile *in the world* Tandahimba, Newala, Masasi na Mtwara ndiyo ambao wana-*produce* korosho nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *I was in India*, nilienda kuongea na watu kwa ajili ya kuwauzia korosho bahati mbaya niliharibu kwa sababu nilikuwa na rafiki yangu kutoka Ghana, wale waliniambia Ghana nao wana korosho nzuri *but still virgin* hawajagundua, basi maneno yale hayajaenda kushoto wala kulia, Ghana wamezindua Mpango wa Miaka Kumi wa Kunyanyua Kilimo cha Korosho, tusubiri tutakayoona, hatuna mipango endelevu. Bodi ya Korosho wanai-*disturb,* korosho ni zao la biashara, linaenda vizuri, linaleta mapato, ghafla unasema *sulphur* ipelekwe bure waliomba, ndiyo mahitaji ya wakulima? Mmeshindwa kuzifikisha kwa wakati korosho zikaingia magonjwa hakuna dawa ya kutibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, magunia, minada imeanza, mtu ana korosho zake nyumbani hamna magunia na yaliyomo chini naomba vyombo vya ulinzi na usalama vikachunguze mnajua wenyewe. Haya leo hii wamerudi tena nyuma, kwa nini tuna-*disturb industry*? Wamerudi nyuma tena wanasema ooh *sulphur* hatuzitoi bure, mliombwa mtoe bure? Kwa nini mna-*disturb* wakulima na watu wanaenda katika njia nzuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mipango endelevu tuliyokuwa nayo leo hii badala ya kutoa korosho kama *raw*

*material* tunaenda kuongeza miche. Mimi napenda kwamba kila sehemu tulime korosho kwa sababu *it is a green gold* lakini nilitoa hapa mchango mwaka wa kwanza nikasema tuweke *agricultural zone,* kila sehemu hapa ina zao lake, kwa nini tusikazanie huko? Unaniletea mikorosho Dodoma hakuna hata Afisa Kilimo mmoja aliyefundishwa utaalamu, hiyo mikorosho ikiota asilimia 10 najiuzulu Ubunge, iko majumbani imekauka. Unawapelekea watu hujawapa utaalam, tena *system* unayo, kuna Maafisa Ugani kila Kata na Kijiji, waite wape elimu halafu ndiyo usambaze, hamtoi elimu mnaenda kugawa mikorosho, tutaona mwisho wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu mimi niwashauri kidogo tu, tuweke mazingira mazuri, huwezi ukampa mazingira sawa mtu anaye-*process* korosho na yule anayeitoa nje, hebu tuwa-*favor* hawa. Kuna kitu kinaitwa *opportunity cost* ingieni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Mbogo, Mheshimiwa Msongozi na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud wajiandae.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ambalo napenda nimuachie Waziri pamoja na Wizara yake waje watuambie nchi yenye fursa kama Tanzania ambayo tunaweza tukuwa tunauza chakula nje ya nchi kwa nini bado tunaagiza chakula kutoka nje? Baada ya hapo naanza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri, ukurasa wa 19 ameelezea vipaumbele nane ambavyo Wizara yake imekuwa ikifanya utekelezaji wa haya majukumu. Cha

kwanza sikigusi, nagusa cha pili kwamba kuongeza kilimo chenye tija kwa kuongeza upatikanaji na utumiaji wa pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pembejeo kwa upande wa kilimo katika nchi yetu ya Tanzania bado ni hafifu sana. Niwapongeze kwa maamuzi ya ununuzi wa mbolea kwa pamoja *(bulk procurement)* lakini changamoto kubwa kwenye suala hili ni kufikisha mbolea kwa wakulima wetu kwa wakati kulingana na eneo husika na msimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Oktoba Mkoa wetu wa Katavi tunaanza kazi za kilimo. Watu wa tumbaku wanaanza kufulia mbegu Julai kuelekea wa Agosti, ikinyesha tu mvua ya kwanza Oktoba wanaanza kupanda. Mazao yote ambayo tunalima ndani ya Mkoa wa Katavi tukianzia tumbaku, mahindi na mpunga utaratibu ni huo. Sasa kama mbolea ya kupandia inachelewa na kilimo chetu tunaenda kwa kudra za Mwenyezi Mungu kwa kutegemea mvua matokeo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wasilisho la Wizara kwenye semina walieleza kwamba wamefanya *saving* nafikiri zaidi ya shilingi bilioni 9 kwenye ununuzi wa mbolea kwa pamoja *(bulk procurement).* Huku kwenye ununuzi wa mbolea kama Wizara mlifanya *saving* lakini wakulima wamepata hasara kwa sababu mbolea ilichelewa, *by the time* wanaweka ile mbolea mvua ikaondoka, wiki mbili hakuna mvua, kwa hiyo mazao yalidumaa, hawajaweza kuvuna ipasavyo. Mbolea waliyoweka haikuyeyuka kuingia ardhini kwa sababu mvua haikuwepo, tatizo mlicheleweshа mbolea. Tuombe Wizara siyo mpaka Mkuu wa nchi aseme ndipo sasa na nyie mkimbizane mpaka na magari ya jeshi kufikisha mbolea kwa wakulima ambao sasa wanapata hasara, hili ni eneo ambalo linaajiri asilimia 70 ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zana za kilimo, tumeona kuna mifuko ya ukopeshaji lakini pia juhudi hii inabidi iongezwe. Iliwahi kutolewa kauli hapa na Serikali kwamba jembe la mkono litaenda kukaa makumbusho, sasa

utekelezaji wa kauli hii umefikia wapi? Kwa hiyo, tutaomba Waziri utuambie kwenye zana za kilimo ni lini jembe la mkono litaondoka na tuingie kwenye zana ambazo tutafanya kilimo chenye tija na kuzalisha zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la viuatilifu na wadudu. Tunajua mna changamoto kubwa katika eneo hili lakini maandalizi ya kukabiliana na hawa wadudu yasiwe ya zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la mbegu sasa hivi zinawachanganya wakulima wetu. Kuna nyingine zina ubora mzuri na nyingine hazina. Ukishavuna mazao yakikauka bado yanawahi kubunguliwa tofauti na zile mbegu za zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye upande wa zao la tumbaku. Makampuni ya tumbaku yamekuwa kama ndiyo wenye maamuzi katika nchi hii. Walishusha kutoka tani 60,000 mpaka tani 55,000 na bahati mbaya uzalishaji ukazidi kiwango na wakulima wetu walihangaika na bei mpaka mbolea zililowa na maji na matokeo yake waliuza mpaka Dola 0.6 kwa kilo kwa sababu ubora umeshashuka, tumbaku zilikaa muda mrefu. Tuombe Serikali watengeneze makubaliano ambayo yatakuwa yananufaisha wananchi hata kama kiwango cha uzalishaji kimezidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kwenye tumbaku kwa Wilaya yetu ya Mpanda kampuni ya *TLTC* imetoa barua ikisema inakusudia kusitisha ununuzi wa tumbaku kwa kisingizo kwamba *go-down* limejengwa ndani eneo la *railway* na ni kweli ni eneo la *railway* na wanatakiwa waliondoe na pili, ni masuala ya kiuongozi kutotimiza matakwa yanatotakiwa. Bodi ya Tumbaku inayo barua, huu wasiwasi wa wakulima wetu kwenye ununuzi wa tumbaku tutaomba kauli ya Waziri ni kweli *TLTC* mnakubali wasitishe ununuzi? Kama mnakubali ni kampuni gani mbadala itaenda kununua tumbaku katika Wilaya ya Mpanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana pia Waziri alikuja na mapendekezo ya kushusha *produce cess* kutoka 5% - 3% lakini haijamfaidisha mkulima kwenye haya mazao ya kibiashara kama tumbaku. Punguzo hili limeenda kutupunguzia mapato kwenye Halmashauri zetu na haijamgusa mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri aje atuambie ni utafiti upi wa kina ambao wameufanya na kwa nini wasirudishe kwa upande wa wanunuzi kuwa 5% kwa sababu mkulima haijamfaidisha. Zile za leseni na kadhalika ambazo mliwapunguzia zibaki kama zilivyo lakini hii ya ununuzi wa haya mazao ya biashara kama tumbaku warudi kwenye 5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Benki ya Maendeleo ya Wakulima. Chanzo cha *CRDB* kinafanana na hii *TADB. CRDB* ilivyoanzishwa ilikuwa kwa ajili ya kusaidia kilimo na vyama vya ushirika lakini imeenda imekuwa benki ya kibiashara. Kwa mfano, wakulima wa tumbaku wanakopa kutoka kwenye mabenki kwa riba ambayo ipo juu na kuanzishwa kwa benki hii ni chachu kwenye kutoa mikopo upande wa kilimo. Ni kwa kiwango gani mpaka sasa wameshatoa mikopo kwenye mazao ya aina mbalimbali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *SAGCOT.* Nimeona kwenye hotuba wanataka waitanue pia ukanda mwingine lakini huu Ukanda wa Kusini *SAGCOT* imekamilika na kufanya kazi kwa kiasi gani? Hebu njooni Mkoa wa Katavi, ile mikoa ilikuwa ni *big four* sasa hivi ni *big six* kwa sababu imegawanyika Njombe na Iringa, Katavi na Rukwa. Kwa hiyo, *SAGCOT* ikamilishe kwanza Nyanda za Juu Kusini ndipo waende kwenye ukanda mwingine na tuweze kuongeza tija na uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kufanya utafiti. Baadhi ya Wabunge wamelalamika kwamba mazao yanaanzishwa sehemu zingine, kama korosho imeanzishwa nchi nzima, maeneo mengi wamechukua wamepanda na haijakua na pamba inatanuliwa maeneo mengine. Mwaka

juzi tulipitisha sheria ya mambo ya utafiti na kwenye bajeti nimeona mmetenga shilingi bilioni 1.4, utekelezaji wa fedha hizi za kufanya utafiti uko kwa namna gani ili tunapotawanya haya mazao tuwe na uhakika kwamba yataenda kukua na kuongeza uzalishaji? Mheshimiwa Waziri akija kuhitimisha tutaomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Jimbo la Nsimbo tumeanzisha zao la pamba na tupo kwenye mikakati ya kwenda kulikuza. Kwa hiyo, tunaomba ile Bodi husika ipitie pia maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii Kampuni yetu ya Mbolea *TFC. TFC* ipo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji lakini kazi kubwa za mbolea wanazofanya zinahusiana na Wizara ya Kilimo. Kwa nini Serikali kiutawala na kiutendaji, japokuwa ni kampuni, basi iwe chini ya Wizara ya Kilimo? Kama tunalaumu kwamba kuna upungufu kwenye utendaji basi anayehusika na usimamizi na usambazaji wa mbolea ambaye ni Wizara ya Kilimo aisimamie hii Kampuni ya Mbolea *(TFC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imelenga kwenye kuwa nchi ya viwanda na mikakati iliyopo sasa hivi vile viwanda ambavyo tunaenda kuvilisha malighafi kwa kupitia shughuli zetu za kilimo, je, tunazi-*link* vipi hizi sekta zote ili tuwe na tija na kufanikisha malengo kwa wakati? Naomba Waziri atuambie katika mazao ya aina mbili tu, mafuta ya kula ambayo yamekuwa na mgogoro...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi na kama nilivyosema atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Engineer Gerson Lwenge ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na utukufu ambaye amenijalia uzima hatimaye niweze kusimama hapa kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wangu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya. Pia nimpongeze Mama Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu pamoja na Waziri wa Wizara ya Kilimo, wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, nimpongeze sana Waziri Mkuu namna ambavyo amekuwa akifanya kazi nchi nzima. Kimsingi hamna asiyejua namna anavyotimka kufuatilia sekta ya kilimo na kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanatendewa haki katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi kuishukuru sana Serikali ya CCM inayoongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli kwa namna ambavyo wametutengea ujenzi wa ghala kubwa katika Mkoa wa Ruvuma. Pale Songea Mjini kunaenda kujengwa ghala kubwa ambalo lina uwezo wa kuchukua tani 81,000 za mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili la ujenzi wa ghala kubwa liende sambamba na hoja kubwa ambayo nimekuwa nikiisema mara nyingi hapa inayohusu pembejeo za kilimo. Kwa Serikali yangu kuona umuhimu wa kujenga ghala kubwa katika Mkoa wa Ruvuma ina maana inatambua wazi namna gani Mkoa wa Ruvuma umekuwa ukizalisha mazao ya mahindi kwa wingi. Katika Tanzania hili ni ghala ambalo linaongoza, hakuna ghala lenye kuchukua tani nyingi kiasi hicho. Kwa hiyo, ujenzi huu wa ghala uende sambamba na suala la pembejeo za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri kwenye suala la pembejeo za kilimo iongezwe ruzuku hapa kwenye mbolea. Nashauri mbolea ya ujazo wa kilo 50 ikiongezewa ruzuku iende ikauzwe Sh.10,000 kwa kila mfuko. Hii itawasaidia sana wakulima lakini pia itaongeza tija ya uzalishaji katika eneo hili kwa sababu kupeleka tu ghala haitoshi, ni lazima kuwe na mkakati mzuri ambao utapelekea uzalishaji wa haya mahindi kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nadhani ni vizuri Wizara ya Kilimo pia ikafanya jitihada za makusudi za kupeleka Benki ya Kilimo katika Mkoa wetu wa Ruvuma ili wananchi wale waweze kukopa na kuongeza tija kwenye mazao yao kwa maana ya kuongeza mtaji. Nimekuwa nikiuliza hili swali mara nyingi ni lini Benki ya Kilimo itapelekwa katika Mkoa wa Ruvuma lakini majibu yake hayana afya, najibiwa juu-juu tu, ni majibu ambayo hayakidhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kulikuwa na umuhimu sana wa kupeleka hii Benki ya Kilimo tofauti na sasa hivi Benki ya Kilimo imewekwa pale Dar es Salaam, kuna mashamba gani pale Dar es Salaam? Watu wamekaa kwenye viyoyozi, wapo maofisini wakitoka wanaingia kwenye magari wanaenda nyumbani, kwa hiyo, haileti tija kuweka Benki ya Kilimo katika Mkoa wa Dar es Salaam. Peleka Benki ya Kilimo katika Nyanda za Juu Kusini ili wakulima wale waweze kuzalisha mazao kwa wingi kwa sababu ni wakulima haswa wanaofanya kazi za kilimo zinaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye suala la masoko. Nimesoma kitabu hiki cha hotuba ya Waziri wa Kilimo, nimekwenda ukurasa wa 75, nilichokiona wanazungumzia kuzalisha katika kilimo lakini pia amezungumzia suala la uhifadhi sijaona akizungumzia suala la masoko ya mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona kama Nyanda za Juu Kusini tumetengwa kwa maana ya kwamba suala la mahindi halijawekewa mkakati madhubuti ambao

utamnyanyua mkulima wa Tanzania ambaye kimsingi amekuwa akizalisha kwa kutumia nguvu nyingi lakini uzalishaji wake hauna tija. Hivi sasa ni mpaka mtu auze madebe matatu ya mahindi ndiyo apate kilo moja ya sukari, ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niombe Wizara ya Kilimo ije na mkakati mzuri. Siku moja Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea katika Mkoa wetu wa Ruvuma, alizungumzia suala hili la kuongeza thamani kwenye zao la mahindi. Akasema kwamba ataangalia namna ya Serikali kuweka mkakati ambao utafanya zao hili la mahindi kuuzwa katika mtindo wa minada kama ilivyo korosho na mazao mengine ambayo kimsingi yamekuwa yakileta tija kwa wananchi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, anafanya kazi vizuri pamoja na wasaidizi wake hasa huyo anayeongea naye hapo, wanafanya kazi vizuri sana, hebu jaribuni kuona namna ya kuongeza thamani ya zao la mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, sasa naomba niende kwa mawakala wa pembejeo za kilimo. Rais wetu anafanya kazi nzuri na amekuwa akisema kwamba yeye ni Rais wa wanyonge na wasaidizi wake wamekuwa wakisimamia hivyo. Mimi nashangaa sana inakuwaje mawakala hawa wa pembejeo wana miaka minne wanadai pesa zao walizohudumia Serikali katika sekta hii ya kilimo? Mawakala hawa walikwenda kukopa fedha kwenye taasisi za fedha, wakajikusuru na wakaenda kuwekeza kwenye pembejeo za kilimo lakini Serikali haioni umuhimu wa kuwalipa, inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijificha kwenye kichaka cha uhakiki miaka minne. Ni kwa nini Serikali haiendi kuwalipa hawa mawakala wa pembejeo? Wapo mawakala ambao wengine walichukua mbolea *TFC* inaeleweka walikwenda kuchukua kule walichukua kiasi gani lakini wengine wanapoteza maisha yao wakisubiri kupata haki yao, Wizara mmekaa lakini Serikali pia imejificha nyuma

ya suala la uhakiki. Ni uhakiki wa aina gani miaka minne, inatia huzuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshuhudia wakala mmoja nilipokwenda ziara kule analia. Nimekuta pale dukani kwake kuna makampuni manne yote yanamdai na kila kampuni imeleta dalali, inasikitisha na yule bwana ametoka pale. Nitoe tu mfano kwa mawakala wachache ambao mnaweza mkafuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dada anaitwa Rose Minjingu, nendeni mkafuatilie pale, amekopa na taasisi zinamdai lakini pia kule alikokopa kwenye kampuni mbalimbali mpaka *TFC* anadaiwa. Imefika mahali amezungukwa na watu wale kama wanne wanadai, kila mmoja kaja na dalali. Pia yupo kijana anaitwa Cosmas Haule, naye pia amezingirwa, imefika mahali ndugu zake wamekaa chini kumshawishi maana alikuwa anataka kuchukua hatua ya kujinyonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi hii ambayo watu wanatafuta haki zao na inafika mahali wanashindwa kupata haki zao, hivi kwa nini kama hawa watu kweli wameiba wasipelekwe Mahakamani? Haki zao zinapotea, wengine wanapoteza maisha, inatia uchungu sana.

*(Maneno ya hapo juu Mheshimiwa Jacqueline N. Msongozi alikuwa akiongea huku akilia)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi hii wako watu ambao haki zao zinapotea, tunakwenda wapi? Wale mawakala walipwe pesa zao, wale ambao wamefanya vizuri walipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyuma yake kunakuwa na suala la uhakiki, uhakiki gani? Mbona tumeona hawa

watumishi wamehakikiwa siku mbili suala limekwenda, wenye vyeti feki wamehakikiwa siku mbili wamekwenda, ni kwa nini huku kwenye Wizara ya Kilimo hawalipwi pesa zao hawa mawakala? Siyo vizuri, msiwadhulumu haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea kwa uchungu kwa sababu yuko mtu ambaye alikuwa anataka kujinyonga lakini ndugu zake wamekaa wamemshawishi, inatia huzuni sana.

*(Maneno ya hapo juu Mheshimiwa Jacqueline N. Msongozi alikuwa akiongea huku akilia)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wale mawakala, wako mawakala saba ambao tayari wameshapoteza maisha, wako Wabunge ambao ni mashahidi hapa kwenye maeneo yao. Mzee wa Makambako yule pale atasema, kuna watu wamekufa. Kuna wengine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, usijinyonge. *(Makofi/ Kicheko)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, tunaendelea, huyo ndiyo Mheshimiwa Jacqueline Msongozi. Tunaendelea na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Lwenge na Mheshimiwa Njalu Silanga ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii muhimu kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake anazochukua siku hadi siku kuhakikisha kilimo kinakua na wakulima wanapata unafuu. Mfano, kuwapunguzia kodi mbalimbali na tumeona kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri kuna changamoto nyingi za kodi na tozo mbalimbali zinakwenda kutatuliwa na kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara. Tumeshuhudia juzi uwekaji wa jiwe la msingi la maghala na vihenge vya kisasa kabisa ambavyo vitachangia kwa kiasi kikubwa kuhifadhi mazao yetu yasiharibike na kupata soko na vilevile katika vihenge na maghala hayo, tutakuwa na uhakika wa usalama wa chakula hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa chakula ni muhimu kwa sababu ni usalama wa Taifa. Tutakapokosa chakula hata hayo majeshi yetu yatashindwa kutulinda sisi na mipaka yetu. Kwa hiyo, nashauri Kitengo hiki cha *NFRA* kiongezewe fedha zaidi ili kuweza kununua mazao mengi kwa ajili ya usalama wa chakula lakini pia kuwasaidia wakulima wetu kupata masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyotambua kwamba karibu asilimia 65 ya malighafi za viwanda zinategemea mazao ya kilimo. Ni vyema sasa sekta hii ya kilimo ikaongezewa fedha zaidi ili kuhimili mahitaji yote ya kilimo ndani ya nchi yetu na kupata malighafi za viwanda vyetu ili tuweze kupata ajira kwa vijana wetu katika kilimo, viwanda na kuongeza Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuliboresha au kulifanikisha suala hili ni lazima tujikite zaidi kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji kitakuwa ndiyo nguzo

muhimu ya kumkomboa mkulima mkubwa na mdogo kwa sababu mabadiliko ya hali ya hewa au mabadiliko ya tabia nchi yanayumbayumba na hivyo kusababisha kilimo chetu pia kiwe kinayumbayumba na hakina uhakika. Kwa hiyo, tukiwekeza zaidi kwenye sekta hii ya umwagiliaji tutaweza kupata masoko ya ndani na nje na tutapata malighafi za viwanda vyetu. Hilo liende sambamba na miundombinu ya barabara kule ambako kunazalishwa mazao mengi ili mazao hayo yasiharibike shambani na yaweze kufika kwenye maeneo ya masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbegu bora ni la msingi zaidi. Ili kupata mbegu bora ni lazima tuviimarishe kwa kuviongezea mtaji vituo vyetu vya utafiti kama *TARI* na vinginevyo. Tukiviongezea fedha vituo hivi vikafanya utafiti wa mbegu bora tutaweza kupata mbegu bora ambazo zitasaidia hata kukabiliana na upungufu wa mafuta na sukari ambao tunao hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuishauri Serikali iongeze fedha au ipeleke fedha kwenye *TFRA* kwa sababu ya majukumu yake. Hii ni kutokana na hali ya sasa hivi ambapo kuna milipuko ya magonjwa na wadudu mbalimbali wanaoharibu mimea yetu, ni bora tukajua ni viuatilifu gani vinafaa kwa maeneo gani na kwa wadudu gani waharibifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha sekta binafsi ili iwekeze katika kilimo cha wawekezaji wadogo na wakubwa, ni vyema kukajengwa mazingira mazuri kwa wawekezaji hawa ili waweze kuwekeza kwa kiwango kikubwa. Hii ni pamoja na hatua mbalimbali zilizoanza kuchukuliwa na nyingine ziko kwenye mikakati ya kuchukuliwa ya kuangalia kodi na tozo mbalimbali ili kuwawezesha wawekezaji wetu kuvutika na uwekezaji katika sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, katika kuwekeza katika fani ya kilimo ni lazima kuwe na zana bora

za kilimo. Kwa hiyo, ni vyema Benki ya Kilimo ikaongezewa mtaji ili itoe mikopo kwa wafanyabiashara au wakulima ili waweze kukopa vifaa vya kilimo kama matrekta kwa bei nafuu. Vinginevyo tutafute njia mbadala ya kuhakikisha wakulima wetu katika kila kijiji wanapata trekta na zana bora za kilimo na baadaye walipe kidogokidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linatakiwa liende sambamba na teknolojia ya usindikaji. Teknolojia yetu ya usindikaji iliyopo sasa tunapoteza mafuta mengi katika mashudu. Kwa hiyo, ni vyema tukapata teknolojia mpya na ya kisasa ili kuhakikisha mafuta yetu mengi hayapotei katika mashudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kuna masuala ya ushirika. Suala la ushirika limeongelewa sana na tumelieleza kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi ukurasa wa 112, Ibara ya 57(a) ambayo inasema, kuhakikisha kuwa shughuli zote zenye mwelekeo wa ushirika zitapewa msukumo stahiki kwa kuhamasisha na kusimamia kwa nguvu uanzishwaji wa vikundi vya ushirika kama vile *SACCOS* na vinginevyo, vyama vya mazao, ufugaji na vinginevyo. Mwisho inamalizia hapa, ushirika ndiyo silaha kuu ya wanyonge na nguzo kuu ya ujenzi wa siasa ya ujamaa na kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufuata kipengele hicho cha Ilani, vyama vya ushirika tulivyonavyo, kama kuna makosa madogomadogo ni vyema sasa tukayafanyia marekebisho, tukaviunda upya ili kweli viwe mkombozi wa mkulima mnyonge na wanyonge wengine hapa nchini Tanzania. Kwa sababu tumeona kwamba ndiyo nguzo kuu na silaha na mkombozi wa mnyonge kwa njia ya ujamaa na kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka jana tulikamata shilingi hapa ya Mheshimiwa Waziri kuhusu zao la minazi. Mwaka huu kitabu hiki cha Waziri sijaona akiongelea kuhusu zao la minazi. Zao hili ni la biashara, sasa hivi tunaagiza

nazi kutoka nje ya nchi na kama sisi Tanzania tutaimarisha kilimo chetu cha minazi tutaweza kusafirisha nje ya nchi mazao yatokanayo na minazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwa mara nyingine kuwatakia kheri, wafanye kazi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija kwa mchango wako.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge, Mheshimiwa Njalu Silanga na Mheshimiwa Ignas Malocha wajiandae.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu na pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, naomba nitoe pole kwa wananchi wangu wa Wanging'ombe kwa kufiwa na watu mashuhuri, makada wa Chama cha Mapinduzi. Tumefiwa na Diwani na Katibu Kata wa Kata ya Igima. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hawa mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu. Waziri na Katibu Mkuu wote ni ma-*engineer,* nategemea

kabisa ma-*engineer* hawatatuangusha katika kulifikisha Taifa hili kwenye uchumi wa kati. Tutafanikiwa kufikia uchumi wa kati kama Wizara hii imekaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hotuba hii, kwa kweli sijaridhika nayo. Kwa jinsi sekta hii ilivyo kubwa lakini hoja iliyoletwa ni kidogo sana na mambo mengi ya msingi yameachwa. Tukumbuke tulio wengi hapa ni watoto wa wakulima na kama Wabunge wote tulioko humu hatujawazungumzia wakulima inavyotakiwa kuhusu matatizo wanayopata kuanzia kupanda mbegu, hawana mbegu bora na hawapati kwa wakati; ukija kwenye kukuza mmea hawapati huduma ya ugani na viuatilifu; ukija kwenye soko ndiyo kabisa. Kwa hiyo, unakuta maeneo yote haya ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia mazao ambayo Mheshimiwa Waziri amewasilisha hapa, sijaona mkakati wowote wa kusaidia wakulima wa mahindi na kuna mikoa karibu kumi inayolima mahindi. Kama alivyosema mwenzangu aliyetangulia kwamba sasa hivi hatusemi mambo ya *subsistence farming,* yaani kilimo cha mahindi siyo kwa chakula tu, ni pamoja na biashara. Tunategemea Serikali imuwezeshe mkulima wa mahindi ambaye hana zao lingine aweze kujikomboa kwenye uchumi. Kama kuanzia kulima hajasaidiwa, inapofika kuuza ndiyo Serikali inasema tunataka *food security,* unazuia asiuze mahindi yake, tutakuwa tumemsaidia vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana *NFRA* iliweza kununua mahindi Mkoa wa Njombe lakini mwaka huu hawakuonekana kabisa. Wananchi wanauza debe moja Sh.2,000 mpaka Sh.3,000, kiasi ambacho hataweza kununua mbolea na kupeleka mtoto shule yaani maisha ni magumu kwelikweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Serikali hii ni ya wananchi lazima tuweke kipaumbele katika kuwasaidia wananchi hawa waweze kujikomboa na kuona faida ya

kuwa na Serikali yao ambayo inasikia. Naamini kabisa Serikali ya Chama cha Mapinduzi imesikia hili na najua tutafanya marekebisho. Mheshimiwa Waziri wakati atakapohitimisha bajeti yake alete kitu ili wakulima wa mahindi wampigie makofi. Mambo ya kuzuia mpakani watu wasiuze mahindi, hii haitusaidii, hatuwezi kutoka hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najua Waziri ni mkulima na mwaka jana nilimfuata kulima mtama, tumelima mtama pamoja nawe lakini mpaka leo hatujauza. Hapa nimeona kuna mkakati wa kuongeza zao la mtama, hivi tutalima mtama halafu iwe nini kama hatuwezi kuuza, magunia yamekaa yanaharibiwa na wadudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwenye eneo hili, pamoja na kwamba wewe ni rafiki yangu lakini tusifanye ngonjera, tunasema tunazalisha mtama kutoka tani 2,000 mpaka 3,000 halafu zitafanya kitu gani? Wanasema watahamasisha sekta binafsi waje wawekeze viwanda, lakini jambo hili ni *long process,* huwezi kulifanya katika msimu wa mwaka mmoja, kwa sababu watu tayari wamelima. Kwa hiyo, nafikiri tuwe na mkakati fulani ambao unamsaidia mkulima kuanzia ku-*plan* alime zao gani na asaidiwe vipi. Kama alivyosema mwenzangu pale, mnaleta mikorosho Dodoma inakauka, hivi kwa nini Serikali tusiwe na *strategy* kama tunawasaidia wakulima wa Mtwara na Lindi basi tungeweka nguvu yetu kule, huku kwingine tuweke nguvu kwenye mahindi, sehemu nyingine tuweke nguvu kwenye mpunga, nadhani kwa namna hiyo tutaweza kuwatoa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Wanging'ombe tunalima sana viazi na tunaanza kupanda Julai, mbolea inaanza kufika Oktoba wakati wameshamaliza kupanda, sasa mkulima umemsaidia hapo? Halafu tuna tatizo kubwa la ugonjwa wa ukungu wa viazi, kuna dawa ambazo zinaletwa kule hazijatatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hawa Maafisa Ugani wanafanya kazi gani? Sehemu nyingi nimeona Maafisa Ugani hawafiki kwa wakulima. Mimi ni mkulima lakini sijawahi kumuona Bwana Shamba anakuja kunitembelea kwenye shamba langu na nafanya hivyo kwa sababu nataka shamba langu liwe shamba darasa, wakulima waone Mbunge wao naye analima anavuna kiasi gani kwa heka, sasa huyu Afisa Ugani hafiki na mnaendelea kuwaajiri. Mimi nafikiri hawa watu kwa kweli kama ndiyo ufanyaji kazi wa namna hiyo, nimeona sehemu nyingi hawa Maafisa Ugani wanashughulika na mashamba yao, hawafiki kwa wakulima, kwa hiyo hatuwezi kutoka hapa tulipo. Tuna miaka zaidi ya 50 ya uhuru, tunataka tuone kilimo kinakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna hili Shirika la *NFRA,* nimeona kwenye kitabu kwamba mwaka huu mna mpango wa kuongeza ununuzi wa mahindi kutoka tani 18,000 mpaka tani 26,000, lakini hamjaonesha hivi mahindi yaliyopo nchini ni kiasi gani ili tuweze kupima ufanisi wa *NFRA.* Mimi nachojua ni kwamba bajeti mnayoweka ya ununuzi wa mahindi ni kidogo na ndiyo maana umeweka tani kidogo lakini umetuficha kujua hivi nchi nzima tunazalisha mahindi kiasi gani, ndiyo tungejua ufanisi wa mpango wa hii *NFRA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeona kwamba kuna mpango wa kuongeza uzalishaji wa pareto. Kwa miaka ya 60 Mkoa wa Njombe tulikuwa tunaongoza kwa ulimaji wa pareto lakini wananchi wale wameacha kulima kwa sababu hakuna soko. Sasa nani atalima pareto kama hakuna soko na hivi tutapataje *foreign exchange* kama hatulimi pareto? Pareto ni zao moja ambalo linaingiza sana mapato ya fedha za kigeni. Kwa hiyo, mngeonesha mkakati namna gani tutawahamasisha wananchi warudi kulima pareto ili tuweze kuongeza pato la nchi. Kwenye kitabu hiki ambacho nimesema hakina maelezo ya kutosha, hakielezei kabisa mkakati wowote wa kukuza mazao haya ili tuweze kuongeza uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mkoa wetu wa Njombe wenyewe tunajiongeza, tunalima kilimo cha parachichi.

Parachichi imeonekana ni zao moja ambalo kwa kweli soko linakuja, watu wanatoka Kenya nakuja kununua parachichi. Kwa hiyo, tunaomba Wizara iji-*zero in* kwenye zao hili la parachichi, mtusaidie masuala ya viuatilifu na namna ya kusindika zao hili. Naamini Mikoa ya Njombe na Mbeya itatusaidia kutoka hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia uchumi wa viwanda, uchumi wa viwanda tunaweza tukafanikiwa tu kama utakuwa-*based* zaidi na mazao ya wakulima. Kama tunajenga viwanda vile ambavyo vitakuwa vina-*process* mazao ya wakulima, nina uhakika kwamba hata soko litajiongeza. Kama hatujaweka mkakati wa kuwasaidia wakulima katika mazao ambayo ni *specific,* yana watu ambao wanawekeza kwenye viwanda, ndiyo tunaweza tukawasaidia. Kwa hiyo, naomba utakapokuwa unahitimisha hoja yako ulizungumzie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia masuala ya kukuza kilimo, hatuwezi kuendelea kukuza kilimo kwa kutegemea hili jembe la mkono. Ni lazima tuanze na mashamba makubwa *(commercial farming)*. Sijaona katika kitabu hiki akiongelea kwa ufanisi *commercial farming,* hatuwezi kuendelea kwa ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Eng.* Lwenge.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Njalu Silanga atafuatiwa na Mheshimiwa Ignas Malocha na Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba hii ya wananchi wanyonge walioko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mitatu mfululizo katika zao la pamba tumekuwa tukipata bei nzuri. Mwaka 2016, 2017 na 2018 na tumevuka kiwango mpaka tumefanikiwa kuzalisha takribani kilo 600,000, haya ni matarajio ambayo tunayatarajia. Hii ni kwa sababu wananchi wamehamasika kwa sababu ya kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uzalishaji wa zao hili la pamba, linaweza likaipatia nchi kipato kikubwa sana. Kwa mwaka huu wa fedha tunatarajia kuwa na Dola za Kimarekani takribani 342 lakini kadri tunavyokwenda na taratibu ambazo Serikali yetu ya Awamu ya Tano ilielekeza, namshukuru Mbunge aliyemaliza kuchangia Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba tuwe na ushirika kwa ajili ya kukomboa wanyonge, nataka nikuhakikishie ushirika unaotengenezwa siyo ushirika ambao tunaufahamu, ni ule ushirika wa miaka yote ya nyuma. Ni watu ambao walishachoka tangu miaka 23 na mwaka huu kama tutawakabidhi huu muziki wakulima wetu wataendelea kupata adha kubwa sana. Ningeiomba Serikali ijaribu kutengeneza upya mfumo wa kuhakikisha kwamba zao hili la pamba linanunuliwa vizuri na kwa umakini mkubwa zaidi. Hata *go-down* walizonazo zilishauzwa, ushirika uliobaki kule ni ushirika ambao ni hoi bini tabani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unatoka katika Wilaya ya Bariadi unayo majimbo mawili, Halmashauri ya Mji na Halmashauri ya Vijijini, ushirika uliopo katika kijiji chenye watu 2,000 kuna washirika watatu, wanne na leo tunataka kwenda kuwakabidhi fedha za wakulima wetu. Niiombe

Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi, kilio hiki iende ikakifanyie kazi upya kuliko hivi sasa ndiyo wanahangaika kule vijijini wanaunda vikundi na hizi ni fedha za watu na mabenki inabidi benki hizi zirudishe fedha na kipato cha ndani kiendelee kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la pembejeo. Tumeshuhudia mwaka huu Mheshimiwa Waziri amefanya kazi nzuri pamoja na watendaji wa Bodi ya Pamba kwa kuhakikisha ametutoa tulipokuwepo na kutufikisha hapa tulikofikia. Matarajio yetu tukiendelea kusimama vizuri na kuimarisha zana zetu katika maeneo yetu ya kilimo cha pamba, katika hotuba yake amesema ifikapo mwaka 2020 tutafikisha tani 1,000,000, naamini bei zikiendelea kuwa nzuri na pembejeo zikiwa za kutosha ifikapo mwaka 2020 tutazalisha tani milioni 2.4. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu mikoa inayolima pamba ni 17, tunazo wilaya 56 utaona tu kwamba hata uzalishaji tulionao kwa mwaka huu tumepiga hatua. Ukigawanya wastani wake ni kama kila wilaya imezalisha tani 10 ambapo tukisisima sasa jukumu hili tukalibeba wote Serikali pamoja na Wabunge kwa kuhamasisha na kuunda *AMCOS* zilizosajiliwa kwa mwaka huu uzalishaji utaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Waziri Mkuu kutoa agizo Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwenda kuunda vikundi kilichofuatia ni Mrajisi kwenda kutengeneza ushirika wake wa miaka 20 ambao umefilisi wananchi wetu na bado watu wanauchukia hata sasa hivi ukisema ushirika wanakimbia. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuliangalia suala hili kwa mapana zaidi, zana ni nzuri lakini si nzuri kwa kipindi ambacho tunakitarajia hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 146, hapa napata kigugumizi kusema, ametuandikia ameamua kufuta Mfuko wa Wakfu wa Kuendeleza zao la Pamba lakini kwenye kukotoa huku kuna Sh.100, sasa angetupa majibu tunafanya kitu gani? Hizi fedha zikienda kwa mkulima moja kwa moja

bei zinaongezeka. Kwa hiyo, naomba sana hili suala la pembejeo Waziri ahakikishe linakuwa katika mipango mizuri ili wakulima wetu wasiendelee kupata adha ambayo wanaendelea kupata kwa mwaka huu tunaoumaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu tutakapoweka usimamizi na uzalishaji mzuri wakulima wetu wa pamba hawasukumwi kwa sababu ni wajibu wao na ni biashara yao lakini tunavyotaka kwenda tunaweza tukatengeneza mazingira ya kuua zao la pamba na litafia hapa Dodoma. Kwa mwaka 2020 tunarajia kuvuna tani 1,000,000 lakini kwa mfumo ambao ameuleta Mheshimiwa Waziri hatutafikia huko, wakulima wataacha kulima kwa sababu hii miti wanalima kwa mwaka, wanakata wanazalisha tena upya. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atafute mfumo ambao ni mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linatuletea masikitiko makubwa sana. Sisi kule kwetu tulikuwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha *SHIRECU* lakini baada ya Ofisi ya Mrajisi kuingia pale alitengeneza madudu mpaka na *go-down* zetu kubwa zilizokuwa maeneo ya Dar es Salam ziliuzwa lakini leo Mrajisi huyu amerudi tena na mifumo ambayo badala ya kuishauri Serikali alete utaratibu mpya utakaokuwa na tija kwa wakulima ameleta *system* ileile ambayo imewatesa wakulima wetu na imewakatisha tamaa. Watu wengine, Mwenyekiti utakuwa shahidi wakati wa kampeni za kuomba kura, watu walikuwa wanakuomba malipo yao ya pili. Kwa hiyo, naomba jambo hili tulichukulie katika misingi mizuri ambayo ina tija lakini kubwa zaidi ni kuweka mifumo itakayokuwa rafiki na wakulima ambao wanazalisha bila kusukumwa na kwa moyo mzuri na ni kwa sababu wanapata pesa nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshauri Waziri aweke mpango mzuri utakaotuwezesha kupata pembejeo na mbegu bora. Niwashukuru sana watafiti wetu wa Ukiliguru kwa sababu kwa mwaka huu fedha tunaenda sasa kuingia

kwenye mbegu za asili ambazo wamezizalisha, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nishauri tuendelee kutunza mbegu zetu za asili. Hili jambo tusipoliangalia ni tatizo na janga kubwa. Wakulima wetu wanahamasika sana kulima, nimeona humu ndani kwenye kabrasha hili kuna mikoa mipya imeanzishwa. Mikoa mipya iliyoanzishwa kama mfumo wetu hautakaa vizuri, nataka nikuhakikishie tutapata madhara makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi tunao, mwaka 2008/2009, Serikali ya Awamu ya Nne ilitoa fedha kwa ajili ya kufidia wakulima takribani shilingi bilioni 2 lakini zile fedha zilitumika ndivyo sivyo. Leo hii Serikali ya Awamu ya Tano tangu iingie madarakani bei zimeendelea kuongezeka kila siku, sasa kuna mdudu ambaye ameingia huyu sijui katoka wapi. Naomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kwa hili atuwekee utaratibu utakaokuwa rafiki kwa wananchi wetu na tusiwe na maswali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna meseji kibao za wananchi wanalalamika kwamba Bunge lilitangaza tarehe 1 lakini mpaka leo hakuna na wamefungua kijiji kimoja pale Igunga kilo 3,000 zilizonunuliwa, hakuna mtu yeyote aliyeingia mule ndani lakini hata maandalizi hayapo, hata msimamizi wa Bodi anapata wakati mgumu. Mrajisi ana mwongozo wake, Bodi ina mwongozo wake, mwisho wa siku tunashindwa kuwaweka wananchi wetu katika mazingira yenye kuleta kipato kikubwa. Nchi hii tumekubaliana kwamba lazima tuwe na uzalishaji mkubwa ili tukidhi mahitaji ya wananchi wetu. Ukizalisha mbegu nyingi tena tutapata mafuta mengi, tuna alizeti, mawese na vitu vingine lakini wananchi watalima pale ambako hakuna usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba amesema amejipanga kuhakikisha kwamba vyama vya ushirika vinakusanya pamba halafu mnunuzi aende kununua. Ni

mwananchi yupi atakayepeleka kwenye vyama vya ushirika ambavyo watu wamekosa imani, hiyo ni kazi ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali jambo hili iliangalie kwa mapana zaidi na tuliwekee utaratibu mzuri utakaokuwa na tija kwa wananchi wetu. Hili jambo wakilipokea itakuwa ni vizuri zaidi kuliko hivi sasa hata ile iliyowekwa kwa mwaka huu Sh.12 inaenda kuimarisha *union*, kwa hiyo, mwananchi huyu ataendelea kupata shida tu. Pangekuwa na mifumo mizuri kule kijijini kama alivyoelekeza Waziri Mkuu katika kikao chake cha Wakuu wa Mikoa kwamba tunataka hizi *AMCOS* zimilikiwe na wenyewe lakini mliporudi ninyi kwenye sheria na utaratibu wenu mkasema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro na Mheshimiwa Haonga wajiandae.

**MHE. IGNAS A MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nitangulie kusema moja kwa moja siungi mkono hoja. Siungi mkono kwa sababu nitakazozieleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima wa mahindi katika nchi hii amekuwa kama mfungwa au kuku ambaye mama yake amekufa. Toka mwaka jana Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakizungumzia shida ya mkulima wa mahindi katika nchi hii na mpaka sasa hivi shida hiyo inaendelea. Nilitarajia kwenye bajeti hii kutakuwa labda na maelezo ya kuwakosha wakulima wa mahindi lakini ndiyo

inazidi kuwaumiza zaidi. Kwa kweli hii si haki hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima wa mahindi anauza gunia Sh.15,000, huyu mtu nadhani yuko mbioni kujinyonga, hakika. Kwa kweli kitendo hiki hakiridhishi na hakifurahishi mtu yeyote. Wakulima wa mahindi katika nchi wanateseka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi Waziri katika hotuba yake anasema kuuza mahindi nje mpaka apewe kibali, apewe kibali ulimsaidia kulima? Amelima kwa jitihada zake mwenyewe, mkulima wa kijijini kule aanze kushughulika na kibali? Jamani, tufike mahali tuwaonee huruma wakulima yaani mkulima wa kijijini aanze kuangalia na kibali, amelima kwa shida aanze kutafuta kibali cha nini? Kama unaona kuna shida si ununue mazao hayo uyahifadhi mwenyewe kwenye ghala lako? Nunua uhifadhi kwenye ghala si kazi ya mkulima kutunza chakula cha nchi hii, mkulima analima kwa ajili ya kujikimu maisha yake yeye mwenyewe. Mimi nadhani tufike mahali tulione jambo hili, si sahihi hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hili kwa niaba ya wananchi. Mimi wananchi wangu wa Jimbo wako karibu 450,000, wamenituma nizungumze kwa nguvu zote jambo hili na linawauma kwelikweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kutotenga fedha za kutosha katika kilimo cha umwagiliaji, hii ni ajabu sana. Duniani kote kilimo cha umwagiliaji ndiyo chenye tija. Bahati nzuri katika takwimu zetu zinaonyesha karibu hekta milioni 29.4 tunazo fursa za kulima kilimo cha umwagiliaji lakini katika utekelezaji zilizoshughulikiwa ni hekta 461 sawa na asilimia 1.6. Hivi kweli tuko *serious* katika kilimo? Hatuko *serious* katika kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa, maendeleo ya viwanda duniani kote yalianza na mapinduzi ya kilimo. Mapinduzi ya kilimo ndiyo yanaleta viwanda. Sasa

ni ajabu sana kilimo kinakuwa pembeni. Hivi vipaumbele mnavyoweka mnamuuliza nani? Mtuulize sisi tunaotoka kwa wananchi, ndiyo, mtuulize sisi ambao tunatoka kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wakati wa uchaguzi alisema wazi kwamba hatambughudhi mkulima, mkulima awe uhuru kuuza kokote anakotaka, sasa haya maneno mnayatoa wapi? Mimi nashangaa Ndugu yangu Mheshimiwa Tizeba siwezi kukulaumu kwa sababu bajeti hii hupangi nyumbani kwako, hivi hawa wataalamu ambao wamesomeshwa na nchi hii wanafanya kazi gani kusaidia wananchi hawa? Kwa sababu hii bajeti Waziri hupangi nyumbani kwako, unakaa na wataalam mnashauriana sasa wanashauri kitu gani, hayo ma-*degree* waliyonayo ni ya kumuumiza mkulima? Mimi nashindwa kuelewa. Kwa kweli tufike mahali tuangalie jitihada anazofanya mkulima kwa kukimu maisha yake tusimtese kwa kiasi hiki. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni pembejeo. Kila mwaka pembejeo zinachelewa, sijawahi kuona mwaka pembejeo zikawahi au zikakidhi, ni stori isiyo na mwisho, hii stori itaisha lini? Kwa sababu ni mazoea, mimi tangia nimeingia Bunge hili hiki ni kipindi cha pili sijawahi kuona pembejeo zikatosheleza au zikawahi. Pembejeo za kupandia zinakuja wakati wa kupalilia mahindi na za kukuzia zinakuja karibu watu wavune mahindi, huu ni utaratibu wa wapi? Tunaomba Mheshimiwa Tizeba anapokuja kujibu afafanue mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la mawakala. Mawakala hawa ni binadamu kama binadamu wengine, ni wafanyabiashara kama wafanyabiashara wengine. Kama lilitokea tatizo la wizi si mmeshachambua basi tangazeni kwamba idadi ya watu fulani ni wezi hamlipwi. Hivi wote ni wezi kweli jamani, hivi mawakala wote ni wezi? Hii ni dhuluma na Mwenyezi Mungu hapendi dhuluma ya namna hii. Lazima mfike mahali mchambue wezi muwapeleke Mahakamani wenye haki wapate, siyo

kwamba mawakala wote walikuwa wezi, hamna kitu cha namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mawakala hawa ndiyo wanaoishi na wananchi na ndiyo wanaosaidia nchi hii katika kuleta maendeleo, sasa leo hii mnawatema kiasi hiki ndugu zangu? Hapana, hii si haki hata kidogo. Jaribuni kuchambua wale waliofanya kazi kwa uaminifu wapate kilicho chao. Kama wengine walivyochangia, wengine wamekufa, wengine nyumba zao zimeuzwa, hii siyo haki hata kidogo. Tunaomba Serikali mjaribu kuliangalia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni suala la mbolea. Tunajua Serikali inataka kuleta mfumo wa mbolea inayotengezwa ndani ya nchi tunakubali na kwa jina mnasema Minjingu, hii Minjingu mmeifanyia utafiti wa kutosha? Kwa sababu kipindi kilichopita wananchi walilalamika sana na wengine walipata hasara, hatukatai kama imeboreshwa mtueleze imeboreshwa kwa kiasi gani lakini hata kama imeboreshwa uwezo wa kukidhi nchi hii kwa Minjingu sidhani kama itaweza. Kwa hiyo, lazima hilo nalo Serikali mliangalie, nia ni njema mnataka tuchukue mbolea ndani ya nchi lakini mtueleze Minjingu imeboreshwa kiasi gani na uzalishaji wake uko kiasi gani kama unaweza ukakidhi mahitaji ya wananchi. Kwa hiyo, jambo hili mnapaswa kuliangalia kwa macho mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kushuka kwa bajeti ya kilimo. Bajeti ya kilimo inashuka mwaka hadi mwaka. Mimi nashindwa kuelewa, kwa mfano mwaka jana bajeti ya kilimo ilikuwa ni Sh.150,253,000,000 zilizotolewa ni Sh.27,231,305,232 sawa na asilimia 18, hapa ndipo unaweza ukaona hivi kuna u-*serious* katika kilimo? Yaani mmetenga bajeti halafu kiasi mnachotoa ni asilimia 18 na mbaya zaidi kwa mwaka huu imeshuka tena hata ile bajeti, kama bajeti imeshuka hivi asilimia itakayokuja ni asilimia 3, hakika. Kwa

sababu unaangalia hata bajeti iliyotolewa imeshuka badala ya bajeti ya kile kiwango kilichopita. Jamani msaidie Rais huyu, tunaona kazi nyingi zinaleta ufanisi pale Rais au Waziri Mkuu wanapoingilia kati ninyi wasaidizi wake msaidieni Rais huyu wa wanyonge. Sasa wanyonge wenyewe hawa wakulima ndiyo wanaanza kuteseka, mnaenda kinyume na matamko ya Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Maafisa Ugani. Tunaomba Serikali iwasimamie hawa Maafisa Ugani. Maafisa Ugani wanafanya kazi wanavyotaka, hakuna anayewasimamia kuleta tija katika kilimo, wanafanya kazi kama wanavyotaka. Tunaomba hawa watu muwasimamie kila Afisa Ugani kwenye eneo lake aeleze ameleta tija kiasi gani na uzalishaji umeongezeka kiasi gani kwa eneo dogo. Wapimwe kwa vigezo vya uzalishaji katika eneo dogo, maana tunaona tu wanakaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine wapeni mafunzo rejea, mmewapeleka tu hawana mafunzo rejea. Juzi tumeelezwa juu ya wadudu wanaoshambulia mazao mbalimbali sina hakika kama Maafisa Ugani wanapewa elimu hiyo, hawapewi. Tunafanya kazi kwa mikupuo, tungeomba Maafisa Ugani wasimamiwe kwanza lakini wapewe elimu rejea na vilevile wapewe malengo kwamba wewe umepewa eneo hili tunataka kiwango cha uzalishaji kiongezeke kutoka mahali hapa kwenda mahali hapa na anafuatiliwa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ongezeni idadi ya Maafisa Ugani kwa sababu utaalam unasema Afisa Ugani anatakiwa kuhudumia wakulima 1,600. Sasa unaweza ukakuta Afisa Ugani ni wa kata nzima yenye vijiji vitano ataweza kweli na hana usafiri? Kwa hiyo, hili nalo tungeomba Serikali iweze kuliona. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja mpaka nitakapopata maelezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro atafuatiwa na Mheshimiwa Haonga dakika kumi na Mheshimiwa Cecil Mwambe dakika tano ajiandae.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nichangie kwenye suala hili la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Songea wamenituma nifikishe ujumbe kwa Wizara ya Kilimo na kwa Serikali. Wananchi wa Songea wanasema kwao zao la mahindi ni chakula, kwao zao la mahindi ni biashara, kwao zao la mahindi ni siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Songea wanasema hawana viwanda wanategemea mahindi. Wananchi wa Songea wanasema mahindi ndiyo uhai wao lakini sasa hivi wana kilio kikubwa sana. Katika msimu uliopita mbolea haikupatikana kwa wakati. Katika msimu uliopita bei ya mbolea ilikuwa inabadilika kama homa za vipindi. Katika msimu uliopita upatikanaji wenyewe wa mbolea ulikuwa ni shida na ukiwanyima mbolea maana yake umewaua kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Songea wanajitahidi sana kuzalisha mahindi. Takwimu za mwaka 2015/2016 wananchi wa Songea na Mkoa wote wa Ruvuma walizalisha mahindi tani milioni 1.9. Mahitaji na matumizi kwa mkoa mzima ni tani 400,000, hivyo kulikuwa na ziada ya tani milioni 1.5. Uwezo wa *NFRA* kununua ilikuwa ni tani 10,000 tu ambayo ni sawasawa na asilimia 0.7 ya ziada yote. Hii inamaanisha kwamba kulikuwa na asilimia 99.3 ya uzalishaji ambao haukuweza kununuliwa, ni ziada hii.

Sasa *NFRA* hawawezi kununua, soko la nje mipaka imefungwa, huku ni kuwaumiza na kuwaua wakulima wa mahindi wa Songea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tunategemea tuzalishe mahindi kwa wingi zaidi kuliko mwaka jana na yale ya mwaka jana bado hatujauza. Tunaiomba Wizara, kuna *option* mbili tu hapa; tuongeze fedha *NFRA* za kununua mahindi na kama hilo haliwezekani tufungue mipaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Songea tuna bahati tuna mipaka miwili, Malawi na Msumbiji, turuhusuni tuuze mahindi. Hakuna sababu ya kumtaka mkulima ambaye amelima kwa juhudi zake, amevuna kwa juhudi zake na hii ni ziada, Serikali inathibitisha kwamba ni ziada, auze kwa kibali, kwa nini? Tunaomba suala la mahindi Songea lipewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kutokana na ugumu wa suala la mahindi, wananchi wa Songea pamoja na wananchi wa Jimbo la Peramiho wameanza kulima *strawberry* na wanategemea ndege ambayo Mheshimiwa Rais aliipeleka Songea *(Bombardier),* ibebe zile *strawberry* kwenda Dar es Salaam kwenye soko lakini sasa hivi ile ndege haipo, haiendi tena Songea mnazidi kutuua. Tunaomba mturudishie ile ndege iendelee kubeba zile *strawberry.* Mheshimiwa Jenista wananchi wetu wanataka ile ndege itubebee *strawberry* zetu na kuzipeleka kwenye soko Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Songea aliagiza Kiwanda cha Tumbaku kifufuliwe. Katika *speech* ya Mheshimiwa Waziri ameahidi kiwanda kitafufuliwa lakini hajasema ni lini kitafufuliwa. Naomba Mheshimiwa Waziri aje na kauli thabiti ni lini Kiwanda cha Tumbaku Songea kitaanza kufanya kazi angalau atufute machungu sisi wananchi wa Songea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunipa tani nyingi sana katika ujenzi wa vihenge. Songea ametoa tani 81,000 lakini *capacity* hiyo haina maana kama ununuzi wake ni mdogo. Kwa nchi nzima ununuzi ni tani 30,000 maana ile shilingi bilioni 15 inaweza kununua tani 30,000 tu, sasa hizi tani 81,000 alizonipa zitakuwa hazina faida kama *NFRA* hawawezi kununua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niongelee suala la mbolea hasa hii mbolea ya Minjingu. Kinachofanya mahindi yaweze kuzaa vizuri ni *nitrogen* katika mbolea ile. Minjingu ni mbolea ambayo ina *nitrogen* kidogo zaidi kuliko mbolea nyingine, *percent* ya *nitrogen* ni 9, sasa mkiandelea kutulazimisha kutumia mbolea ya Minjingu wakati kuna tatizo hili la kitaalam hamtatusaidia. Ni wazo zuri la kufufua viwanda vya ndani lakini nalo liangaliwe. Tunachotaka sisi mbolea ambayo inatumika iweze kutumika vizuri, iweze kusaidia uzalishaji siyo tu kukuza mahindi. Kwa hiyo, hili suala la kulazimisha kutumia Minjingu nalo tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameongelea mambo mtambuka katika bajeti yake na mimi naomba niongee mambo mtambuka katika hoja yangu. Moja, nimelisema hatuna viwanda sisi, kiwanda chetu ni mahindi lakini pili kama tukiruhusiwa kuuza soko letu ni Msumbiji, barabara ya kwenda Msumbiji ni ya vumbi, inapitika kwa shida. Kwa hiyo, huku *NFRA* hawanunui mahindi, soko la nje limefungwa, hata likifunguliwa barabara ni mbovu. Kwa hiyo, tunaomba hilo nalo liangaliwe ili na sisi tuweze kuuza mazao yetu nchi nyingine za jirani ikiwemo Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ametembelea Songea na anajua kwamba Songea mbolea ndiyo kila kitu. Nitaomba atakapokuja kuhitimisha aje na kauli thabiti kuwahakikishia wananchi wa Songea kwamba msimu huu unaokuja watapata mbolea kwa wakati, kwa bei nafuu na kwa bei ambayo itakuwa ni moja kwa msimu mzima. Mpango ambao umewekwa wa kununua mbolea kwa pamoja ni mzuri sana, lakini ni sawa na mtu kununua gari zuri, kuwa na hilo gari zuri ni kitu kimoja lakini kuliendesha ni

kitu kingine. Tunataka usimamizi na utekelezaji wa mpango huu wa kununua mbolea kwa pamoja *(bulk procurement)* ufanyike kwa ufanisi wa hali ya juu ili kuondoa hii kero ambayo imewakuta wananchi wa Songea katika msimu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Pascal Haonga, Mheshimiwa Mwambe na Mheshimiwa Sokombi dakika tano tano tu.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami niweze kuchangia Wizara hii ya kilimo, lakini naomba niseme tu kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi hatujajua tatizo liko wapi na ndiyo maana wakati mwingine tunamlalamikia Mheshimiwa Tizeba. Hiyo Wizara tukimweka hata Waziri Mkuu ndiyo awe Waziri wa Kilimo kesho tu mtamuondoa kwenye Wizara hiyo kwa sababu tatizo kubwa ninaloliona ni mtiririko wa fedha usioridhisha. Suala la mtiririko wa fedha usioridhisha si la kumlaumu mtu mmoja, mimi nailaumu Serikali ya Awamu ya Tano *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya Awamu ya Tano, ukiangalia kuanzia bajeti ya mwaka 2015/2016 fedha za maendeleo zilizokuwa zimetengwa ni shilingi bilioni 32.7 lakini zilizotolewa ni shilingi bilioni 5.1 sawa na asilimia 16. Mwaka 2015/2016 aliyekuwa Waziri ni Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. Bajeti ya mwaka 2016/2017, fedha za maendeleo zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge ni shilingi bilioni 101.5 lakini fedha zilizotolewa ni shilingi bilioni 3.3, sawa na asilimia 3.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017/2018, bajeti hii ambayo tunaimalizia sasa, zilitengwa shilingi bilioni 150.2

zilizotolewa ni shilingi bilioni 27, sawa na asilimia 18. Hapa ndipo naposema kwamba hoja hapa si suala la mtu mmoja ni Serikali ya Awamu ya Tano tangu imeingia madarakani haina mpango, haina mkakati wa kuwasaidia wakulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize, tumesema kwamba mapato yanaongezeka, makusanyo yanaongezeka, haya makusanyo yanayoongezeka kwa nini hampeleki kwenye Wizara ya Kilimo? Makusanyo yanaongezeka hatuoni lakini kila siku tunaambiwa makusanyo yameongezeka. Serikali ya Awamu ya Tano naona ni tatizo kubwa na lazima tuchukue hatua sisi Waheshimiwa Wabunge wote bila kujali itikadi ya vyama vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niweze kuzungumzia hoja ya pili ambayo ni kununua kahawa kupitia vyama vya ushirika na nimesikia tunaanza msimu huu kwa kahawa, pamba pamoja na mazao mengine. Suala hapa ni kwamba vyama vya ushirika vilishakuwepo siku za nyuma, kulikuwa na ubadhirifu wa hali ya juu sana na kulikuwa na wizi, je, Serikali imewakamata wale wezi walioiba siku za nyuma? Je, hawa wezi kwa sasa hawapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye zao la kahawa kulitokea jambo moja ambalo ni la ajabu sana. Wakulima wanauza kahawa mwezi wa saba wanakuja kupewa fedha baada ya miezi sita wakati mwingine baada ya mwaka mmoja, malipo yanacheleweshwa. Je muarobaini wa matatizo haya umeshapatikana? Kulikuwa na mambo mengi sana ya ajabu. Watu waliuza majengo ya vyama vya ushirika, waliuza mali za vyama vya ushirika, kwa sababu Serikali hii ya Awamu ya Tano imekuwa ni Serikali ya mizuka, imekuja bila kufanya angalau tathmini, tumekimbilia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na vikundi vya wakulima ambavyo vilikopa fedha Benki, wakanunua *CPU* kwa ajili ya kuboreshea zao la kahawa, hizi fedha atakayelipa

ni nani leo tunakwenda kwenye vyama vya ushirika? Hizi *CPU* watapeleka wapi? Tusipochukua hatua makini kwenye hili tutakwenda kuangukia pua muda si mrefu. Nachoshauri katika hili, hivi vyama vya ushirika vinavyoanzishwa kwenye kahawa, pamba na mazao mengine tungesitisha kwanza, tuweke kipindi cha mpito, tuweze kufanya tathmini vizuri baada ya hapo tuvianzishe tukiwa tayari tumeshatafuta muarobaini wa matatizo ambayo yamewahi kujitokeza siku za nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu masoko ya mazao. Nimesikia Waheshimiwa Wabunge hapa wanalalamika sana mahindi, mahindi; ndipo sasa msingi wa ile hoja yangu ya kwanza kwamba shida ni Serikali ya Awamu ya Tano inapokuja. Ni kwamba, tatizo si mahindi peke yake, angalia kwenye suala la mbaazi. Mbaazi ilikuwa inauzwa kilo Sh.2,000, leo inauzwa Sh.150, Sh.120 hadi Sh.80 naambiwa hapa. Mbaazi inalimwa Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Lindi, Mtwara, Morogoro na maeneo mengine ya nchi, watu wengi wameshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao lingine lenye changamoto ni tumbaku. Leo navyozungumza msimu wa tumbaku unakwenda mwingine lakini tumbaku iko kwenye maghala haijanunuliwa, hali ni mbaya sana. Tumbaku inalimwa Katavi, Tabora, Ruvuma pamoja na maeneo mengine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao lingine ndiyo hili la mahindi. Kule kwetu Mkoa wa Songwe mwaka mmoja na nusu uliopita tuliuza debe moja la mahindi Sh.20,000. Hivi navyozungumza na wewe debe la mahindi linauzwa Sh.3,000, kutoka Sh.20,000 limefika Sh.3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ni mengi yenye changamoto, nenda kwenye kahawa hali ni mbaya, nenda kwenye ufuta, tuliuza Sh.3,000 leo ni Sh.1,000 na kitu . Kwa hiyo, hapa Serikali ya Awamu ya Tano ndiyo mliosababisha matatizo haya na mimi naamini mwarobaini wa haya ni

Serikali hii kuweza kupisha ili Serikali mbadala iweze kuingia na iweze kushika dola kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la pembejeo. Bei ya pembejeo ya mbolea imekuwa ghali sana. Hivi navyozungumza, Mkoa wa Songwe *DAP* inauzwa Sh.59,000, *Urea* inauzwa Sh.55,000 lakini bei elekezi ya Serikali mwaka jana, tuliambiwa Mkoa wa Songwe tungeuza *Urea* kwa Sh.41,500.

**TAARIFA**

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Kutoka Sh.41,500 leo ni Sh.55,000.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Subiri kidogo Mheshimiwa Haonga, taarifa!

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji anayeendelea kuongea, amelitoa neno akimaanisha Serikali hii ni Serikali ya mzuka. Nilivyokwenda kwenye Kamusi ya Kiswahili Sanifu inaniambia mzuka ni *nomino* na *plural* yake ni mizuka ikimaanisha pepo au zimwi na matamshi yake ni mzuka. Nilitaka aliweke sawa hili, je, alikuwa anamaanisha hii ni Serikali ya mazimwi au ya mapepo?

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivi ndivyo, si lugha stahiki inayopaswa kutumika katika Bunge lako Tukufu. Nampa taarifa hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mapunda, nikushukuru sana lakini umeingilia kwenye Kanuni ambayo haitanisaidia nilitaka uende kwenye utaratibu ili ningeyaweka sawa tu lakini namuomba Mheshimiwa mchangiaji aendelee kutumia lugha ya Kibunge tu. Kama umelisema hilo, nitumie madaraka yangu niliyonayo nikusihi tu, wewe ni mchangiaji mzuri tu, hebu futa neno mzuka ili twende vizuri.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba umeniamuru nifute, nitafuta kwa sababu umeniamba nifute. Hata hivyo, naomba nimwambie tu ndugu yangu Mheshimiwa Mapunda kwamba kuna kitu kinaitwa Tatu Mzuka. Sasa ikiwezekana kama ingeweza kumpendeza waambie hata *Vodacom* wakafute neno Tatu Mzuka na inawezekana hajajua maana ya neno hili. Kwa hiyo, nimeshafuta kwa sababu umeniambia nifute lakini akaangalie maana ya neno hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia bei ya pembejeo, kwa mfano, mbolea kuwa ghali sana. Serikali imeweza kutoa bei elekezi kwenye mbolea ya *Urea* na *DAP* lakini bei hiyo elekezi haijafuatwa. Tunasema kwamba *DAP* kwa Mkoa wa Songwe na maeneo mengine iuzwe Sh.54,000 leo inauzwa Sh.59,000. Mbolea ya *Urea* kutoka Sh.41,500 leo inauzwa Sh.55,000. Mimi naona muarobaini wa suala hili ni kujenga viwanda vyetu, tuache sasa kuagiza mbolea na hapa ndipo tutakapoepukana na matatizo hayo. Tutakuja na mambo mengi sana, tutakuja na mikakati mingi sana lakini bila kujenga viwanda vyetu vya mbolea; kulikuwa na mkakati wa kujenga Kiwanda cha Mbolea kule Lindi kule Kuisni, kiwanda kile kimefikia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Taifa letu ni vipaumbele. Tunasema kwamba tunataka kuboresha kilimo tunapeleka pesa kwenda kununua *Bombardier,* fedha hizi tungeweza kuwekeza kwenye viwanda vya mbolea. Tunajua kwamba bila kuanzisha viwanda vya mbolea, bila kuboresha kilimo hata viwanda vingine vitayumba kwa sababu malighafi ya viwanda vingine zaidi ya asilimia 70 inategemea

kwenye kilimo. Nashauri tuanzishe viwanda vyetu vya mbolea kama nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu uchache au uhaba wa rasilimali watu kwenye sekta ya kilimo. Kwa utafiti walioufaya *ANSAF* mwaka 2013 watumishi wanaohitajika kwenye sekta ya kilimo ni 19,228, watumishi waliopo ni 8,756.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana…

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie dakika moja tu.

**MWENYEKITI:** Hapana, hapana.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amekula muda wangu yule.

**MWENYEKITI:** Hapana, hapana, tulikutunzia. Ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Cecil Mwambe dakika tano, Mheshimiwa Joyce Sokombi dakika tano na Mheshimiwa Lucia Mlowe dakika tano.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi tena niweze kuchangia kwenye hii Wizara. Hii ni Wizara nyeti sana kwa sababu asilimia 85 ya wakazi wa Jimbo langu na Tanzania nzima ni wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda huu, naomba tu niende moja kwa moja kwenye mambo machache ambayo napenda Wizara ya Kilimo ikayarekebishe ili watakapokuja hapa waweze kutupatia majibu. Kwanza kabisa, nataka niwakumbushe kwamba pamoja na nia njema kabisa ya Serikali ya kutaka wakulima wa korosho

walipwe kupitia kwenye *bank account* lakini zoezi hili limekuwa na usumbufu mkubwa. Kwa hiyo, tunaomba upande wa Serikali waangalie namna bora ya kufanya kuwasaidia hawa wakulima. Wamekuwa wakikesha kwenye benki ukifika pale Masasi, Ndanda kwa kweli imekuwa kero mpaka watu wanajuta kwa nini walikuwa wanalima korosho ili pesa zao wakapatie kule benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna hujuma nyingine inafanyika kwenye zao la korosho ambayo ni ucheleweshwaji mkubwa wa malipo ya wakulima. Tulipokutana hapa na hata tulipokaa kikao cha wadau wa korosho, tulisema kwamba ndani ya siku saba mnunuzi atakuwa amelipwa malipo yake na ndani ya siku hizo hizo saba tunategemea mpaka mkulima naye atakuwa amepata pesa zake. Kwa hiyo, tunaomba hili nalo likaboreshwe Mheshimiwa Waziri akija hapa aje na majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nikufahamishe kwamba kuna hujuma kubwa sana zinafanyika ndani ya zao la korosho zaidi kwenye ugawaji wa viatilifu. Serikali imepanga na wanasema wataboresha uzalishaji wa zao la korosho. Ni kweli dalili zinaonesha hali nzuri kabisa na kwamba Serikali ina nia njema lakini wasimamizi wa jambo hili hawana nia njema ndiyo ambao wanamwangusha Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015/2016, korosho zilivunwa tani 155 na hela nyingi tu zilipatikana, tukaendelea kuboresha zao hili. Mwaka 2016/2017, zilivunwa tani 265,000 lakini baadaye 2017/2018 tunaratajia kwenda kupata tani 311,000. Sasa ili tupate tani hizo lazima kuwe na mipango mizuri kutoka hatua za awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo mimi limekuwa likinishangaza kila mara. Nilipoanza tu kwa mara ya kwanza kuchangia hapa Bungeni nilitoa taarifa za kampuni moja, mimi naendelea kuiita ya kitapeli mpaka pale nitakapojithibitishia, inaitwa Hammers iko Mkoa wa Mtwara ndiyo ambayo kila mwaka imepata tenda za usambazaji

wa viuatilifu vya zao la korosho. Mwaka jana walishindwa ku-*delive*r tani 700 katika tani 3,000 walizopewa *order,* na ukienda kwenye ripoti ya *CAG* anaeleza sababu za msingi kwamba hii kampuni haina uwezo na nina taarifa kwamba hata sasa hivi imepewa kazi ya kusambaza. Wenye kampuni hii wanafahamika, wanafanya hujuma kubwa sana kwenye zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wengi wanashikiliwa kwenye vituo vya polisi kwa kuambiwa wanahujumu uchumi. Huu uhujumu uchumi wa waziwazi tunaowaonesha hapa sasa hivi mkaufanyie kazi. Kuna Jukwaa la Wakulima wa Korosho liko kule Wilayani Masasi na wanafanya vikao vingi sana kwa Mheshimiwa Bwanausi kule Lulindi, tumeazimia Serikali isipochukua hatua juu ya ubadhirifu unaofanywa na kampuni ya Hammers kwa sababu wenyewe wanafahamika, sisi tutakwenda kufungua kesi mahakamani kwa maana ya kutaka kusaidia wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye taarifa ya *CAG*, anasema kwamba wamegundua Hammers walipopewa tenda ya kupelekea viuatilifu ikiwa ni pamoja na salfa walikuwa wanapunguza kwenye ile mifuko kwa hiyo kumepatikana hasara ya tani 144 sawasawa na thamani ya Sh.837,000,000 sasa hii ni uhujuma kiasi gani? Tunasema Serikali inataka kwenda kuboresha uzalishaji wa korosho, wanaopewa tenda kuleta viuatilifu wamekuwa wakihujumu kila mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine tumeambiwa kwamba nchi yetu inaelekea kuwa nchi ya viwanda hatuoni kabisa mkakati wa wazi unaounganisha Wizara ya Viwanda pamoja na Wizara ya Biashara. Hili zao la korosho ni la moja kwa moja ambalo linatakiwa liwe *processed* kabla ya kusafirisha ili tuweze kuongeza *forex* hapa sisi tulipo lakini hakuna mkakati wa moja kwa moja, Wizara hii imekuwa haipewi pesa za kusimamia shughuli zake za maendeleo, Wizara hii imekuwa na yenyewe inalalamika kama ambavyo wananchi wa kawaida kabisa wamekuwa

wakilalamika. Sasa hatuoni juhudi za moja kwa moja za Serikali hasa zaidi za Chama cha Mapinduzi kwa sababu ndiyo kinachoongoza ya kutaka kweli kuwakomboa wakulima hawa ambao tunaambiwa kilimo ni uti wa mgongo wa nchi yetu. Sasa leo tuko karne ya 21 lakini bado tunaambiwa kilimo ni uti wa mgongo na wazee wetu bado wanatumia jembe la kukokota na ng'ombe na wengine jembe la mkono ili kuweza kupata mazao. Tutapata kweli mazao ya kuweza kushindanisha na soko la dunia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la umwagiliaji. Tunatambua kabisa Wizara ya kilimo, wao wanasema hili suala liko upande wa Wizara ya Maji lakini kwa nini hiki Kitengo cha Umwagiliaji kisiwekwe pamoja na kitengo hiki cha Wizara ya Kilimo? Kwa sababu wao ndiyo wanatakiwa kuhakikisha mazao ya kilimo yanapatikana kwa wakati lakini pia kuonesha namna ambavyo watatumia hiyo ardhi yao. Matokeo yake kitengo hiki kimepelekwa kwenye sehemu ambapo wao wanachoangalia ni upatikanaji tu wa maji, nani ataendeleza yale mashamba ambayo yanatakiwa kuwepo pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Mwambe. Tunaendelea na Mheshimiwa Joyce Sokombi, Mheshimiwa Mlowe na Mheshimiwa Cecilia Pareso wajiandae.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami namshukuru Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara hii ya Kilimo kusema ukweli ni ndogo sana. Ukiangalia nchi yetu ni ya wakulima na wafanyakazi na haya makundi mawili asilimia 80 ni wakulima lakini bajeti inayotengwa hapa ni asilimia 4.8. Kusema ukweli hii asilimia haikidhi kabisa mahitaji ya wakulima hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea pia ni janga la kitaifa. Mbolea bei yake ni kubwa sana ukilinganisha na hali halisi ya wakulima wetu hapa nchini. Cha kushangaza mbolea hii hii haifiki kwa wakati. Kwa mfano, mkulima analima mazao yakishaota mbolea ya kupandia ndiyo inakuja, wakati tayari mkulima ameshalima mazao yake. Inapofika kipindi cha mkulima kuvuna mazao, mbolea ya kukuzia ndiyo inafika. Kwa hiyo, niishauri Serikali kwamba mawakala wawe wa maeneo yaleyale husika kwa sababu kama kijiji fulani kinajulikana kabisa, kama mkisema chagua wakala wao wenyewe wanajuana, kwa nini wasifanye utaratibu huu kuliko kuweka wale mawakala wanaochaguliwa na Serikali? Kusema ukweli hawa mawakala hawafanyi kazi bali ni wachakachuaji tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tuna upungufu wa mafuta hapa nchini. Kusema ukweli ni jambo la kushangaza na ni aibu kwa nchi yetu. Ukiangalia tuna wakulima wanaolima ufuta na alizeti, kwa nini tusiweke kipaumbele kwa wakulima hawa ili tuweze kuzalisha mafuta ya kutosha katika nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mazao kama mahindi mengi hufikia wakati huharibika, kwa nini tusitafute wataalam wakaweza kutengeneza mafuta ya mahindi? Hakuna mafuta mazuri sana kama mafuta ya mahindi na yanashindana na mafuta ya *olive oil.* Wewe mwenyewe unajua kabisa jinsi *olive oil* ilivyo ya bei ghali na mafuta ya mahindi ni hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaangalia viwanda vingi vinategemea sana kilimo. Kwa mfano, katika Mkoa wangu wa Mara Kiwanda cha *MUTEX* kilikuwa kinazalisha nguo zenye *quality* nzuri sana. Hata hivyo, sasa hivi wakulima wa Mkoa wa Mara hawalimi tena pamba kwani imekuwa ni janga la kitaifa kwa sababu mkulima atalima ataenda kuiuza wapi? Tuangalie namna ya kumfufua mkulima wa zao la pamba kwa sababu hivyo viwanda tunavyosema Tanzania ya

viwanda tunategemea tutauza vitu gani katika hivyo viwanda au tutangeneza kitu gani katika viwanda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tujitahidi sana kuwasaidia wakulima wetu katika nchi yetu kwa sababu tunategemea sana kilimo. Kama kweli tunategemea kilimo na kilimo kinatusaidia na tunavyoangalia kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo na asilimia kubwa kati yetu tumesomeshwa kutokana na kilimo walichofanya wazazi wetu sasa iweje leo hii tumdharau mkulima? Naomba tuweke kipaumbele kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni upatikanaji wa mikopo. Kusema ukweli tumemminya sana mkulima kwenye hili suala la mikopo. Tunatoa asilimia 2 tu unategemea mkulima itamsaidia kwa kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hizi benki naomba zifike vijijini. Benki hizi mara nyingi ziko mijini, wakulima vijijini mnategemea kwamba auze mazao yake apate nauli, aende kukopa kule mjini kwa kutumia mazao hayo hayo, kusema ukweli ni kuwatesa hawa wakulima. Kwa kweli naomba tuamshe akili zetu, Mheshimiwa Waziri naomba mnisikilize, tuamshe akili zetu tuwaone na tuweke kipaumbele kwa wakulima, tuwasaidie wakulima hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao hasa ya mahindi katika Mkoa wa Mara, kwa kweli limekuwa ni tatizo kubwa sana. Sasa hivi wakulima wengi wanalima mahindi kwa ajili ya chakula tu na si kwamba ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa Suzana Mgonukulima, dakika tano.

**MHE. LUCIA M. MLOWE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania. Ripoti ya *CAG* ya mwaka 2016/2017 inaonyesha kuwa kiasi kikubwa cha fedha kinawekwa amana ya kudumu. Kwa mwaka 2016/2017, inaonyesha kwamba fedha zilizowekwa amana ni shilingi bilioni 54.7. Badala ya kutoa mikopo kwa wakulima fedha inakwenda kuwekwa kwenye amana na shughuli kubwa ya benki hiyo ilikuwa ni kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2016/2017, benki hiyo imetoa shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya watumishi. Kwa hiyo, kiasi kidogo ambacho kilitolewa mkopo kwa ajili ya sekta ya kilimo, shilingi bilioni 2.2 tu. Vilevile benki hiyo imekuwa maeneo ya mjini tu na hasa Dar es Salaam. Waziri atueleze ni kwa nini benki hiyo haiendi mikoani na hatimaye wilayani na vijijini? Naomba kuishauri Serikali ifanye haraka sana kuhakikisha benki hiyo inafika huko chini kwa wakulima. Kwa sababu Dar es Salaam hakuna wakulima kule, wakulima wako huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo napenda kuchangia ni upatikanaji wa pembejeo kwa wakati. Mwaka jana tualiahidiwa hapa Bungeni kwamba mbolea zitafika kwa wakati na kwa bei nafuu lakini cha kushangaza wakulima wetu wamepata shida sana, kuanzia mwaka jana Oktoba walipoanza kufanya shughuli za kilimo mbolea ikachelewa na Januari hapakuwepo mbolea ya kukuzia. Kama kweli tunataka kwenda kwenye Tanzania ya viwanda, tunaendaje kama hatutekelezi yale ambayo tunawaahidi wananchi wetu? Mheshimiwa Waziri kwa kweli inasikitisha wananchi wetu mwaka huu wamekata tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia suala la ukosefu wa soko. Wananchi wetu pamoja changamoto walizo nazo wamehamasika, wamelima kwa wingi lakini hakuna soko, mazao yote hakuna soko. Katika Mkoa wangu

wa Njombe tunalima kwa wingi mahindi, viazi na matunda lakini hivyo vyote havina soko. Kwa mfano, mwaka 2016/2017 tumezalisha mahindi tani 571,000 na matumizi yanatakiwa tani 172,000 hivyo kuwa na ziada tani 399,000. Inasikitisha, baada ya kuzalisha kwa wingi namna hiyo wananchi hawa walitakiwa wapate faraja, wapate fedha za kuweza kusomeshea watoto wao lakini wakazuiliwa wasipeleke mahindi haya nje. Kwa kweli inasikitisha, inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake atueleze wananchi hawa watafanya nini na mahindi hayo? Maana sasa hivi tunaingia kwenye msimu mwingine, mahindi sasa hivi yamestawi nchi nzima, je, tutafanyaje na mahindi hayo? Naomba tuone ni namna gani tunawahurumia hawa wananchi ambao wanatumia gharama kubwa kununua pembejeo lakini mwisho wa siku wanakuja kuuza debe moja Sh.3,000 au Sh.2,000 kwa kweli inasikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa Suzana Mgonukulima.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii, kwa sababu ya muda nitaenda haraka haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya kilimo inaajiri asilimia 65 ya nguvu kazi ya Taifa; inachangia asilimia 9.9 ya pato la Taifa; inachangia asilimia 65 ya malighafi viwandani na inachangia asilimia 100 ya chakula kinachopatikana hapa nchini. Sekta hii ya kilimo kama ikiwekezwa vizuri itatoa ajira ya kutosha; itaondoa umaskini; tutafikia hicho mnachokitaka

kinaitwa Serikali ya viwanda na tutaweza kufikia uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, sekta hii imekuwa haipewi fedha kama inavyotakiwa. Fedha tunazozitenga hapa Bungeni hazifiki kwenye Wizara na kwenda kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa miaka 10 fedha ambayo imepitishwa na Bunge lako ambayo imefika kwenye Wizara hiyo ni asilimia 2 tu. Mwaka huu fedha hizo za miradi ya maendeleo ambazo zinaombwa imekuwa ni pungufu ya asilimia 23 ya bajeti ambayo tulipitisha mwaka 2017/2018. Maana yake ni kwamba sekta hii ya kilimo imeendelea kupuuzwa, kuachwa nyuma na haipewi msisitizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa sekta ya kilimo kwa mujibu wa Ripoti ya Benki Kuu ni kama ifuatavyo: Mwaka 2011 ilikua kwa asilimia 1.9; 2012 ilikua kwa asilimia 3.2; 2013 ilikua kwa asilimia 4; 2014 ilikua kwa asilimia 3.4; 2015 ilikua kwa asilimia 3.2; 2016 ilikua kwa asilimia 1.9; 2017 ilikua kwa asilimia 1.3. Serikali ya Awamu ya Nne wakati inaondoka madarakani iliacha sekta ya kilimo ikikua kwa asilimia 3.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mmeingia madarakani Serikali ya Awamu ya Tano mmejiita Serikali ya Hapa Kazi, Serikali ya Viwanda, mmeweka mikakati ya kufikia uchumi wa kati lakini sekta ya kilimo ambayo inategemewa na asilimia 65 ya Watanzania, ambayo inachangia pato la Taifa imeendelea kushuka na kufikia kiasi cha asilimia 1.3. Kwa wastani maana yake ni kwamba sekta ya kilimo imekua asilimia 1.9 tu. Kila siku mnatuambia uchumi unakua kwa asilimia 7, Watanzania asilimia 65 wanategemea kilimo, halafu uchumi huu wa sekta ya kilimo tu unakua kwa asilimia 1.9 halafu mnataka miujiza mfikie kitu kinachoitwa uchumi wa kati? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa nchi hii ni lazima wajue adui yao ni Serikali hii ambayo ina mipango mibovu ya kutoweza kuiwezesha sekta ya kilimo. Asilimia 65 ya Watanzania wanategemea kilimo lakini uwekezaji

unaofanywa kwenye sekta hii ni kiasi cha asilimia 0.52 ya bajeti kuu ya Taifa lakini asilimia 5 ya Watanzania ambao wanategemea usafiri wa ndege inapewa kipaumbele ndege unawaacha asilimia 65 ya Watanzania ambao wanategemea kilimo. Huku ni kuwahadaa Watanzania, ni kuwahadaa wakulima, ni kuwadanganya wakulima wa Tanzania. Wakulima wa nchi hii adui yenu ni Serikali hii ya CCM iliyoko madarakani. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia hapa michango ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakilalamikia suala la mahindi kutokuuzwa. Nimeona leo mzigo anashushiwa Mheshimiwa Tizeba pale, hivi tumesahau ni nani alikataza mahindi yasiuzwe. Kauli zikatolewa hapa kwamba mahindi yasiuzwe na Mheshimiwa Waziri Mkuu alisimama hapa akasema hakuna kuuza mazao nje ya nchi. Sasa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanasimama wanampongeza Waziri Mkuu, wanampongeza Rais, wanamshushia mzigo Mheshimiwa Tizeba pale na Mheshimiwa Tizeba ataubeba tu mzigo huu kwa sababu kama huwashauri tunafanyaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana na ushauri. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Suzana Mgonukulima na Mheshimiwa Rehema Migila.

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mvua za kwanza ndiyo za kupandia. Kwa masikitiko makubwa sana mvua za kwanza za kupandia mbolea na mbegu hazipatikani, hili limekuwa ni tatizo sugu sana katika Taifa letu. Tunaposema kilimo ni uti

wa mgongo kwa Taifa letu la Tanzania ukizingatia asilimia 75 ni wakulima, kati yao asilimia 65 ni wanawake na wanawake ndiyo nguzo kuu katika familia zetu. Ni kwa nini basi Serikali kwa kutumia wataalam tulio nao wasiwe na mpango mkakati kuanzia sasa wajue ni wakati gani mbegu na mbolea zifike kwa wakulima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye tafiti imeonekana asilimia 25 ya wakulima hutumia mbegu bora. Katika kutumia mbegu bora asilimia 40 huchangia kupatikana kwa mavuno. Kwa maana hiyo, huyu mkulima atakavyokuwa amepewa mbegu bora mavuno yake yanapatikana kwa asilimia kubwa hivyo kipato chake kinamkwamua kutoka kwenye umaskini kwenda kwenye kundi la kati. Kwa ujumla wake Watanzania tulio wengi watoto wetu tunawasomesha kwa njia ya kilimo, hii haipingiki. Naomba Waziri wa Kilimo anapokuja kuhitimisha hoja yake hii atuambie ni lini sasa Serikali imejipanga kuhakikisha mbegu na mbolea zinaenda kwa wakati muafaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini inasikitisha, wamekiri kuwa asilimia 36 ndiyo sasa mbegu bora zinapatikana, asilimia 64 tunaagiza. Hebu fikiria, tuna vyuo vyetu vya kilimo, ni tatizo lipi linalotukumba sisi Watanzania tusitumie hivi vyuo vyetu kuweza kuwa na wataalam wanaoweza kuzalisha hizi mbegu bora zikapatikana Tanzania tukaepusha gharama ya kutumia kuagiza mbegu katika Taifa lingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukulia mfano Mkoa wa Iringa kuna Kiwanda cha Dash ambacho ni cha kusakata nyanya, hadi navyozungumza kimeshindwa kufanya kazi hiyo kutokana na kwamba wakulima wanaolima zao la nyanya hawatumii mbegu bora hivyo wameshindwa kuzalisha nyanya ambazo zinaweza zikaenda kwenye kiwanda hicho hatimaye na kiwanda kuendelea kufanya kazi. Tuna Maafisa Ugani katika nchi yetu wamebaki maofisini na ndiyo maana wakulima wanalima kwa kubahatisha hatimaye mazao hayapatikani ya kutosha, kama hili zao la nyanya nililotolea mfano la Kiwanda cha Dash. Naomba Serikali basi ifikie wakati wa hawa maafisa wetu kwenda

kule kwenye vijiji wakashirikiane na wakulima wetu ili waweze kuwapa elimu ya kutumia mbegu bora na mbolea ili waweze kupata mazao yanayoendana na hitaji ambalo tunataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge jioni ya leo katika Wizara hii wanachangia Wizara hii kwa machungu makubwa sana hasa watani wetu wa jadi. Nachosikitika tutakapokuja kushika shilingi hiyo ya Waziri yatatoka maelekezo, tutaachia shilingi Wizara hii itabaki kama ilivyo. Nawashauri Waheshimiwa Wabunge kwa vile imeonekena wote tunataka katika Taifa letu la Tanzania kilimo kipewe kipaumbele hii shilingi ya Waziri wa Kilimo ishikiliwe mpaka mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia mustakabali wa nchi ya viwanda, viwanda hivi vinategemea mazao na mazao haya ndiyo tunayosema mbegu bora. Ukitaka mahindi mbegu bora na mbolea, ukitaka pamba mbegu na mbolea na dawa. Kama Wizara hii inakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kuwa bajeti inayotengwa na kupitishwa kwenye Bunge hili Serikali haitaki kutoa basi na wenyewe watuonyeshe kutuunga mkono kwamba Serikali imekaa kimya kwa kutokutoa fedha kwa wakati ili kilimo hiki tunachosema tunataka nchi ya viwanda kiweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitarudi kwenye zao la mahindi kwenye Mkoa wangu wa Iringa. Tunapozungumzia zao la mahindi Mkoa wa Iringa ndilo zao la ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Rehema Migila, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Katani Katani ajiandae.

**MHE. REHEMA J. MIGILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni katika Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo wa nchi yetu katika uchumi na maendeleo ya wananchi wake. Tunajua kabisa asilimia 80 ya wananchi wa Tanzania wamejikita katika kilimo. Hata hivyo, kilimo leo hakipewi kipaumbele hali inayopelekea wananchi waone kilimo si jambo lenye tija kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze zaidi katia zao la tumbaku. Zao la tumbaku ni muhimu sana kwa wakazi wa Tabora na Tanzania kwa ujumla kwani linapelekea nchi yetu na Serikali kwa ujumla lipate pato kubwa hasa katika fedha za kigeni. Hata hivyo, zao hili leo hii limekuwa halina tija kwa mkulima wa Tabora kutokana na changamoto mbalimbali mfano suala la masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi soko la tumbaku si la uhakika, wananchi wanalima mazao kwa shida sana, wanatumia muda mrefu na gharama kubwa lakini hawajui zao lao la tumbaku wataliuza wapi na hata wakija kuliuza bado wanapangiwa bei ndogo sana tofauti na gharama za uzalishaji. Hivyo, naiomba Serikali yetu basi iwahakikishie hawa wakulima wa Tabora soko la uhakika ili kilimo hiki kiwe chenye tija. Serikali ituambie, hivi zao hili ina mpango wa kulifuta kabisa au vipi? Kama ndivyo, kuna zao gani mbadala ambalo Serikali imewaandalia wakulima wa Tabora ili shughuli zao za kiuchumi ziendelee? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda niongelee matumizi ya *Tanzania shilling* badala ya dola. Kulitolewa tamko la matumizi ya *Tanzania shilling* badala ya dola kwenye shughuli mbalimbali za ununuaji wa tumbaku na uagizaji wa pembejeo kutoa nje ya nchi. Naomba nijue, je, Serikali ilifanya utafiti kujua ni gharama kiasi gani ambayo inawa-*face* wakulima wanapotumia shilingi badala ya dola? Nasema hivi nikiwa na sababu kwamba, mkulima anapoingia mkataba na wanunuzi huwa anaingia kwa

gharama ya dola lakini inapokuja kwenye suala la manunuzi anaambiwa auze kwa *Tanzania shilling.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kabisa kwamba shilingi yetu ya Tanzania inashuka thamani siku baada ya siku, lakini inapokuja kwenye suala la uuzaji anauza kwa dola ambayo kwa wakati huo inaweza kuwa imepanda. Tunaomba Serikali ituambie, je, walifanya tafiti za kutosha kubadilisha matumizi ya dola kwenda kwenye shilingi kwa sababu shilingi inamuumiza mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu pembejeo hususani mbolea. Mbolea imekuwa ni janga kubwa sana kwa wakulima wetu pamoja na kwamba Serikali imekuja na mfumo mzuri wa ununuzi wa pamoja lakini ununuzi huo au mfumo huu kwa sasa inaonekana kama vile umefeli kutokana na ukweli kwamba mbolea haiji kwa wakati. Wakati mkulima anahitaji kupanda mbolea haipo akishapanda ndiyo mbolea inakuja, wakati anapotaka kukuza mazao yake mbolea haipo, anapotaka kuvuna ndiyo mbolea inakuja, sasa tunamsaidia huyu mkulima au tunamchezea makidamakida? Naomba Serikali ije na majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imewekwa bei elekezi lakini haifuatwi. Kwa hiyo, tunataka tujue kwa nini Serikali inatoa maagizo ambayo hayatekelezeki? Kama hayatekelezeki ni hatua gani mnachukua kwa watu hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni utitiri wa kodi. Kumekuwa na tatizo la kodi na tozo nyingi sana kwenye suala la tumbaku na anatozwa mununuzi. Kutokana na kwamba mnunuzi huyu anatozwa kodi na tozo nyingi na yeye sasa anaamua kwenda kumbana huyu mkulima wa chini hali ambayo inamuathiri katika bei ya tumbaku. Tunaomba hizi tozo zipunguzwe au zifutwe kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni hivi vyama vya msingi *(AMCOS)* vimekuwa ni shida. Kwanza, havipewi

bajeti ya kutosha kwa ajili ya kujiendeleza lakini pia vimekuwa vinawadhulumu sana hawa wakulima wetu. Tunaomba hili suala liangaliwe hawa wakulima wasiteseke sana, wanalima kwa kuteseka bado waje kudhulumiwa, hapana hili jambo haliwezekani na halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia watendaji wa hivi vyama vya ushirika na hata Bodi za Tumbaku wanateuliwa tofauti na watu wanaojua tumbaku. Mtu hana taaluma ya tumbaku lakini anakwenda kuchaguliwa kufanya kazi kwenye *AMCOS* na kwenye Bodi la Tumbaku. Kama mtu hana utaalam wa tumbaku unafikiria ataifanya kazi hii *effectively?* Tunaomba kabisa Serikali iwaaangalie hawa watendaji wa kwenye hivi vyama vya ushirika pia hawa watu wanaoteuliwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzunguzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. ZUBER M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nichangie na mimi mada iliyopo mbele yetu jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niende moja kwa moja kwenye uchangiaji na mchango wangu niuelekeze kwenye vyama vya ushirika. Ushauri wangu kwenye vyama vya ushirika kuna mambo ya kufanya, aidha, turekebishe Sheria ya Vyama vya Ushirika kwa sababu sheria hii bado ina mgongano mkubwa sana. Mimi mwenyewe nimeshuhudia mwaka huu, kwanza nilikwenda na Mkuu wangu wa Wilaya kukagua ghala tukafungiwa mlangoni tukaambiwa hakuna ruksa, sheria hairuhusu hata kuukaribia mlango wa ghala pale ambapo vyama vya ushirika vinafanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, kuna mgogoro mkubwa sana kwenye vyama vya ushirika kwa sababu

mpaka sasa hivi vyama vya ushirika vimepoteza fedha za wakulima wa korosho takribani zaidi ya shilingi milioni 150. Nilipokwenda kumfuata Afisa Ushirika wa Wilaya majibu anayoniambia anasema yeye hana mamlaka kwa mujibu wa sheria ya kukagua vyama vya msingi, wenye mamlaka hayo ni Tume ya Ushirika. Tume ya Ushirika wako mbali sana na hivi vyama vya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Mheshimiwa Waziri ajaribu kauangalia Sheria hizi za Vyama vya Ushirika. Haiwezekani Mkuu wa Wilaya, Mbunge, Mkuu wa Mkoa hawaruhusiwi kukagua ama hata kuingia tu kwenye ghala eti Sheria ya Vyama vya Ushirika inakataza na hili ndilo linalotuletea matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine, mwaka huu kwenye Vyama vya RUNALI na Lindi Mwambao mpaka leo hii hatujui hatma ya *sulphur* iko wapi. Ukijaribu kuuliza unaambiwa kuna mgongano kati ya Bodi ya Korosho pamoja na vyama vya ushirika. Vyama vikuu vya ushirika bado wanavutana ni nani mwenye haki ya kuagiza *sulphur,* jambo hili limetuletea matatizo makubwa sana. Wenzetu Mtwara chama chao cha ushirika walishaagiza *sulphur* na sasa hivi inafanya kazi lakini sisi bado tunababaishwa tu kwamba kulikuwa na mvutano kati ya Bodi ya Korosho pamoja na Vyama Vikuu vya Ushirika kati ya Lindi Mwambao na RUNALI, nani aagize *sulphur*. Jambo hili Mheshimiwa Waziri naomba mlifanyie kazi ili sheria hii iletwe kama ni kufanyiwa *amendment* basi ifanyiwe *amendment,* ionekane mipaka kwamba Mkuu wa Wilaya mpaka wake ni wapi, Mbunge mpaka wake ni wapi na hiki chama cha ushirika kina kazi gani na Bodi ya Mazao mipaka yake iko namna gani, jambo hili limetuletea shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niongelee Maafisa Ugani. Kwa kweli ndani ya Wizara hii Maafisa Ugani wanaonekana kama vile hawana kazi za msingi, wakati huo sisi tunasema kwamba asilimia 80 au 70 ya wananchi wa nchi hii ni wakulima lakini Maafisa Ugani wameonekana kama hawana kazi wamepelekwa tu kule. Kwa mfano,

kunapotokea shida ya Maafisa Watendaji wa Vijiji au Kata watu wa kwanza wanaoangaliwa ni Maafisa Ugani. Zamani tulikuwa tunachukua hata Walimu Wakuu lakini sasa hivi kwa sababu imeonekana walimu wakuu ni muhimu sana tukaamua kuwaaacha sasa tumechukua Maafisa Ugani ndiyo tumewafanya Watendaji wa Kata na Vijiji. Tena basi wanafanya kazi ambazo si zao na kwa hiyo ufanisi kwenye utendaji wa vijiji haupo kwa sababu hawajasomea na huku kazi ambayo wamesomea wameiacha haina ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye halmashauri zetu huyakuti mashamba ya mfano kwa sababu Maafisa Ugani wana kazi nyingi, wanakuambia ni muda gani niandae shamba wakati huo huo natakiwa nifanye kazi za utendaji? Kwa nini tumewapeleka huko? Tumewapeleka huko kwa sababu tunawaona hawana kazi, jambo hili linatuharibia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hata wale wachache waliopo hawana vitendea kazi. Namwomba Mheshimiwa Waziri kama kweli tunataka kusimamia kilimo kitupatie tija basi jambo hili la Maafisa Ugani ni muhimu sana, watengenezewe mazingira na wakafanye kazi ambazo wamesomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine mimi naona sasa hivi Serikali imeamua kuvuruga kilimo. Zamani mimi wakati nasoma kuna swali unaulizwa pale la jiografia, unatajiwa zao unaambiwa taja mkoa unaolima. Zao la pareto, unataja mkoa unaolima, ukiulizwa chai unaambiwa Rungwe, ukitaja mahindi unaambiwa Iringa lakini leo tumeanza sasa vurugu. Mnataka korosho, pamba na pareto zilimwe nchi nzima, yaani hiyo mnayoanzisha ni vurugu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, navyofahamu Maafisa Ugani wanagawiwa kulingana na taaluma zao. Kuna mtu aliyesomea mambo ya pamba atapelekwa Mwanza na Shinyanga, watu wengine wamesomea alizeti watapelekwa Singida lakini leo hii mnaanza vurugu mnasema korosho na

pamba italimwa nchi nzima hii tunaenda kuvuruga, haiwezekani lazima tuwe na mgawanyo wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana siku zote tunasema hii Serikali muwe na vipaumbele. Maana ya vipaumbele ndiyo hiyo. Sasa haijulikani ninyi korosho, pareto au chai mnalima wapi ni vurugu tu, haiwezekani. Pamoja na kwamba korosho ni fursa lakini alizeti, pamba na kahawa nazo ni fursa lazima mjipange tugawanye tujue. Mimi wakati nasoma jiografia ilikuwa inanieleza hivyo, nikiulizwa tu chai najua Rungwe, mahindi najua Iringa lakini hii vuruga mnayotuletea mimi sikubaliani nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nijielekeze kwenye upatikanaji wa mbegu. Upatikanaji wa mbegu hasa za mahindi, maana kule kwetu kijijini kwetu kwenye Kata ya Mpigamiti kule sisi ndiyo tunaolisha…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa, ukapige miti vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ZUBER M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si ni dakika kumi?

**MWENYEKITI:** Hapana, ni dakika tano tu wewe. Mheshimiwa Katani dakika kumi.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru lakini kabla sijaendelea kuchangia niseme tu kwamba siungi mkono hotuba hii ya Wizara ya Kilimo. Kama mimi ningekuwa Waziri mwenye dhamana kwa namna mambo yalivyo ningejiuzulu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Na. 18 ya mwaka 2009 ukiisoma pamoja na Sheria ya Fedha Na.15 ya mwaka 2010, kifungu cha17A(2) kinaeleza wazi kuwa asilimia 65 ya *export levy* inakwenda kwenye tasnia ya korosho. Msimu wa korosho

2016/2017, asilimia 65 ya *export levy* ambayo ni shilingi bilioni 77, ukijumlisha na maduhuli ya nyuma jumla ya shilingi bilioni 91 haijaenda kwenye tasnia ya korosho. Msimu huu tuliomaliza wa 2017/2018, asilimia 65 ya *export levy* ni shilingi bilioni 115 haijaenda kwenye tasnia ya korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atuambie kama fedha hii ya korosho shilingi bilioni 206 imekwenda kulipia Bombardier wakulima wa korosho wajue. Leo hakuna pembejeo wakati fedha hizi asilimia 65 ndizo zinatumika kwenye pembejeo. Wapo watu wamezalisha miche inayokuja mpaka Dodoma mpaka leo hawajalipwa, wapo watu mwaka jana wamegawa pembejeo mpaka leo hawajalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 30 Mei, 2017, *TRA* ilitoa taarifa na walimuandikia Katibu Mkuu Fedha kwamba *export levy* shilingi bilioni 75 imekusanywa, inatakiwa iende Bodi ya Korosho, haikwenda. Tarehe 15 Desemba, Katibu Mkuu wa Kilimo kaandika barua kumpelekea Katibu Mkuu wa Fedha, fedha haijaenda. Juzi amekuja Waziri wa Fedha anatupa blabla, anasema kuna shilingi bilioni 10, hakuna shilingi bilioni 10, ni sanaa tu, hii Serikali imekuwa ni Serikali ya kubeti. Kwenye kilimo tunabeti? Ndugu zangu kilimo si suala la kubeti mnalolifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukisoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa 30, ili ujue kwamba hii fedha haipo, Waziri anasema:-

*"Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2018/2019 kiatilifu aina ya sulphur pamoja na vifungashio vya korosho (magunia) havitatolewa kwa njia ya ruzuku kama ilivyokuwa msimu wa kilimo 2017/2018. Wakulima watauziwa kwa bei ambayo itatangazwa na Bodi ya Korosho."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake mpaka leo bei haijatangazwa. Hata hivyo, ukienda kwa wakulima wa korosho *sulphur* inauzwa Sh.32,000. Ukiendelea kusoma ukurasa huu, utaona mchakato unaendelea unawahusisha

na watu wa benki kwenye kukopa huko. Kwa hiyo, inaonyesha wazi kabisa kwamba fedha za korosho zile za *export levy* ambavo zipo kisheria hazipo, ndiyo maana Mheshimiwa Waziri ameandika haya. Atakapokuja ku-*wind up* atuambie kama fedha zimelipa *Bombardier,* shilingi bilioni 206 miaka miwili mfululizo, tunakwenda mwaka wa tatu hazionekani mtuambie. Mnacheza kwenye kilimo mnawadanganya Watanzania, mnawadanganya wakulima wa korosho. *(Makofi)*

Mhesimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi ukienda Mtwara, Tandahimba na Newala kuna Chama Kikuu cha Ushirika kinaitwa TANECU. Hiki Chama wenyewe hawa wanadanganywa, Chama hakifanyi vizuri, kinaendeshwa na Serikali. Nami nakuwa na mashaka, inawezekana TANECU Waziri ana hisa nacho. Moja, mwaka jana TANECU imekopa fedha *TIB* imeshindwa kulipa Waziri ameindikia Bodi ya Korosho wameikopesha TANECU shilingi bilioni 2 za Bodi ya Korosho, huyu huyu Waziri Tizeba*,* shilingi bilioni 2. Leo Waziri amekuwa mtu wa benki, wameshindwa kuilipa benki halafu anakaa anakuja anakwambia TANECU wanafanya vizuri kwa kuwapa fedha Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006 Waziri Kikwete ameinusuru TANECU ikiwa inadaiwa. Mwaka 2008, 2009, 2010 wameshtakiwa na *River Valley* wamechukua fedha za wakulima zaidi ya shilingi bilioni moja na kitu wamemlipa *River Valley*, nimekwambia na kwenye takwimu za korosho zenyewe nimemuonyesha tofauti Mheshimiwa Waziri. Msimu wa korosho wa 2016/2017 ukienda kwenye Bodi ya Korosho Tandahimba wamekusanya tani zaidi ya 70,000 lakini maelezo ya TANECU aliowakopesha fedha wametupa maelezo kwamba tumekusanya tani 68,000, kuna tani zaidi ya 2,500 zimepigwa, ziadi ya shilingi milioni 600 za wana-Tandahimba, anajua, nimempa na takwimu wanaendelea kuibeba TANECU. Kumbe nilikuwa sijajua kwamba wanaibeba TANECU kwa sababu kuna maslahi, wameikopesha shilingi bilioni 2 wanatafuta namna ya kurejesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ambazo zina matatizo makubwa ni kwenye tasnia ya korosho. Leo Waziri huyu hawezi akatuambia sababu ya msingi ya kumuondoa Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho. Kama fedha hawapeleki, kama yeye ndiye amemuandikia Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho akopeshe shilingi bilioni 2 lakini juzi wamemtoa kafara Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho. Kama tatizo lilikuwa Bodi ya Korosho kwa nini wasingeondolewa watumishi wote wa Bodi ya Korosho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya si ya leo, Mkurugenzi wa kwanza ameondolewa hakuna maelezo yanayojitosheleza, Mkurugenzi huyu ameondolewa hakuna maelezo yanayojitosheleza, kumbe maelezo ndiyo yale wanatuma vikaratasi wenyewe maana nina barua yake ya kumuagiza Mkurugenzi kuwakopesha shilingi bilioni 2 TANECU ambapo mpaka leo wamekusanya shilingi bilioni 3 kwa wakulima wamerejesha shilingi bilioni mbili *CBT*. Kwa hiyo, wana maslahi yao na inawezekana kuna biashara ndani yake wanafanya, mwisho wa siku wanakaa wanatuambia unajua, TANECU ile, kumbe wenyewe wana mipango yao kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wakulima wa korosho tuwaonee huruma sana. Mnasema mna nia njema kwenye mazao haya, juzi mtu mmoja sijui ni Waziri sijui ni nani anauliza suala la mbaazi hapa anasema mbaazi ni chakula. Sisi Lindi na Mtwara mbaazi ni chakula na ni zao la biashara na siyo chakula tu. Mnawavunja moyo wakulima, mwishowe mtawaambia watu wa Rukwa kwamba mahindi ni zao la chakula tu na si zao la biashara. Ni Serikali ya namna gani hii? Serikali ya kubetibeti, inakuwaje? Inakuwaje tunabeti kwenye masalhi ya wakulima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapozungumza kumekuwa na danadana kwenye *sulphur,* kumekuwa na danadana kwenye mambo haya, wanakaa Bodi ya Korosho na...

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, Kanuni ya 64(1)(g), inazungumzia lugha ambazo zinadhalilisha watu wengine. Ukitumia neno la kubeti maana yake ni kubahatisha bahatisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inapofanya kazi Mheshimiwa Mbunge hawezi ku-*generalize* shughuli za Serikali hii kwamba ni za kubahatisha wakati matokeo ya maendeleo ya Taifa hili katika maeneo mengi yanajidhihirisha wazi na ni mambo ambayo yanaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge neno hili si neno zuri kulitumia. Anao uwezo wa kuchangia hoja yake na kudhihirisha tu maeneo muhimu katika sekta ya kilimo lakini *generalisation* ya Serikali kwamba inafanya kazi kwa kubahatisha si sahihi na ni lugha ambayo kwa kweli haiwezi kuturidhisha, ni lugha ambayo inatudhalilisha sisi tunaofanya kazi ndani Serikali hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI.** Ahsante. Mheshimiwa ngoja sijaamua, mbona una haraka sana? Kubeti ni kubahatisha bahatisha, mchezo wa bahati nasibu.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, uamuzi wangu, kwa sababu lazima Mbunge unapoongea humu tunayoyasema tuwe na hakika nayo..

**WABUNGE FULANI:** Kwani uwongo.

**MWENYEKITI:** Tuwe na hakika nayo.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Maadamu wewe Mheshimiwa uliyekuwa unachangia umetumia, maana nilikuwa naandika mambo mazito hapa mbele yangu, kwa vile neno hilo lina utata, Mheshimiwa Katani nakutaka tu ufute neno kubahatisha uendelee kuchangia vizuri tu kwa hoja ambayo umeianzisha, nilikuwa naisikiliza vizuri tu, hiyo ya shilingi bilioni 2. Hebu futa tu mara moja.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kwa tafsiri yako, maana ungenitaka tafsiri yangu ningeifafanua, nakubaliana na tafsiri yako, niendelee kuchangia.

**MWENYEKTI**. Futa sasa.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nimekubaliana na tafsiri yako.

**MWENYEKITI:** Futa basi.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta ili niweze kuendelea kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayazungumza maneno haya, mfano mzuri kwa nini tunasema tunabahatisha bahatisha. Mheshimiwa Pascal Haonga akiwa anatoa rekodi ya bajeti tunayoipanga humu na namna ya fedha inavyopelekwa kama si kubahatisha ni kitu gani? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Haya kaa basi, muda wako umeisha. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Oran Njeza mtagawana dakika tano, tano.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, niipongeze Wizara ya Fedha na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kazi nzuri iliyofanyika leo ambayo Mheshimiwa Rais ameitolea maamuzi pale bandarini. Nawaomba na Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuweze kupongeza hatua hiyo ambayo Mheshimiwa Rais ameionesha pale bandarini leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati Mheshimiwa Rais anafanya kazi leo bandarini ilikuwa *live* amesema iletwe *amendments* tuweze kuweka sheria ya kuwabana watu wasilete *raw material* ya vyakula kutoka nje ili kuwasaidia wakulima wetu wa ndani. Kwa *slogan* hii, ndugu yangu Mheshimiwa Tizeba, jirani yangu, umesikiliza michango ya Wabunge na mimi tangu nimekuwa Mbunge, lazima niseme wazi kwa kweli leo kimenuka, si cha kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kuhusiana na ununuzi wa pamba, mimi natoka maeneo ya pamba na bahati nzuri Mheshimiwa Tizeba tuko jirani. Ukienda Jimbo la Geita hakuna *go-down* hata moja la chama cha ushirika, jimbo zima na sisi tumewahamasisha wananchi walime na pamba iko nyingi. Hebu nikuulize Waziri mnapoweka haya masharti ya vyama vya ushirika wanunue wanaiweka wapi hii pamba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati zao hili limeachwa kulimwa tumefanya kazi kubwa sana ya kuwahamasisha wananchi. Naamini hata Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu pengine labda hawakupata taarifa sahihi. Hakuna mtu kwa sasa aliyeupokea huu ushirika, hayupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika ni mzuri tunautaka lakini haujaboreshwa kutoka kule tulikoharibikiwa mpaka

tulipo sasa. Ukimwambia leo mwananchi apeleke pamba kwenye ushirika yaani ushirika uwe *broker* wa wenye pesa? Maana yake mkulima ataenda kuuza siku ya kwanza na kwa hesabu nyepesi tu ni kwamba labda kijiji kimoja kinaweza kuwa na vituo nane mpaka kumi; sasa kituo kimoja kinaweza kununua kilo 200, 500 kwa siku, pamba hiyo haiwezi kuchukuliwa na gari gharama ni kubwa, ili ipatikane tani 10 pengine itachukua siku saba, aliyeuza siku ya kwanza atakuwa na siku saba anasubiri pesa, ni kitu ambacho hakiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wewe mwenyewe ni shahidi, unazunguka kule unaona hali halisi. Ushirika uliopo sasa hivi ni uleule umejibadilisha kwa maneno, kwamba walewale waliotuibia ikafa Nyanza na SHIRECU mmewarudisha tena, yaani mtu akasimamie ushirika amejaa viraka matakoni halafu tukampe kazi ya kusimamia hela za wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, Mheshimiwa, nakuheshimu sana.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unisamehe, lugha yetu Wasukuma Kiswahili kidogo kilitupiga chenga, nafuta maneno hayo.

**MWENYEKITI:** Haya, endelea.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali na michango ya Waheshimiwa Wabunge mmeiona mliangalie suala hili. Mheshimiwa Waziri kabla hujafika mwisho wa kuhitimisha hoja yako naomba kesho asubuhi uje na kauli ya kuondoa ushirika kwa sasa ili tufanye maandalizi ya kuweka ushirika mwaka ujao. Naamini kila mtu analalamika kwa upande wake, kuna watu wanalalamikia mahindi, mahindi tulishakosea tusiende kukosea na kwenye pamba ambayo sasa iko sokoni. Tusilimbikize tena matatizo ya mahindi tukaweka na pamba tutaua soko hili la wakulima na wakulima hawatakuwa na moyo tena wa kulima kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia suala la bei, tulikubaliana kabisa kwenye kikao kwamba tupunguze hizi kodi na bahati nzuri kwenye ukurasa wa 46, umesema umefuta mfuko wa *CDTF*, kwa nini tena unaweka Sh.100? Maana yake unatugeuza huku tukiangalia huku unasema tena tulipe Sh.100 ni kwa sababu wakulima wengi hawajui kusoma au hii ni *design* gani? Kwa hiyo, tunakuomba usimamie suala la bei mkulima afaidike ili mwakani tuwe na pamba nyingi hamtakuwa na shida ya kuagiza mafuta machafu kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine, Mheshimiwa Waziri wewe mwenyewe ni shahidi sisi tunatoka maeneo ya wananchi waliotuleta hapa, kuna tatizo gani la kuwalipa mawakala? Tatizo ni nini? Uhakiki gani usioisha? Kila mtu analalamikia mawakala na kila mwaka tunazungumza tunaambiwa mnafanya uhakiki. Mheshimiwa Waziri kwenye kuhitimisha tueleze kwamba pesa haipo ili kama Bunge linaweza kuamua kukuombea pesa likuombee pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wamekufa. Usione watu wamefanya biashara ya kuwakopesha wananchi siyo pesa zao wamekopa kwenye taasisi za benki. Watu wameuziwa nyumba, watu wana matatizo huko, vitu vyao vinapigwa minada Serikali ipo tu inaangalia. Mheshimiwa Waziri, bahati nzuri wewe unatoka sehemu ya wakulima wa pamba, rudisha moyo, kama hii kazi ni ngumu, pia kazi ya kukaa huku kuwasaidia Mawaziri kujibu ni nzuri tu unakuja tunakukaribisha huku nyuma. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekti, suala lingine, nawashangaa sana Waheshimiwa Wabunge, yaani mtu anasimama anasema tumekosea sana kununua ndege. Mimi nikiwaangalia ninyi wote si wa kupanda basi, mbona mnazipanda? Kwa hesabu nyepesi tu ya kibiashara lazima uwe na vitu vya kuingiza. Sasa kuhusu suala la ndege, ndege inasaidia kuleta pesa kwenye utalii. Hii kauli kila siku ya kuponda kununua ndege tunataka tuwaone msiwe

mnapanda *Bombardier* muendeshe magari yenu kwenda Dar es Salaam. Haiwezekani mnaponda humu halafu jioni tunadandia wote *Bombardier* kwenda Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo teknolojia na nchi inayoendelea lazima iwe na vitu vya kuwawahisha watu wafanye kazi Dar es Salaam, asubuhi tuwe Dodoma kwenye Bunge. Kwa hiyo, mimi nawashangaa sana wote mnaobwabwaja kuzungumzia suala la ndege. Pengine ni suala la wivu ambalo kimsingi Watanzania tunahitaji kulipuuza na tusilisikilize kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakuomba Mheshimiwa Waziri, Maafsisa Ugani wawe wanaleta mrejesho kama tulivyomuona Rais anawataka Mabalozi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, unga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaunga mkono hoja mpaka atoe majibu ya kueleweka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kutokana na muda mfupi nitaenda moja kwa moja kwenye suala la mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rejea ukurasa wa 41 wa kitabu hiki cha bajeti ya Wizara. Utafiti wa udongo unaonesha kuwa mbolea inayofaa karibu kwa kanda nyingi zinazolima mahindi na nafaka nyingine *ni Nitrogen Phospharus Sulphur (NPS) na NPS* Zinki. Huo ndiyo utafiti aliotuletea kwenye bajeti yake Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye ukurasa wa 26 Mheshimiwa Waziri anatuambia kuwa mbolea ambayo inaagizwa kwa pamoja *(Bulk Procurement System)* ni mbolea ya *DAP* na *Urea*. Sasa kitaalam maana yake nini? Tunasisitiza tufanye utafiti, wakulima walime kwa tija, sasa wewe unang'anga'ania *DAP* na *Urea* kwa sababu tumeizoea. *DAP* ni kwa ajili ya mizizi na *Urea* inatengenezwa kutokana na zao la petroli, asilimia 70 ukiiweka inayeyuka, inapotea. Sasa mnatulepeka wapi? Kwa kweli hivi ndiyo vitu nafikiri Waziri alipotoka kidogo tu labda akija kesho ajaribu kutuambia kwa nini hafuati utafiti unavyosema? *(Makofi)*

Mheshmiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulisemea ni kahawa. Uzalishaji wa kahawa unapungua mwaka hadi mwaka. Tulikuwa na tani 61,000 mwaka 2015/2016 zikapungua kuja tani 48,000, zikapungua mwaka jana kuja tani 36,000 na sasa hivi kuna *projections* kidogo na tulitegemea kwamba zitafika tani 100,000. Tatizo nalo liko wapi hapa? Tatizo lipo kwenye usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la kahawa linasimamiwa na *TCB*. Nikiangalia muundo wa *TCB* mpaka leo nashindwa kuuelewa. Kwa sababu *TCB* alitakiwa kuwa *regulator* lakini vilevile ndiye anayehusika na masoko. Mnada wa kahawa unasimamiwa na *TCB*, kwa kiasi kikubwa wakulima wananyonywa sana. Leo hii mnada wa kahawa ya Tanzania arabica ni dola 3 kwa kilo, kwa Kenya jirani zetu kahawa hiyo hiyo ya arabica ni kati ya dola 7 -10, angalia tofauti hiyo. Ukienda Ethiopia bei inakuwa ni nzuri zaidi, ni kwa nini? Kwa sababu huwezi ukamuweka *regulator* mtu mmoja huyo anasimamia uuzaji wa kahawa na pale bei hazipangwi kwenye mnada, watu wanakubaliana nje ya mnada. Wakienda pale ni kuthibitisha tu kwamba hii kahawa tunatainunua kwa dola, anayenyonywa ni nani? Anayenyonywa ni mkulima na ndiyo sababu wakulima hataki kuendelea tena na kulima kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kununua mbolea, achilia mazao mengine, kwa sasa hivi ukilima mahindi huwezi kununua ambolea. Kwa hiyo, tukisema kuwa

tunaongeza mazao, tunaongeza uzalishaji, tunaongeza *productivity*, sasa hivi huu mfumo tulio nao ukilinganisha masoko na uzalishaji haviendi pamoja. Leo mfuko wa mbolea kwa ajili ya kahawa ni zaidi ya Sh.70,000 unahitaji mifuko mitatu, ukiuza kwa dola 3,000 huwezi tena kulihudumia hilo shamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna chombo kipya cha bidhaa za mazao *(Tanzania Commodity Exchange Market),* hiyo ndiyo tuifuate. Inafanya vizuri Nairobi na Ethiopia, itaweka bei wazi. Vilevile hata ukwasi *(liquitidy)* kwa ajili ya wakulima itakuwa nzuri. *TCB* tunalipa baada ya wiki mbili lakini nina imani kwa Sheria ya *Tanzania Commodity Exchange Market* ni siku moja, wanaita T+1, siku ya pili unalipwa hela yako. Sasa hizi siku 14 zile hela zikikaa *TCB* ni nani anayefaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo wakulima wananyonywa sana ni kwamba kahawa tunauza kwa *forex* na halmashauri zetu ile *service levy* nayo anakatwa mkulima kwa *forex* lakini *exchange rate* inayotumiwa na *TCB* wanaamua wenyewe, ni pesa nyingi sana inayopotea. Naomba Wizara au Serikali kwa ujumla ielekeze kwamba haya mazao yote, iwe nafaka, korosho, kahawa ziende kwenye soko la bidhaa, ndivyo duniani kote biashara za namna hiyo ndiko zinakokwenda huko. Huku tulikozoea huku, ushirika ndiyo nakubaliana wakusanye wapeleke sokoni, lakini sokoni kule ziuzwe kisasa na chombo hicho tunacho, tukitumie.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Njeza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru sana, kwa leo tunaishia hapo. Naelewa kwa upande wa *CUF* ni nafasi tatu wameweza kupata wawili tu kwa sababu ya dakika 10, Mheshimiwa Vedasto Ngombale hakupata nafasi lakini kwa

upande wa CCM kwa sababu ya maelekezo ya viongozi nimeweza kuingiza majina mawili ambayo hayakuwepo kwenye orodha. Kwa hiyo, lazima tuwatendee haki, kesho mnapoandaa orodha ya wachangiaji Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Joseph Mhagama, Mheshimiwa Rashid Chuachua na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, viongozi mtaona kwenye kambi zenu namna ya kuwaweka vizuri ili wapate nafasi ya kuchangia kama ilivyokusudiwa leo.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo ya wageni waliopo Bungeni jioni hii, wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni tisa wa Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini ambao ni mke wake Bi. Lucia Feet na wanafunzi nane kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wanne wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Mbunge na Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi ambao ni wadau wa maendeleo kutoka Taasisi ya *Tanzania Development Mates Trust* (*TANDEM Trust)* kutoka Mkuranga. Karibuni sana, najua mmekaa sana lakini ndiyo taratibu hizo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo lingine, niwashukuru sana kwa michango yenu mizuri ya ushauri kwa Serikali naamini mtaendelea na kesho kufanya hivyo ili tuhitimishe vizuri hoja hii.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Bunge hadi kesho tarehe 16 saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.10 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 16 Mei, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*